

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 19 Aprili, 2021

(Bunge Lillanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kikao chetu cha Kumi na Mbili, katika Mkutano wetu huu wa Tatu.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO - MAKAMU
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA
NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

SPIKA: Ahsante sana. Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na TAMISEMI, swali litaulizwa na Mheshimiwa Katani Ahmad Katani, kwa niaba yake Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda atamwulizia swali hilo. Mheshimiwa Maimuna, tafadhali.

Na. 94

Kumalizia Vituo Vya Afya – Tandahimba

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA K.n.y. MHE. KATANI A.
KATANI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudzi za wananchi wa Kata za Mnyawa, Nanyanga, Nambahu, Kitama na Nguja ambao wameanza kujenga vituo vya afya kwa nguvu zao wenyewe kwa kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa vituo hivyo?

SPIKA: Majibu ya Serikali kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikano ana Serikali za Mitaa, Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Katani Ahmad Katani, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuitia mpango wa uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi ulioanza katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kituo cha Afya Mahuta, ambapo ujenzi na upanuzi umekamilika na kituo kinatoa huduma ikiwemo ya upasauji wa dharura.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2021 Serikali imeipatia Halmashauri ya Tandahimba shilingi milioni 150 kwa ajili ya kumalizia maboma ya zahanati nne za Miuta, Chikongo, Mnazi Mmoja na Mabamba. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu ya zahanati na shilingi milioni 500 zitatengwa katika mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Kitama.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuunga mkono juhudii za wananchi kwa kutenga fedha za kukamilisha maboma ya zahanati, vituo vya afya na hospitali kwa awamu vikiwemo vituo vya afya katika Kata za Nanhyanga, Nambahu, Kitama na Nguja.

SPIKA: Mheshimiwa Maimuna, swalii la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Jimbo la Tandahimba pamoja na Newala Vijijini lina changamoto ya upatikanji wa vifaatiba pamoja na vitenganishi hali ambayo wakati mwingine inasababisha akinamama wanaojifungua kwenda kutafuta kadi za kliniki mitaani. Je, upi mpango wa dharura wa Serikali wa kunusuru hali hiyo ya upatikanaji wa vifaa tiba pamoja na vitendanishi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; Jimbo la Newala Vijijini lenye Kata 22 lina vituo vitatu tu vya kutolea huduma za afya hali ambayo inaleta changamoto kubwa ya upatikanaji wa

huduma bora za afya kwa wananchi wake. Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Jimbo la Newala Vijijini ili wananchi wale wapate huduma za afya kama ambavyo inahitajika? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya utoaji huduma za afya katika vituo vya afya kwanza kwa kutenga fedha kwa ajili ya kununua vifaatiba, vitendanishi lakini pia ununuzi wa dawa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha huu tunaoendelea nao Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 26 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba na tayari shilingi bilioni 15 zimekwishanunua vifaatiba na vimekwishapelekwa kwenye vituo vya afya vya awamu ya kwanza na awamu ya pili. Kiasi cha shilingi bilioni 11 kiko katika hatua za manunuzi na mara moja vifaa hivyo vitanunuliwa na kupelekwa kwenye vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kituo cha afya katika Jimbo la Newala ni moja ya vituo vya afya vilivyojengwa katika awamu ya tatu na ya nne na hivyo vituo hivi vitakwenda kutengewa fedha za ununuzi wa vifaatiba katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Maimuna Mtanda kwamba vituo vyake hivi vya afya vitawekewa mpango wa kununuliwa vifaatiba ili viendelee kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na idadi ya vitu vya afya katika kata za Jimbo la Newala Vijijini, ni kweli Serikali

inatambua kwamba bado kuna uhitaji mkubwa wa vituo vya afya katika kata za Jimbo la Newala Vijiji na nchini kote kwa ujumla na ndyo maana katika mwaka wa fedha ujao ambapo Mheshimiwa Waziri atawasilisha Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunatarajia kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya katika kata za Jimbo hili la Newala na nchini kote kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hili litaendelea kufanyiwa kazi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaona lakini leo ni Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hiyo mjiandikishe kuchangia.

Tunaendelea na Mambo ya Ndani ya Nchi, swalii la Mheshimiwa Haji Makame Mlenga, Mbunge wa Chwaka.

Na. 95

Malipo ya Mafao Ya Ex E.2152 Makame Haji Kheir

MHE. HAJI MAKAME MLENGE aliuliza:-

Je, ni lini warithi wa askari E.152 (Makame Haji Kheir) aliyefariki tangu Mwaka 2003 akiwa mtumishi wa Jeshi la Polisi Kituo cha Madema watapewa mafao yake?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Haji Makame Mlenga Lengelenge, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Makao Makuu Dodoma na Ofisi ya Polisi Kamisheni ya Polisi Zanzibar hazijapata kumbukumbu za maombi ya mafao wala nyaraka za mirathi kumhusu Askari tajwa hapo juu kutoka kwa msimamizi wa mirathi. Aidha, kwa sasa Jeshi la Polisi Kamisheni ya Zanzibar limeshafanya jithhada ya kufanya mawasilinao

na msimamizi wa mirathi ndugu Mlenge Haji Kheir ili kupata nyaraka zinazohusiana na maombi ya malipo ya mafao ya mirathi ya askari huyo ili ziweze kushughulikiwa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Makame Mlenge, swali la nyongeza nilikuona.

MHE. HAJI MAKAME MLENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yametolewa, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa sababu ni muda mrefu sasa toka marehemu alipofariki na hadi leo hajapata na alikuwa ni mtendaji wa Jeshi la Polisi. Je, ni lini sasa Serikali itawapatia mafao yao hawa wahusika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; naamini changamoto hii haiko kwa hawa tu, iko kwa watu wengi. Sasa je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Tanzania ambao wana matatizo kama haya juu ya kutatua tatizo hili? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimia Khamis Hamza Khamis.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Haji Makame Mlenge, Mbunge wa Jimbo la Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, je ni lini warithi wa marehemu watapata urithi wao. Baada ya kukaa na kupekua, kwanza tumegundua kwamba kweli marehemu alikuwa ni mtumishi wa Jeshi la Polisi, lakini changamoto kubwa ambayo tulifika tukakutana nayo, tulifika wakati tukakosa kujua ni nani anayesimamia mirathi ya marehemu. Sasa hii kwa kweli kwetu ikaja ikawa ni changamoto. Kwa kuwa tayari msimamizi wa mirathi hii tumeshampata, kikubwa tumwahidi tu Mheshimiwa Mbunge, tutashirikiana tuhakikishe kwamba mirathi au mafao

haya yanapatikana kwa wale ambao wanasmamia mirathi hii.

Mheshimiwa Spika, kikubwa nimwambie binafsi niko tayari kwenda kukutana na huyo msimamizi wa mirathi na wengine wanaohusika na mirathi hii ili tuone namna ambavyo tunahakikisha watu hawa wanapata mafao yao au mirathi yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lakini je ni nini sasa kauli ya Serikali katika suala hili au tuna mpango gani? Kikubwa ambacho nataka nimwambie Mheshimiwa cha mwanzo linapojitokeza jambo kama hili kwa wananchi wengine basi cha kwanza kabisa wateue au wafanye uchaguzi wa kuteua msimamizi wa mirathi, kwa sababu sisi la mwanzo tukutane na msimamizi. Yeye ndiye atakayesimamia na kutupa taarifa zote zinazohusika.

La pili, tuhakikishe kwamba wanawasilisha vielelezo kwa sababu hatutaweza kujua nini shida yake kama hakuna vielelezo vilivyowasilishwa vikiwemo vytaarifa ya kifo, vikiwemo labda kituo ambacho alikuwa akifanya kazi, mkoa na kadhalika. Hivyo ni vitu ambavyo vitatusaidia sisi katika kuhakikisha kwamba anapata mirathi yake kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kingine wakati wanawasilisha hivyo vielelezo viende kwa watu husika. Wengine huwa wanawapa tu kwa sababu jirani yake ni askari atampa nipekee. Sasa pengine sio mhusika, matokeo yake sasa lawama zinakuja kwenye Serikali, Wizara au kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho nataka niseme, ufuatilaji wa mara kwa mara, kwa sababu na sisi tutakuwa tunalifuatilia lakini na wao sasa wawe wanalifuatilia kuhakikisha kwamba hii mirathi inapatikana kwa wakati. Nakushukuru.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Swalii la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga. Mheshimiwa Janeth.

Na. 96

Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Kupata Bima za Afya

MHE. JANETH E. MAHAWANGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wajasiriamali wadogo kupata Bima ya afya kuititia utaratibu wa vikundi ambao ulikuwa msaada mkubwa sana kwenye jamii?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Siha, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya inatoa kitita mahususi cha mafao kwa makundi maalum ya wajasiriamali ambao wamejirasimisha shughuli zao kuititia mwamvuli wa jumuiya au vyama vyao vilivyorasimishwa.

Mheshimiwa Spika, makundi ya wajasiriamali yanayonufaika na utaratibu wa bima ya afya ni pamoja na makundi ya wakulima kuititia Vyama vya Ushirika 225 vyenye idadi ya wanachama 6,196; vikundi 17 vya umoja wa wamachinga; wajasiriamali wadogo; wachimbaji wa madini; wavuvi; na mamalishe ambavyo vina idadi ya wanachama 2,315; na vikundi vya umoja wa madereva bodaboda, malori na daladala ambavyo vina idadi ya wanachama 303.

Mheshimiwa Spika, kwa makundi ya wananchi ambao ni wajasiriamali lakini hawamo katika mwamvuli wa jumuiya za wajasiriamali zilizorasimishwa, Mfuko umeanzisha

vifurushi vya bima ya afya vya hiari ambavyo vinazingatia umri, ukubwa wa familia, aina ya huduma na gharama halisi za matibabu nchini ambapo hadi tarehe 31 Machi, 2021 wanachama 32,343 wameshajunga na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya kwa jamii na kwa kutambua matatizo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyaainisha, Serikali inakamilisha Rasimu ya Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo itawasilishwa Bungeni mwezi Juni, 2021.

SPIKA: Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swalii la nyongeza.

MHE. JANETH E. MAHAWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza; kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa dawa katika zahanati zetu na vituo vya afya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuyaruhusu maduka ya dawa ambayo yamesajiliwa kutoa huduma ya upatikanaji wa dawa ambazo wagonjwa wameandikiwa kupitia Bima ya Afya?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; Serikali ina mpango gani wa kuanzisha upatikanaji wa Bima za Afya kwa wajasiriamali wadogo na wananchi wenye vipato dunii kulinia Bima za Afya kwa awamu lakini vile vile kuendelea kupata matibabu? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu, tafadhalli.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swalii ambalo ni muhimu sana hasa kwa mustakabali wa afya ya Watanzania. Swalii la kwanza, Serikali ina mpango gani wa kuruhusu maduka yanayouza dawa kutumia bima. Mpango huo upo na una utaratibu wake ili kuweza kuruhusiwa kufanya

hivyo. Kwa hiyo, kimsingi mpango huo upo labda kama kuna eneo la kuboresha na kuongeza ufuatiliaji zaidi ili kuhakikisha kwamba yanafika sehemu nyingi. Hilo tunaenda kulifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kuhusu wajasiriamali wadogo na kuhakikisha watu wanapata bima ya afya. Sisi tunachofikiri leo kwa sababu kwenye bajeti hii tunaenda kujadili Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, tuko tayari kupokea mawazo yenu na kupokea namna nyingi ambazo tunaweza tukaboresha hii huduma.

Hata hivyo, tunawashauri kwa sasa kuna hicho kitita ambacho kinatumika kwa wajasiriamali ambaao hawajajisajili kwenye makundi maalum ambayo yanaangalia umri, ukubwa wa familia na kadhalika, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge aendeleee kuwahamasisha wajunge kwa hilo, lakini wazo lake la kwamba tunafanyaje wawze kujunga kidogo kidogo nalo hilo ni wazo tunalichukua, wakati tunajadili huu muswada mpya wa sheria tuone tunalifanyaje na wakati hata mwagine kwenye simu na vitu vingine ili wazo lako ambalo ni zuri liweze kutekelezeka. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Bado tuko Wizara ya Afya. Swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau. Mheshimiwa Martha uliza swali lako.

Na. 97

Kiasi cha Zebaki kinachoingizwa Nchini

MHE. MARTHA N. GWAU aliuliza:-

Je, ni kiasi gani cha Zebaki kinaingizwa nchini kila Mwaka?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Elias, Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia...haya!

SPIKA: Umechanganya Mheshimiwa Naibu Waziri. Huyu ni Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019 kiasi cha Zebaki kilichoingizwa nchini kilikuwa ni tani 24.42, ambapo mwaka 2020 kilikuwa ni tani 22.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba zebaki ni kemikali inayotakiwa kudhibitiwa kwasababu ina madhara ya afya ya binadamu kama vile kusababisha upofu, kutetemeka viungo, kupoteza kumbukumbu, kuharibika ngozi, tatizo la ini na figo.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi Serikali, kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeendelea kuchukua hatua za kudhibiti uingizaji wa Zebaki kwa kuwasajili wale wanaoingiza Zebaki nchini na kuchukua hatua kwa wale wanaokiuka sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Martha Gwau, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoa na majibu mazuri ya Serikali, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza. Je, ni mamlaka gani hasa inayosimamia uingizaji wa zebaki nchini?

Mheshimiwa Spika, lakini kingine, Serikali iko tayari kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kutoa elimu ya madhara ya kemikali hiyo ya zebaki kwa wananchi wanaojihusisha na uchimbaji wa madini, hususan Mkoa wangu wa Singida, lkungi na Wilaya ya Iramba? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Dkt. Mollel Tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza swali lake la kwanza ni mamlaka gani inayohusika na kusimamia uingizaji wa kemikali hizi nchini:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema kwenye swali la msingi, ni Mkemia Mkuu wa Serikali, lakini ili tuweze kufanikiwa kwenye hili ni suala ambalo linahitaji kushirikisha mamlaka mbalimbali. Kwa hiyo, kikubwa ni kwamba, kuititia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mamlaka mbalimbali ambazo zinahusika zitashirikishwa, ili kuhakikisha kunakuwepo na udhibiti wa kina.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili. Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu suala hilo:-

Mheshimiwa Spika, ni swali zuri, na nafikiri iko tayari na kwa sababu tunahitaji kwakweli kutoa elimu pamoja na kudhibiti kwa maana ya kuwasajili watu kama hao wanaoingiza, lakini vilevile kuna umuhimu wa ufuatiliaji, ili zebaki isiweze kuingia kwa njia za panya. Wakati huohuo kwenda kutoa elimu hasa kwenye maeneo ya madini ambayo wanachimba dhahabu, kwenye makaa ya mawe ambaao wanahitaji kutumia zebaki. Wakati huohuo kwenye hospitali zetu ambazo vilevile zenaki inatumika, kuhakikisha kwamba, wakati wa ku-*despose* hivyo vitu vinakuwa *disposed*

vizuri. Vilevile kuwalijisha wananchi namna nzuri ya kutumia, lakini kununua vifaa ambavyo wakati wachimba madini wanapokuwa wanatumia basi kuwe na mashine na vifaa maalum ambavyo vinasababisha hivyo vitu visiweze kutoka na kuingia kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri swali lake Serikali iko tayari na nafikiri kwa ajili ya kufanya hatua hiyo fedha zinahitajika.

SPIKA: Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, uliza swali lako sasa.

Na. 98

Chuo cha Ualimu Nachingwea kuwa Chuo Kikuu

MHE. TECLA M. UNGELE aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja kukipandisha hadhi Chuo cha Ualimu Nachingwea kuwa Chuo Kikuu cha Ualimu kutokana na mahitaji ya Walimu kuwa makubwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Juma Omar Kipanga, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla Mohamed Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha vyuo vya ualimu hapa nchini, kikiwemo Chuo cha Ualimu Nachingwea, ni kuhakikisha kuwepo kwa walimu mahiri na wanaotosheleza mahitaji ya walimu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya watu wazima. Vilevile, Vyuo hivi vina

rukumu kubwa la kuwezesha mafunzo ya walimu kazini ambapo walimu walio karibu na vyuo hivyo hupata nyenzo mbalimbali za kitaalamu ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji shulenii.

Mheshimiwa Spika, ongezeko kubwa la wanafunzi na shule katika ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari kutokana na Sera ya Elimu Bila Malipo, limesababisha kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa walimu katika ngazi hizo. Ili kukidhi mahitaji ya walimu katika ngazi hizo, Serikali inaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya vyuo vya ualimu, uwekaji wa samani pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Chuo cha Ualimu Nachingwea ni miongoni mwa vyuo vilivyofanyiwa ukarabati na ujenzi kwa gharama ya shilingi bilioni 1.9.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mahitaji ya walimu, hususan katika ngazi ya elimu ya awali na msingi ni makubwa kutokana na ongezeko kubwa la shule na wanafunzi katika ngazi hiyo, Chuo cha Ualimu Nachingwea bado kinahitajika katika kuandaa walimu wa stashahada na astashahada.

Mheshimiwa Spika, hivyo, wanafunzi wa shahada wanawenza kuendelea kudahiliwa na vyuo vikuu vilivyopo nchini kwa kuwa, bado vina uwezo wa kufanya hivyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Tecla ulishauliza swali la nyongeza? Endelea.

MHE. TECLA M. UNGELE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa ya Wizara ya Serikali kufanya ukarabati wa chuo hiki cha Ualimu Nachingwea, lakini kuna uhaba mkubwa wa samani, yani viti, meza, kwa ajili ya wanafunzi hao, lakini pia chuo hakina uzio. Je, Serikali ipo tayari kupanga bajeti kukamilisha mahitaji hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutokana na jitihada kubwa ya vijana wa Mkoa wa Lindi kuwa na ufaulu mzuri katika kidato cha sita kwa miaka mitatu mfululizo inaonesha kabisa vijana hawa wako tayari kwa ajili ya elimu ya juu.

Je, ni lini Serikali itajenga chuo kikuu Mkoa wa Lindi kwa ajili ya kuchochaea maendeleo kielimu, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo mawili tafadhali Chuo cha Nachingwea, chuo maarufu hiki kimefundisha watu wengi sana.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba, Serikali imeendelea kukarabati vyuo hivi kwa kuhakikisha kwamba, tunakwenda kuimarishe, lakini tunakwenda kuongeza nguvu ili kuongeza udahili kutokana na uhitaji mkubwa sana wa walimu. Nikaeleza katika swali lile la msingi kwamba, Serikali bado inakihitaji chuo hiki ili kiweze kutoa taaluma hiyo ya astashahada na stashahada ili kuongeza idadi hiyo ya walimu.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile katika swali lake ambalo linauliza suala la miundombinu ya samani, kwa takwimu tulizokuanazo chuo chetu cha Nachingwea kina jumla ya viti 400 mpaka hivi sasa, kwa rekodi tulizonazo, lakini wanafunzi waliopo ni 295. Katika muktadha huo haioneshi kwamba, kuna uhaba wa samani kama viti na meza, lakini sambamba na hivyo tuna *computer* 30 ambazo zinawezesha vitengo vyetu vile vya kutumia *computer* kupata mafunzo kwa kutumia *computer*, lakini tuna *projector* tano ambazo zimenunuliwa hivi sasa na *computer* mbili ambazo zilikuwa za zamani.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeendelea na juhudhi zake za kuhakikisha kwamba, tunatengeneza mazingira mazuri ya kupata walimu wa kutosha. Na katika kipindi kilichopita Serikali imeweza kutumia jumla ya shilingi bilioni 84.1 kwa ajili

ya kuhakikisha kwamba, tunatengeneza miundombinu, lakini vilevile samani zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, suala la uzio; Serikali bado inaendelea na mkakati wa kuhakikisha tunaboresha mazingira haya. Na hili sasa tunaliingiza kwenye bajeti kuhakikisha maeneo haya yanapata uzio ili kuweza kutengeneza usalama wa mali pamoja na samani za vyuo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili kuhusiana na suala la chuo kikuu:-

Mheshimiwa Spika, nipende tu kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa hivi sasa bado vyuo vyetu vilivyopo hapa nchini, vyuo vikuu, vina nafasi za kutosha. Na tunawashauri tu wananchi wa Lindi waweze kuvitumia vyuo ambavyo vipo kwasababu, vyuo havijengwi kwa kufuata mikoa wala kanda, bali vyuo hivi vinakuwa ni vya kitaifa, basi wanafunzi hawa wanaweza kwenda katika vyuo vingine ambavyo pale Mtwara tuna chuo kile cha *St. Marius* wanaweza kupata taaluma yao pale, lakini tuna matawi ya vyuo vikuu huria karibu katika mikoa yote ikiwemo na Mkoa huu wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Chuo chetu cha Dodoma walihitajika kudahiliwa wanafunzi au kuna nafasi 40,000 lakini mpaka hivi sasa wanafunzi waliodahiliwa ni 29,595 kwa hiyo, tuna nafasi za kutosha katika vyuo hivi ambavyo vinatosheleza ku-absorb wanafunzi wote. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Nimekuona Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, Mheshimiwa Amandus Chinguile, uliza swali lako.

MHE. AMANDUS J. CHINGUILE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwanza nipende kuipongeza Serikali kwa kutuletea zaidi ya billioni 1.9 kwa ajili ya ukarabati mkubwa kwenye Chuo hiki cha Nachingwea:-

Mheshimiwa Spika, swali langu, chuo hiki ni kikongwe, Je, Serikali sasa haioni haja ya kuanzisha kozi maalum ya masomo ya sayansi, ili tuzalishe wataalam wengi, na hasa kwenye masomo haya ya sayansi kwenye Chuo cha Nachingwe?

SPIKA: Majibu ya swali hilo *specific* Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwa vile ametuletea wazo, basi tunaomba tulichukue twende tukalifanyie utafiti, tuangalie uhitaji wa kozi hiyo katika eneo hilo. Iwapo kama Serikali itabaini kwamba, upo huo uhitaji tutaweza kuingiza kwenye mipango yetu. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Ujenzi na Uchukuzi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Stella Simon Fiyao.

Na. 99

Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni

MHE. STELLA S. FIYAO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mbalizi – Mkwajuni ili kuepusha adha wanayokutana nayo Wananchi hususani kipindi cha mvua?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Kasekenya Msongwe.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbalizi – Chang'ombe – Mkwajuni – Patamela – Makongolosi yenye

urefu wa kilometra 117 ni barabara ya Mkoa inayounganisha Mkoa wa Mbeya na Songwe na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mbalizi hadi Galula yenyе urefu wa kilometra 56.

Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zizonaendelea kwa sehemu ya Galula - Mkwajuni - Makongolosi kilometra 61 zinaendelea. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Mbalizi hadi Galula chenye urefu wa kilometra 56 ambayo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika.

Mheshimiwa Spika, wakati ujenzi kwa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*), inaendelea kuifanya matengenezo ya aina mbalimbali kila mwaka barabara hii. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Stella Fiyao, nimekuona.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hali ya barabara ni mbaya sana kwa wananchi wa Wilaya ya Songwe na hali hii imesababisha wananchi kupoteza maisha, ikiwa ni pamoja na kuzikosa huduma za muhimu na za msingi ambazo wanatakiwa kuzipata katika Ofisi ya Mkoa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kulichukulia jambo hili kwa dharura, ili wananchi waweze kuepukana na changamoto ambayo imekuwa ikiwakabili kila mwaka katika Wilaya ya Songwe? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Geofrey Msongwe *Engineer*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara anayoisema mwaka huu ilikuwa imesimama kwasababu ya mvua nyingi ambayo inaendelea kunyesha. Na kuna daraja linalounganisha Kijiji cha Tanga na Mbala ambapo mto ilitoka kwenye njia yake ukakata barabara na ukawa umetengeneza bwawa.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea na hasa kupitia Mbunge Mulugo wa Jimbo la Songwe tumekuwa mara nyingi tunawasiliananae na anafahamu fika kwamba, hadi sasa wakandarasi wako *site*. wameanza Alhamisi ya wiki iliyopita, tumapata fedha shilingi milioni 700 kwa ajili ya kukarabati batabata hiyo na kurejesha mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya hiyo barabara kukatika kuna barabara nyingine ambayo walikuwa wanapitia sasa Chunya – Mbeya kwenda Songwe. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hilo lipu na tayari wakandarasi wako *site* na milioni 700 ziko tayari kwa ajili ya kuendesha mawasiliano ya barabara. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. nimekuona Mheshimiwa Aysharose Matembe, uliza swali lako tafadhali.

MHE. AYSHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona, kwa kuwa, changamoto ya barabara ya Mbalizi – Mkwajuni inafanana kabisa na changamoto ya barabara inayoanzia Sepuka – Ndago hadi Kizaga. Na barabara hii tumekuwa tukiilizia mara kwa mara, lakini tunaambiwa ipo kwenye upembuzi yakinifu. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami, ili kuchochaea maendeleo ya Wilaya ya Ikungi pamoja na Wilaya ya Iramba? Nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer Geofrey Kasekenya Msongwe*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nimpungeze Mheshimiwa Aysharose Matembe ambaye kwa kweli mara nyingi amekuwa akifuatilia, si tu barabara hii ya Sepuka – Ndago hadi Kisanga, lakini amekuwa akifuatilia barabara nyingi za Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hizi barabara ni kati ya zile barabara ambazo zimeainishwa kwenye llani yetu ya Uchaguzi kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu, lakini pia na usanifu wa kina, ili iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute Subira tupitishe bajeti tuone kama hizi barabara zitakuwa ni kati ya ambazo tutaanzanazo kwa mwaka huu. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, bado tunaendelea na Wizara yako lakini nina matangazo kama mawili. La kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu hatuko naye leo hapa Bungeni yupo Dar es Salaam kwa kazi maalum. Kwa hiyo, mwenye kuhitaji huduma basi yupo Mheshimiwa George Simbachawene. Mnakaribishwa sana kumuona Mheshimiwa Simbachawene. (*Makof*)

Tangazo la pili, nina wageni maalum kabisa ambao napenda niwatambulise nasita kusubiri. Wageni hawa mkiangalia kwenye *gallery* mtawaona wapo na mashati meupe ya yange yange na wanapendeza sana kwenye *gallery* zote mbili. Hawa mabinti ni 166 kwa ujumla wake wakiwemo walimu 12, wanafunzi 150 na watumishi nne wa Shule ya Wasichana ya Bunge iliyoko Kikombo. (*Makof/ Vigelegele*)

Naomba msimame, hao ni Bunge *Girls*. Ni matokeo ya kazi ya mikono yetu wenyewe sisi Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Moja. Ni mchango mkubwa sana kwa Serikali na kwa nchi yetu. Watoto hawa ni wa *PCM, PCB* na *CBG*. (*Makof*)

Hongereni sana, Bunge lina matumaini makubwa sana na shule hii na tunawatachia kila la kheri. Waheshimiwa Wabunge baadaye basi mpige picha na watoto wetu hawa hapo nje itapendeza. Ahsanteni sana mnawea mkakaa. (*Makofi*)

Kipekee nimirambulisha Mwalimu Mkuu wa Shule hii, Mwalimu Salome Eliya Mkombola. Ahsante sana Mwalimu Salome, karibu sana. Nikuhakikishie Bunge litakupa kila aina ya ushirikiano kwa kadri mnavyoendelea. (*Makofi*)

TWPG msisahau shule hii ni zao la mkono wenu, muwe karibu nayo, muitembelee mara kwa mara, mjitahidi kutafuta wadau kwa ajili ya kuziba baadhi ya mapengo ambayo yapo. Msisahau hata siku moja kwamba watoto hawa kwa kweli ni matokeo ya kazi ya mikono yetu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza. (*Makofi*)

Na. 100

**Kusuasua kwa Ujenzi wa Barabara ya
Muheza – Amani**

MHE. HAMIS M. MWINJUMA aliuliza:-

Kasi ya ujenzi wa barabara ya Muheza – Amani sio ya kuridhisha na hadi sasa maeneo korofit bado hayajafikiwa:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na awamu ya pili katika ujenzi wa barabara hiyo kuanzia Amani kuelekea Muheza ili kutatua changamoto zilizopo wakati ujenzi wa barabara ukiendelea?

SPIKA: Majibu wa swali hilo bado tupo Ujenzi wa Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara ya Muheza – Amani yenye urefu wa kilometra 40, Serikali iliamua kujenga kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha baada ya kukamilika kwa upembusi yakinifu na usanifu wa kina mwaka 2015. Awamu ya kwanza ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sasa yenye urefu wa kilometra saba kuanzia Muheza kuelekea Bombani inaendelea na imefikia asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kukamilika kwa sehemu ya kwanza ya mradi huu unaoendelea, ujenzi wa sehemu ya pili ya kuanzia Bombani hadi Amani utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Lengo ni kukamilisha ujenzi wa barabara yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha za kukamilisha ujenzi wa sehemu ya barabara iliyobaki, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*) inaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hii ikiwemo sehemu korofiki ili kuhakikisha inapitika majira yote. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, barabara hii ilitengewa shilingi milioni 600 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mwana FA, swali la nyongeza.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Najua barabara yote kilometra 40 ina umuhimu mkubwa, lakini kipande katikati ya Kisiwani na Kibaoni ndiyo kipande hasa ambacho kina matatizo makubwa, Je, Serikali ina mpango wowote wa kuhakikisha kipande hiki kwa namna ya kidharula ili kuhakikisha kwamba kinapitika wakati wote wa mwaka? (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer Msongwe* bado tupo na wewe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, barabara hii inaendelea kutengenezwa. Jana nimepita maeneo ya Tanga na nilikuwa na Meneja wa *TANROADS* na moja ya maelekezo ambayo tumempa ni kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yana shida likiwepo hili la kati ya Kisiwani na Kibaoni wahakikisha kwamba wanapeleka nguvu zao ili pasije pakatokea tatizo la kutokuwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu barabara hii ipo kwenye matengenezo ndiyo maana tumeendelea kutenga hizo shilingi milioni 600 kwa ajili ya kurekebisha sehemu zozote ambazo ni korofi ikiwemo pamoja na hili eneo kati ya Kisiwani na Kibaoni. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Swali la mwisho kwenye Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi litaulizwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela.

Na. 101

Barabara ya kutoka Kilyamatundu – Illemba – Muze - Mfinga - Majimoto Kujengwa kwa Lami

MHE. DEUS C. SANGU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kilometra 200 kutoka Kilyamatundu kupitia Illemba, Muze, Mfinga mpaka Majimoto?

SPIKA: Bado tupo tupo Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer Msongwe*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilyamatundu – Muze – Mfinga – Kasansa hadi Majimoto yenye urefu wa kilometra 206 ni barabara ya Mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini yaani *TANROADS*. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Songwe eneo la Kilyamatundu na Kamsamba katika Daraja la Momba.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, Serikali ilianza kuchukua hatua za kuimarisha barabara hii kwa kuanza na kukamilisha ujenzi wa Daraja la Momba lenye urefu wa mita 84 na barabara za maingilio zenye urefu wa kilometra 1.2 ambalo lilikuwa ni kikwazo kikubwa sana cha mawasiliano baina ya Mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu ambao unahusisha sehemu ya Kilyamatundu – Muze yenye urefu wa kilometra 142. Kazi ya usanifu imefikia asilimia 50. Mara usanifu wa kina utakapokamiliika, maandalizi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami yataanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mbunge wa Kwela, Mheshimiwa Sangu, uliza swalii lako.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanayoleta matumaini makubwa kwa wananchi wa Jimbo

la Kwela naomba nitoe *alert* kwa Serikali, mtaalam wa upembuzi yakinifu ambaye yupo *site speed* yake ni ndogo sana. Niombe tu *close follow-up* kuhakikisha anamaliza kazi hiyo ndani ya kipindi cha mkataba.

Mheshimiwa Spika, swalilangu la nyongeza; kwa kuwa barabara ya kutoka Mji Mdogo wa Laela kupitia Mnokola, Mwimbi mpaka kuunganisha nchi jirani ya Zambia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni. Wananchi wa maeneo ya Kata hizo zilizopo pembezoni mwa barabara wamekubali kuachia *reserve* ya barabara ili ijengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu ni muhimu kwa uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla. Naomba kupata *commitment* ya Serikali ni lini barabara hii itafanyiwa upembuzi yakinifu ili baadaye iweze kujengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, swalilangu la pili, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alipofanya ziara Mkoa wa Rukwa aliahidi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka katika Kijiji cha Kaengesa - Seminari ya Kaengesa - Kitete kilometra saba na tayari upembuzi yakinifu umekamilika. Ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kuwa wananchi wanaisubiria kwa hamu na wanataka sana kuipata hiyo barabaa ya lami? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deus Sangu, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumechukua ushauri wake na tutahakikisha kwamba *TANROADS* wanamsimamia mkandarasi ili aweze kukamilisha usanifu wa kina unaoendelea ndani ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, maswali yake mawili ya barabara ya Lahela kwenda nchi jirani lakini pia Kaengesa kwenda Kitete kilometra saba, kama alivyosema hizi ni ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kwela, tumesikia na huo ndio ukweli kwamba ahadi zote zilizoahidiwa na viongozi wetu wa kitaifa zitaendelea kama zilivyoahidiwa. Kwa hivyo, Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba tunapoanza upembuzi na usanifu tayari ni hatua ya utekelezaji wa ahadi hizo. Tukishakamilisha basi nimhakikishie kwamba barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha kama viongozi wetu wa kitaifa walivyoahidi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tuvuke tuelekee Nishati, Mheshimiwa Ridhiwani hayupo kwa niaba yake Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

Na. 102

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Miradi ya
Umeme – Chalinze**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI K.n.y. MHE. RIDHIWANI J.
KIKWETE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Chalinze waliopisha ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi na Bwawa la Mwalimu Nyerere?

SPIKA: Majibu wa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme

wa msongo wa kilovolti 400 kutoka Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Mwalimu Julius Nyerere hadi Chalinze lakini pia ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme katika Kijiji cha Chagua - Chalinze.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia *TANESCO* imekamilisha tathimini ya mali za wananchi na Taasisi zilizopisha utekelezaji wa mradi huu na fidia kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 42.3 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi walipisha mradi. Fidia ya wananchi hao itaanza kulipwa muda wowote kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 baada ya taratibu zote kukamilika.

SPIKA: Mheshimiwa Bonnah Kamoli, uliza swali lako tafadhalii.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nataka kujua ni lini Serikali italipa fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu mradi huu umekaa sasa ni miaka minne, je, Serikali ipo tayari kuwapa kifuta jasho wananchi ambao wamesubiri kwa muda wote huo wakati wakisubiri malipo haya? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri Nishati, Mheshimiwa Byabato Lujwahuka, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Bonnah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nieleze kidogo kwamba fidia inayotakiwa kufanyika katika maeneo haya ni fidia ambayo ni ya miradi ambayo tunaweza kuiita miradi ambatanishi. Kimsingi umeme unaozalishwa katika Bwawa letu la Mwalimu Nyerere *megawatt* 2,115 unatakiwa utoke Mwalimu Nyerere kuja kuingia katika Gridi ya Taifa na

unaingilia kwenye Gridi ya Taifa pale Chalinze. Kwa hiyo, itajengwa hiyo njia ya kutoka Mwalimu Nyerere kuja Chalinze, lakini Chalinze kwenda Kinyerezi na Chalinze kuja Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuhusu *exactly* fidia italipwa lini ni tusema ni kabla ya kufika mwezi wa kumi mwaka huu, kwa sababu lazima kwanza tulipe fidia ndiyo tutaweza kujenga njia hiyo ya kupeleka umeme. Njia hiyo ya kupeleka umeme lazima ikamilike kabla ya tarehe 14 Juni, 2022 ili iweze kusafirisha ule umeme utakaozalishwa pale Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fidia itatolewa kwa wakati na haitochelewa kwa sababu kuchelewa kwa fidia hiyo kutasababisha mradi wa Mwalimu Nyerere usiweze kuingiza umeme wake kwenye *grid*.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili kama Serikali ipo tayari kuwapa kifuta jasho, niwahakikishie waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoendeshwa na Mama yetu Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ni Serikali sikivu na isyoonea mwananchi taratibu za fidia zipo na zinafahamika kwamba inalipwa kwa namna gani na ndani ya wakati gani. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa fidia stahiki italipwa kwa kila anayestahili kulipwa kwa mujibu wa viwango vyta kisheria vilivyowekwa na muda uliowekwa kwa ajili ya hesabu hizo.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo ni la Wizara ya Maji, litaulizwa na Mheshimiwa Paulo Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, simuoni, Mheshimiwa Flatei kwa niaba yake.

Na. 103

**Mpango wa Wakala wa Maji Vijijini Kuchimba
Visima Mbulu Mjini**

MHE. FLATEI G. MASSAY K.n.y. MHE. ZAKARIA P. ISSAAY
aliuliza:-

Je, ni lini Wakala wa Maji Vijijini atachimba visima sita katika Vijiji vya Aicho, Gidamba, 7 Gunyoda, Silaloda, Boboa na Titiwi katika Jimbo la Mbulu Mjini?

SPIKA: Majibu wa swali hilo, Naibu Waziri Maji Mheshimiwa Eng. Maryprisca Winfred Mahundi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zakaria Paulo Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuchimba visima kwa ajili ya kutumika kama vyanzo vya maji inafanyika maeneo mengi hapa nchini hivyo ili kuepuka ucheleweshaji inabidi kushirikisha makampuni binafsi kuchimba visima baada ya Wataalam wa Mabonde kufanya utafiti na kuainisha maeneo yenye maji chini ya ardhi. Hivyo, kazi hii zabuni imetangazwa kupitia Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mkoa - Babati (BAWASA) ambapo Visima virefu vitatu katika vijiji vya Aicho, Boboa na Titiwi vitachimbwa kuanzia mwezi Mei, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, visima vilivyobaki katika vijiji vya Gidamba, Silaloda na Gunyoda vitachimbwa katika mwaka wa fedha 2021/22.

SPIKA: Mheshimiwa Flatei, swali la nyongeza

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijiji vya Aicho vina vijiji pacha vya Gembak, Kamtananat, Maretadu-Chini, Khaloda, Umburu, je, ni lini vijiji hivi vitachimbiwa visima vya maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwakuwa Wakala wa Maji alishachimba visima sita Jimbo la Mbulu Vijijini katika Kijiji

cha Khababi, Labai, Endagichani, N'ghorati, Gendaan Madadu-Juu, je, lini sasa watamalizia kazi ya usambazaji kwa sababu walishamaliza kazi ya uchimbaji? (*Makof*)

SPIKA: Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa *Engineer Maryprisca Mahundi*, tafadhali majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lini vijiji pacha ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge vitapata visima vya maji. Wizara tumeendelea kujipanga kwa dhati kabisa kuona kwamba kwa miezi hii miwili iliyobaki katika mwaka huu wa fedha kuna maeneo ambayo visima vitaendelea kuchimbwa na kwa mwaka ujao wa fedha tumetenga visima vingi vya kutosha karibia majimbo yote. Kwa hiyo na vijiji hivi tutaendelea pia kuvipa mgao kadri fedha tutakavyoendelea kuzipata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu visima sita vilivyo chimbwa usambazaji wa maji utaanza lini, tayari tumeendelea kujipanga, maeneo ya aina hii tunahitaji kuona wananchi wanapata maji kutoka kwenye mabomba. Kwa hiyo, usambazaji utaendelea kuwa wa haraka. Kwa eneo hili la visima sita naagiza watu wa Babati (*BAWASA*) wajipange vizuri kwa sababu ipo ndani ya uwezo wao waweze kukamilisha kazi hii.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtaona muda wetu wa maswali umeisha, sasa niendeleee kuwatambulisha wageni tulionao.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Riziki Shemdoe. Ahsanteni sana, karibuni sana na hongera sana Katibu Mkuu na wenzako kwa kuteuliwa hivi majuzi kwa nafasi hiyo nzito na nyeti. Sisi Wabunge ni wadau wako

wakubwa na tutakupa kila aina ya ushirikiano. Ahsante sana.
(Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wageni sita wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambao ni wapiga kura wake, wakiongozwa na ndugu Seraphino Lanzi. Ooh, karibuni sana. Hawa ni Machifu wa Kihehe. Karibuni sana, sana hapa Bungeni, kwa kweli mmependeza kweli kweli. Ahsanteni sana, mnaweza kukaa chini. *(Makofi)*

Mmoja wa Maspika waanzilishi wa Bunge hili baada ya uhuru ni Mzee Adam Sapi Mkwawa na mzee Mkwawa alikuwa havai mavazi haya tunayovaa leo, yeye alikuwa anavaa mavazi haya ya Machifu wa Kihehe. Sasa naangalia utaratibu kama inawezekana, kama Mheshimiwa Kiswaga ataniruhusu na Wabunge wa Mkoa wa Iringa, nami nivae mavazi hayo kama Spika hapa. Ahsante sana wazee wangu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Shigongo James ambao ni mpwa wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Ndugu Zakayo Shushu karibu sana.

Wageni 16 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, ambao ni wasanii wa muziki waigizaji wa filamu, watangazaji pamoja na wabunifu wa mitindo ya mavazi kutoka Dar es Salaam. Sasa hawa niwatambulish kama ifuatavyo:-

Kwamba tuna wageni watatu ambao mwezi huu walipata tuze nchini Zambia ambao ni Malkia Caren, yupo? Hawapo. Ziza Munna! Inaelekea hawajaingia hawa, tutawatambulisha baadaye. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Aweso Waziri wa Maji kutoka *Clouds Media* Jijini Dar es Salaam ambao ni Shafii Daudi, Mkuu wa Vipindi vya *Clouds FM* na ndugu Redemta Siza, Mkuu wa Ubunifu na *Biashara Clouds Media Group*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Simon Songe ambaye ni rafiki yake kutoka Musoma Mkoani Mara. Ndugu Steven Martin, ahsante. (*Makof*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Festo Lugange ambaao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Ndugu David Mtandala na Emmanuel Mndeme, ahsanteni sana. (*Makof*)

Wageni 10 wa Chama cha Skauti Tanzania kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Kamishna wa Skauti Mkoa wa Dodoma, ndugu Salama Katunda, ahsanteni sana. (*Makof*)

Nina matangazo machache mengine. Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Ndugu Tarimba Abbas anaomba Kamati ya Utendaji ya *Bunge Sports Club* mukutane pale Msekwa saa 9.00 jioni ya leo saa 9.00 alasiri. *Bunge Sports Club* mukutane pale Msekwa Kamati ya Utendaji. (*Makof*)

Halafu Meneja wa *Bunge Sports Club* anawaomba Waheshimiwa tuzidi kujitokeza katika mazoezi kule Uwanja wa Jamhuri kila siku asubuhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Rashid Shangazi anaomba Waheshimiwa Wabunge wote baada ya shughuli za mchana huu kusitishwa, basi mukutane pale Msekwa kwa ajili ya agenda ya kuanzisha Mfuko unaoitwa Mfuko wa Faraja. (*Makof*)

Ndugu Hussein Nassor Amar, Mwenyekiti wa Wabunge Waislamu ananitaka niwatangazieni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Umoja wa Wabunge Waislamu kwamba kutakuwa na kikao kitakachofanyika leo tarehe 19 Aprili, 2021 saa 7.00 mchana katika ukumbi Na. 229 ghorofa ya pili, Jengo la Utawala. Kamati ya Uongozi ya Wabunge Waislamu mukutane ukumbi 229 mchana wa leo.

Katibu.

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA
MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, sasa moja kwa moja inabidi nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa ajili ya kuwasilisha hotuba yake. Mheshimiwa Ummy, karibu sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2 na Mafungu 26 ya Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* pamoja na viambatisho 25.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan

kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia kauli mbiu yake ya "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi lendelee." Watanzania wana imani na matumaini makubwa naye na kuwa katika Awamu ya Sita nchi yetu itapiga hatua kubwa zaidi za kimaendeleo hususan katika nyanja za kiuchumi na kijamii na hivyo kuwanufaisha wananchi walio wengi na hasa wanyonge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pole zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuondokewa na mpendwa wetu na kipenzi cha Watanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuondokewa na Jemedari wetu mahiri Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ni pigo kubwa siyo kwa Tanzania tu, bali ni pigo kwa Afrika Mashariki, Bara la Afrika na dunia nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mchango mkubwa wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Taifa hili hautasahaulika kizazi hadi kizazi. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuenzi mchango wake hususan katika kuboresha Huduma za Afya ya Msingi, uboreshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari ikiwemo Elimumsingi Bila Malipo, miundombinu ya barabara za vijijini na mijini chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini ambao ulianzishwa chini ya uongozi wa Rais Hayati Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na kuboresha usafiri na usafirishaji na uboreshaji wa mazingira ya kufanya kazi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na Chama cha Mapinduzi na baadaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu kwa kuendelea kusimamia shughuli za Serikali kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika, Tulia Ackson, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuongoza mhimili wa Bunge.

Tunawaahidi kuwapa ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ninamshukuru pia kwa kuendelea kuwaamini Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na Mheshimiwa David Ernest Siliinde, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kuwa Naibu Mawaziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunamwahidi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Watanzania pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuwa tutafanya kazi kwa bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu kwa Mheshimiwa Rais na kwa nchi yetu katika kumsaidia kusimamia shughuli za utawala na maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan kwa kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kukusanya zaidi mapato ya ndani ili mapato hayo yaweze kutumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha huduma za jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilijadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kupitisha kwa kauli moja. Vilevile, Kamati imekuwa ikitoa ushauri ambaao umesaidia kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu na Taasisi nyingine zilizopo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi wangu, naomba sasa kufanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zake Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuzingatia dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi, imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuratibu uimarishwaji wa utoaji wa huduma za afya ya msingi kwa kujenga na kukarabati miundombinu na kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kuratibu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu katika Shule za Msingi, Sekondari pamoja na kujenga nyumba za walimu ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuratibu usimamizi wa mpango wa utoaji wa Elimu Msingi Bila Malipo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pia imeendelea kuratibu usimamizi wa rasilimaliwatu na kuongeza ajira, kuratibu uimarishwaji wa miundombinu ya barabara za vijijini na mijini, kuratibu uboreshaji wa mazingira ya biashara ya uwekezaji, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Halmashauri, kuratibu usimamizi wa rasilimali fedha, kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi, kuratibu usimamizi wa uwezeshaji wananchi kiuchumi, kuimarisha matumizi ya TEHAMA, kujenga miundombinu ya kiuchumi katika miji na vijijini, pamoja na kuendeleza na kusimamia utumishi wa walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maduhuli, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya shilingi bilioni 860.95. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 814.96 ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Februari, 2021, jumla ya shilingi bilioni 495.25 zimekusanya sawa na asilimia 57.52 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zake, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

ziliidhinishiwa shilingi trillioni 7.01 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, shilingi trillioni 3.87 ni kwa ajili ya Mishahara, shilingi bilioni 851.14 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi trillioni 2.28 ni za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2021, shilingi trillioni 3.90 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 55.66 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zake Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Watumishi ya Walimu imetekeliza Mpango na Bajeti kama nilivyoeleza katika aya ya 32 hadi aya 137 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nitafanya tu mapitio kwa ufupi kwa upande wa huduma za afya za msingi, aya 33 hadi ya 49 ya hotuba yangu, nimeonyesha kazi zilizotekeliza ikiwemo kuboresha mfumo wa utoaji huduma za afya ya msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kusimamia ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Halmashauri 99, vituo vya afya 487 na ujenzi wa zahanati 1,198. Aidha, kwa kutumia mapato ya ndani Halmashauri za Jiji la Arusha, Mwanza na Manispaa ya Kinondoni zimeanza ujenzi wa hospitali na kufanya Hospitali za Halmashauri zinazojengwa kufikia 102.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha tulikuwa tumetenga shilingi bilioni 119.75 kwa ajili ya kuendelezaji wa miundombini ya kutoa huduma za afya ikiwemo kununua dawa, kujenga wodi 201 katika hospitali 67, ununuzi wa vifaa tiba kwa hospitali 67, ujenzi wa hospitali mpya 27 na ukamilishaji wa maboma ya zahanati 555, ikiwa ni wastani wa maboma matatu kwa kila Halmashauri. Hadi Februari, 2021, jumla ya shilingi bilioni 58.99 sawa na asilimia 49.26 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, pia tumeendelea kutoa Huduma za Afya ngazi ya Msingi. Katika

mwaka huu 2021 tumehudumia takribani wagonjwa milioni 23.2.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kwa ufupi kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari ambapo nimeeleza katika hotuba yangu aya 50 – 78, tumeendelea na majukumu ya kutoa elimu msingi na sekondari kwenye Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikiwemo kuwahudumia wanafunzi milioni 14.9 ambapo wanafunzi 1,198,564 ni wa Shule za Awali, wanafunzi milioni 11 Shule za Msingi; Darasa la Kwanza hadi Darasa la Saba na wanafunzi 2,757,216 ni wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pia tumeendelea kuratibu na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari ikiwemo kujenga vyumba vya madarasa 5,224, matundu ya vyoo 15,616, mabweni 223, mabwalo 40, majengo ya utawala 21 na vyumba vya maabara ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kuboresha kiwango cha elimu ngazi ya awali, msingi na sekondari kwa kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimu Msingi bila malipo pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hadi Februari, 2021 uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali ulifikia wanafunzi 1,057,919 sawa na asilimia 83 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,272,515.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanafunzi wa Darasa la Kwanza hadi Februari, 2021 jumla ya wanafunzi 1,400,145 sawa na asilimia 92 ya lengo waliandikishwa tukilinganisha na mwaka uliopita ambapo tuliandikisha wanafunzi 1,516,598. Kuendelea kupungua kwa uandikishwaji unatokana na mafanikio ya mpango wa Elimu Msingi Bila Malipo ulioasisiwa na Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli uliowezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kwa sababu ya kuondolewa kwa ada na michango mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za ukamilishaji wa maboma, tulitenga bilioni 26.9 na ambapo

madarasa 2,088 yamejenga katika Halmashauri 184 na kiasi cha shilingi bilioni 18.22 kimetolewa, pamoja na ukamilishaji wa maboma 1,360 ya vyumba nya madarasa ya Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi wa vyumba nya madarasa imekwenda sambamba na utengenezaji wa madawati takribani 61,200. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Shule za Sekondari nchini imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Sekondari. Katika mwaka wa fedha 2021 jumla ya wanafunzi 833,872 walichaguliwa kuijunga na Kidato cha Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi 759,737 waliochaguliwa kuijunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kujenga madarasa mapya 396, matundu ya vyoo 1,035, mabweni 223, mabwalo 40, maktaba 8, maabara za sayansi 18, majengo ya utawala 21 na nyumba za walimu 18. Vile vile tumekarabati shule kongwe 13 za sekondari kwa gharama za shilingi bilioni 19.88.

Mheshimiwa Spika, katika kuimrisha Elimu ya Sayansi kwa Vitendo, Serikali imefuta mitihani ya sayansi mbadala wa vitendo (*alternative to practices*) iliyodumu tangu miaka 1990. Wanafunzi wote wa Kidato cha Nne katika mwaka 2020 wamefanya mitihani ya sayansi kwa vitendo na hadi kufikia Februari, 2021 jumla ya shilingi bilioni 26.5 zimetolewa sawa na asilimia 62. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia tumeimarisha Shule za Sekondari za Ufundu kwa kuajiri na kuwapangia vituo walimu wa masomo ya ufundi wa fani mbalimbali katika shule zote tisa na tumeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Elimu Msingi Bila Malipo ambapo hadi kufikia Februari, 2021 Serikali imetoea jumla ya shilingi bilioni 166.44 kwa ajili ya kutekeleza mpango huo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 80 zilitumika katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande kuwawezesha wananchi kiuchumi katika mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya shilingi bilioni 64.5 zilitengwa na hadi kufikia Februari, 2020, jumla ya shilingi bilioni 26.81 sawa na asilimia 41 zilikuwa zimetolewa kwa vikundi nya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pia tumeendelea kutambua umuhimu wa kutumia vitambulisho nya wajasiliamali wadogo ambapo kuanzia tarehe 1 Machi, 2020 hadi Februari, 2021 wafanyabiashara 716,776 wamepatiwa vitambulisho ambavyo vimewezeshwa kukusanya kwa jumla ya shilingi bilioni 14.33 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kutekeleza miradi ya kimkakati ambapo jumla ya shilingi bilioni 44.17 zimetolewa sawa na asilimia 88 ya lengo. Kwa upande wa huduma za kiuchumi na uzalishaji, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuweka kipaumbele katika kutenga maeneo ya uwekezaji kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hadi Februari, 2021, jumla ya hekta milioni 2.3 zimetengwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ikiwemo kwa ajili ya viwanda vikubwa vidogo na nya kati. Hivyo nitumie Bunge lako Tukufu kuwahimiza wadau mbalimbali kutumia fursa hii ya uwekezaji katika mikoa na halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu aya ya 95 hadi 107 nimeeleza kazi zilizotekelawa kwa upande wa Utawala Bora na usimamizi wa rasilimali ikiwemo kuanzisha Kituo cha Huduma ya Mawasiliano kwa Mteja, ambapo katika mwaka huu wa fedha wananchi 7,443 wamehudumiwa bila kuja Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, pia katika hotuba yangu nimeonyesha taarifa ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo imeonyesha halmashauri 53 sawa na asilimia 29 zimepata hati zenye mashaka na halmashauri nane sawa na asilimia nne zimepata hati zisizoridhisha.

Mheshimiwa Spika, tumefanya uchambuzi wa taarifa hizi na tutachukua hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote watakaothibitika kuwa chanzo cha kutofanya vizuri katika halmashauri zao. Vile vile, tumbaini kuwa ziko halmashauri zimepata hati zinazoridhisha, lakini pia kuna mambo ambayo yamebainishwa na CAG kuhusu matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwa hiyo, hata hizo zimepata hati safi tutafanya uchambuzi na kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu kwa wote waliohusika na ubadhirifu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika mapitio yangu naomba nijikite katika masuala ya kuimarisha mifumo ya kietroniki na miundombinu ya *TEHAMA* ambapo tumejaribu kutekeleza ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji. Kwa upande wa Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini hadi Februari, 2021, *TARURA* imekamilisha ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 97.7 na matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita elfu 7753.13, ikiwa ni matangenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam umetekelezwa ikiwemo kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 28.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia utumishi wa Walimu; hadi Februari, 2020, Tume imepokea na kusajili rufaa 148 za Walimu ambapo kati yake rufaa 111 zimetolewa uamuza.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza taarifa ya kina ya utekelezaji ya kazi zilizotekelizwa katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 zipo katika aya ya 32 hadi 137 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijikite katika kueleza mpango na makadirio ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Fungu 56,

Mafungu 26 ya Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 umeandaliwa kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatoo wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Hotuba ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, wakati anazindua Bunge la Kumi na Mbili, Mwongozo wa Kuandaa Mpango pamoja na maelekezo ya Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa, Sera za Kisekta, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza Mipango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele sita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha kwanza ni Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi ikijumuisha ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba pamoja na ujenzi wa miundombinu ya zahanati, vituo vya afya na Hospitali za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili ni utoaji wa haduma za elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kununua vitabu, vifaa vya maabara pamoja na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, maabara, nyumba za Walimu, shule za sekondari za sayansi za wasichana, ujenzi wa shule za kutwa za kata pamoja na utengenezaji wa madawati kwa shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tatu ni ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za mjini na vijiji.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha nne ni uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tano ni kuimarisha utawala bora na usimamizi wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele chetu cha sita ni kujenga mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji wa viwanda mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu shughuli zitakazotekelawa nimezbainisha katika aya ya 140 hadi 157 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, malengo mahususi yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, nimebainisha katika aya 158 ambayo ni kwanza kuimarisha na kuhakikisha vituo vya kutolea huduma vilivyoamilika vinaanza kutoa huduma za afya na elimu ikiwa ni pamoa na ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba na utengenezaji wa madawati kwa shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, pili kujenga vituo vya afya vipyta 121 kwa gharama ya Shilingi bilioni 60.50 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, tatu, kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya 52 kwa gharama ya Shilingi bilioni 15.60 vilivyoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, nne, kuendeleza ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 68 za awamu ya kwanza zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2018/2019 ikiwemo Hospitali ya Uhuru iliyopo Chamwino, Dodoma ambapo jumla ya shilingi bilioni 55.70 zimetengwa kutoka fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, tano, kuendeleza ujenzi wa hospitali 27 za awamu ya pili zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Hospitali nne za awamu ya kwanza ambapo jumla ya shilingi bilioni 11.40 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, sita, kuanza ujenzi wa Hospitali mpya 28 katika Halmashauri zote 28 ambazo hazina Hospitali za Serikali ambapo jumla ya shilingi bilioni 14.0 zimetengwa, fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, saba, ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya hospitali 31 za awamu ya pili ambapo jumla ya shilingi bilioni 12.30 zimetengwa, fedha za ndani;

Mheshimiwa Spika, nane, ukamilishaji wa maboma ya zahanati 763 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika Majimbo yote ya Uchaguzi yatakayogharimu shilingi bilioni 38.15 ambapo kila zahanati imetengewa shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Spika, tisa, kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule 10 kati ya shule 26 za sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya sayansi. Shule hizi zitakapokamilika zitakuwa na kidato cha kwanza hadi cha sita na wanafunzi kati ya 1,000 hadi 1,200 ambapo kiasi cha bilioni 40 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, kumi, kujenga shule mpya 300 za sekondari za kutwa kwenye kata ambazo hazina shule za sekondari kwa gharama ya shilingi milioni 650 hadi 700 kwa kila shule.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, ukamilishaji wa maboma ya vyumba 1,840 vya madarasa ya shule za sekondari kwa gharama ya shilingi bilioni 23.00;.

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili , kujenga nyumba 300 (*two in one*) za walimu kwa gharama ya shilingi milioni 50 kwa kila nyumba;

Mheshimiwa Spika, kumi na tatu, kuendelea kugharamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo ambapo jumla ya shilingi bilioni 312.05 zimetengwa zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kumi na nne, ununuzi wa vitabu vya shule za msingi na sekondari kwa gharama ya Shilingi bilioni 50.00, fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kumi na tano, ukamilishaji wa maboma ya vyumba 3,268 kwa madarasa ya shule za msingi kwa gharama ya Shilingi bilioni 40.85.

Mheshimiwa Spika, kumi na sita, kuhakikisha upatikanaji wa madawati ya shule za msingi 710,000 ili kukabiliana na upungufu wa madawati katika shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, kumi na saba, ukamilishaji wa vyumba 1,043 vya maabara za sayansi katika shule za sekondari kwa gharama ya Shilingi bilioni 27.07, fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kumi na nane, kuendelea na ujenzi wa majengo ya Utawala ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 57.92 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, kumi na tisa, ujenzi wa majengo ya Utawala kwa Halmashauri 96 kwa gharama Shilingi bilioni 83.75 na ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara katika Halmashauri 51 ikijumuisha Halmashauri 30 zilizohamia kwenye maeneo yao ya utawala utakaogharimu Shilingi bilioni 7.6.

Mheshimiwa Spika, ishirini, utekelezaji wa Miradi mkakati katika Halmashauri 26 ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 68.70 kimetengwa.

Mheshimiwa Spika, ishirini na moja, kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambapo ambapo Shilingi bilioni 67.66 zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, ishirini na mbili, ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kwa gharama ya Shilingi bilioni

627.044 kupitia *TARURA* ambapo Shilingi bilioni 272.50 zinatokana na Mfuko wa Barabara, Shilingi bilioni 127.50 zinatokana na Mfuko Mkuu wa Serikali na Shilingi bilioni 12.75 zinatokana na mapato ya ndani ya *TARURA* ambapo jumla ya kilomita 136.82 barabara za lami, kilomita 500 za barabara za changarawe na Kalvati na madaraja 90 yatatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, Kiasi cha Shilingi bilioni 214. ni fedha za ndani kwa ajili ya kuendeleza miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam na kiasi cha Shillingi bilioni 22.263 ni fedha za Mradi wa Uboreshaji wa Barabara Maeneo ya Uzalishaji wa Kilimo pamoja na Shilingi bilioni 36.00 ni Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini.

Mheshimiwa Spika, Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 91 kwa kiwango cha lami maeneo ya Vijijini, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua kilomita 17, ujenzi wa masoko manne (4), kulipa fidia na upembuzi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, naomba kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge.

Vilevile, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Humphrey Hezron Polepole, Mwenyekiti wa Kamati; na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Maoni na ushauri wa Kamati vimesaidia sana kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, napenda na kutambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli mbalimbali

za Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hawa nimewatambua katika aya ya 160 ya hotuba yangu naomba nisiwataje.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwashukuru wananchi kwa mchango wao mkubwa katika utekelezaji wa miradi na *programmes* mbalimbali kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwenye hili napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakijitoa kwenye fedha zao binafsi kwa ajili ya kuboresha huduma za afya, elimu na miundombinu katika halmashauri zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hapa mchango wa Bunge lako unaonekana leo tuna wasichana wetu ambao wanasoma masomo ya sayansi kuititia Bunge *Secondari School. Legacy* yako hii haiwezi kufutika na itaendelea kuthaminiwa vizazi hadi vizazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kipekee, nawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, Mbunge wa Wanging'ombe na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Tunduma, kwa msaada mkubwa wanaotoa kwangu. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Profesa Riziki Shemdoe kwa mchango wake katika kufanikisha maandalizi ya Mpango na Bajeti na bila kusahau mchango wa aliyekuwa Katibu Mkuu *Engineer Nyamhanga* na nawashukuru Naibu Makatibu Wakuu Bw. Gerald G. Mweli na Dkt. Grace Magembe katika usimamizi wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, namshukuru Bi. Paulina Mbena, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Mkurugenzi wa Bahi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais. Kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano wanaotoa katika katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa kipekee nimshukuru Waziri aliyetoka, Mheshimiwa Suleiman Jafo kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya katika kusimamia Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nawashukuru wananchi wa Jimbo la Tanga Mjini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao mwezi Oktoba, 2020 na hivyo kuniwezesha kuweka historia ya kuwa Mbunge wa kwanza Mwanamke wa Jimbo hili toka lilipoanzishwa mwaka 1965. Nawaahidi Wanatanga Mjini kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuifanya Tanga yetu ipate maendeleo zaidi ya kiuchumi na kijamii. Kipekee, naishukuru familia yangu kwa kuniombea na kwa uvumilivu wao muda wote ninapokuwa mbali nao katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nipunguze *speed* ili niweze kuomba fedha. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 184 inaomba idhini ya Bunge lako Tukufu kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani jumla ya shilingi 916,445,409,198. Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, ada za wanafunzi, tozo na ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika jedwali la kwanza la hotuba yangu nimeonyesha mchanganuo wa makusanyo ya mapato haya.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya Shilingi trillioni saba, bilioni mia sita themanini na tatu, milioni mia tatu ishirini na tisa, mia sita arobaini na nne elfu na mia nane (Sh.7,683,329,644,800.00) kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI - Fungu 56; Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na.2 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojojumuisha Halmashauri 184.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zinazoombwa, Shilingi trillioni nne, bilioni mia saba ishirinini na nane, milioni nane na laki mbili na saba elfu (Sh.4,728,008,207,000.00) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojojumuisha Mishahara Shilingi trillioni tatu, bilioni mia tisa sabini na mbili, mia moja arobaini na tisa milioni, mia sita na tatu elfu (Sh.3,972,149,603,000.00) na Shilingi bilioni mia saba hamsini na tano milioni, mia nane hamsini nane mia sita na nne elfu (Sh.755,858,604,000.00) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya Shilingi trillioni mbili, milioni mia tisa hamsini na tano, mia tatu ishirini na moja elfu mia nne thelathini na saba na mia nane (Sh.2,955,321,437,800.00) tunaziomba kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo Shilingi trillioni moja, bilioni mia sita sabini na sita, milioni mia nne hamsini na tisa, mia saba sabini na tisa elfu na mia nane (Sh.1,676,459,779,800.00) ni fedha za ndani na Shilingi trillioni moja, bilioni mia mbili sabini na nane, milioni mia nane sitini na moja, mia sita hamsini na nane elfu (Sh.1,278,861,658,000.00) ni fedha za nje .

Mheshimiwa Spika, Jedwali Na.2 nimeweka mchanganuo wa makisio katika Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Tume ya Utumishi wa Walimu; Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, naomba nisilisome.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI - Fungu Na. 56; Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na.2; Mikoa na Halmashauri - Mafungu 26 ambayo nimeyaambatisha katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipa fursa hii, naomba kusema kwamba hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

Mheshimiwa Spika,naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

A. UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, naomba Bunge lako tukufu lijadili na kuitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2 na Mafungu 26 ya Mikoa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/22.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha tena kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

3. *Mheshimiwa Spika*, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nampongeza **Mheshimiwa Samia Suluhi Hassan** kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia kauli mbiu yake ya ‘‘Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi lendelee’’, Watanzania wana Imani na matumaini makubwa nae na kuwa katika Awamu ya Sita nchi yetu itapiga hatua kubwa zaidi za kimaendeleo hususan

katika nyanja za kiuchumi na kijamii na hivyo kuwanufaisha wananchi walio wengi na hasa wanyonge.

4. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pole zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa msiba mkubwa kwa Taifa letu kwa kuondokewa na mpendwa wetu na kipenzi cha Watanzania Hayati **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeaga dunia tarehe 17 Machi, 2021. Kuondokewa na Jemedari wetu mahiri Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ni pigo kubwa si kwa Tanzania tu bali ni pigo kwa Afrika Mashariki, Bara la Afrika na Dunia nzima kwa ujumla.

5. Mheshimiwa Spika, mchango mkubwa wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa Taifa hili hautasahaulika kizazi hadi kizazi. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kuenzi mchango wake hususan katika kuboresha Huduma za Afya ya Msingi, uboreshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari ikiwemo Elimumsingi Bila Malipo, miundombinu ya barabara za Vijijiini na Mijini chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Vijijiini na Mijini (TARURA), usafiri na usafirishaji na uboreshaji wa mazingira ya kufanya kazi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

6. Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba kutoa pole zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Rais Mstaifu wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Hayati Benjamin William Mkapa; Maalim Seif Sharif Hamad*, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na *Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi*, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

7. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pole nyingi kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu *Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla*, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoaa wa Manyara na *Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye*, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambarwe. Taifa litakosa

mchango wao katika kuisimamia Serikali kufanikisha maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu na marafiki wa watanzania wenzangu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

8. *Mheshimiwa Spika*, nampongeza Mheshimiwa **Dkt. Philip Isidor Mpango** kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na Chama Cha Mapinduzi na baadae kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia shughuli za Serikali kwa mafanikio makubwa.

9. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika, **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansansu**, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuongoza Mhimili wa Bunge. Tunawaahidi kuwapa ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa majukumu yenu.

10. *Mheshimiwa Spika*, kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunteua kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Ninamshukuru pia kwa kuendelea kuwaamini **Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange**, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na **Mheshimiwa David Ernest Silinde**, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kuwa Naibu Mawaziri Ofisi ya Rais TAMISEMI. Tunamuahidi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na watanzania kuwa tutafanya kazi kwa bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu kwake na kwa nchi yetu katika kumsaidia kusimamia shughuli za utawala na maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan kwa kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kukusanya zaidi mapato ya ndani ili mapato hayo yaweze kutumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha huduma za jamii katika maeneo yao ikiwemo huduma za Afya ya Msingi, Elimu ya Msingi na Sekondari, Miundombinu

ya barabara na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Aidha, tutaongeza jitihada za kusimamia matumizi ya fedha za umma katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

11. *Mheshimiwa Spika*, kipekee, nampongeza *Mheshimiwa Humphrey Hezron Polepole (Mb)*, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, *Mheshimiwa Abdallah Jaffari Chaurembo (Mb)*, Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, Kamati ilijadili kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2021/22 na kupitisha kwa kauli moja. Vilevile, Kamati imekuwa ikitoa ushauri ambao umesaidia kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu na Taasisi nyingine zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika kuhudumia wananchi.

12. *Mheshimiwa Spika*, kwa namna ya pekee naomba niipongeze Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na *Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan*, kwa kusimamia kikamilifu, kwa dhati na kwa umakini mkubwa utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambao umeiwezesha nchi kufikia Uchumi wa Kati na kutangazwa na Benki ya Dunia tarehe 01 Julai, 2020 kabla ya muda uliotarajiwा mwaka 2025.

B. MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS – TAMISEMI (FUNGU 56), OFISI ZA WAKUU WA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAFUNGU 26) NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (FUNGU NA. 2)

13. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D), uratibu wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na maendeleo ya Miji na Vijiji;

- ii) Kuwezesha Tawala za Mikoa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;
- iii) Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;
- iv) Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma Mijini na Vijiji kama vile usafiri na usafirishaji, na usafi wa mazingira;
- v) Kuiwezesha Tume ya Utumishi wa Walimu kutekeleza majukumu yake; vi) Kusimamia utoaji wa huduma za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari; vii) Kusimamia utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- viii) Kujenga uwezo wa watumishi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi; na
- ix) Kusimamia utendaji wa Mashirika, Taasisi, Programu na Miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

14. *Mheshimiwa Spika*, majukumu yanayotekelawa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa ni kama ifuatavyo:

- i) Kuhakikisha kunakuwepo amani, usalama na utulivu katika Mikoa na Wilaya;
- ii) Kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iii) Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi;
- iv) Kufuatilia utekelezaji wa Mipango, Programu na Miradi mbalimbali zinazotekelawa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo yao;
- v) Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vi) Kusimamia na kuratibu utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

vii) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

15. *Mheshimiwa Spika*, majukumu yanayoteklezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

i) Kuhakikisha na kuwezesha utekelezaji wa Sheria na Ulinzi wa wananchi katika maeneo yao;

ii) Kukuza ustawi wa jamii na uchumi wa wananchi wote katika maeneo yao;

iii) Kukuza demokrasia na kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi yanayohusu ustawi na maendeleo yao;

iv) Kuhifadhi na kuendeleza mazingira ili kuweza kuwa na maendeleo endelevu ikiwa ni pamoja na kuwa na Mpango Mkakati wa Matumizi ya Ardhi;

v) Kutekeleza upelekaji wa madaraka ya kisiasa, fedha na utawala wa majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yanayohusu kazi, uwezo, madaraka na huduma kwenye ngazi zote za Halmashauri;

vi) Kubuni na kuimarisha vyanzo vya mapato na matumizi ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato;

vii) Kutoa huduma za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Watu Wazima;

viii) Kutoa Huduma za Afya ya Msingi katika Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati na ngazi ya jamii;

ix) Kuendeleza huduma za kilimo, uvuvi, ufungaji na ushirika;

- x) Kuendeleza shughuli za utamaduni, michezo na burudani;
- xi) Kusaidia na kuwezesha uratibu wa taasisi zisizo za kiserikali na taasisi za kijamii;
- xii) Kuendeleza biashara, kuchochlea ukuaji wa uchumi, maendeleo ya viwanda na kuondoa umaskini;
- xiii) Kukuza ajira, ustawi wa jamii na vijana; na
- xiv) Kusimamia matumizi ya ardhi na maendeleo ya makazi.

16. *Mheshimiwa Spika*, majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu yameainishwa kwenye Kifungu cha 5 cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015 kama ifuatavyo:

- i) Kuendeleza na kusimamia utumishi wa walimu;
- ii) Kumshauri Waziri katika kusimamia na kuendeleza utumishi wa walimu;
- iii) Kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu;
- iv) Kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa walimu katika Halmashauri na kwenye shule;
- v) Kushughulikia masuala ya rufaa zinazotokana na maamuzi ya Mamlaka ya Nidhamu;
- vi) Kutunza daftari la kumbukumbu za walimu wote waliopo kwenye Utumishi wa Umma;
- vii) Kusimamia programu za mafunzo ya walimu kazini;
- viii) Kufanya utafiti na tathmini kuhusu masuala yanayohusu utumishi wa walimu na kumshauri Waziri;

- ix) Kutathmini hali ya walimu na kushauri Wizara yenye dhamana ya masuala ya walimu juu ya mafunzo, idadi na uhitaji wa walimu nchini;
- x) Kuandaa Kanuni na kusimamia maadili ya utendaji kazi wa walimu; na
- xi) Kuhakikisha kuwa waajiri na Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya wanatekeleza kazi zao kwa mujibu wa Sheria.

C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA OFISI YA RAIS – TAMISEMI (FUNGU 56), MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAFUNGU 26) NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (FUNGU NA. 2) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

17. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuzingatia dhana ya uguatuaji wa madaraka kwa wananchi imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na; kuratibu uimarishaji wa utoaji Huduma za Afya ya Msingi kwa kujenga na kukarabati miundombinu na kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; kuratibu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu katika Shule za Msingi, Sekondari na nyumba za walimu kwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuratibu usimamizi wa mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo.

18. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI pia imeendelea kuratibu usimamizi wa rasilimaliwatu na kuongeza ajira; kuratibu uimarishaji wa miundombinu ya barabara za Vijijini na Mijini; kuratibu uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Halmashauri; kuratibu usimamizi wa rasilimali fedha; kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa watumishi; kuratibu usimamizi wa uwezeshaji wananchi kiuchumi; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kujenga miundombinu ya kiuchumi na kijamii inayowezesha kufungua fursa za kiuchumi Mijini na Vijijini, kuendeleza na kusimamia utumishi wa walimu; pamoja na kuziwezesha Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) na Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) kwa Mwaka wa Fedha 2020/21

19. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani jumla ya **Shilingi bilioni 860.95**. Kati ya fedha h**Shilingi bilioni 45.77** ni Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, **Shilingi milioni 209.69** ni Maduhuli ya Mikoa na **Shilingi bilioni 814.96** ni Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 495.25** zimekusanyaawa sawa na **asilimia 57.52** ya bajeti iliyoidhinishwa.

20. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa **Shilingi trilioni 7.01** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 3.87** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 851.14** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi trilioni 2.28** ni za Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 1.29** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 992.97** fedha za nje. Hadi Februari 2021, **Shilingi trilioni 3.90** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 55.66** ya bajeti iliyoidhinishwa.

Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56)

21. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Taasisi zake (Fungu 56) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 703.44** kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 578.04** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 276.53** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 301.51** ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi bilioni 125.40** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 53.45** ni fedha za Mishahara na **Shilingi bilioni 71.95** ni fedha za Matumizi Mengineyo ikijumuisha **Shilingi bilioni 61.28** za Kiinua Mgongo cha Madiwani.

22. *Mheshimiwa Spika*, hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 384.54** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 54.66** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 103.79** ni fedha za Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 32.21** ni fedha za Mishahara na **Shilingi bilioni 71.58** ni fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi bilioni 280.75** ni fedha za Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 171.45** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 109.30** ni fedha za nje. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake imekusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani kiasi cha **Shilingi bilioni 22.77** sawa na **asilimia 50.00** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 45.77**, makusanyo hayo yametokana na mauzo ya vifaa chakavu, mauzo ya huduma, ada ya maegesho ya magari, ada za wanafunzi na tozo mbalimbali.

Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu - TSC (Fungu Na. 2)

23. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 14.77**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 14.27** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 8.17** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 6.10** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Tume iliidhinishiwa **Shilingi milioni 500.00** ambazo ni fedha za ndani.

24. *Mheshimiwa Spika*, hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 7.64** zimepokelewa sawa na **asilimia 51.72** ya bajeti iliyoishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 7.64** ni fedha za Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi bilioni 4.13** ni fedha za Mishahara na **Shilingi bilioni 3.51** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Bajeti za Mikoa Mafungu 26

25. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mikoa 26 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 221.88** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 135.88** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo

kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 76.89** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 58.99** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi bilioni 85.99** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 57.72** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 28.27** ni fedha za nje. Hadi Februari 2021, **Shilingi bilioni 113.93** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 51.35** ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi bilioni 87.48** za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 26.45** ni fedha za Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 24.17** ni fedha za ndani.

26. Mheshimiwa Spika, hadi Februari 2021, Mikoa imekusanya Maduhuli ya **Shilingi milioni 74.45** sawa na **asilimia 36** ya lengo la kukusanya **Shilingi milioni 209.69**. Makusanyo ya Maduhuli yametokana na mauzo ya vifaa chakavu. Makusanyo ya Maduhuli ya Mikoa yamepungua kwa sababu ya kuanzishwa kwa utaratibu wa kuomba zabuni kupitia mfumo wa kielektroniki wa TANEPS unaosimamiwa na Mamlaka ya Uhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), hivyo mapato ya maombi ya zabuni yanawasilishwa PPRA.

Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa 26

Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri

27. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Halmashauri zilikasimiwa kukusanya **Shilingi bilioni 814.96** kutoka vyanzo vya Mapato ya Ndani. Hadi Februari, 2021 Halmashauri zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 473.94** sawa na **asilimia 58.16** ya bajeti iliyoidhinishwa. Makusanyo haya ni ongezeko la **Shilingi bilioni 5.95** ikililinganishwa na makusanyo ya **Shilingi bilioni 466.45** yaliyokusanya hadi Februari 2020, kwa mwaka wa fedha 2019/20.

28. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa iliongezeka kutoka **Shilingi bilioni 765.48** katika mwaka wa fedha 2019/20 hadi **Shilingi bilioni 814.96** katika mwaka wa fedha 2020/21 sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 49.48** (*Rejea Kiambatisho Na. 1*).

Ruzuku ya Serikali Kuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kwenye Mikoa 26

29. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa kutumia **Shilingi trilioni 5.26**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 3.97** ni Matumizi ya Kawaida zikijumuisha Mishahara **Shilingi trilioni 3.74** na **Shilingi bilioni 232.21** ni Matumizi Mengineyo. Miradi ya Maendeleo illidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.29** ambazo kati yake **Shilingi bilioni 629.10** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 663.18** ni fedha za nje. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi trilioni 2.92** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 55.51** ya bajeti, ambapo **Shilingi trilioni 2.50** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 422.78** ni fedha za Miradi ya Maendeleo kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 370.12** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 52.66** ni fedha za nje.

Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

30. *Mheshimiwa Spika*, hadi Februari 2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu zilipokea jumla ya **Shilingi trilioni 3.90** kati ya bajeti ya **Shilingi trilioni 7.01** sawa na **asilimia 55.63**. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi trilioni 3.03** ambapo Mishahara ni **Shilingi trilioni 2.42** na **Shilingi bilioni 615.91** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, **Shilingi bilioni 870.77** ni fedha za Maendeleo ambapo **Shilingi bilioni 706.54** ni fedha za ndani na kiasi cha **Shilingi bilioni 164.23** ni fedha za nje (*Rejea Kiambatisho Na. 2*).

Utekelezaji wa Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi Februari, 2021 kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) na Mafungu 26 ya Mikoa

31. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21 Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tume ya Utumishi wa Walimu imetekeliza mpango kama ifuatavyo:

HUDUMA ZA AFYA YA MSINGI

32. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika uboreshaji wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uboreshaji huu utawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii na kuchochea maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa afua hizi katika Halmashauri zote nchini.

Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya

33. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Halmashauri **99**, Vituo vya Afya **487** na ujenzi wa Zahanati **1,198**. Aidha, kwa kutumia Mapato ya Ndani, Halmashauri za Jiji la Arusha, Mwanza na Manispaa ya Kinondoni zimeanza ujenzi wa Hospitali na kufanya Hospitali za Halmashauri zinazojengwa kuongeza na kufikia **102**.

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 119.75** kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba, ambapo **Shilingi bilioni 32.50** ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Wodi **201** katika Hospitali **67**, ununuzi wa vifaa tiba kwa Hospitali **67 Shilingi bilioni 32.50**, ujenzi wa Hospitali Mpya **27 Shilingi bilioni 27.00** na **Shilingi bilioni 27.75** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya Zahanati **555**, ikiwa ni wastani wa maboma **3** kwa kila Halmashauri. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 58.99** sawa na **asilimia 49.26** zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo (*Rejea Kiambatisho Na. 3*).

Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi

35. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa Huduma za Afya ngazi ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia Februari 2021, vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi **5,838** vimetoa huduma kwa wagonjwa

wapatao **23,209,724** ambapo wanawake ni **13,943,539** na wanaume ni **9,266,185**. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa, wagonjwa **15,619,410** sawa na **asilimia 67** walipatiwa huduma za Wagonjwa wa Nje (OPD) na wagonjwa **7,590,314** sawa na **asilimia 33** walipatiwa huduma za Wagonjwa wa Ndani (IPD).

Usafi wa Mazingira

36. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya RaisTAMISEMI imeendelea kusimamia shughuli za usafi wa mazingira katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenye ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambapo vituo vya afya ya msingi **860** vinaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji safi na vyoo bora katika Halmashauri **86** nchini. Hadi Februari 2021, zimetolewa **Shillingi bilioni 18.9** kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo.

Udhhibit wa Magonjwa ya Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imesimamia ugawaji wa vyandarua **12,797,038** vyenye viuatilifu vya muda mrefu kupitia programu za ugawaji wa vyandarua ngazi ya jamii, shule na vituo vya kutolea huduma za afya. Vyandarua hivi viligawiwa kwenye Mikoa **10** yenye maambukizi ya wastani ya Rukwa, Songwe, Njombe, Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Manyara, Kilimanjaro na Tanga. Aidha, vyandarua vilitolewa kwenye Mikoa **14** yenye maambukizi makubwa ya Lindi, Ruvuma, Mtwara, Morogoro, Pwani, Katavi, Tabora, Kigoma, Kagera, Geita, Mwanza, Simiyu, Mara na Shinyanga. Vilevile, Mikoa yote imepata vyandarua kupitia kliniki za mama, baba na mtoto.

38. Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na UKIMWI umeboreshwa kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyoko katika Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu UKIMWI na Virusi vya

UKIMWI. Elimu inayotolewa katika vituo hivi imetua mchango mkubwa katika kupunguza unyanyapaa kwenye jamii na kuongeza idadi ya wagonjwa wanao jitokeza kupima afya zao ikiwa ni pamoja na kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Huduma Za Lishe

39. *Mheshimiwa Spika*, katika kukabiliana na changamoto ya lishe duni katika jamii, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha Kamati za Lishe za Mikoa **26** na Halmashauri **184** kote nchini zenye jukumu la kujadili na kutatua changamoto za lishe katika maeneo yao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo. Katika kufanikisha jukumu hili, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusaini mikataba ya utendaji na usimamizi wa masuala ya lishe katika ngazi zote na kufanyiwa tathmini. Mikataba hii imeongeza uwajibikaji katika usimamizi wa afua za lishe.

40. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha tathmini ya shughuli za lishe, Ofisi ya Rais TAMISEMI imefanya maboresho ya Mfumo Jumuishi wa Tathmini na Ufutililaji (*Integrated Monitoring and Evaluation System – IMES*) kwa ajili ya kukusanya taarifa za kiuchumi na kijamii zikiwemo taarifa za lishe katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazojumuisha taarifa ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya. Taarifa hizi zitatumika kuboresha mikakati ya nchi dhidi ya utapiamlo na itasaidia kuelekeza rasilimali fedha kulingana na ukubwa wa tatizo kwa mujibu wa takwimu.

Huduma za Watu Wenye Ulemavu

41. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea kuratibu huduma za Watu Wenye Ulemavu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo hadi Februari 2021, jumla ya Watu Wenye Ulemavu wapatao **124,900** katи yao wanawake **59,059** na wanaume **65,841** wametambuliwa sawa na **asilimia 83** ya lengo. Vilevile, kaya **196,372** zimetambuliwa kupertia mfuko wa TASAF na zinasubiri kuhakikiwa ili ziweze kupatiwa ruzuku.

Aidha, Kamati za Watu Wenye Ulemavu zimeundwa na kuratibiwa kwenye Mikoa **26** sawa na **asilimia 100.00** na Halmashauri **184** sawa na **asilimia 99.46**. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imetumia kiasi cha **Shilingi bilioni 1.30** kwa ajili ya kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu wapatao **15,596** kupatiwa huduma mbalimbali zikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii, vifaa saidizi kama vile viti mwendo, baiskeli na pikipiki za magurudumu matatu, fimbo nyeupe na miwani.

Huduma ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto

42. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mtoto na Mwanamke zimeundwa katika Mikoa **26**, Halmashauri **184**, Kata **2,840** kati ya **3,956** na Vijiji **7,970** kati ya Vijiji **12,319**. Hatua za kuunda Kamati kwenye Kata na Vijiji vilivyobaki zinaendelea. Aidha, kampeni za kutokomeza mimba na ndoa za utotoni zinaendelea kutekelezwa katika Halmashauri zote. Vilevile, Wataalam wa Ustawi wa Jamii **684** kati ya **740** wamepatiwa mafunzo kuhusu namna ya kutoa huduma ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika maeneo yao.

43. Mheshimiwa Spika, mashauri ya watoto wanaokinzana na Sheria na waliofanyiwa ukatili yanaeendelea kupokelewa na kushughulikiwa ambapo hadi Februari 2021, jumla ya mashauri **27,470** ya watoto waliofanyiwa ukatili na watoto **11,837** wanaokinzana na sheria yameshughulikiwa. Aidha, jumla ya watoto **39,307** waliofanyiwa vitendo vya ukatili na watoto wanaokinzana na sheria walipatiwa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii na kuunganishwa na familia zao.

44. Mheshimiwa Spika, huduma za watoto walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani zimeendelea kuwa kipaumbele kwa kuwatambua na kuwaunganisha na huduma mbalimbali

zikiwemo huduma za Afya, Elimu, Bima ya Afya na VVU/UKIMWI. Hadi Februari 2021, jumla ya watoto **472,790** wanaoishi katika mazingira hatarishi wametambuliwa ambaao ni sawa na **asilimia 90.00** ya lengo.

Huduma za Wazee

45. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuwatambua na kuwapatia wazee wasiojiweza vitambulisho vya matibabu bila malipo kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2007. Hadi Februari 2021, jumla ya Wazee **366,252** wametambuliwa katika Mikoa yote wakiwemo wanawake **195,771** na wanaume **170,481** ambapo kati ya hao waliopatiwa vitambulisho vya wazee baada ya kukidhi vigezo vya Sera hiyo ya Afya ni **214,141**.

46. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha utendaji wa Mabaraza ya Ushauri ya Wazee ambapo hadi Februari 2021 Mabaraza **3,456** ya Ushauri ya Wazee yameundwa kwa ajili ya kushughulikia masuala ya wazee katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jumla ya wazee **128,820** wamepatiwa huduma za matibabu ya afya bila malipo na jumla ya **Shilingi bilioni 3.2** zimetumika kugharamia matibabu ya wazee kwa ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo.

Matibabu ya Afya kwa Msamaha

47. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais -TAMISEM imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa makundi maalum ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 29.3** zimetumika kugharamia matibabu bila malipo kwa wagonjwa **11,423,444** kutoka makundi maalum ambayo yanayohusisha wazee wenye umri wa miaka zaidi ya 60 na wasio na uwezo, wafungwa, watoto chini ya miaka mitano, wajawazito, wasiojiweza kiuchumi, watu wenye magonjwa sugu na Watu Wenye Ulemavu.

Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshw (iCHF)

48. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa na Mamlaka za

Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 katika **Ibara ya 186** inaelekeza kuimarisha utaratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) ili iwafikie wananchi walio wengi na hasa wanyonge. Aidha, Ilani inaelekeza kutekeleza mikakati ya kuhamasisha wananchi wajunge na huduma za Bima ya Afya.

49. Mheshimiwa Spika, hadi Februari 2021 Mikoa yote nchini imefanikiwa kutekeleza Mfuko wa Afya ya Jamii Iliyoboreshwa (iCHF) ambapo uandikishaji unaendelea katika Mitaa na Vijiji vyote nchini. Maendeleo ya utekelezaji huu yamewezesha kufikiwa kwa mafanikio yafuatayo:

- i) Jumla ya wanachama **3,300,000** wamejunga na Bima ya Afya ya Jamii Iliyoboreshwa (iCHF) sawa na asilimia 6 ya Watanzania wote;
- ii) Jumla ya **Shilingi bilioni 17.1** zimekusanywa kutokana na michango ya wanachama;
- iii) Jumla ya **Shilingi bilioni 2.3** zimelipwa na Serikali ikiwa ni fedha za tele kwa tele na kufanya kiasi cha makusanyo yote kuwa **Shilingi bilioni 19.4**; Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Februari, 2021 wanachama **milioni 1** wamenufaika na Bima hii kwa kuweza kufikia Huduma za Afya kwa kupata matibabu katika vituo vya kutolea Huduma za Afya ya Msingi, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 6.7** zimelipwa kwenye vituo hivyo.

Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari

50. Mheshimiwa Spika, hadi Februari 2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Elimu ya Msingi na Sekondari kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutekeleza yafuatayo:-

- i) Kusimamia utoaji wa huduma kwa wanafunzi **14,990,844** ambapo wanafunzi **1,198,564** ni wa Shule za Awali, **11,035,064** Shule za Msingi (Darasa la Kwanza hadi Darasa la Saba) na Wanafunzi **2,757,216** ni wa Shule za Sekondari (Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Nne). Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inasimamia jumla ya walimu **261,253** ambapo walimu **175,887** ni wa Shule za Msingi na walimu **85,366** ni wa Shule za Sekondari.
- ii) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari. Miundombinu inayoendelea kujengwa ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi ni pamoja na vyumba vya madarasa **5,224**, matundu ya vyoo **15,616**, nyumba za walimu **38**, mabweni **223**, mabwalo **40**, majengo ya utawala **21** na vyumba vya maabara za sayansi **902**; iii) Kubainisha watoto wenye mahitaji maalum katika Halmashauri 184 ambapo jumla ya wanafunzi 28,698 (wavulana **16,461** na wasichana **12,237**) walibainishwa na kupangiwa shule kulingana na mahitaji yao;
- iv) Jumla ya vituo **510** vya walimu vimeainishwa kwa ajili ya kuviboresha ili kutoa mafunzo ya walimu kazini karibu na maeneo yao;
- v) Kuratibu mitihani ya kitaifa ya Darasa la Saba, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita na upimaji Darasa la Nne na Kidato cha Pili; vi) Kuratibu ajira na kupanga vituo vya kazi kwa walimu na Mafundi Sanifu wa maabara **8,000** wa Shule za Msingi na Sekondari; na vii) Kuwapangia shule wanafunzi wote **833,672** waliofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2020.

51. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha na kuboresha kiwango cha elimu kuanzia ngazi ya Awali, Msingi na Sekondari kwa kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo, uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari kama ifuatavyo:

Elimu ya Msingi

Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Msingi kwa mwaka 2021

52. **Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2021, uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali ulifikiwanafunzi **1,057,919** sawa na **asilimia 83.14** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,272,513** ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo wanafunzi **1,278,016** sawa na asilimia **92.48** waliandikishwa katika lengo la kuandikisha wanafunzi **1,382,761** (*Rejea Kiambatisho Na. 4*).

53. **Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2021, jumla ya wanafunzi wa Darasa la Kwanza **1,400,145** sawa na **asilimia 92.32** ya lengo la uandikishaji wa wanafunzi **1,516,598** ulifikiwa ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo wanafunzi **1,526,474** wallandikishwa sawa na **asilimia 96** ya lengo la uandikishaji wa wanafunzi **1,597,612**. Kuendelea kupungua kwa uandikishaji unatokana na mafanikio ya Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo uliowezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kwa sababu ya kuondolewa kwa ada na michango mbalimbali (*Rejea Kiambatisho Na. 5*).

Uboreshaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi

54. **Mheshimiwa Spika**, hadi Februari 2021 jumla ya vyumba vya madarasa **3,049** vya Shule za Msingi vimejengwa na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **125,719** vilivyokuwepo Februari, 2020 hadi vyumba vya madarasa **128,768**. Jumla ya matundu ya vyoo **14,581** yamejengwa katika Shule za Msingi na kuongeza matundu ya vyoo kutoka **205,663** vilivyokuwepo Februari, 2020 hadi kufikia matundu ya vyoo **220,244** mwezi Februari, 2021. Ongezeko la miundombinu hii imesaidia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Vilevile, jumla ya nyumba za walimu **20** zimejengwa katika Shule za Msingi katika kipindi hicho.

55. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali iliidhinisha jumla ya **Shilingi bilioni 26.10** kwa ajili ya

ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa **2,088** katika Halmashauri **184**. Hadi Februari 2021, kiasi cha **Shilingi bilioni 18.22** kimetolewa sawa na **asilimia 69.81** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **1,360** ya vyumba vya madarasa ya Shule za Msingi. (*Rejea Kiambatisho Na.6*).

56. Mheshimiwa Spika, kazi za ujenzi wa vyumba vya madarasa imekwenda sambamba na utengenezaji wa madawati. Hadi Februari 2021, idadi ya madawati imefikia **3,113,741** ikilinganishwa na madawati **3,052,541** yaliyokuwepo mwezi Februari 2020, ikiwa ni ongezeko la madawati **61,200**.

Mtihani wa Upimaji wa Darasa la Nne na Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba

57. Mheshimiwa Spika, katika matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **1,531,120** kati ya wanafunzi **1,665,863** sawa na **asilimia 91.9** walikidhi sifa za kuendelea Darasa la Tano, ikilinganishwa na wanafunzi **1,551,599** kati ya wanafunzi **1,704,286** sawa na **asilimia 91.04** ya waliofanya mtihani huo mwaka 2020.

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020, ufaulu wa mtihani wa kuhitimu Darasa la Saba umeongezeka kutoka **asilimia 81.50** mwaka 2019 hadi **asilimia 83.15** mwaka 2020. Kwa mwaka 2020, jumla ya wanafunzi **833,872** walifaulu sawa na **asilimia 83.15** kati ya wanafunzi **1,008,307** waliofanya mtihani, ikilinganishwa na wanafunzi **759,737** sawa na **asilimia 81.50** waliofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi kati ya wanafunzi **933,369** waliofanya mtihani mwaka 2019.

Elimu ya Sekondari

Usajili wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza

59. Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika Shule za Sekondari nchini imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoptera na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi. Kwa mwaka 2021, jumla ya wanafunzi **833,872** walichaguliwa kuijunga na Kidato

cha Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi **759,737** waliochaguliwa kujunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2019 (*Rejea Kiambatisho Na. 7*).

Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Shule za Sekondari

60. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuboresha miundombinu ya Shule za Sekondari ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujunga na Elimu ya Sekondari wanapata fursa ya kuendelea na masomo. Hadi Februari 2021, jumla ya madarasa mapya **936**, matundu ya vyoo **1,035**, mabweni **223**, mabwalo **40**, maktaba **8**, maabara za sayansi **18**, majengo ya utawala **21** na nyumba za walimu **18** zimejengwa. Vilevile, ukarabati wa Shule Kongwe **13** za Sekondari ambazo ni Shule za Sekondari za Iringa Wasichana, Tumaini Wasichana, Mwanza, Masasi Wasichana, Ashira Wasichana, Kibasila, Tarime, Shinyanga, Rungwe, Lindi, Moshi, Arusha Wasichana na Tunduru ambazo ziko katika hatua ya ukamilishaji kwa gharama ya **Shilingi bilioni 19.88**. Idadi hii inafikisha Shule Kongwe **86** zilizokarabatiwa katи ya Shule **89** sawa na **asilimia 96.63** ya lengo.

Ukamilishaji wa Vyumba vya Maabara za Masomo ya Sayansi

61. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kutoa kipaumbele katika ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo kwenye Shule za Sekondari. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imefuta mitihani ya sayansi mbadala wa vitendo (Alternative to Practicals) iliyodumu tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990 baada ya miaka zaidi ya 25. Wanafunzi wote wa Kidato cha Nne 2020 wamefanya mitihani ya Sayansi kwa vitendo. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 26.51** zimetolewa katи ya **Shilingi bilioni 42.33** sawa na **asilimia 62.63** zilizoidhinishwa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya maabara **1,411** za sayansi (*Rejea Kiambatisho Na. 6*)

62. Mheshimiwa Spika, sambamba na uboreshaji wa miundombinu mingine ya Shule za Sekondari, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kutoa kipaumbele katika ujenzi wa

matundu ya vyoo, mabweni na nyumba za walimu. Hadi Februari 2021, jumla ya matundu ya vyoo **1,035** yamejengwa kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 1.14**, mabweni **223** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **80** kila moja kwa kiasi cha **Shilingi bilioni 17.84** na nyumba za walimu **18** kwa kiasi cha **Shilingi milioni 900**.

63. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha Shule za Sekondari za Ufundi kwa kuajiri na kuwapangia vituo walimu wa masomo ya ufundi wa fani mbalimbali katika Shule zote tisa (9) za Sekondari za Ufundi ambazo ni Moshi Ufundi, Musoma Ufundi, Iyunga Ufundi, Ifunda Ufundi, Mtwara Ufundi, Tanga Ufundi, Bwiru Ufundi, Mwadui Ufundi na Chato Ufundi. Shule hizo zimekarabatiwa na kupewa kipaumbele cha kupangiwa walimu. Aidha, Shule hizo zimetengewa **Shilingi milioni 500.00** kwa kila shule kwa ajili ya kununua vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia ili kuwawezesha wahitimu kuwa na uwezo wa kujajiri au kuendelea na masomo ya juu katika vyuo vyaa ndani na nje ya nchi.

Mtihani wa Upimaji wa Kidato cha Pili na Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne na Sita

64. Mheshimiwa Spika, matokeo ya Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili katika mwaka 2020 yameonesha ongezeko la ufaulu kati ya mwaka 2019 na 2020 kwa **asilimia 1.57** ambapo mwaka 2019 jumla ya wanafunzi **514,251** kati ya wanafunzi **571,137** waliofanya mtihani sawa na **asilimia 90.04** walifaalu mtihani huo na kuendelea na Kidato cha Tatu, ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo jumla ya wanafunzi **601,948** waliofanya mtihani huo na wanafunzi **550,979** walifaalu sawa na **asilimia 91.61**.

65. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kidato cha Nne, ufaulu umeongezeka kutoka **asilimia 80.65** mwaka 2019 hadi **asilimia 85.84** mwaka 2020. Mwaka 2019 wanafunzi **340,914** walifaalu kati ya wanafunzi **422,722** waliofanya mtihani na mwaka 2020 wanafunzi **373,958** walifaalu kati ya wanafunzi **437,698** waliofanya mtihani sawa na ongezeko la **asilimia 5.19**.

66. Mheshimiwa Spika, ufaulu wa Kidato cha Sita kwa mwaka 2020 ulikuwa ni **asilimia 99.51** ambapo watahiniwa **73,537** kati ya watahiniwa **73,901** waliofanya mtihani walifaulu ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo watahiniwa **78,666** kati ya **79,770** ya waliofanya mtihani walifaulu sawa na **asilimia 98.61** ya watahiniwa. Ufaulu wa Kidato cha Sita umeendelea kuwa bora zaidi kila mwaka.

Utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo

67. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo ulioanza Desemba, 2015. Kuanzia Julai, 2020 hadi Februari 2021, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 166.44** kwa ajili ya kutekeleza Mpango huo. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi bilioni 80.51** na **Shilingi bilioni 85.93** zilitumika katika Shule za Msingi na Shule za Sekondari mtawalia (*Rejea Kiambatisho Na.8 kwa Shule za Msingi na Rejea Kiambatisho Na.9 kwa Shule za Sekondari*). Aidha, kiasi cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya Elimumsingi Bila Malipo kuanzia Desemba 2015 hadi Februari 2021, ni **Shilingi trilioni 1.26**

68. Mheshimiwa Spika, hadi Februari 2021, maeneo yaliyopatiwa fedha za ruzuku za ElimuMsingi Bila Malipo ni: uendeshaji wa shule **Shilingi bilioni 54.59**, chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi na wanafunzi wa bweni wa Shule za Sekondari **Shilingi bilioni 49.49**.

69. Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyopatiwa fedha ni fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na bweni wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne **Shilingi bilioni 20.53**, posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata **Shilingi bilioni 41.83**. Posho ya madaraka inayotolewa kila mwezi kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata imeongeza ufanisi wa utendaji kazi wa viongozi hao.

Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

70. *Mheshimiwa Spika*, uandikishaji wa wanafunzi wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Matokeo ya uandikishaji kwa mwaka 2020 yanaonesha kupungua ambapo wanafunzi **56,560** wakiwemo wavulana **31,728** na wasichana **24,832** waliandikishwa. Idadi hiyo imepungua kwa **asilimia 15.6** ikilinganishwa na wanafunzi **66,978** wakiwemo **wavulana 38,567 na wasichana 28,411** walioandikishwa mwaka 2019.

71. *Mheshimiwa Spika*, kupungua kwa uandikishaji kunatokana na mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Elimummsingi Bila Malipo ambapo kuanzia mwaka 2015 hadi Februari 2021 mpango umewezesha wanafunzi wenyе umri wa kwenda shule kuandikishwa kutokana na kuondolewa kwa ada na michango mbalimbali ambayo ilikuwa ni mionganoni mwa vikwazo viliviyopunguza kiwango cha uandikishaji. Hii inaashiria kwamba wanafunzi waliokuwa wanakosa nafasi ya elimu katika mfumo rasmi sasa wanapata fursa hiyo. Aidha, uandikishaji wa watoto wenyе umri wa kwenda shule unafanyika kwa wakati.

72. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Elimu ya Watu Wazima kupitia Programu ya Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo Rasmi wa Shule (*Integrated Programme for Out of School Adolescent - IPOS*). Mpango huu unalenga kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na stadi za maisha vijana wenyе umri wa miaka **14** hadi **19** katika maeneo ya ufugaji nyuki, samaki, kuku, useremala, uashi, utengenezaji batiki, usindikaji vyakula, utengenezaji mishumaa, sabuni, utengenezaji mafuta ya mwili pamoja na ushonaji. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, jumla ya walimu **258** walipatiwa mafunzo haya na jumla ya wanafunzi **9,939** wamesajiliwa na kuanza kusoma katika vituo **72** kwenye Mikoa nane (8) ya Kigoma, Tabora, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Dar es Salaam na Dodoma.

Elimu Maalum

73. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inasimamia Shule Maalum **37** za bweni, Vitengo Maalum **709** vinavyoshughulikia wanafunzi wenyewe mahitaji maalum katika Shule za Msingi na Shule Jumuishi **2,952** zenyewe wanafunzi wenyewe mahitaji maalum wa Shule za Msingi. Kwa upande wa Sekondari, kuna Shule Maalum moja (**1**) ya Patandi na vitengo maalum **81**. Hadi Februari 2021, uandikishaji wa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum umeongezeka hadi kufikia wanafunzi **66,083** ambapo Shule za Msingi zina wanafunzi **55,758** na Shule za Sekondari zina wanafunzi **10,325** ikilinganishwa na wanafunzi **55,185** wenyewe mahitaji maalum waliokuwepo mwaka 2020. Idadi hii inahusisha wanafunzi wenyewe ulemavu wa masikio, macho, uoni hafifu, usonji, viungo na akili.

74. Mheshimiwa Spika, mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **1,461** wenyewe mahitaji maalum sawa na **asilimia 77.22** walifaulu mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi na kuchaguliwa kujunga na Shule za Sekondari kati ya wanafunzi **1,892** waliofanya mtihani. Katika mwaka 2020, jumla ya wanafunzi **2,487** sawa na **asilimia 98.1** walifaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi. Matokeo haya yanaonesha ongezeko la ufaulu kwa **asilimia 20.88**.

75. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeajiri walimu **766** waliosomea taaluma ya Elimu Maalum ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum wanapata elimu sawa na wanafunzi wengine. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza vifaa visaidizi **51,339** vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 3**.

Michezo Shulenii

76. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeendelea kuhimiza na kusimamia maendeleo ya michezo katika Shule za Msingi na Sekondari. Wanafunzi na walimu waliendelea kuhamasishwa kushiriki katika mazoezi ya michezo kama njia mojawapo ya kujikinga na maradhi. Ili kuendeleza michezo,

jumlaha ya wanafunzi **1,669** katika Shule **79** za michezo walifanya mitihani wa somo la Elimu kwa Michezo katika mitihani ya Kidato cha Nne iliyofanyika mwezi Novemba, 2020.

77. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inaendelea kuimarisha michezo kwa kuanzisha tahasusi ya Elimu ya Michezo kwa Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari na kutoa mafunzo kwa walimu **400** wa michezo ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo katika Shule za Msingi na Sekondari.

Ajira Zilizotolewa Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

78. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mahitaji ya walimu katika Shule za Msingi na Sekondari, Serikali imeendelea kutoa ajira za walimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kukabiliana na upungufu uliopo. Hadi Februari 2021, walimu **4,700** wa Shule za Msingi na walimu **3,300** wa Shule za Sekondari walajiriwa na Serikali inakamilisha taratibu za ajira ya walimu wengine **6,734**.

Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Utawala na Nyumba za Viongozi Katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

79. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuratibu usimamizi wa ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, nyumba za makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na nyumba za Maafisa Waandamizi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea na ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Songwe, Njombe, Geita na Mbeya. Aidha, ujenzi wa nyumba za Wakuu wa Mikoa ya Katavi na Njombe unaendelea, ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe umekamilika na zinatumika, nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe zipo katika hatua ya ukamilishaji. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba kumi (**10**) za Maafisa Waandamizi katika Mkoa wa Shinyanga, ambapo nyumba moja imekamilika.

80. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea na ujenzi wa majengo ya utawala ya Wakuu wa Wilaya ambapo majengo matano **(5)** ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Mkalama, Ikungi, Mbogwe, Nyang'hwale na Buhigwe pamoja na Ofisi za Maafisa Tarafa **38** ujenzi unaendelea katika Mikoa ya Tanga Ofisi ishirini na moja **(21)**, Mwanza Ofisi kumi na nne **(14)** na Kigoma Ofisi tatu **(3)**. Aidha, nyumba nne **(4)** za Wakuu wa Wilaya za Bagamoyo, Kisarawe, Mkuranga na Bunda zimefanyiwa ukarabati. Hadi Februari 2021, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya utawala na nyumba za Viongozi ni **Shilingi bilioni 11.77** kati ya **Shilingi bilioni 50.43** zilizoidhinishwa.

81. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kutoa huduma kwa wananchi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kujenga majengo ya utawala na nyumba za makazi ya Wakurugenzi na Wakuu wa Idara. Jumla ya majengo ya utawala **100** yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kati ya majengo hayo, majengo **31** yapo katika hatua ya ukamilishaji, majengo **36** ujenzi unaendelea na **33** yamepangwa kuanza ujenzi yakiwemo majengo ya Halmashauri **30** zilizohamisha Makao Makuu kwenda katika maeneo yake ya utawala. Katika mwaka wa fedha 2020/21, **Shilingi bilioni 80.42** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa majengo ya utawala katika Halmashauri **100** ambapo hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 44.19** zimetolewa sawa na **asilimia 54.94**. (**Rejea Kiambatisho Na. 10**)

82. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kuishi kwa Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi bilioni 1.35** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara katika Halmashauri za Wilaya za Wanging'ombe, Arusha, Karatu, Longido, Meru, Monduli, Ngorongoro, Pangani na Halmashauri ya Mji wa Mafinga na Halmashauri ya Jiji la

Arusha. Hadi Februari 2021, **Shilingi milioni 593.17** sawa na **asilimia 43.94** zimetolewa.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

83. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya RaisTAMISEMI imeendelea kusimamia utoaji wa Mikopo ya Uwezeshaji kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenyе Ulemavu kwa mujibu wa Kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenyе Ulemavu za mwaka 2019.

84. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi bilioni 64.5** zilitengwa na Halmashauri zote nchini kwa ajili ya mikopo kwa Vikundi **18,244** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenyе Ulemavu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 25.8** zilitengwa kwa ajili ya Vikundi **8,223** vya Wanawake, **Shilingi bilioni 25.8** kwa ajili ya Vikundi **6,966** vya Vijana na **Shilingi bilioni 12.9** kwa ajili ya Vikundi **3,055** vya Watu Wenyе Ulemavu.

85. Mheshimiwa Spika, utoaji wa mikopo ya **asilimia 10** kutokana na Mapato ya Ndani ya Halmashauri umeendelea kuimarika ambapo hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 26.81** sawa na **asilimia 41.61** ya lengo la **Shilingi bilioni 64.46** zilikuwa zimetolewa kwa Vikundi **5,973** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenyе Ulemavu. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imehuisha Kanuni za Utekelezaji wa uwezeshaji wa asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwa ajili ya Wanawake, Vijana na Watu Wenyе Ulemavu kwa kupunguza idadi ya wanachama wanaoweza kuunda kikundi kutoka wanachama 10 hadi watano (5) ambapo kwa upande wa Watu Wenyе Ulemavu kikundi kinaweza kuundwa na watu wasiopungua wawili (2) kutoka idadi ya watu watano (5); kutumia sehemu ya fedha za marejesho kwa ajili ya Ufutiliaji na Tathmini ya vikundi; mafunzo ya ujasiriamali; uongozi; usimamizi wa fedha na utoaji wa taarifa.

86. Mheshimiwa Spika, Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo nchini wameendelea kutambua umuhimu

wa kutumia vitambulisho vya wajasiriamali ili biashara zao zitambulike na kuondokana na usumbufu waliokuwa wanaupata. Kuanzia tarehe 1 Machi, 2020 hadi Februari 2021, wafanyabiashara **716,776** wamepatiwa vitambulisho ambavyo vimewezesha kukusanya kwa jumla ya **Shilingi bilioni 14.33** katika Mikoa yote **26** ya Tanzania Bara. Aidha, tangu kuanza kwa zoezi la utoaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo nchini jumla ya vitambulisho **2,335,711** vimegawiwa ambavyo vimewezesha kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 46.71**. Lengo ni kuendelea kuwatambua wafanyabiashara wadogo na kuwawekea mazingira rafiki ya ufanyaji biashara. Katika mwaka 2020/21, Serikali imefanya maboresho ya vitambulisho vya Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo Nchini kwa kuweka picha na jina la mjasiriamali ili kuongeza udhibiti na kufungua fursa kwa wajasiriamali kuweza kutumia vitambulisho hivyo kupata huduma za kibenki na bima ya afya.

Miradi ya Kimkakati

87. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali ilitenga jumla ya **Shilingi bilioni 50** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Miradi **38** ya Kimkakati yenyeye thamani ya **Shilingi bilioni 273.06**. Miradi hii inatekelezwa katika awamu mbili ambapo katika awamu ya kwanza jumla ya Halmashauri **17** zenyeye Miradi **22** zilifuzu vigezo na kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 131.77** na awamu ya pili jumla ya Halmashauri **13** zenyeye miradi **16** zilifuzu vigezo na kutengewa jumla ya **Shilingi bilioni 141.59**. Hadi Februari, 2021 kiasi cha **Shilingi bilioni 44.15** kimetolewa sawa na asilimia **88.3** ya lengo la **Shilingi bilioni 50**.

88. Mheshimiwa Spika, hadi Februari, 2021 utekelezaji wa miradi ya Kimkakati umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Miradi sita (6) katika Halmashauri za Wilaya za Kakonko (Soko la Muhange), Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu (Kituo cha Mabasi) na Ruangwa (Ghala la Mazao), Manispaa ya Morogoro (Soko la Chifu Kingalu), Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Soko la Kisutu) na

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo (Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli kilichopo Mbezi Luis), utekelezaji wa miradi hii umekamilika na kuanza kutoa huduma. Aidha, miradi thelathini na mbili (**32**) inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Huduma za Kiuchumi na Uzalishaji

Maeneo ya Uwekezaji

89. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuweka kipaumbele katika kutenga maeneo ya uwekezaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, jumla ya hekta **2,359,379.33** zimetengwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uwekezaji zikiwemo hekta **117,379.62** sawa na **asilimia 4.97** kwa ajili ya viwanda vikubwa, vidogo na vya kati. Aidha, hekta **1,216,242.17** sawa na **asilimia 51.54** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya madini, biashara, kilimo na skimu za umwagiliaji. Vilevile, hekta **1,025,756.64** sawa na **asilimia 43** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya malisho ya mifugo. Hivyo, wadau mbalimbali wanahamasishwa kutumia fursa hiyo ya uwekezaji.

Sekta ya Kilimo na Viwanda

90. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wadau mbalimbali katika sekta ya Kilimo imeendelea kuratibu shughuli za kilimo hususan eneo la huduma za ugani. Hadi Februari 2021, jumla ya mashamba darasa **214** yameandaliwa ili kutoa elimu kwa vitendo kwa wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

91. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Taasisi ya Alliance for Green Revolution in Africa (AGRA) imewajengea uwezo Wataalam wa Kilimo kuhusu kuandaa Mipango bora ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (DADPs) katika Mikoa **12** na Halmashauri za Wilaya **30** nchini. Mikoa hiyo ni Kagera (Muleba, Misenyi, Biharamulo); Kigoma (Kasulu,

Kibondo, Kakonko); Katavi (Tanganyika, Mpimbwe, Nsimbo); Rukwa (Kalambo, Nkasi, Sumbawanga); Ruvuma (Songea, Madaba, Mbanga); Njombe (Wanging'ombe, Ludewa); Iringa (Mufindi, Kilolo); Manyara (Babati, Hanang', Kiteto); Arusha (Meru, Karatu, Arusha); Kilimanjaro (Hai, Siha, Rombo); Simiyu (Maswa) na Tanga (Kilindi). Aidha, jumla ya wataalam **588** kutoka kwenye Mikoa hiyo na Halmashauri wamejengewa uwezo.

92. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuboresha mifumo ya kuhifadhi mazao ya nafaka ili kuimarisha usalama wa chakula. Hadi Februari 2021, maghala sita **(6)** ya kuhifadhia mazao yenye uwezo wa kuhifadhi tani zaidi ya **18,000** yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Muleba, Rufiji na Momba kwa gharama ya **Shilingi milioni 278.06**. Vilevile, masoko matano **(5)** ya mazao ya kilimo yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Geita, Ulanga, Muheza na Halmashauri ya Mji wa Kibaha kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.35**. Masoko haya yatawezesha wakulima kuwa na sehemu ya uhakika na salama ya kuuzia mazao yao. Aidha, kwa upande wa uendelezaji viwanda hadi Februari 2021, jumla ya viwanda **1,490** vimejengwa vikiwemo viwanda vikubwa **45**, vya kati **153**, vidogo **593** na vidogo sana **699**. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kuhamasissha ujenzi wa viwanda ili kuzalisha ajira na kupunguza umasikini.

Sekta ya Mifugo

93. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na magonjwa ya mifugo yanayotokana na kupe na aina nyingine ya maambukizi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeratibu ujenzi na ukarabati wa majosho **277** kwa gharama ya **Shilingi milioni 357.28**. Majosho haya yapo katika Mikoa **15** ya Kigoma, Katavi, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Ruvuma, Morogoro, Mwanza, Rukwa, Tabora, Shinyanga, Tanga, Simiyu na Songwe. Aidha, zaidi ya mifugo **milioni 12** imeogeshwa ambapo gharama za madawa zilichangiwa na wananchi ambao ni wafugaji.

Maliasili na Mazingira

94. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia Sera na Mikakati mbalimbali ya kuhifadhi mazingira kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali. Hadi Februari 2021, Ofisi imeratibu uandaaji wa vitalu ambapo jumla ya miche ya miti ya matunda, mbao na ya kuhifadhi mazingira **milioni 170** imepandwa kwenye Mamlaka za Serikali ya Mitaa zote kwa gharama ya **Shilingi biliioni 50.78**. Natoa rai kwa Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wadau wengine kuendelea kuimarisha vitalu vya miche na kupanda miti ya kutosha ili kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi.

Utawala Bora na Usimamizi wa Rasilimali

95. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na maeneo yaliyopatiwa kipaumbele ni kama ifuatavyo:

Ushughulikiaji wa Kero na Malalamiko ya Wananchi Katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

96. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais TAMISEMI imeendelea kuimarisha uratibu wa madawati ya malalamiko na kero katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, jumla ya malalamiko **787** yalipokelewa kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali. Kati ya malalamiko hayo, **508** yalifanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi na malalamiko **279** yanaendelea kufanyiwa kazi kupitia Kamati zilizoundwa katika Mikoa na Halmashauri chini ya usimamizi wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri. Aidha, Viongozi wa Kitaifa, Mikoa na Wilaya wameendelea kufanya ziara na kupitia ziara hizo wamesikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

97. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendelea kuimarisha utendaji na uwajibikaji wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutekeleza dhana ya TAMISEMI ya Wananchi, Ofisi ya Rais –

TAMISEMI imeanzisha Kituo cha Huduma ya Mawasiliano kwa Mteja (Contact Centre) chenye mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi bila ya kuhitajika kufika katika ofisi zetu. Kituo hiki kimewezeshwa na mifumo na miundombinu inayosaidia wananchi kuwasiliana na Ofisi kwa njia mbalimbali za mitandao ya kijamii, kupiga simu, kutuma ujumbe mfupi na kupata ufanuzi, majibu, na utatuzi wa masuala yanayowakabili. Huduma hii imesaidia kutoa huduma kwa haraka na kwa gharama nafuu kwa wananchi wote na kuwezesha Viongozi wa Wizara kujua namna jamii inavyohudumiwa. Hadi Februari 2021, Kituo hiki kimeweza kuhudumia jumla ya wananchi **7,443** tangu kilipoanza kutoa huduma tarehe 06 Agosti, 2020.

98. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais- TAMISEMI imepanga kuongeza kasi ya kutatua kero na kushughulikia malalamiko ya wananchi katika masuala ya kisheria ambapo itashirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanzisha utaratibu maalumu wa kuwatumia Wanasheria wa Serikali walioko katika Wilaya na Mikoa kushughulikia kero na malalamiko na kuyatafutia ufumbuzi, ikiwemo kuzishauri ipasavyo Mamlaka mbalimbali za Serikali.

Usimamizi wa Fedha Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

99. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya RaisTAMISEMI imeendelea kutoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa fedha kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Miongozo inayotolewa mara kwa mara ili kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kuhakikisha kazi zinazotekelawa zinalingana na thamani ya fedha iliyotumika. Aidha, taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa makusanyo ya Mapato ya Ndani katika Halmashauri zote imeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari kila robo mwaka.

100. *Mheshimiwa Spika*, taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20 imebainisha kwamba Halmashauri **124** sawa na **asilimia 67** zimepata **Hati Zinazoridhisha (Hati Safi)**, Halmashauri **53**

sawa na asilimia **29** zimepata **Hati Zenye Shaka** na Halmashauri **8** sawa na asilimia **4** zimepata **Hati Zisizoridhisha (Hati Chafu)**. Matokeo haya ya ukaguzi yanaonesha kutofanya vizuri kwa Halmashauri nyingi ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2018/19 ambapo Halmashauri zilizopata **Hati Zinazoridhisha** zilikuwa **176** sawa na asilimia **95** na **Hati Zenye Shaka** Halmashauri **9** sawa na asilimia **5**. Hapakuwepo na Halmashauri zilizopata **Hati Chafu**.

101. Mheshimiwa Spika, kufuatia matokeo hayo yasiyordhisha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI itafanya uchambuzi wa taarifa za Halmashauri zote zilizopata Hati Chafu na Hati zenye Shaka kubainisha sababu za matokeo hayo na kuchukua hatua stahiki za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wote watakaothibitika kuwa chanzo cha kutofanya vizuri kwa Halmashauri zao.

102. Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja ambazo zimesababisha hati mbaya na hati zenye shaka katika Hesabu za Halmashauri, Taarifa ya CAG imebainisha hoja nyingine ambazo hazikutajwa kwenye hati mbaya au hati zenye shaka ambazo tumebaini kuwa hoja hizo ni muhimu kufuatiliwa kwa karibu. Hivyo, Ofisi ya Rais TAMISEMI itazifuatilia na kuzisimamia Halmashauri zote ili kuhakikisha kwamba masuala yote yaliyobainishwa na CAG yanafanyiwa kazi kikamilifu ikiwemo kuchukua hatua kwa watumishi wote wa Halmashauri ambao hawakutekeleza majukumu yao ipasavyo au kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu wa fedha za umma.

Ununuzi wa Magari ya Viongozi wa Mikoa na Halmashauri

103. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali ilitenga jumla ya **Shilingi bilioni 29.83** kwa ajili ya kununua magari **238**. Kati ya magari hayo, **16** ni kwa ajili ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na magari **38** kwa ajili ya Halmashauri **38** zenye makusanyo madogo ya Mapato ya Ndani ambapo kwa mapato hayo hazina uwezo wa kumudu gharama za ununuzi wa magari. Aidha, magari **184** ni kwa ajili ya Halmashauri **184**

ili kuwezesha na kurahisisha utendaji wa Idara za Elimu katika Halmashauri yamenunuliwa. Vilevile, magari **43** yametolewa na Serikali kutoka Taasisi mbalimbali kwa ajili ya Wakuu wa Wilaya ili kusaidia utendaji katika ofisi za Wakuu wa Wilaya. Hadi Februari, 2021 jumla ya magari **194** yamenunuliwa yakiwemo magari manne (**4**) kwa ajili ya Makatibu Tawala wa Mikoa ya Mtwara, Simiyu, Njombe na Kagera, gari moja (**1**) la Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, magari matano (**5**) kwa ajili ya Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya za Bukombe, Rufiji, Butiama, Itigi na Halmashauri ya Mji wa Bunda.

Uendelezaji Miji na Vijiji

104. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta katika kuandaa na kutekeleza mipango ya Uendelezaji wa Vijiji na Miji nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri za Miji ya Geita, Njombe na Tunduma zimekamilisha uandaaji wa Mipango Kabambe ya Uendelezaji Miji. Mipango hiyo inaandaliwa kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta kwa lengo la kuwa na mipango ya pamoja ili utekelezaji wake uwe shirkishi na wenye tija. Aidha, mipango hiyo inasaidia katika uboreshaji wa miundombinu ya masoko, vituo vya mabasi na malori, madampo ya kisasa, viwanda vidogo na vya kat, maduka makubwa, afya, elimu, maji, umeme na barabara.

105. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea na usimamizi wa utekelezaji wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Mwongozo wa Mwaka 2018. Hadi Februari, 2021 kati ya maombi **7,161** yaliyopokelewa, vibali **5,497** vilitolewa sawa na **asilimia 76.76**. Aidha, ukaguzi umeimarishwa ili kuleta ubora wa ujenzi.

106. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Halmashauri zililenga kukusanya **Shilingi billioni 7.06** kutokana na ada ya vibali vya ujenzi. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi billioni 3.54** sawa na **asilimia 50.1** ya lengo zimekusanywa. Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi

umesaidia kupunguza ujenzi holela, urasimu, muda wa kutoa vibali na kuongeza mapato ya Serikali. Katika mwaka ujao wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatarajia kukamilisha uandaaji wa mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya ujenzi pamoja na kuimarisha utekelezaji wa Mwongozo wa Anwani za Makazi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

107. *Mheshimiwa Spika*, hadi Februari 2021, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Mfumo wa Taarifa za Kijiografia (Geographical Information System - GIS) imekamilisha uandaaji wa Ramani Mnato za maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya na Halmashauri. Ramani mnato husaidia katika kuonyesha hali halisi ya mtawanyiko wa huduma za kiuchumi na kijamii kama vile minara ya simu, barabara, umeme, uoto wa asili, shule, hospitali na maji. Kazi hiyo imefanyika kwa kushirikisha Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Aidha, katika kuonesha mwenendo wa ukuaji wa miji nchini, kanzidata ya viashiria vya ukuaji wa miji imeandaliwa ambayo itawezesha utekelezaji wa mipango ya uendelezaji wa Miji nchini hususan Miji Midogo inayochipukia.

Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA

108. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki na miundombinu ya TEHAMA kwenye Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi zilizo chini yake na vituo vya kutolea huduma ambapo imeongeza ufanisi na uwajibikaji. Mifumo mbalimbali imefanyiwa usanifu na kujengwa kwenye maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imewezesha mifumo kutumika kwenye vituo **26,939** vya kutolea huduma ambavyo ni Shule za Msingi, Shule za Sekondari, Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati.

109. *Mheshimiwa Spika*, Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Takwimu za Elimumsingi (BEMIS) ambao umeimarishwa kwa kujengewa Mfumo wa Maombi ya Ajira za Walimu (OTEAS), Mfumo wa Taarifa za kila siku za Usimamizi na

Uendeshaji wa Shule (SIS), Mfumo wa Usajili na Uandikishaji wa Wanafunzi (PReM/PReMs) na Mfumo wa Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza, Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundji (Students' Selection MIS).

110. *Mheshimiwa Spika*, Mifumo mingine ambayo Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kusimamia ni Mfumo wa Kuandaa Mipango, Bajeti na Utoaji Wa Taarifa (PlanRep); Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na Utoaji wa Taarifa za Kihasibu kwa ngazi ya Kituo (FFARS); Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS); Mfumo wa Kuratibu zoezi la Upangishaji wa maeneo ya Biashara kwenye Miradi ya Kimkakati (PANGISHA); Mfumo wa Uendeshaji wa Tovuti za Serikali (GWF); Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Shughuli za Vituo vya Kutolea Huduma za Afya (GoTHOMIS); Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma (Epicor) ambao kuanzia Julai Mosi, utaondolewa na kuanza kutumia Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE).

111. *Mheshimiwa Spika*, katika kukabiliana na changamoto ya kuwasilisha kwa wakati kumbukumbu za madeni ya watumishi hasa walimu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imesanifu na kusimika Mfumo wa Kuratibu Madai na Madeni ya Watumishi (MADENIMIS) kwa lengo la kumrahisishia mtumishi kuanzisha na kufuatilia ombi lake la madai na madeni. Mfumo huu utaunganishwa na Mfumo wa Serikali wa Madeni (GAMS).

112. *Mheshimiwa Spika*, matumizi ya mifumo hii ya kielektroniki imeendelea kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa muhimu za utendaji kutoka ngazi za vituo na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mifumo hii imewezesha kupungua kwa matumizi ya karatasi katika utendaji wa kila siku na utoaji wa taarifa, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuongeza uwazi na uwajibikaji, utunzaji wa kumbukumbu; ushirikishwaji wa wananchi na utoaji wa huduma kwa haraka.

D. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI

WAKALA WA BARABARA ZA VIJJINI NA MIJINI (TARURA)

113. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA) umeendelea na utekelezaji wa majukumu ya ukarabati, matengenezo na ujenzi wa barabara na madaraja katika Halmashauri zote nchini. Wakala pia umefanya usanifu wa barabara na madaraja pamoja na kusimamia makusanyo ya ada na tozo za matumizi ya hifadhi ya barabara. Aidha, Wakala umeendelea kusimamia mtandao wa barabara wenyewe jumla ya **kilomita 108,946.19** ambapo **kilomita 2,250.69** ni za lami, **kilomita 27,809.26** ni za changarawe na **kilomita 78,886.25** ni za udongo. Aidha, jumla ya **kilomita 16,168.47** za mtandao wote wa barabara sawa na **asilimia 15** upo kwenye hali nzuri, **kilomita 39,027.62** sawa na **asilimia 36** upo kwenye hali ya wastani na **kilomita 53,750.10** sawa na **asilimia 49** upo kwenye hali mbaya.

114. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 275.03** kwa ajili ya ukarabati, matengenezo na ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilomita 23,402.61**, **madaraja 77**, **makalvati 271** na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua **kilomita 79.98**. Hadi Februari 2021, **Shilingi bilioni 172.85** zilikwa zimepokelewa sawa na asilimia **63**. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa **kilomita 97.7** na matengenezo ya barabara zenye urefu wa **kilomita 7,757.13** ikiwa ni matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofii na matengenezo ya muda maalum. Aidha, **ajira 8,044** za muda na mikataba zimezalishwa katika eneo la matengenezo, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya barabara za Vijiji na Mijini kupitia TARURA.

Mradi wa Uboreshaji wa Barabara Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (EUAGriconnect Project)

115. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya RaisTAMISEMI kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU) inaendelea na ujenzi wa

barabara za lami zenyе urefu wa **kilomita 87.6** katika Halmashauri za Wilaya ya Mufindi, Kilolo, Mbeya na Rungwe kwa gharama ya **Shilingi bilioni 40.76**. Lengo la mradi huu ni kufungua barabara kwenye maeneo yenye kilimo cha mazao ya chai, kahawa na mbogamboga ili kurahisisha usafirishaji wa mazao na kuongeza soko la mazao ya kilimo. Hadi Februari 2021, fedha zote zilikuwa zimepokelewa ambazo ni **Shilingi bilioni 40.76** ambapo ujenzi wa barabara za lami zenyе urefu wa **kilomita 12.2** umekamilika na ujenzi wa **kilomita 75.4** zilizobaki uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Ujenzi wa Barabara za Mji wa Serikali Eneo la Mtumba

116. Mheshimiwa Spika, Wakala unaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara za lami zenyе urefu wa **kilomita 51.2** katika Mji wa Serikali Eneo la Mtumba kwa gharama ya **Shilingi bilioni 89.11**. Mradi huu unatekelezwa ndani ya miezi **18** na unatarajwa kukamilika mwezi Julai, 2021. Hadi Februari 2021, jumla ya **Shilingi bilioni 22.41** zilikuwa zimetolewa na kutumika ambapo jumla ya **kilomita 15.2** zimekamilika kwa kiwango cha lami, makalavati **83** kati ya **118** yamekamilika, boxi kalavati zote **10** zimekamilika na utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 71**.

Utekelezaji wa Ujenzi wa Barabara za Ahadi za Viongozi

117. Mheshimiwa Spika, Wakala umeendelea kutekeleza ahadi za ujenzi wa barabara na miundombinu mingine zilizotolewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alizozitoa katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi Februari, 2021 **Shilingi bilioni 9.39** zilipokelewa na kutumika kwenye ujenzi wa barabara zenyе urefu wa **kilomita 64** kwa kiwango cha lami na **kilomita 15** za changarawe katika Halmashauri **65** nchini. Halmashauri **22** zimekamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami **kilomita 22**. Halmashauri zilizokamilisha ujenzi ni Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Kyerwa, Bukombe, Muleba, Mpwapwa, Kongwa, Missenyi, Ruangwa, Malinyi, Busokelo, Ludewa, Madaba, Nyasa, Itigi, Kwimba, Misungwi,

Songwe na Halmashauri za Miji ya Kondoa, Kasulu, Makambako na Masasi na Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ambapo utekelezaji wa miradi umekamilika kwa asilimia 100.

Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini

118. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala umeendelea na matayarisho ya Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii nchini, *Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities Programme (RISE)*. Mradi huu unakadiriwa kugharimu Dola za Kimarekani **milioni 350** kwa kipindi cha miaka mitano (5) ambapo **Dola za Kimarekani milioni 300** ni Mkopo wa Masharti Nafuu kutoka Benki ya Dunia na **Dola za Kimarekani milioni 50** ni mchango wa Serikali ya Tanzania. Lengo la mradi ni kujenga jumla ya **kilomita 535** za barabara za lami ambapo **kilomita 400** zitajengwa kwenye Mtandao wa barabara za Wilaya na **kilomita 135** zitajengwa kwenye barabara za Mikoa katika Halmashauri za Wilaya za Mufindi, Kilolo, Iringa, Ruangwa, Handeni na Mbogwe, kufanya matengenezo ya sehemu korofi zenye urefu wa **kilomita 2,900** na matengenezo ya kawaida **kilomita 23,000** katika Barabara za Halmashauri zote na kujenga uwezo wa Wakala katika kusimamia majukumu yake. Mradi umelenga kuboresha barabara maeneo ya Vifijini. Aidha, barabara za Mikoa (Regional Roads) zinazounganisha maeneo hayo zitajengwa kupitia TANROADS. Serikali ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Benki ya Dunia ili kupata fedha za kuwezesha utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP)

119. *Mheshimiwa Spika*, Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam (*Dar es Salaam Metropolitan Development Project - DMDP*) una vipengele vitatu vya utekelezaji ambavyo ni uboreshaji wa barabara za kipaumbele, uimarishaji barabara na miundombinu

mingine maeneo ya kaya maskini na uimarishaji wa taasisi, kujenga uwezo pamoja na uperembaji wa masuala ya kiuchumi na uendelezaji Miji. Katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi ulitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 186.80** ambapo hadi Februari 2021, kiasi cha **Shilingi bilioni 104.31** kilikuwa kimetolewa. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na ujenzi wa barabara zenye wa **kilomita 28** kwa kiwango cha lami na kuweka taa za barabarani, kukamilisha ujenzi wa vituo viwili vya mabasi eneo la Kijichi na Mbagala Kuu, ujenzi wa masoko manne ya Kijichi, Mbagala Kuu, Kilakala na Makangarawe na ujenzi wa vizimba **12** vya kuhifadhihia takangumu.

120. Mheshimiwa Spika, miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilomita 32**, mifereji mikubwa ya maji ya mvua (storm wáter drains) yenye urefu wa **kilomita 17.9** kwenye maeneo ya Mto Sinza, Kiboko, Gerezani, Kizinga, Bonde la Sungura, Mafuriko, Yombo, Buguruni Kisiwani, Msimbazi Tenge-Liwiti pamoja na ujenzi wa mabwawa makubwa (detention ponds) ya kuhifadhi maji ya mvua. Ujenzi wa masoko **manne (4)** ya kisasa ya Mtoni, Mbagala, Kinyerezi na Buza, ujenzi wa vituo vinne vya mabasi vya Buza, Kinyerezi, Mtoni na Mbagala.

121. Mheshimiwa Spika, Mradi umenunua vifaa vya kufanya usafi miundombinu ya barabara na mifereji ya maji ya mvua, ununuzi wa vifaa vya kudhibiti takangumu kwa Halmashauri za Manispaa za Temeke, Kinondoni na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambapo jumla ya magari **20** yamenunuliwa na kugawiwa. Aidha, yamefanyika maboresho ya mfumo wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuunganishwa na mfumo wa kijigrafia wenye taarifa muhimu za vyanzo vya mapato.

WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA DAR ES SALAAM (DART)

122. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) umeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi yafuatayo: kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa Mfumo

wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam; kuweka mpangilio makini wa matumizi ya barabara kuu na ndogo kwa watumiaji wote ili kupunguza msongamano; na kuhakikisha kuwepo kwa Menejimenti ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka yenye kuleta tija na ufanisi.

123. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala ulikadiria kukusanya mapato ya ndani jumla ya **Shilingi bilioni 4.75** kutokana na ushuru wa kutumia miundombinu, ada ya eneo la matangazo, ushuru wa vyoo na ushuru wa maegesho ya magari. Hadi Februari 2021, Wakala ulikuwa umekusanya jumla ya **Shilingi billion 2.19** sawa na **asilimia 46** ya lengo.

124. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala umeendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Ulipaji fidia kama sehemu ya maandalizi ya Awamu ya Tatu ya mradi inayohusisha barabara za Azikiwe, Maktaba, Lindi, Shaurimoyo, Uhuru, Bibi Titi, Nyerere kutokakatikati ya Jiji la Dar es salaam hadi Gongo la Mboto zenye urefu wa **kilomita 23.6**. Hadi Februari, 2021 malipo ya fidia ya **Shilingi bilioni 2.68** yalikuwa yamefanyika kwa wananchi **26** waliopisha mradi;
- ii) Usimamizi wa uendeshaji wa huduma za Mpito awamu ya kwanza ya Mfumo wa DART kulingana na Mkataba;
- iii) Kuimarisha ulinzi na usalama na kusimamia matengenezo ya miundombinu ya BRT kwenye vituo vikuu vitano **(5)**, vituo vidogo **27**, madaraja ya watembea kwa miguu matatu **(3)** na karakana ya Jangwani;
- iv) Kuboresha vituo vya mlisho vya Muhimbili na Mbezi kwa kujenga mabanda ya abiria;
- v) Kuendelea kushiriki katika kuratibu ujenzi wa Miundombinu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili unaohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Chang'ombe, Gerezani, Sokoine, Bandari zenye urefu wa **kilomita 20.3**;

- vi) Kufanya mapitio ya usanifu wa kina ikiwemo michoro ya miradi ya Awamu ya Nne na ya Tano pamoja na kufanya uthamini wa eneo la kujenga daraja la waenda kwa miguu kwenye miundombinu ya Awamu ya Pili;
- vii) Kuendelea na kazi ya kuunda mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli kwenye mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka utakaokamilika Agosti 2021; na
- viii) Usimamizi wa mitambo ya mfumo wa kukusanya nauli katika vituo mahiri vya TEHAMA.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

125. *Mheshimiwa Spika*, Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia utumishi wa walimu nchini. Hadi Februari 2021, Tume ilikuwa imepokea na kusajili rufaa **148** za walimu ambapo kati yake rufaa **111** zimetolewa uamuzi; vikao **230** vya Kisheria vya Kamati za Wilaya vimefanyika katika Wilaya **139** na kuwezesha walimu **4,575** kuthibitishwa kazini; walimu **3,770** kubadilishwa vyeo baada ya kujiendeleza kielimu na mashauri **4,010** ya kinidhamu yalitolewa uamuzi. Vilevile, ziara kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za walimu zilifanyika kwenye Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Songwe, Mwanza, Tanga, Singida na Pwani ambapo walimu **1,101** walipatiwa elimu kuhusu masuala ya ajira, nidhamu na maadili ya kazi ya ualimu.

126. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu imeanza kusimika Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (Teachers Management Information System - TSCMIS). Mfumo utaharakisha ushughulikiaji wa masuala ya rufaa, nidhamu na malalamiko ya walimu. Aidha, Tume imenunua kiwanja katika eneo la Chinyoya – Ntyuka Jijini Dodoma kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu.

CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA HOMBOLO

Uendeshaji wa Mafunzo ya Muda Mrefu na Mfupi

127. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Serikali za Mitaa kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni: kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi; kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uendeshaji na usimamizi wa Serikali za Mitaa. Mafunzo ya muda mrefu yanatolewa katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada. Katika mwaka wa masomo 2020/21, Chuo kimedahili wanafunzi **4,984** katika ngazi ya Astashahada, wanafunzi **1,601** katika ngazi ya Stashahada na wanafunzi **53** katika ngazi ya Shahada. Hivyo, jumla ya wanafunzi **7,224** walidahiliwa kati ya lengo la kudahili wanafunzi **7,000** sawa na ongezeko la **asilimia 3.2**.

128. *Mheshimiwa Spika*, Chuo kinaendelea kuanda mazingira ya kuboresha mifumo, miundombinu, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kuwajengea uwezo watumishi na kutengeneza mitaala ya Shahada ya Kwanza ya Maendeleo ya Jamii; Rasilimaliwatu; na Utunzaji wa Kumbukumbu. Shahada hizo zinategemea kuanzishwa katika mwaka wa masomo 2021/22. Chuo kinaendelea kujenga uwezo wa watumishi katika fani mbalimbali ambapo jumla ya watumishi **45** wapo katika mpango wa mafunzo kama ifuatavyo, Shahada ya Uzamivu **21**, Shahada ya Uzamili **18** na Shahada ya kwanza sita (**6**). Chuo kimeendelea kuwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa Viongozi na Watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Chuo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI kiliwezesha mafunzo ya awali ya Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (*Opportunities and Obstacles to Development - O&OD*) Ulioboreshwa katika Sekretarieti **16** za Mikoa na Halmashauri **107** ambazo hazikupata mafunzo ya awamu ya kwanza.

129. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Serikali za Mitaa kimefanya jumla ya tafiti **19** ambazo ziko katika hatua mbalimbali za machapisho. Tafiti hizi zinafanyika katika Halmashauri, lengo likiwa ni kubaini na kutatua changamoto mbalimbali

zinazokwamisha utoaji wa huduma za kijamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutoa ushauri wa kitaalam.

130. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo kwa kutumia mapato ya ndani kimeendelea na jithada za kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Hadi Februari 2021, Chuo kimekamilisha ujenzi wa kumbi mbili (2) za kufundishia kwa utaratibu wa *Force Account* ambazo zina uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa gharama ya **Shilingi milioni 282.**

SHIRIKA LA ELIMU KIBAHA

131. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Elimu Kibaha limeendelea kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwake ambayo ni kupambana na maadui watatu wa maendeleo yaani Ujinga, Umaskini na Maradhi kuititia Idara na Vitengo vilivyo chini yake. Hadi Februari 2021, Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi imetoa matibabu kwa wagonjwa **82,941**, kati yao wagonjwa **76,866** walitibiwa na kuondoka na wagonjwa **6,075** walilazwa.

132. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na Hospitali hii kuwa karibu na barabara kuu ya Morogoro – Dar es Salaam, pamoja na kuhudumia wagonjwa wa kawaida imekuwa na msaada mkubwa kwa majeruhi wa ajali za barabarani ambapo hadi Februari 2021, jumla ya majeruhi wa ajali za barabarani **710** wakiwemo wanawake **162** na wanaume **548** wamehudumiwa. Aidha, Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi imeanzisha huduma kwa watoto wachanga wanaohitaji uangalizi wa karibu, *Neonatal Intensive Care Unit* ambayo ina uwezo wa vitanda **24** na inalaza watoto kati ya **5** hadi **11** kwa siku na huduma kwa waraibu wa dawa za kulevyu ambapo waraibu **49** wamesajiliwa na wanaendelea na tiba. Vilevile, mafunzo ya utabibu na uuguzi yametolewa kwa wanachuo **470** katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha.

133. *Mheshimiwa Spika*, Shirika linasimamia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi ambacho kinatoa mafunzo ya

ujasiriamali ya muda mfupi na muda mrefu. Hadi Februari 2021, jumla ya wanachuo **292** walipatiwa mafunzo katika fani za kilimo, mifugo, uashi, bomba, useremala, ushonaji, upishi, fundi magari, uundaji na ufuaji vyuma na umeme wa majumbani. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wajasiriamali **267** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za udereva, ufugaji nyuki, kuku, elimu ya kuweka na kukopa, kilimo bustani na uundaji wa vikundi ambapo kiasi cha fedha **Shilingi 120,919,951** fedha za Mapato ya Ndani kilitumika kugharamia mafunzo hayo.

134. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kutunza shamba la ng'ombe wa maziwa lenye ng'ombe **65** kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na kuuzia wananchi maziwa. Kati ya hao, ng'ombe **15** wanakamliwa kwa sasa na wanatoa lita **2,700** kwa mwezi. Vilevile, Shirika linasimamia Shule tatu za Sekondari ambazo ni Shule ya Sekondari Kibaha, Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, Shule ya Sekondari Tumbi na Shule ya Msingi Tumbi zenyeye jumla ya wanafunzi **2,902**.

SHIRIKA LA MASOKO YA KARIAKOO

135. Mheshimiwa Spika, Shirika la Masoko ya Kariakoo limeendelea kutekeleza majukumu yake ya Msingi kwa Mujibu wa Sheria kwa kutoa huduma za masoko katika Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika lilikadiria kukusanya Mapato ya Ndani **Shilingi bilioni 4.01** kutokana na ushuru wa mazao, kodi ya pango, ada ya kutumia soko na ada ya ulinzi wa maegesho. Hadi Februari 2021, Shirika lilikuwa limekusanya **Shilingi bilioni 2.15** sawa na asilimia **54** ya lengo. Makusanyo haya yameongezeka kwa **asilimia 1.4** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/20 ambapo katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020, Shirika lilikusanya wastani wa **Shilingi bilioni 2.12**.

136. Mheshimiwa Spika, hadi Februari 2021, Shirika kuitia mapato yake ya ndani limekamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa paa katika eneo la soko dogo mzunguko lilipo maeneo ya Soko la Kariakoo Mtaa wa Sikukuu. Aidha, Shirika linaendelea na kazi ya kuandaa michoro ya usanifu (detailed

design) na taarifa ya upembuzi yakinifu (feasibility study) kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa soko la kisasa katika eneo la soko dogo. Vilevile, Shirika limefanikiwa kuimarisha hali ya usafi na mazingira ndani na nje ya soko kwa kutekeleza mikakati ya uondoshaji wa takangumu na maji taka, hivyo kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa watumiaji.

BODI YA MIKOPO YA SERIKALI ZA MITAA

137. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais -TAMISEMI kupitia Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) imeendelea kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2021, Halmashauri sita (6) ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, Halmashauri ya Mji wa Mbinga na Halmashauri za Wilaya za Mbinga, Tunduru, Ruangwa na Kishapu kati ya Halmashauri 11 zinazodalwa zimerejesha sehemu ya mikopo yake yenye thamani ya **Shilingi milioni 337.66** kati ya **Shilingi bilioni 3.99**. Aidha, Bodi imeendelea kukusanya michango ya akiba kwa mujibu wa Sheria ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 55.38** kimekusanywa kati ya **Shilingi bilioni 3.91** zinazopaswa kuchangwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

E. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 KWA OFISI YA RAIS - TAMISEMI (FNGU 56), MIKO NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAFNGU 26) NA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (FNGU NA. 2)

138. *Mheshimiwa Spika*, Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 umeandaliwa kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatoo wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Hotuba ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyoitao wakati wa kuzindua Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 13 Novemba 2020, Mwongozo wa Kuandaa Mpango

na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/22, maelekezo ya Viongozi wengine wakuu wa Kitaifa, Sera za Kisekta, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati iliyohuishwa ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Fungu 56, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) na Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2) kwa kipindi cha 2021/22-2025/26.

Ofisi ya Rais –TAMISEMI (Fungu 56)

139. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

- i) Utoaji wa Huduma bora za Afya ya Msingi ikijumuisha ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba pamoja na ujenzi wa miundombinu ya zahanati, vituo vya afya na Hospitali za Halmashauri;
- ii) Utoaji wa Huduma bora za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa kununua vitabu, vifaa vya maabara pamoja na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, maabara, nyumba za walimu, Shule za Sekondari za sayansi za wasichana, ujenzi wa shule za kutwa za Kata pamoja na utengenezaji wa madawati kwa Shule za Msingi;
- iii) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za Vijiji na Mijini;
- iv) Kuwawezesha wananchi kiuchumi; na
- v) Kuimarisha Utawala bora na usimamizi wa rasilimali; na
- vi) Kujenga mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji wa viwanda Mijini na Vijiji.

140. *Mheshimiwa Spika*, kupitia Vipaumbele hivi, shughuli zifuatazo zitatekelezwa:

- i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

- ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma ya Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo;
- iv) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudzi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- v) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Raís – TAMISEMI;
- vi) Kuendeleza rasilimali watu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa lengo la kuongeza ufanisi;
- vii) Kuchochea na kuhimiza ukuaij wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;
- viii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya Ukaguzi, Ufuatiliaji na Tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, Programu na Miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ix) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- x) Kuratibu shughuli za utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI;

- xi) Kuratibu usafiri na usafirishaji, ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara, afya na elimu inayotekelawa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xii) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, Halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri **30** ambazo zimehamia katika maeneo yake ya utawala;
- xiii) Kusimamia matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na
- xiv) Kuratibu uendelezaji wa Vijiji na Miji na kuimarisha utangamano wa Vijiji na Miji (Rural-Urban Intergration).

Tawala za Mikoa (Mafungu 26)

141. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Tawala za Mikoa zimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;
- ii) Kuratibu utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan katika usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi, Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, lishe na ustawi wa jamii;
- iii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa majengo ya Ofisi na nyumba za makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Makatibu Tawala Wasaidizi, Maafisa Tarafa na Maafisa Waandamizi; iv) Kufanya Ufuatililaji na Tathmini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi na Sera nyingine za kisekta ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi;
- iv) Kusimamia rasilimaliwateru na rasilimali fedha katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

- v) Kuratibu na kufanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi) Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vii) Kuratibu uanzishwaji wa viwanda kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara Mijini na Vijijiini, uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa na kuhimiza shughuli za kuongeza mnyororo wa thamani katika bidhaa zinazozalishwa na wananchi;
- viii) Kutatua migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ix) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika kuimarisha uchumi kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- x) Kusimamia na kuimarisha Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; xii) Kuratibu uanzishaji wa viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, misitu, mifugo na uvuvi;
- xi) Kufanya mapitio ya Mipango Mikakati ya Sekretarieti za Mikoa na kuratibu mapitio ya Mipango Mikakati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; xiv) Kuratibu uendelezaji wa maeneo maalum ya shughuli za kiuchumi na uwekezaji;
- xii) Kuratibu utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake (**asilimia 4**), Vijana (**asilimia 4**) na Watu Wenye Ulemavu (**asilimia 2**); xvi) Kuhamasisha na kusimamia kilimo cha mazao ya kimkakati ambayo ni Korosho, Chai, Tumbaku, Katani, Kahawa, Pamba na Michikichi; na
- xiii) Kuhamasisha uwekezaji katika maeneo yao ya utawala.

Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 ndani ya Mafungu 26 ya Mikoa

142. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji kwa kuhakikisha mikutano ya kisheria inafanyika na taarifa za mikutano hiyo zinawekwa katika maeneo ya wazi na katika tovuti za kila Halmashauri hasa taarifa za mapato na matumizi.
- ii) Kuimarisha na kubuni mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ikiwemo mapato ya kodi ya majengo na ushuru wa mabango;
- iii) Kusimamia ulinzi na usalama;
- iv) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi katika sekta zote hususan kujenga na kuboresha Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati, vyumba vya maabara za sayansi katika Shule za Sekondari, nyumba za watumishi, matundu ya vyoo, na vyumba vya madarasa;
- v) Kusimamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo katika Shule za Msingi na Sekondari;
- vi) Ukamilishaji na kuanza ujenzi wa majengo ya Ofisi, nyumba za makazi ya Viongozi na watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo Halmashauri 30 zilizohamia katika maeneo yake ya utawala;
- vii) Kukamilisha ujenzi wa miradi viporo ya miundombinu mbalimbali ya huduma za kijamii;
- viii) Kubuni, kuandaa maandiko na kutekeleza Miradi ya Kimkakati itakayosaidia kuongeza Mapato ya Ndani ya Halmashauri;

- ix) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuimarisha utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- x) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa na maeneo ya Wafanyabiashara Wadogo na Watoa Huduma Wadogo;
- xi) Kusimamia shughuli za uendelezaji Miji na Vijiji; na
- xii) Kusimamia utunzaji wa mazingira na shughuli mtambuka.

F. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)

143. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza yafuatayo:

- i) Kupokea, kusajili na kuchambua rufaa za walimu;
- ii) Kuzijengea uwezo Ofisi za Wilaya 139 za Tume katika masuala ya usimamizi wa rasilimaliwatu;
- iii) Kuandaa Mwongozo wa masuala ya ajira na nidhamu;
- iv) Kufanya mikutano na wadau kuhusu masuala ya ajira, maadili, nidhamu na maendeleo ya walimu;
- v) Kufanya tathmini kuhusu upangaji wa walimu mashulenii na kuwezesha Ofisi za Tume katika ngazi ya Wilaya kuhuisha Tange ya Walimu;
- vi) Kuandaa na kuratibu Mikutano sita (6) ya Tume na Vikao vinne (4) vya Kamati tatu (3) za Tume; na vii) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Tume Makao Makuu Jijini Dodoma.

Wakala wa Barabara za Vijiji ni na Mijini (TARURA)

144. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara za Vijiji ni na Mijini (TARURA) katika mwaka wa fedha 2021/22 utaendelea kutekeleza kazi mbalimbali za matengenezo, ukarabati na ujenzi wa barabara na madaraja kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kupitia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na Mpango Mkakati wa Wakala wa mwaka 2021/22 – 2025/26.

145. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais- TAMISEMI itatoa Mwongozo kwa Halmashauri zenyne mapato makubwa namna ya kuchangia fedha za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kwa TARURA. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaweka utaratibu wa mahusiano kati ya Halmashauri na TARURA ili kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi na ushirikishwaji wa Halmashauri wakiwemo Waheshimiwa Madiwani.

Ujenzi, Ukarabati na Matengenezo ya Barabara na Madaraja

146. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo;

i) Matengenezo ya barabara za Vijiji ni na Mijini zenyne urefu wa **kilomita 24,630.42** ambapo **kilomita 16,300.22** ni matengenezo ya kawaida, **kilomita 5,341.82** ni matengenezo ya maeneo korofi na **kilomita 2,988.38** ni matengenezo ya muda maalum;

ii) Ujenzi wa barabara za lami zenyne urefu wa **kilomita 136.82**;

iii) Ujenzi wa barabara za changarawe zenyne urefu wa **kilomita 469.16**;

iv) Ujenzi wa madaraja **93** na ukarabati wa madaraja **27**;

v) Ujenzi wa makalavati **206** na matengenezo ya makalavati **197**; na

vi) Ujenzi wa mifereji yenyе urefu wa **kilomita 62.7**.

Mradi wa Uboreshaji wa Barabara katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (Agri-Connect Programme)

147. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya RaisTAMISEMI inaendelea kutafuta fedha za matengenezo ya barabara za Vijijini na Mijini kuititia TARURA. Katika mwaka wa fedha 2021/22, TARURA itatetekeleza mradi huu ambaо unalenga kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yenyе uzalishaji mkubwa wa mazao ya mbogamboga, chai na kahawa ili kuimarisha mnyonyoro wa thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko.

148. Mheshimiwa Spika, Mradi huu utatekelezwa katika Mikoa ya Njombe, Ruvuma, Songwe, Mbeya na Iringa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya (EU) kwa ajili ya uboreshaji wa barabara maeneo ya Vijijini zenye urefu wa **kilomita 40.00** kwa kiwango cha lami.

Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP)

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Programu ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam (DMDP) itakamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilomita 16** kwa kiwango cha lami; mifereji ya maji ya mvua yenyе urefu wa **kilomita 17.9** pamoja na ujenzi wa masoko manne (4) ya Mtoni, Mbagala, Kinyerezi na Buza.

Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE)

150. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii nchini, *Roads to Inclusion and Social Economic Opportunities Programme (RISE)*. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka wa fedha 2021/22. Lengo la mradi ni kujenga jumla ya **kilomita 535** za barabara za lami ambapo **kilomita**

400 zitajengwa kwenye Mtandao wa barabara za Wilaya na **kilomita 135** zitajengwa kwenye barabara za Mikoa.

151. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mradi wa RISE, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kupitia TARURA inatarajia kulipa fidia, kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **kilomita 468** katika Mikoa ya Lindi, Tanga na Geita na kuendelea na utekelezaji wa ujenzi wa barabara za lami katika Halmashauri za Wilaya za Kilolo, Mufindi na Iringa.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART)

152. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umepanga kutumia **Shilingi bilioni 7.27** kama Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 1.80** ni Mishahara na **Shilingi bilioni 5.46** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha za Matumizi Mengineyo, **Shilingi milioni 696.39** ni fedha kutoka Serikali Kuu na **Shilingi bilioni 4.76** ni fedha za Mapato ya Ndani.

153. Mheshimiwa Spika, Wakala umepanga kutelezea majukumu yafuatayo:

- i) Kujenga kituo cha kibiashara cha uwekezaji Gerezani - Kariakoo ili kuongeza mapato ya Wakala;
- ii) Kusimika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya nauli (AFCS) na Mfumo wa kuongoza mabasi (ITS) itakayoleta huduma bora ya usafiri;
- iii) Kuendelea na usimamizi wa uendeshaji wa huduma za mpito awamu ya kwanza ya Mfumo wa DART katika kipindi hiki kulingana na Mkataba;
- iv) Kuendelea na usimamizi wa matengenezo ya miundombinu katika BRT awamu ya kwanza kwenye vituo vikuu vitano (**5**), vituo vidogo **27** na madaraja matatu (**3**) ya waenda kwa miguu;

- v) Kuimarisha usafi, ulinzi na usalama katika Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka awamu ya kwanza kwenye vituo vikuu vitano **(5)**, vituo vidogo **27**, madaraja matatu **(3)** ya waenda kwa miguu pamoja na karakana ya Jangwani;
- vi) Kuendelea kushiriki katika kuratibu ujenzi wa miundombinu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka awamu ya pili unaohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Chang'ombe, Gerezani, Sokoine, Bandari zenye urefu wa **kilomita. 20.30**; na
- vii) Kuendelea kufanya mapitio ya usanifu wa kina ikiwemo michoro ya miradi ya awamu ya sita.

Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo

154. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Chuo cha Serikali za Mitaa kinatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kudahili wanafunzi wapya **7,000**;
- ii) Kuendeleza na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa kozi za muda mrefu pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi yenye kuzingatia uhitaji;
- iii) Kuanzisha mafunzo ya kozi tatu za Shahada katika fani za Maendeleo ya Jamii; Menejimenti ya Rasilimaliwatu; na Utunzaji Nyaraka na Kumbukumbu;
- iv) Kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- v) Kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Mikutano Hombolo;
- vi) Kujenga ukumbi wa kufundishia wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **400**;

vii) Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala awamu ya pili; na

viii) Kuendelea na ujenzi wa kumbi za kufundishia na ofisi ya Kampasi ya Dodoma mjini.

Shirika la Elimu Kibaha

155. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Shirika la Elimu Kibaha linatarajia kutekeleza yafuatayo:

i) Kuendelea kutoa huduma za afya za kinga na tiba katika Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi;

ii) Kuendelea kutoa elimu ya uuguzi na utabibu katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;

iii) Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari na Msingi;

iv) Kuendelea kutoa huduma za maktaba;

v) Kutoa mafunzo ya ufundi, ujasiriamali, kilimo na mifugo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha;

vi) Kuongeza uzalishaji wa maji tiba kwa ajili ya matumizi ya Hospitali kutoka chupa **36,000** hadi chupa **72,000** kwa mwaka; na

vii) Kuendeleza mradi wa upanuzi wa Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi kwa kukamilisha jengo litakalokuwa na wodi ya upasuaji yenye vitanda **248**, huduma za dharura, chumba cha upasuaji na ofisi za utawala.

Shirika la Masoko ya Kariakoo

156. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika la Masoko ya Kariakoo limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Shirika ili kuendana na mazingira ya sasa ya kibashara;
- ii) Kuendelea na ujenzi wa soko la jumla katika eneo la Makonde - Mbezi Beach;
- iii) Kujenga maduka mapya **30** katika eneo la Tabata Bima;
- iv) Kufanya maboresho (Partitioning) katika duka namba G/ 039 katika jengo la Soko Kuu kwa kujenga maduka madogo nane (**8**);
- v) Kuendelea na ukarabati wa miundombinu chakavu katika maeneo mbalimbali; na
- vi) Kuendelea kusimamia usalama wa soko na shughuli za usafi wa mazingira na uondoshaji wa takangumu na maji taka.

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

157. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

- i) Kukamilisha marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Bodi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa Bodi;
- ii) Kuboresha muundo wa Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi;
- iii) Kupokea, kuchambua na kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo; na
- iv) Kufanya ufuatiliaji wa urejeshwaji wa mikopo na uwasilishwaji wa michango kutoka Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi.

MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/22

158. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza malengo mahsusi yafuatayo:

- i) Kuimarisha na kuhakikisha vituo vya kutolea huduma viliv yokamili ka vinaanza kutoa huduma za Afya na Elimu ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba na utengenezaji wa madawati kwa Shule za Msingi na Sekondari;
- ii) Kujenga vituo vya afya vinya **121** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 60.50** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (*Rejea Kiambatisho Na. 11*);
- iii) Kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya **52** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 15.60** vilivyoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa kutumia fedha za ndani; (*Rejea Kiambatisho Na. 11*);
- iv) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali za Halmashauri **68** za awamu ya kwanza zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2018/19 ikiwemo Hospitali ya Uhuru ili yopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 55.70** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 12*);
- v) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali **27** za awamu ya pili zilizoanza kujengwa mwaka wa fedha 2019/20 na Hospitali nne (4) za awamu ya kwanza ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 11.40** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 12*)
- vi) Kuanza ujenzi wa Hospitali mpya **28** katika Halmashauri ambazo hazina Hospitali za Serikali ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 14.00** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 12*);

- vii) Ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali **31** za awamu ya pili ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 12.30** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 12*);
- viii) Ukamilishaji wa maboma ya zahanati **763** yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika Majimbo yote ya Uchaguzi yatakayogharimu **Shilingi bilioni 38.15** ambapo kila zahanati imetengewa **Shilingi milioni 50** (*Rejea Kiambatisho Na. 13*);
- ix) Kuanza Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa **shule 10 kati ya shule 26** za Sekondari za wasichana za bweni kwa masomo ya Sayansi (shule moja kwa kila Mkoa) ambayo katika Awamu hii itajengwa miundombinu ya Kidato cha Tano na Sita. Aidha, shule hizi zitakapokamiliika zitakuwa na Kidato cha Kwanza hadi cha Sita na wanafunzi kati ya **1,000** hadi **1,200** kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 40** zimetengwa;
- x) Kujenga Shule mpya **300** za Sekondari za kutwa kwenye Kata ambazo hazina Shule za Sekondari kwa gharama ya **Shilingi milioni 650 hadi 700** kwa kila shule kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP);
- xi) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba **1,840** vya madarasa ya Shule za Sekondari kwa gharama ya **Shilingi bilioni 23.00** (*Rejea Kiambatisho Na. 14*);
- xii) Kujenga nyumba **300** (Two in One) za walimu kwa gharama ya **Shilingi milioni 50** kwa kila nyumba;
- xiii) Kuendelea kugharamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 312.05** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 15*);
- xiv) Ununuzi wa vitabu vya Shule za Msingi na Sekondari kwa gharama ya **Shilingi bilioni 50.00** fedha za ndani;
- xv) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba **3,268** kwa madarasa ya Shule za Msingi kwa gharama ya **Shilingi bilioni 40.85** (*Rejea Kiambatisho Na. 16*);

- xvi) Kuhakikisha upatikanaji wa madawati ya Shule za Msingi **710,000** ili kukabiliana na upungufu wa madawati **1,048,561** kwa kuanzia kiasi cha **Shilingi bilioni 6.73** kimetengwa;
- xvii) Ukamilishaji wa vyumba **1,043** vya maabara za sayansi katika Shule za Sekondari kwa gharama ya **Shilingi bilioni 26.07** - fedha za ndani (*Rejea Kiambatisho Na. 17*);
- xviii) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya Utawala ya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 57.92** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 18*);
- xix) Ujenzi wa majengo ya Utawala kwa Halmashauri **96** kwa gharama **Shilingi bilioni 83.75** na ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara katika Halmashauri **51** ikijumuisha Halmashauri **30** zilizohamia kwenye maeneo yao ya utawala utakaogharimu **Shilingi bilioni 7.65** fedha za ndani (*Rejea Kiambatisho Na. 19*);
- xx) Ununuzi wa magari **66** kwa ajili ya Viongozi wa Mikoa na Halmashauri, kiasi cha **Shilingi bilioni 14.80** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 20*);
- xxi) Utekelezajiwa Miradi **31** ya Kimkakati katika Halmashauri **26** ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 68.70** fedha za ndani kimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 21*);
- xxii) Utoaji wa mikopo ya **asilimia 10** kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenyewe Ulemavu kuititia Mapato ya Ndani ya Halmashauri ambapo **Shilingi bilioni 67.66** fedha za ndani zimetengwa (*Rejea Kiambatisho Na. 22*);
- xxiii) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kwa gharama ya **Shilingi bilioni 627.044** kuititia TARURA ambapo **Shilingi bilioni 272.50** zinatokana na Mfuko wa Barabara, **Shilingi bilioni 127.50** zinatokana na Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 12.75** zinatokana na Mapato ya Ndani ya TARURA ambapo jumla ya **kilomita 136.82** barabara za lami, **kilomita 500** za barabara za changarawe na Kalvati/

madaraja **90** yatatengenezwa. Aidha, kiasi cha **Shilingi bilioni 214.294** ni fedha za nje ambapo **Shilingi bilioni 156.031** ni kwa ajili ya kuendeleza miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam na kiasi cha **Shillingi bilioni 22.263** ni fedha za Mradi wa Uboreshaji wa Barabara Maeneo ya Uzalishaji wa Kilimo (EU – Agriconnent Project) pamoja na **Shilingi bilioni 36.00** ni Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (Roads to Inclusion and Socio-Economic Opportunities Programme - RISE). Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenyet urefu wa **kilomita 91** kwa kiwango cha lami maeneo ya Vijijini, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua **kilomita 17.9**, ujenzi wa masoko manne (4), kulipa fidia, na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya matengenezo ya barabara **kilomita 468**;

G. SHUKRANI

159. Mheshimiwa Spika; kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, naomba kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Humphrey Hezron Polepole (Mb), Mwenyekiti wa Kamati, na Makamu wake Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo (Mb), kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Maoni na ushauri wa Kamati vimesaidia kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

160. Mheshimiwa Spika; Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa Programu, Miradi na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hao wa Maendeleo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya Ulaya (EU), *Global Partnership for Education*, Shirika la Maendeleo la Uingereza (Foreign, Commonwealth and Development OfficeFCDO),

Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujeruman (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Nchi zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya ambazo ni Denmark, Ireland, Jamhuri ya Korea (KOICA) na Switzerland.

161. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa Miradi na Programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sehemu kubwa ya mafanikio ambayo Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepata katika uboreshaji huduma za afya, elimu na sekta nyingine za kiuchumi na kijamii yametokana na ushirikiano wa wananchi na Wadau mbalimbali wa Maendeleo.

162. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuishukuru Serikali kwa kukubali na kuweka kisheria mfumo wa ujenzi wa miundombinu kwa kutumia *Force Account* ambao umeokoa ghamama kubwa na kuwezesha upatikanaji wa mindombinu mingi kwa ghamama nafuu. Aidha, mfumo huu umeongeza ari ya wananchi kushiriki na kuchangia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekeliza katika maeneo yao na hivyo kufanya miradi hiyo kuwa endelevu.

163. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Kipekee, nawashukuru Naibu Mawaziri, *Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange*, Mbunge wa Jimbo la Wanging'ombe na *Mheshimiwa David Ernest Silinde*, Mbunge wa Jimbo la Tunduma, kwa msaada mkubwa wanaotoa kwangu katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Aidha, namshukuru *Katibu Mkuu, Prof. Riziki S. Shemdoe* kwa mchango wake katika kufanikisha maandalizi ya Mpango na Bajeti na Naibu Makatibu Wakuu *Bw. Gerald G. Mwelina Dkt. Grace E. Magembe* katika usimamizi wa majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Vilevile, nimpongeze Bi. Paulina

Mbena Nkwama Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuteuliwa katika nafasi hiyo. Aidha, ninawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

164. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais, *Mheshimiwa George Huruma Mkuchika (Mb)*, Waziri Ofisi ya Rais Kazi Maalum, *Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (Mb)*, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe *Deogratius Ndejemb*i Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais. Aidha, ninawashukuru *Dkt. Laurean Ndumbaro*, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, *Dkt. Moses Kusiluka Katibu Mkuu*, Ofisi ya Rais Ikulu na Dkt. Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao.

165. *Mheshimiwa Spika*, kwa namna ya pekee, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhandisi Hamadi Masauni (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba, Mlipaji Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao wanaoutoa katika maandalizi na utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

166. *Mheshimiwa Spika*, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

167. *Mheshimiwa Spika*, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Tanga MJINI kwa kunichagua kuwa Mbunge wao katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2020 na hivyo kuniwezesha kuweka historia ya kuwa Mbunge wa kwanza Mwanamke wa Jimbo hili toka lilipoanzishwa mwaka 1965. Ninawaahidi wana Tanga MJINI kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuifanya Tanga yetu ipate maendeleo zaidi ya kiuchumi na kijamii. Kipekee, ninaishukuru familia yangu kwa kuniombea na kwa uvumilivu wao muda wote ninapokuwa mbali nao katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kitaifa.

H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani

168. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/22, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa **26** na Halmashauri **184** inaomba idhini ya kukusanya Maduhuli na Mapato ya Ndani jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Tisa Kumi na Sita Milioni Mia Nne na Arobaini na Tano Mia Nne na Tisa Elfu Mia Moja Tisini na Nane (Shilingi 916,445,409,198)**, makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, ada za wanafunzi, tozo na ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Mapato ya Ndani kwa mwaka wa fedha 2021/22

O F I S I / T A A S I S I	M A K A D I R I O
O fisi ya Rais – TAMISEMI	4 , 5 0 0 , 0 0 0 . 0 0
T a a s i s i	5 2 , 3 6 2 , 2 2 5 , 8 8 6 . 0 0
M i k o a	2 2 0 , 6 8 3 , 3 1 2 . 0 0 . 0 0
H a l m a s h a u r i	8 6 3 , 8 5 8 , 0 0 0 , 0 0 0 . 0 0
J U M L A K U U	9 1 6 , 4 4 5 , 4 0 9 , 1 9 8 . 0 0

169. *Mheshimiwa Spika*; sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22 jumla ya **Shilingi Triliioni Saba Bilioni Mia Sita Themanini na Tatu Milioni Mia Tatu Ishirini na Tisa Mia Sita Arobaini na Nne Elfu na Mia Nane (Shilingi 7,683,329,644,800.00) kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 2 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri **184**.**

170. Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zinazoombwba, **Shilingi 4,728,008,207,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara **Shilingi 3,972,149,603,000.00** na **Shilingi 755,858,604,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,955,321,437,800.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 1,676,459,779,800.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,278,861,658,000.00** ni fedha za nje (*Mchanganuo wa fedha zinazoombwba katika mwaka wa fedha 2021/22 umeoneshwa katika Jedwali*

Na. 2 na Kiambatisho Na. 23, 24, 25 na 26).

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Makisio katika Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/22

A I N A Y A M A T U M I Z I	B A J E T I K W A M W A K A W A F E D H A 2 0 2 1 / 2 2
M a l u m i z i y a K a w a i d a O f i s i y a R a i s - T A M I S E M I	
M i s h a h a r a	
M i s h a h a r a M a k a o M a k u u	1 0 , 2 7 8 , 5 0 7 , 0 0 0 . 0 0
M i s h a h a r a y a T a a s i s i	4 7 , 2 3 5 , 9 9 1 , 0 0 0 . 0 0
J u m la M i s h a h a r a O f i s i y a R a i s - T A M I S E M I	5 7 , 5 1 4 , 4 9 8 , 0 0 0 . 0 0
M a l u m i z i M e n g i n e y o	
M a k a o M a k u u	1 0 , 0 5 4 , 2 8 4 , 0 0 0 . 0 0
T a a s i s i	1 , 3 1 8 , 8 7 0 , 0 0 0 . 0 0
J u m la y a M a t u m i z i M e n g i n e y o	1 1 , 3 7 3 , 1 5 4 , 0 0 0 . 0 0
J u m la M a t u m i z i y a K a w a i d a	6 8 , 8 8 7 , 6 5 2 , 0 0 0 . 0 0

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

AINA YA MATUMIZI	BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22
TUME YA UTUM ISHI WA WALIMU (TSC)	
Mishahara	7,760,568,000.00
Matumizi Mengineyo	6,608,202,000.00
Jumla ya Matumizi ya Kawaida TSC	14,368,770,000.00
M IKOA NA HALMASHAURI	
M IKOA:	
Mishahara	71,269,064,000.00
Matumizi Mengineyo	57,449,078,000.00
Jumla ya Matumizi ya Kawaida	128,718,142,000.00
H ALMASHAURI	
Mishahara	3,835,605,473,000.00
Matumizi Mengineyo (SK)	147,659,832,000.00
Matumizi Mengineyo (MSM)	532,768,338,000.00
Jumla Matumizi ya Kawaida	4,516,033,643,000.00
M IRADI YA MAENDELEO	
OFISI YA RAIS - TAMISEMI	
Fedha za Ndani	451,506,768,800.00
AINA YA MATUMIZI	BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22
Fedha za Nje	199,836,336,000.00
Jumla Maendeleo	651,343,104,800.00
TUME YA UTUM ISHI WA WALIMU	
Fedha za Ndani	500,000,000.00
Jumla	500,000,000.00
M IKOA	
Fedha za Ndani	62,942,998,000.00
Fedha za Nje	21,548,505,000.00
Jumla Maendeleo	84,491,503,000.00
H ALMASHAURI	
Fedha za Ndani (SK)	830,420,351,000.00
Fedha za Ndani (MSM)	331,089,662,000.00
Fedha za Nje	1,057,476,817,000.00
Jumla Maendeleo Halmashauri	2,218,986,830,000.00
JUMLA KUU	7,683,329,644,800.00

SK – Serikali Kuu na MSM – Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

171. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na. 2), Mikoa na Halmashauri (Mafungu 26) ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

172. *Mheshimiwa Spika*, hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz.

173. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri hoja imetolewa na imeungwa mkono na Serikali, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy kwa hotuba nzuri sana ambayo *ime-cut across* upana wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Sasa kabla hatujaendelea na matangazo mawili moja wale wasanii wetu wameambiwa wamekuja sasa wana majina magumumagumu lakini ngoja kuna mmoja ni Wansekula Roti Akadola, wale wasanii mpo huyu Dola hayupo msimame mmoja mmoja ahsante halafu yupo mwininge Leah Mwenda Mseke, yuko Mariane Mdee, yuko Romeo George, yuko Aboti Mandrake, yuko Irene Paul, yuko Shumbana Warwa, pia yuko Omari Tambwe karibuni sana wasanii wetu.

Tangazo la pili Waheshimiwa Wabunge, nanaomba tusikilizane vizuri, tarehe 22 siku ya Alhamisi tutapeana taarifa vizuri zaidi jioni kuanzia kwenye saa kumi jioni, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan atakuja hapa Bungeni kwa ajili ya kulihutubia Bunge, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais atakuja kulihutubia Bunge na kwa

maana hiyo na kuwahutubia wananchi wa Tanzania wote kuititia Bunge tarehe 22 siku ya Alhamisi kuanzia saa kumi jioni. Na baada ya hotuba yake, tutapata futari ya pamoja ambaye atakuwa ametuandalia yeche. (*Makofii*)

Futari hiyo itahusisha Wabunge wote, watumishi wa Bunge, na wageni waalikwa amba o watakuwa wamejaa kwenye *Gallery* wa kutoka sehemu mbalimbali kama mnavyojua Mheshimiwa Rais anapohutubia Bunge basi *Gallery* zetu zote zinajaa maana yake tunaarika mabalozi, Marais wastaa fu, na viongozi wengine wa ngazi mbalimbali wanakuwepo hapa Bungeni,

Kwa hiyo, kwa Mbunge anayetaka kusafiri nakuombia jaribu kushedo ratiba yako kwa namna ambayo siku hiyo ya Alhamisi jioni utakuwa hapa Dodoma. Na kwa Mbunge ambaye hayuko Dodoma tufanye juhudhi zote kuwarudisha Dodoma kwa ajili ya hotuba hiyo muhimu kwa Bunge na kwa Taifa. (*Makofii*)

Ahsante sasa nimuite Mwenyekiti wa kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa TAMISEMI Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Humprey Polepole karibu sana.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala.

SPIKA: Mheshimiwa Ane Kilango Malecela atakuwa mchangiaji wa kwanza baada tu ya Mheshimiwa Polepole

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Taarifa ya kamati Bunge ya utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati hii imepewa jukumu la kuisimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Aidha, Kifungu cha 7(1)(a), kimetoa kwa kamati jukumu mahususi la kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia vyema masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa siku zisizozidi saba, kabla ya kuanza uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla ya mafungu ishirini na nane (28) kama yanavyoonekana katika ukurasa wa pili wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha unaoanza, ulifanyika kuanzia tarehe 15 hadi 30 Machi, 2021. Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais - TAMISEMI inajikita katika maeneo manne (4) yafuatayo: -

- (i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi iliyotembelewa na Kamati;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika ninaomba taarifa yote hii iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ufanuzi wa Miradi iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ziliidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi 2,289,919,896,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ili kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelzwa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyotembelewa ni pamoja na Ujenzi wa Barabara ya Shekilango, Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali na Uwezeshaji kiuchumi Wanawake, Vijana na watu Wenye Ulemavu kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri, maelezo kuhusu miradi iliyotembelewa mafanikio na changamoto kama ilivyoonekana katika ukurasa wanne hadi wa kumi na moja wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya mwaka wa fedha 2021 kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi katika Mikoa ya Dar es Salaam Pwani na Morogoro kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali ningependa kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(i) Ukarabati mkubwa wa Shule Kongwe za Sekondari umerejesha hadhi ya shule hizo na kuboresha mazingira ya kufundishia kwa walimu na kujifundishia kwa wanafunzi hivyo kuongeza morali ya kazi na ari ya kusoma;

(ii) Matumizi ya *force account* katika ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari kwa sehemu kubwa yameleta tija ikilinganishwa na kutumia wakandarasi hata hivyo, umakini zaidi unahitajika kuhusu viwango vya ufundi na ubora vinavyotumika;

(iii) Hakuna uwiano wa kiasi cha fedha kilichotolewa na ubora wa kazi iliyofanyika katika ukarabati wa baadhi wa Shule Kongwe za Sekondari;

(iv) Ucheleweshwaji wa malipo ya Wakandarasi unachangia kucheleweshwa utekelezaji wa kukamilisha kwa miradi. Aidha, utaratibu huo unaitia hasara Serikali kwa kulipa faini kutokana na ucheleweshwaji wa malipo;

(v) Mikopo ya asilimia kumi ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu imechangia kuyainua kiuchumi makundi hayo hata hivyo umakini zaidi unahitaji katika kusimamia sheria na kanuni za utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo;

(vi) Mikopo ya asilimia kumi ya mapato ya ndani ya halmashauri ikisimamiwa nakuratibila vizuri, inaweza kutumika kuhamasisha uanzishwaji wa miradi mikubwa kama viwanda, kilimo cha kisasa makampuni nakadhalika na hivyo kuondoa utoaji wa mikopo midogo ambayo tija yake ni ndogo.

(vii) Idara ya Maendeleo ya Jamii Ustawi wa jamii na biashara hazijatumika kikamilifu katika kuelemisha na kusaidia makundi yanayonufaika na fedha asilimia kumi ya mapato ya ndani ya halmashauri.

(viii) Kukosekana kwa umakini katika usanifu wa awali wa miradi ya maendeleo kuna athiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama kutokana kuongeza kazi na

(ix) Serikali iweke utaratibu wa kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi inayotengewa fedha ili kuepusha ubadirifu na hivyo kuwezesha kupatikana kwa thamani ya fedha ya *value for money*.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati katika mwaka wa fedha 2020/2021, uchambuzi wa kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais

- TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Njia kubwa zilizotumika kwa uchambuzi ni kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa ufanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zillizo chini yake kwa kifupi nasema ni (*LGTI, KEC, DART na LGLB*) ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 45,787,792,148 katika vyanzo vya ndani. Mapato hayo yanatokana na kuuza vifaa chakavu na zabuni kwa upande wa makao makuu (Fungu 56) na ada za wanafunzi, ukusanyaji wa madeni, tozo, ushuru na mauzo ya bidhaa mbalimbali kwa upande wa taasisi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2021 kiasi cha Shilingi 22,775,536,917.37 kilikuwa kimekusanya, sawa na asilimia 49.76 ya malengo yaliyowekwa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa:-

(i) Ofisi ya Rais – TAMISEMI Makao Makuu haikukusanya kiasi chochote kutokana na kutouza nyaraka za zabuni au vifaa chakavu;

(ii) Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA) ndiyo uliongoza katika makusanyo ya taasisi kwa kukusanya kwa asilimia 55;

(iii) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ilifanya vibaya zaidi kwa kukusanya kwa asilimia 11 tu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa kimepungua kwa asilimia 30.44 ikilinganishwa na asilimia 80.2 iliyoshuhudiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kiwango hicho cha makusanyo kinaonesha kwamba, wastani wa makusanyo kwa kila robo ulikuwa asilimia 16.59 ambayo ni chini ya wastani wa asilimia 25 ambao unapaswa kufikiwa kwa kila robo ya mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikoa hadi kufikia mwezi Februari, 2021 makusanyo yalikuwa ni Shilingi 74,451,560 kiasi ambacho ni sawa na asilimia 36 ya lengo liliowekwa. Kiasi hicho kimepungua kwa asilimia 3 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, aldha, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya Shilingi 814,683,049,426 na hadi kufikia mwezi Februari, 2021 zilikuwa zimekusanya asilimia 61 ya lengo liliokusudiwa. Wastani wa makusanyo kwa TAMISEMI Makao Makuu na Taasisi zake, Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi hicho ulifikia asilimia 48.92 kiwango ambacho kimepungua kwa takribani asilimia 8.6 ikilinganishwa na wastani uliofikiwa katika mwaka wa fedha uliopita. Kamati imebaini kwamba, halmashauri zimeendelea kuwa na makusanyo mengi ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na wigo mkubwa wa vyanzo vya mapato na idadi kubwa ya watu, ambavyo ni muhimu katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI umebaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2020/21 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba: -

(i) Fedha zinazotolewa ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (*cash flow plan*) uliowekwa zimepungua ikilinganishwa na miaka mingine;

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wingi (asilimia 80) ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo (asilimia 30); na

(iii) Fedha za Maendeleo za Ndani zinatolewa kwa kiasi kikubwa (asilima 62) ikilinganishwa na fedha za maendeleo za nje (asilimia 2).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea Shilingi 384,545,560,071/= kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 54 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kwamba, kiasi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 19.4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo kiasi kilichopatikana kilikuwa ni asilimia 73.4.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2021 Ofisi hiyo na taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 103,793,363,125 sawa na asilimia 80 ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimeongezeka kwa asilimia 26.2 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambacho kilikuwa asilimia 53.8. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo Kamati ilibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya shilingi 280,752,196,946, sawa na asilimia 49 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 27.1 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2019/2020 ambacho kilikuwa ni asilimia 76.1.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na.02) katika mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 14,773,473,000/= kwa ajili ya matumizi ya

kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 8,165,271,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 6,108,202,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea shilingi 7,655,467,644 sawa na asilimia 52 ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi 4,136,302,674 ni kwa ajili ya mishahara, na Shilingi 3,519,164,969/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, hakuna fedha yoyote iliyotolewa kwa fungu hili kuhusiana na maendeleo licha ya kuwa na bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2020/2021 ziliidhinishwa bajeti ya Shilingi 6,021,005,090,076 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi 4,616,009,739,686 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,404,995,350,389 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Shilingi 3,400,948,706,511 zilikuwa zimepokelewa hii ikiwa ni sawa na asilimia 56 ya bajeti yote iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo shilingi 2,837,372,867,996 sawa na asilimia 61 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo ziliikuwa shilingi 563,575,838,514 sawa na asilimia 40. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba fedha za maendeleo za ndani zilitolewa kwa kiwango kikubwa (asilimia 52) ikilinganishwa na fedha za nje ambazo zilipatikana kwa asilimia 2 tu. Hii ni ishara njema kwamba, miradi ya maendeleo inaweza kutekelezwa kwa uhakika zaidi kwa fedha za ndani kuliko kutegemea fedha za nje ambazo hazina uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina wa Kamati umberaini kwamba kwa wastani upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake katika mwaka wa fedha 2020/2021 ulikuwa ni asilimia 57.52, kiwango ambacho kimepungua ikilinganishwa na wastani wa asilimia 64.95 katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Aidha, wastani huo wa upatikanaji fedha katika kipindi kama hicho cha bajeti, ikiwa ni takribani robo ya tatu ya mwaka wa fedha, ni chini ya kiwango cha angalau asilimia 25 ambacho kinatakiwa kwa kila robo katika mwaka wa fedha. Kiwango hicho ni sawa na wastani wa asilimia 19.17 kwa robo mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, uchambuzi umebaini kwamba, wastani wa upatikanaji wa fedha ulikuwa ni kwa asilimia 50.5.

Aidha, bado fedha za matumizi ya kawaida zimeendelea kupatikana kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamkala za Serikali za Mitaa na kiasi kilichopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2021, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Miradi ya Maendeleo. Ufafanuzi zaidi kwa baadhi ya maeneo hayo umeoneshwa kupitia Jedwali Na. 02 & Jedwali Na.03

Mheshimiwa Spika, Mapito ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati katika uchambuzi na mapitio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo kumi na tatu (13) ili ofisi hii iyazingatie katika utekelezaji wa vipaumbele vyake vya bajeti ili kuongeza ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhishwa na jitihada zilizooneshwa katika kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati kwa kutatua changamoto zilizobainishwa. Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati umechangia katika uboreshaji wa huduma za msingi kwa wananchi na maendeleo ya jamii. Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanya kazi maoni na ushauri kwa baadhi ya maeneo yaliyosalia ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na:-

(i) Halmashauri kusaidia Vikundi nya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kutumia fedha za mapato ya ndani kuanzisha miradi mikubwa ya maendeleo ili kutoa ajira na kuchangia mapato ya Serikali. Mfano ni Viwanda nya kutengeneza Samani nya *STAMICO* na *ALLELUYA* nya mji mdogo wa Katoro Geita vyenye thamani ya Shilingi milioni 100; na

(ii) Halmashauri kubuni vyanjo vipyta nya mapati ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu ambapo halmashauri 30 zimebuni jumla ya miradi ya kimkakati 38 yenye thamani ya Shilingi bilioni 273 ambayo utekelezaji wake huko katika hatua mbalimbali kukamilika miradi hiyo kutachangia kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, licha ya baadhi ya maoni kufanyiwa kazi na Serikali bado kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kuhahikisha Halmashauri zinazodaiwa na benki mikopo ya Waheshimiwa Madiwani iliyotolewa na dhamana ya posho ya kila mwezi zinakamilisha ulipaji wa madeni hayo baadhi ya Mikoa ambayo halmashauri zake hazijakamilisha ulipaji wa madeni hayo ni Simiyu, Ruvuma, Singida Geita na Morogoro;

(ii) Kuhakikisha halmashauri zinasimamia kikamilifu ulejeshaji wa fedha za mikopo kutokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani ya halmashauri inayopelekwa kwenye vikundi nya wanawake vijana na watu wenye ulemavu;

(iii) Kuhakikisha halmashauri zinatenga na kupeleka kikamilifu fedha za asilimia 40 na 60 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwenye miradi ya maendeleo;

(iv) TARURA kuendelea kuongezewa fedha na Serikali ili kuwezesha kuhudumia mtandao mkubwa wa barabara zaidi ya 144,000 iliyochini yake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na:-

(i) Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

(ii) Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;

(iii) Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020;

(iv) Hotuba ya Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwenye uzinduzi wa Bunge la Kumi na Mbili; na

(v) Maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa, Sera, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati ya Taasisi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 7,683,329,644,800. Kati ya fedha hizo, Sh. 4,728,008,207,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.2,955,321,437,800 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, Sh.3,972,149,603,000 sawa na asilimia 51.67 ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara, na Sh.755,858,604,000 sawa na asilimia 9.84 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Bajeti ya maendeleo ni sawa na asilimia 34.46

ya bajeti yote ya ofisi hii. Ufafanuzi zaidi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 04.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinakadiria kukusanya jumla ya Sh.916,445,409,198. Mapato hayo yameongezeka kwa asilimia 6.48 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa Sh.860,678,914,502/=. Ulinganisho wa makusanyo kati ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 na 2021/2022 umefafanuliwa zaidi katika Jedwali Na. 05.

Mheshimiwa Spika, makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na uuzaji wa kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, mauzo ya huduma, ada za wanafunzi na tozo kwa makao makuu na taasisi zake. Aidha, kwa upande wa halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivypopo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati, makusanyo yote yanatarajiwa kuongezeka kwa Sh.55,766,494,696 (sawa na asilimia 6.48) ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha unaomalizika. Ongezeko hilo limepungua kwa asilimia 1.52 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 8 katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Ingawa kiwango cha ongezeko la makusanyo kwa upande wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na taasisi zake kimepungua kutoka asilimia 45 hadi hadi asilimia 15, bado ongezeko hilo ni kubwa ikilinganishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, na mikoa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa pili mfululizo Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini (*TARURA*) utachangia kwa kiwango kikubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ikilinganishwa na taasisi nyingine chini ya TAMISEMI. Sababu kubwa ya ongezeko hili kuwepo kwa Kanuni za ukusanyaji wa tozo ya maegesho ya magari itakayoruhusu mapato kukusanywa katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, bado halmashauri zinatarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na maduhuli yake kuongezeka kwa shilingi 48,897,009,924 sawa na takribani asilimia 6 ikilinganishwa na makusanyo ya halmashauri katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho cha ongezeko kimeitungua kwa asilimia 0.47 ikilinganishwa na mwaka unaomalizika. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, huenda kuna ulegevu katika matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo, Serikali itazame mwenendo wa matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato, sambamba na kuhamasisha mamlaka hizo kubuni vyanzo vipyta vya mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa pamoja zinaomba kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya Sh.7,683,329,644,800/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa. Kati ya fedha hizo, Sh.4,728,008,207,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.2,955,321,437,800/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika fedha hizo zinazoombwaa kuidhinishwa na Bunge, Sh.14, 868,770,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu – Fungu 02. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia 4.17 ikilinganishwa na Sh.14,273,473,000 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake bajeti inayoombwaa kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeongezeka kwa Sh.663,529,291,800 sawa na asilimia 9.45 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaomalizika wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la asilimia 29.06 kutoka Sh.2,289,919,896,000/= kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi Sh.2,955, 321,437,800/= katika mwaka wa fedha ujao. Uchambuzi zaidi umebaini kwamba, ongezeko la bajeti kwa ujumla wake, limetokana na Serikali kuongeza fedha za maendeleo kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu nchini na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kulinganisha Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, uchambuzi wa Kamati umebaini kuna ongezeko katika pande zote mbili. Hata hivyo, ongezeko la bajeti ya Taifa ni dogo kwani ni asilimia 3.95 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021, wakati ongezeko la Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika kipindi hicho ni asilimia 9.45.

Mheshimiwa Sppika, aidha, bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni sawa na asilimia 21.19 ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeongezeka kwa asilimia 1.06 ikilinganishwa na uwiano katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ambao ulikuwa ni asilimia 20.13. Ulinganisho zaidi wa Uwiano wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Bajeti ya Taifa umefafanuliwa zaidi kupitia Jedwali Na. 06.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuongeza bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwani inaonesha kutambua na kuthamini umuhimu wa ofisi hii ambayo ina jukumu la kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohudumia na kugusa wananchi moja kwa moja na hivyo kuunga mkono juhudhi zao katika shughuli za maendeleo. Ni rai ya Kamati kwamba, fedha zitakazoidhinishwa zitolewe na kupelekwa kwa wakati ili kuwezesha kutekelezwa kwa shughuli zilizokusudiwa. Aidha, kuwe na usimamizi na udhibiti mzuri wa matumizi ya fedha hizo ili kuwezesha kupatikana kwa tija na thamani ya fedha kwa shughuli zitakazotekelzwa, sambamba na kuzuia ubadhirifu. (*Makofu*)

Mheshimiwa Spika, aidha, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa umefafanuliwa zaidi kupitia Jedwali Na. 07 ambalo ni Kiambatisho A cha Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya maendeleo na kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

SPIKA: Bado dakika tano.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, moja, Ofisi ya Rais – TAMISEMI izisimamie kikamilifu Halmashauri nchini ili kuhakikisha zinaongeza makusanyo kwa kuweka malengo halisia. Uchambuzi umebaini kwamba, kumekuwa na ongezeko dogo la malengo ya ukusanyaji kutoka mwaka mmoja wa fedha hadi mwingine na wakati mwingine lengo hilo limekuwa halifikiwi kikamilifu licha ya kuwa dogo.

Mheshimiwa Spika, pili, Ofisi ya Rais – TAMISEMI isimamie na kuhakikisha halmashauri nchini zinatenga fedha kwa ajili ya miradi ya barabara ili kuunga mkono na kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (*TARURA*). Kabla ya kuanzishwa *TARURA*, halmashauri zilitenga bajeti ya kuhudumia barabara katika maeneo yake, hata hivyo, nyangi zimeacha jukumu hilo kwa *TARURA* pekee ambayo ina bajeti finyu.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iandae Kanuni za kuiwezesha *TARURA* kuwa na nguvu ya kisheria ya kukusanya ushuru wa maegesho katika maeneo mbalimbali nchini. Wakala hii imekuwa ikifanya kazi vizuri katika kukusanya ushuru wa maegesho, licha ya kukumbana na changamoto

za ukusanyaji kutoka kwa baadhi ya halmashauri na taasisi za umma kutokana na kutokuwepo na mwongozo wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali isimamie kikamilifu halmashauri zinazokiuka kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kuhusu utengaji na utoaji wa fedha za 10% ya mapato ya ndani ili kuwezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Mikoa ya Lindi, Njombe na Morogoro pekee ndiyo iliyozingatia utoaji wa asilimia 10 kwa ukamilifu.

Aidha, Mikoa ya Lindi na Singida ilitoa halmashauri tatu zilizooongoza katika utengaji na utoaji wa fedha za asilimia 10. Kwa upande mwingine, Mikoa ya Dodoma, Ruvuma na Manyara ilitoa halmashauri tatu zillzofanya vibaya zaidi katika utengaji na utoaji wa asilimia 10. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tano, halmashauri ziendelee kubuni na kutekeleza vyanzo vipyta vya mapato ili kuongeza wigo wa mapato Serikalini na hivyo kuepuka kadhia ya kuongeza kodi mara kwa mara kwenye vyanzo vilevile, jambo linalokera wananchi. Aidha, kuwe na udhibiti katika matumizi ya fedha za mapato yatakayokusanywa ili kuwezesha kufikiwa kwa tija na malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa. Mionganoni mwa njia za kuongeza mapato ni kubuni miradi ya kimkakati, kuandaa maandiko na kuyawasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI ili kuyaombea fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimeomba taarifa hii ichukuliwe yote kwenye Taarifa za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, sita, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihamasishe na kuzisaidia kaya zinazohitimu au ku-graduate kutoka kwenye Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) kuunda vikundi ili kutumia fedha za asilimia kumi ya mapato ya ndani kuanzisha miradi ya kiuchumi itakayowapatia ajira na uhakika wa kipato.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali ichukue hatua ili kurekebisha hali ya kukosekana kwa ulinganifu baina ya fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za sekondari nchini na kazi ya ukarabati iliyofanyika. Ziara ya ukaguzi wa Kamati katika baadhi ya shule zilizokarabatiwa ilibaini kwamba, kiasi cha fedha kilichotolewa ni kikubwa ikilinganishwa na kiwango na ubora wa kazi zilizofanyika. Aidha, shule zote ambazo ukarabati wake ulianza kutekelezwa na Wakala wa Majengo (*TBA*), ukarabati wake haukukamilika na hakukuwa na taarifa kuhusiana na gharama za mradi (*BOQ*), jambo lililosababisha iwe vigumu kufanya tathmini ya gharama halisi za mradi. Vilevile, Kamati imebaini kwamba matumizi ya *Force Account* katika utekelezaji wa miradi ya Serikali ikiwa ni pamoja na ukarabati wa shule kongwe za sekondari yameleta tija ikilinganishwa na matumizi ya wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru sana kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli kwamba, Kamati hii ndiyo inayoshughulikia mafungu mengi ya bajeti (36) ikilinganishwa na Kamati nyingine za Bunge na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa muda mrefu na wakati mwингine hadi usiku wa manane. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, hii ikiashiria utayari wao wa kulitumikia Bunge, Taifa na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalim, mwanamama shupavu, kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake. Utendaji wake na Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa David Ernest Silinde na Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange umedhihirisha jinsi walivyo hazina kubwa kwa ustawi na maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini na maendeleo ya Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Prof. Riziki Shemdoe, akisaidiana na Naibu Makatibu Wakuu, Ndg. Gerald Mweli na Dkt. Grace Maghembe, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Rais - TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, shukrani za Kamati ziwaendee pia Wakuu wa Mikoa yote nchini, Sekretarieti za Mikoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati katika kipindi chote alichohudumu katika wadhifa huo. Alifanya kazi na Kamati kwa moyo wa kujituma na weledi wa kiwango cha juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndg. Gerald Magili; Makatibu

wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima na Ndg. Rabisante Moshi, wakisaidiwa na Ndg. Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati hii imepewa jukumu la kuisimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya

Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR - MUUB) pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Aidha, Kifungu cha 7(1) (a), kimetoa kwa Kamati jukumu mahususi la kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia vyema masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa siku zisizozidi saba (7), kabla ya kuanza uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla ya mafungu ishirini na nane (28) yafuatayo: -

- i. Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- ii. Fungu 02 - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC);
- iii. Fungu 36 – Mkoa wa Katavi;
- iv. Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu;
- v. Fungu 54 – Mkoa wa Njombe;
- vi. Fungu 63 – Mkoa wa Geita;
- vii. Fungu 70 – Mkoa wa Arusha;
- viii. Fungu 71 – Mkoa wa Pwani;
- ix. Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma;
- x. Fungu 73 – Mkoa wa Iringa;
- xi. Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma;
- xii. Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro;
- xiii. Fungu 76 – Mkoa wa Lindi;
- xiv. Fungu 77 – Mkoa wa Mara;
- xv. Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya;
- xvi. Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro;
- xvii. Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara;
- xviii. Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza;
- xix. Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma;
- xx. Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga;
- xxi. Fungu 84 – Mkoa wa Singida;
- xxii. Fungu 85 – Mkoa wa Tabora;
- xxiii. Fungu 86 – Mkoa wa Tanga;

- xxiv. Fungu 87 – Mkoa wa Kagera;
- xxv. Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam;
- xxvi. Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa;
- xxvii. Fungu 90 – Mkoa wa Songwe; na
- xxviii. Fungu 95 – Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha unaoanza, ulifanyika kuanzia tarehe 15 hadi 30 Machi, 2021. Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne (4) yafuatayo: -

- (i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi iliyotembelewa na Kamati;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWAMWAKA WA FEDHA 2020/2021

2.1 Ufafanuzi wa Miradi iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ziliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 2,289,919,896,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ili kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi iliyotekelawa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2020/2021. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na Ujenzi wa Barabara ya Shekilango, Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali na Uwezeshaji kiuchumi Wanawake,

Vijana na Wenyewe Ulemavu kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri,kama ifuatavyo:-

2.1.1 Ujenzi wa Barabara ya Shekilango

Mheshimiwa Spika, huu ni miongoni mwa miradi 8 inayotekelawa na Manispaa ya Kinondoni katika Jiji la Dar es Salaam chini ya Mpango wa Kuendeleza Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Mradi unajumuisha kilomita 6.3 za barabara ngumu ya lami ikiwemo kubwa ya Shekilango yenye njia nne (km 3.65) na ndogo nne (Akachube (0.94 km); Igese (0.64 km); Mori (0.93 km) na TRA (1.09 km) umegharimu jumla ya **shilingi bilioni 26.2** na ulipangwa kuchukua miezi 12, kuanzia Juni, 2019 hadi Disemba, 2020. Hata hivyo, kutokana na changamoto kubwa ya mvua katika mwaka uliopita Mkandarasi aliongezewa muda wa miezi miwili, na hivyo mradi ulikamilika mwanzoni mwa Machi, 2021.

Shughuli nyingine zilizotekelawa katika mradi huu ni uwekaji wa taa 280 za barabarani zinazotumia umeme wa juu, taa za kuongozea magari katika makutano ya Barabara ya Shekilango na Barabara ya Simu 2000, ujenzi wa madaraja, mifereji ya maji, njia za watembæa kwa miguu na uhamishaji wa miundombinu ya umeme TANESCO, maji (DAWASCO) na simu (TTCL).

2.1.2 Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari ni utaratibu unaotekelawa na Serikali kwa lengo la kurejesha shule hizo katika hali nzuri itakayowezesha Walimu kufundisha na Wanafunzi kujifunzia katika mazingira bora. Mpango huo ulioanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 unajumuisha shule Kongwe za Sekondari zipatazo 89 na unatekelezwa kwa awamu. Kamati ilitembelea mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro ili kukagua utekelezaji wa mradi huu kama ifuatavyo:-

(a) Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Jangwani

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa shule hii ambayo ilijengwa mwaka 1928 wakati wa ukoloni wa Uingereza, ulianza mwaka 2017 na kutekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilitekelezwa na Wakala wa Majengo - TBA kwa gharama ya **shilingi milioni 944.57** kwa kukarabati hosteli, bwalo la chakula, jiko, maabara 3 na madarasa 26, maktaba, vyoo vya walimu na wanafunzi, ofisi ya walimu, na ofisi ya mhasibu na usajili.

Hata hivyo, kutokana na kazi iliyotekelawa kutokuwa ya kuridhisha ikiwa ni pamoja na kutokuwa na gharama za mradi (BOQ), Mkandarasi huyo aliondolewa na awamu ya pili ya ukarabati ilitekelezwa kwa utaratibu wa Force Account chini ya usimamizi wa Kamati mbalimbali za shule.

Kazi zilizotekelawa katika awamu ya pili ya ukarabati ambayo iligharimu jumla ya **shilingi milioni 76** ni ukarabati wa ofisi ya Mwalimu Mkuu, na Makamu Mkuu wa Shule, ofisi ya mhasibu, maabara 3 hosteli, jiko na kuweka milango ya vyoo, zahanati na resource room.

Aidha, shule ilipokea **shilingi milioni 95.4** kutoka Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) katika awamu hii ya ukarabati ambayo pia imehusisha ujenzi wa mabweni mapya mawili na hivyo kuongeza nafasi ya malazi kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na ukarabati katika shule hii, hasa ule uliotekelawa katika awamu ya kwanza na TBA kwani hauoneshi thamani halisi ya fedha iliyotumika na haukuwa na gharama ya mradi (BOQ), hivyo kuielekeza OR – TAMISEMI kuandaa ripoti maalum na kuiwasilisha kwenye Kamati kabla ya kukamilika kwa Bunge hili.

(b) Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Azania

Mheshimiwa Spika, shule hii ilianzishwa mwaka 1933 chini ya raia wa Tanganyika wenye asili ya Asia hadi ilipotaifishwa na Serikali na kubadilishwa jina kuwa Azania mwaka 1952.

Ukarabati wa shule hii ulifanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza ilifanyika kuanzia Septemba, 2017 hadi Januari, 2019 na ilitekelezwa na Wakala wa Majengo - TBA kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.4** na kuhusisha madarasa, ukumbi, maabara, bwalo na jiko, ingawa ukarabati haukukukamilika jambo lilirosababisha Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuvunja mkataba na TBA kutokana na kutoridhishwa na kazi. Aidha, awamu ya pili ya ukarabati ambayo ilitekelezwa kwa utaratibu wa Force Account chini ya usimamizi wa kamati za shule na kugharimu jumla ya **shilingi milioni 140.5** ilianza Julai 2019 na bado inaendelea kwa kuhusisha ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa shule, makamu mkuu wa shule, ofisi ya mhasibu na nidhamu, ukumbi, maabara 3, idara za biashara, uchoraji, jiografia na hesabu, madarasa, maktaba na zahanati.

Mheshimiwa Spika, bado kuna maeneo hayajaguswa na ukarabati hivyo, Serikali iendelee kutoa fedha ili kuwezesha zoezi la ukarabati kugusa maeneo yote muhimu ya shule.

(c) Ukarabari wa Shule ya Sekondari ya Kibaha

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa shule hii ulianza mwaka 2017 na kutekelezwa kwa awamu mbili. Katika awamu ya kwanza ambayo ilitekelezwa na Wakala wa Majengo – TBA, mabweni matano (5) na vyumba kumi na tatu (13) vya kulala wanafunzi vilikarabatiwa. Mradi huu ulisimama kwa mwaka mzima ndipo Serikali iliama kuwanyang'anya TBA na kuukabidhi kwa uongozi wa shule.

Katika awamu ya pili ya mradi ambayo ilianza kutekelezwa Novemba, 2019 kwa utaratibu wa Force Account chini ya usimamizi wa Kamati mbalimbali za shule, jumla ya **shilingi bilioni 1.19** zilitumika kwa ajili ya ukarabati wa madarasa, maabara nne (4), jengo la utawala, maktaba, bwalo na jiko, mabweni matatu na ofisi za walimu tatu.

Mheshimiwa Spika, pia katika shule hii Kamati haikuridhishwa na ukarabati hasa ule uliotekeliza katika awamu ya kwanza na TBA kwani hauoneshi thamani halisi ya fedha iliyotumika na haukuwa na gharama ya mradi (BOQ), hivyo kuielekeza

OR – TAMISEMI kuandaa ripoti maalum na kuiwasilisha kwenye Kamati kabla ya kukamilika kwa Bunge hili.

(d) Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Kilakala

Mheshimiwa Spika, shule hii ilianzishwa mwaka 1957 na Watawa wa Kanisa Katoliki wa Shirika la Mary Knoll kutoka nchini Marekani na awali ilijulikana kama Marian College hadi mwaka 1970 ilipotaifishwa na Serikali na kubadilishwa jina kuwa Sekondari ya Kilakala kwa ajili ya Wasichana.

Ukarabati wa shule hii ulifanyika katika awamu mbili ambazo zote zilitkelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC); awamu ya kwanza ilifanyika kuanzia Juni, 2017 hadi Aprili, 2020 Januari, 2019 kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.12**. Maeneo yaliyofanyiwa ukarabati ni jengo la utawala, madarasa 8, mabweni 13, bwalo, maabara 6 na sehemu ya kufulia nguo.

Katika awamu ya pili ambayo ilianza Aprili, 2020 jumla ya **shilingi milioni 42.92** zilitolewa mwezi Aprili, 2020 kwa ajili ya umaliziaji wa mifumo ya ndani ya maabara ya baiolojia kwa kuweka mfumo wa maji safi na maji taka, samani, feni, mfumo wa gesi n.k.

Aidha, Mwezi Juni, 2020 Serikali iliongeza **shilingi milioni 100** kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la chakula ambalo hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu ulikuwa unaendelea ukiwa umefikia asilimia 25.

(e) Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Mzumbe

Mheshimiwa Spika, shule hii ilianza kama Bush School “shule ya watu weusi” huko Kibiti, Delta ya Rufiji, Kusini mwa Dar es Salaam mwaka 1923

Mwaka 1930 ilihamishiwa Dar es Salaam eneo ilipo Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko hivi sasa, na ilipofika mwaka 1953 shule ilihamishiwa Morogoro mahali ilipo sasa kama Middle School na ilipofika mwaka 1957 ilisajiliwa kuwa shule ya Sekondari.

Ukarabari wa shule hii ulianza Juni, 2017 na ulitekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.22** na kuhusisha madarasa 19, maabara ya kompyuta, mabweni 22, ukumbi wa mikutano, bwalo la chakula na jiko, na majengo matatu ya utawala.

2.1.3 Uwezeshaji kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hii unatokana na uzingatiaji wa Kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya **shilingi bilioni 64.5** zilitengwa na Halmashauri zote nchini kwa ajili ya vikundi 18,244 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa

RUNDI	IDADI YA VIKUNDI	KIASI TENGWA
Wanawake Vijana Halmashauri iliyoitengwa kwa ajili ya Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu Watu wenye Ulemavu	8,223 6,966 3,053	Tsh. Bilioni 25.8. Tsh. Bilioni 25.8 Tsh. Bilioni 12.9
JUMLA	18,244	Tsh. Bilioni 64.5

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa utoaji wa mikopo kwa makundi hayo Kamati ilitembelea Vikundi vya Kasi Mpya Silk kinachofuma Masweta na Smart Score kinachozoa taka, vyote katika Manispaa ya Morogoro. Aidha, Kamati ilitembelea Kikundi cha Ajira (Ajira Gropu) eneo la Sangasanga Mvomero kinachojihusisha na masuala ya chakula na lishe kwa kusindika na kuza vyakula ndani na nje ya Mkoa wa Morogoro.

(a) Kikundi cha Kasi Mpya Silk (Ufumaji Masweta)

Mheshimiwa Spika, Kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2014 kikiwa na wanachama 30 na kusajiriwa na Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya kujishughulisha na silk (ufumaji wa nyuzi za Hariri). Mwaka 2018 kiliamua kuanzisha mradi wa ufumaji wa masweta kikiwa kimebaki na wanachama 12 baada ya wengine kujitoa.

Kikundi hiki kimenufaika na mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kupatiwa mkopo wa **shilingi milioni 36.7** ambao kimeutumia kununua mashine za kisasa tano (5), kununua malighafi na kuajiri wafanyakazi wanne (4). Kikundi kimefanikiwa kupata tenda kwenye shule 11 katи ya hizo shule 6 ziko ndani ya Manispaa ya Morogoro na shule tano (5) za Mkoani Mbeya.

(b) Kikundi cha Smart Score (Utunzaji wa Mazingira)

Mheshimiwa Spika, kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2015 na wanachama 30 wote wakiwa ni wahitimu wa chuo kikuu kwa lengo la kujikita katika kilimo. Mwaka 2017 kikundi kikiwa kimebaki na wanachama watano (5) kiliamua kusajili kampuni ijulikanayo kama **M2 - SMART COMPANY** kwa lengo la kujishughulisha na usafi na utunzaji wa mazingira.

Kikundi hiki kimekuwa kikinufaika na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa kuanza na mkopo wa **shilingi milioni 2** mwaka 2015 na kuendelea kuongeza kiwango kila kilipokamilisha marejesho ya mkopo.

Katika mwaka 2021 kikundi kimekopeshwa **shilingi milioni 20** ambazo zitatumika kuongeza vifaa vya kuzolea taka, kuajiri vijana 50 ili kuhudumia maeneo ya kazi katika mitaa mitatu na uzoaji wa taka katika maeneo mapya ambayo ni makazi ya watu, ofisi na majengo ya biashara katika kata ya Mazimbu kwa kusaini mkataba wa miaka mitatu.

Aidha, kikundi kitatumia sehemu ya mkopo huo kuanzisha mradi wa kuzalisha chaki katika Mtaa wa Ngerengere, Kata ya Kihonda Maghorofani ambao utachangia kuongeza mapato ya kikundi na kutoa ajira zaidi.

(c) Kikundi cha Ajira Group (Usindikaji wa vyakula)

Mheshimiwa Spika, kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2018 kikiwa na wanachama 8 na kusajiriwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kwa ajili ya kujishughulisha na masuala ya chakula na lishe, hususan usindikaji wa vyakula.

Mwaka 2020 kikundi 18 kiliamua kuanzisha mradi wa ufumaji wa masweta kikiwa kimebaki na wanachama 12 baada yaw engine kujitoa.

Kikundi hiki kimenufaika na mkopo wa **shilingi milioni 8** kilioupara mwaka 2020 ambao umekisaidia kununua mashine za kusaga na kusindika vyakula na kuvisambaza katika maduka "min supermarkets" ndani ya nje ya Mkoa wa Morogoro.

Kikundi hicho ambacho sasa kimebakiwa na Wanachama watano (5) baada ya wengine kuhamia nje ya Mvomero, kina mpango wa kujenga jengo lake kwa ajili ya usindikaji wa vyakula na duka, ili kiweze kupata hati na nambari ya utambulisho kutoka shirika la viwango la taifa (TBS).

2.2 Matokeo ya Ulaguzi

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo hiyo inayotekelizwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika mwaka wa fedha 2020/2021, naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tufuku kuhusu mambo ambayo Kamati iliyabaini kama ifuatavyo: -

2.2.1 Ujenzi wa Barabara ya Shekilango

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa mradi huu katika Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam ulibaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

(a) Mafanikio

i. Kuokolewa kwa **shilingi bilioni 5.94** kutokana na usimamizi mzuri wa mradi, mbazo zinajenga mifereji ya maji ya urefu

wa kilomita 9 katika eneo la Mbweni ili kuondoa shida ya mafuriko katika eneo hilo;

ii. Ajira kwa wananchi 200 katika kipindi cha utekelezaji wa mradi;

iii. Adha ya mafuriko imepungua katika maeneo yaliyopitiwa na mradi kutokana na ujenzi wa mifereji ya maji;

iv. Kuongezeka kwa usalama kwa watumiaji wa barabara kutokana na njia za waenda kwa miguu (walk ways) na taa za kuongezea magari; na

v. Barabara imesaidia kupunguza msongamano wa magari katika Barabara za Ali Hassan Mwinyi, Morogoro na Mandela.

(a) **Changamoto;**

i. Mkandarasi kutolipwa madai yake kwa wakati;

ii. Shughuli za ujenzi kuchelewa kukamilika kutokana na mvua nyingi;

iii. Kutopatikana kwa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kumeathiri utekelezaji wa mradi; na

iv. Baadhi ya Wananchi waishio kando ya mradi kutozingatia usafi kwa kutupa taka katika mifereji ya maji iliyojengwa kando ya barabara.

2.2.2 Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali
Mhesimiwa Spika, katika Halmashauri za Ilala (Dar es Salaam) Halmashauri ya Mji Kibaha (Pwani), Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ambako Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu, mambo yafuatayo yalibainika:-

a) Mafanikio;

i) Kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia kwa Walimu na kujifunzia kwa Wanafunzi kutokana na majengo ya ofisi,

maabara, madarasa na maktaba kurejeshwa katika hali nzuri;

ii) Kuboreshwa kwa mabweni ya Wanafunzi na mabwalo ya chakula na hivyo kuwafanya kuishi katika mazingira bora;

iii) Kuongezeka kwa nafasi za udahili wa Wanafunzi kutokana na ukarabati uliofanyika kuwezesha miundombinu na majengo ambavyo vilikuwa havitumiki kuanza kutumika;

iv) Kurejesha majengo na mazingira ya shule katika ubora uliokuwepo awali katika shule za Sekondari za Serikali;

v) Ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya elimu nchini kwa kutumia mfumo wa Force Account katika ukarabati ambapo ujenzi unasimamiwa na Kamati za mbalimbali zinazoundwa na Bodi za shule;

b) Changamoto;

i) Kukosekana kwa uwiano wa kiasi cha fedha kilichotumika na ubora wa kazi iliyofanyika kati ya shule moja na nyingine;

ii) Ukarabati uliotekelawa na TBA kutokamilika au kuwa chini ya kiwango, na hivyo kulazimika kusitisha mkataba;

iii) Kukosekana kwa taarifa za gharama za mradi (BOQ) kwa sehemu ya ukarabati uliotekelawa na TBA;

iv) Baadhi ya miundombinu ya shule kutoguswa na ukarabati kutokana na ufinyu wa bajeti; na

v) Ukarabati kufanyika huku shughuli za ufundishaji zikiendelea kutokana na ukosefu wa majengo ya ziada.

2.2.3 Uwezeshaji kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa Kamati kuhusu uwezeshaji kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu

kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ulibaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo: -

(a) Mafanikio;

- (i) Wanavikundi wameboresha hali ya maisha ya familia zao kutokana na kipato wanachokipata katika miradi yao;
- (ii) Kuzalishwa kwa nafasi za ajira kwa wanavikundi na wananchi wengine kutokana na miradi ya uzalishaji na huduma zinazotekelawa na vikundi;
- (iii) Kuongezeka kwa mapato ya Serikali kutokana na miradi na shughuli zinazotekelawa na vikundi kwa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri;
- (iv) Wananchi kuongeza imani kwa Serikali kwa namna inavyounga mkono juhudzi zao za kijikwamua kiuchumi; na
- (v) Wananchi kutumia mikopo ya asilimia 10 kuanzisha miradi mikubwa inayonufaisha jamii. Mfano ni miradi ya mazingira, viwanda, na uzalishaji.

(b) Changamoto;

- i. Kukosekana kwa elimu ya ujasiriamali, uendeshaji wa miradi na biashara kwa Wanavikundi;
- ii. Ukoefu wa masoko ya uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na vikundi;
- iii. Mitaji inayotolewa kutokidhi mahitaji ya kuanzisha miradi mikubwa kwa wanavikundi;
- iv. Kukosekana kwa muunganiko (linkage) kati ya vikundi na majukwaa ya kibiashara, teknolojia na masoko;
- v. Baadhi ya vikundi kukosa ushirikiano kutoka kwa Wanajamii (Mfano Wanajamii kugoma kulipa ada ya uzoaji taka kwa kikundi);

vi. Baadhi ya vikundi (hasa vikundi vya vijana) kukosa uaminifu katika urejeshaji wa mikopo jambo linalosababisha mfarakano na Halmashauri husika; na

vii. Migogoro mionganini mwa Wanavikundi jambo linalosababisha baadhi ya Wanachama kujitoa katika vikundi hivyo.

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na ingependa kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

i. Ukarabati mkubwa wa shule kongwe za Sekondari umerejesha hadhi ya shule hizo kwa kuboresha mazingira ya kufundishia kwa Walimu na kujifunzia kwa Wanafunzi, na hivyo kuongeza morari ya kazi na ari ya kusoma;

ii. Matumizi ya Force Account katika ukarabati wa shule kongwe za Sekondari kwa sehemu kubwa yameleta tija ikillinganishwa na kutumia Wakandarasi. Hata hivyo, umakini zaidi unahitajika kuhusu viwango vya ufundi vinavyotumika;

iii. Hakuna uwiano wa kiasi cha fedha kilichotolewa na ubora wa kazi iliyofanyika katika ukarabati wa baadhi ya shule kongwe za Sekondari;

iv. Ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi unachangia kuchelewesha utekelezaji na kukamilika kwa miradi. Aidha, utaratibu huo unaitia hasara Serikali kwa kulipa faini kutokana na ucheleweshaji wa malipo;

v. Mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu imechangia kuyainua kiuchumi makundi hayo. Hata hivyo, umakini zaidi unahitajika katika kusimamia sheria na Kanuni za utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo;

vi. Mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ikisimamiwa na kuratibiwa vizuri inaweza kutumika kuhamasisha uanzishaji wa miradi mikubwa kama viwanda, kilimo cha kisasa, makampuni n.k, na hivyo kuondoa utoaji wa mikopo midogo ambayo tija yake ni ndogo;

vii. Idara za Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii na Biashara hazijatumika kikamilifu katika kuelimisha na kusaidia makundi yanayonufaika na fedha za asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri;

viii. Kukosekana kwa umakini katika usanifu wa awali (*feasibility study*) wa miradi ya maendeleo kunaathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama kutokana na kuongeza kazi; na

ix. Serikali iweke utaratibu wa kusimamla na kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha ili kupusha ubadhirifu na hivyo kuwezesha kupatikana kwa thamani ya fedha “value for money”.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa.

Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vyta Kamati.

Kwa ufanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake (LGTI, KEC, DART na LGLB) ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 45,787,792,148** kutoka vyanzo vya ndani. Mapato hayo yanatokana na kuuza vifaa chakavu na zabuni kwa upande wa makao makuu (Fungu 56) na ada za wanafunzi, ukusanyaji wa madeni, tozo, ushuru na mauzo ya bidhaa mbalimbali kwa upande wa taasisi.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2021 kiasi cha **Shilingi 22,775,536,917.37** killikuwa kimekusanya, sawa na **asilimia 49.76** ya malengo yaliyowekwa. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa:-

- i. Ofisi ya Rais – TAMISEMI Makao Makuu haikukusanya kiasi chochote kutokana na kutouza nyaraka za zabuni au vifaa chakavu;
- ii. Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA) ndiyo uliongoza katika makusanyo ya taasisi kwa kukusanya kwa asilimia 55;
- iii. Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ilifanya vibaya zaidi kwa kukusanya kwa asilimia 11 tu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanya kimepungua kwa **asilimia 30.44** ikilinganishwa na **asilimia 80.2** iliyoshuhudiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Kiwango hicho cha makusanyo kinaonesha kwamba, wastani wa makusanyo kwa kila robo ulikuwa **asilimia 16.59** ambayo ni chini ya wastani wa **asilimia 25** ambao unapaswa kufikiwa kwa kila robo ya mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikoa hadi kufikia mwezi Februari, 2021 makusanyo yalikuwa ni **shilingi 74,451,560** kiasi ambacho ni sawa na **asilimia 36** ya lengo lilitlowekwa. Kiasi hicho kimepungua kwa **asilimia 3** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya **shilingi 814,683,049,426** na hadi kufikia mwezi Februari, 2021 zilikuwa zimekusanya **asilimia 61** ya lengo lilitlokusudiwa.

Wastani wa makusanyo kwa TAMISEMI Makao Makuu na Taasisi zake, Mikoa na Serikali za Mitaa kati kipindi hicho ulifikia **asilimia 48.92** kiwango ambacho kimepungua kwa takribani **asilimia 8.6** ikilinganishwa na wastani uliofikiwa katika mwaka wa fedha uliopita.

Kamati imebaini kwamba, Halmashauri zimeendelea kuwa na makusanyo mengi ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na wigo mkubwa wa vyanzo vya mapato na idadi kubwa ya watu, ambavyo ni muhimu katika ukusanyaji wa mapato.

3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI umebaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2020/21 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba: -

- i. Fedha zinazotolewa ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (*cash flow plan*) uliowekwa zimepungua ikilinganishwa na miaka mingine;
- ii. Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wingi (**asilimia 80**) ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo (**asilimia 30**); na

iii. Fedha za Maendeleo za Ndani zinatolewa kwa kiasi kikubwa (**asilima 62**) ikilinganishwa na fedha za maendeleo za nje (**asilimia 2**).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **Shilingi 384,545,560,071/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 54** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kwamba, kiasi hicho kimepungua kwa takribani **asilimia 19.4** ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo kiasi kilichopatikana kilikuwa ni **asilimia 73.4**.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2021 Ofisi hiyo na taasisi zake ilikuwa imepokea **shilingi 103,793,363,125** sawa na **asilimia 80** ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimeongezeka kwa **asilimia 26.2** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambacho kilikuwa **asilimia 53.8**.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo Kamati ilibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi 280,752,196,946**, sawa na **asilimia 49** ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa takribani **asilimia 27.1** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2019/20 ambacho kilikuwa ni **asilimia 76.1**.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na.02) katika mwaka wa fedha 2019/2020 iliyodhinishiwa kiasi cha **shilingi 14,773,473,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 8,165,271,000/=** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 6,108,202,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea **shilingi 7,655,467,644/=** sawa na **asilimia 52** ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi 4,136,302,674/=** ni kwa ajili ya mishahara, na **shilingi 3,519,164,969/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, hakuna fedha yoyote iliyotolewa kwa fungu hili kuhusiana na maendeleo licha ya kuwa na bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2020/2021 ziliidhinishwa bajeti ya **shilingi 6,021,005,090,076/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi 4,616,009,739,686/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **1,404,995,350,389/=** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2021 **shilingi 3,400,948,706,511** zilikuwa zimepokelewa hii ikiwa ni sawa na asilimia 56 ya bajeti yote iliyoidhinishwa.

Kati ya fedha hizo **shilingi 2,837,372,867,996** sawa na asilimia **61** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo zilikuwa **shilingi 563, 575, 838, 514/=** sawa na **asilimia 40**.

Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba fedha za maendeleo za ndani zilitolewa kwa kiwango kikubwa (**asilimia 52**) ikilinganishwa na fedha za nje ambazo zilipatikana kwa **asilimia 2** tu. Hii ni ishara njema kwamba, miradi ya maendeleo inaweza kutekelezwa kwa uhakika zaidi kwa fedha za ndani kuliko kutegemea fedha za nje ambazo hazina uhakika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini kwamba kwa wastani upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake katika mwaka wa fedha 2020/2021 ulikuwa ni **asilimia 57.52**, kiwango ambacho kimepungua ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 64.95** katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, wastani huo wa upatikanaji fedha katika kipindi kama hicho cha bajeti, ikiwa ni takribani robo ya tatu ya mwaka wa fedha, ni chini ya kiwango cha angalau asilimia 25 ambacho kinatakiwa kwa kila robo katika mwaka wa fedha. Kiwango hicho ni sawa na wastani wa asilimia 19.17 kwa robo mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, uchambuzi umebaini kwamba, wastani wa upatikanaji wa fedha ulikuwa ni kwa **asilimia 50.5**. Aidha, bado fedha za matumizi ya kawaida zimeendelea kupatikana kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo.

Kamati ilifanya ulinganishwa wa uwiano wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamkala za Serikali za Mitaa na kiasi kilichopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2021, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Miradi ya Maendeleo. Ufafanuzi zaidi kwa baadhi ya maeneo hayo umeoneshwa kupitia **Jedwali Na. 02 & Jedwali Na.03**

Jedwali Na.02: Bajeti iliyoidhinishwa kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana hadi Februari, 2021

Mgawanyo wa Bajeti	Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21	Kiasi kilichopokelewa hadi Februari, 2021	Asilimia ya kiasi kilichopokelewa
OC	76,365,953,552	71,588,485,236	94
Mishahara	53,446,890,000	32,204,877,889	60
Maendeleo	578,047,184,000	280,752,196,946	49
Jumla	707,860,027,552	384,545,560,071	54

Jedwali Na.03: Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana hadi Februari, 2021

Chanzo Jedwali Na 02 & 03: Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mwaka wa Fedha 2021/2022.

3.1.3 Mapito ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi na mapitio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kamati ilioita maoni na ushauri wa mambo kumi na tatu (13) ili ofisi hii iyazingatia katika utekelezaji wa vipaumbele vyake nya bajeti ili kuongeza ufanisi na tija.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhishwa na jitihada zilizooneshwa katika kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati kwa kutatua changamoto zilizobainishwa. Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati umechangia katika uboreshaji wa huduma za msingi kwa wananchi na maendeleo ya jamii.

Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanyia kazi maoni na ushauri kwa baadhi ya maeneo yaliyosalia ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na: -

i. Halmashauri kusaidia Vikundi nya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu kutumia fedha za mapato ya Ndani kuanzisha miradi mikubwa ya maendeleo ili kutoa ajira na kuchangia mapato ya Serikali. Mfano ni Viwanda nya kutengeneza Samani nya STAMICO na ALLELUYA nya mji mdogo wa Katoro Geita vyenye thamani ya **shilingi milioni 100**; na

ii. Halmashauri kubuni vyanzo vipyta nya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, ambapo Halmashauri 30 zimebuni jumla ya miradi ya kimkakati 38 yenye thamani ya **shilingi bilioni 273** ambayo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali. Kukamilika kwa miradi hiyo kutachangia kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, licha ya baadhi ya maoni kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na: -

i. Kuhakikisha Halmashauri zinazodaiwa na benki mikopo ya Waheshimiwa Madiwani iliyotokana na dhamana ya posho za kila mwezi, zinakamilisha ulipaji wa madeni hayo. Baadhi ya mikoa ambayo halmashauri zake hazijakamilisha ulipaji wa madeni hayo ni Simiyu, Ruvuma, Singida, Geita na Morogoro;

ii. Kuhakikisha Halmashauri zinasimamia kikamilifu urejeshwaji wa fedha za mikopo kutokana na asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri inayopelekwa kwenye Vikundi nya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe ulemavu;

iii. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga na kupeleka kikamilifu fedha za asilimia 40 na 60 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri kwenye Miradi ya Maendeleo; na

iv. TARURA kuendelea kuongezewa fedha na Serikali ili kuiwezesha kuhudumia mtandao mkubwa wa barabara (zaidi ya 144,000) ulio chini yake.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na:-

- i. Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022;
- ii. Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26;
- iii. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020;
- iv. Hotuba ya Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwenye uzinduzi wa Bunge la Kumi na Mbili (12); na
- v. Maelekezo ya Viongozi wa Kitaifa, Sera, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati ya Taasisi;

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais - TAMISEMI), imepanga kutekeleza malengo yake kwa kuzingatia vipaumbele kumi (13). Baadhi ya vipaumbele hivyo ni hivi vifuatavyo:-

- i. Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa umma (D by D);
- ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu msingi bila ada; afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii katika mamlaka za serikali za mitaa;

- iii. Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;
- iv. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatililaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, programu na miradi katika ngazi ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa;
- v. Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya ya msingi, elimu ya msingi na sekondari inayotekelizwa katika mamlaka za serikali za mitaa;
- vi. Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi katika mamlaka za serikali za mitaa;
- vii. Kusimamia matumizi ya raslimali na TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na
- viii. Kuratibu shughuli za utendaji kazi wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 7,683,329,644,800/=**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,728,008,207,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,955,321,437,800/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 3,972,149,603,000/=** sawa na asilimia 51.67 ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 755,858,604,000/=** sawa na asilimia 9.84 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Bajeti ya maendeleo ni sawa na asilimia 34.46 ya bajeti yote ya ofisi hii. Ufafanuzi zaidi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 04**.

Jedwali Na. 04 Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2021/2022

Chanzo: Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2021/2022)

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 916,445,409,198/=**. Mapato hayo yameongezeka kwa asilimia 6.48 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo yalikuwa **shilingi 860,678,914,502/=**. Ulinganisho wa makusanyo kati ya mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 umefafanuliwa zaidi katika **Jedwali Na. 05**.

Makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na uuazaji wa kuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, mauzo ya huduma, ada za wanafunzi na tozo kwa makao makuu na taasisi zake. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vyta mapato vilivyopo kwa mujibu wa sheria.

Jedwali Na.5 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya Ndani

Chanzo: Randama ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI (2021/2022)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati makusanyo yote yanatarajiwa kuongezeka kwa **shilingi 55, 766,494,696** (sawa na asilimia 6.48) ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha unaomalizika. Ongezeko hilo limepungua kwa asilimia 1.52 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 8 katika jedwali za mafunzo 2020/2021.

	Ofisi/ Taasisi	Bajeti 2020/2021	Bajeti 2021/2022	Tofauti (+ au -)	Asilimia (%)
Ingawa kiwanja wa Ofisi ya Rais	CR-TAMSEM na Taasisi	45,508,225,514	52,366,725,886	6,858,500,372	15.0%
asilimia 45 hadi ikilinganishwa	Mkoa	20,984,912	22,083,312	1,100,400	5.2%
Kwa mwaka vya Mijini (TARURA) uta	Halmashauri	814,960,990,076	863,858,000,000	48,897,009,924	5.9%
ukusanyaji wa mapato ya ndani ikilinganishwa na nyingine chini ya TAMISEMI. Sababu kubwa ya ongezeko hili kuwepo kwa Kanuni za ukusanyaji wa tozo ya maegesho ya Magari itakayoruhusu mapato kukusanywa katika maeneo yote.	ndani	863,689,450	916,454,091,924	52,764,641,924	6.48%

Bado Halmashauri zinatarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na maduhuli yake kuongezeka kwa **shilingi 48,897,009,924**awa na takribani asilimia 6 ikilinganishwa na makusanyo ya Halmashauri katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Kiwango hicho cha ongezeko kimepungua kwa asilimia 0.47 ikilinganishwa na mwaka unaomalizika. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, huenda kuna ulegemu katika matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo, Serikali itazame mwenendo wa matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato, sambamba na kuhamasisha mamlaka hizo kubuni vyanzo vypya vya mapato.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa pamoja zinaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 7,683,329,644,800/=** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 4,728,008,207,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,955,321,437,800/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha hizo zinazoombwa kuidhinishiwa na Bunge, **Shilingi 14, 868,770,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) – Fungu 02. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia 4.17 ikilinganishwa na **shilingi 14,273,473,000** zilizoidhinishiwa katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake bajeti inayoombwa kuidhinishiwa na Bunge lako tukufu kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imeongezeka kwa **Shilingi 663,529,291,800** sawa na asilimia 9.45 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaomalizika wa 2020/2021.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la asilimia 29.06 kutoka **shilingi 2,289,919,896,000/=** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi **shilingi 2,955, 321, 437,800/=** katika mwaka kwa mwaka wa fedha ujao.

Uchambuzi zaidi umebaini kwamba, ongezeko la bajeti kwa ujumla wake, limetokana na Serikali kuongeza fedha za maendeleo kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya afya na elimu nchini na hivyo kuimarishe utoaji wa huduma katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kulinganisha Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, uchambuzi wa Kamati umebaini kuna ongezeko katika pande zote mbili. Hata hivyo, ongezeko la bajeti ya Taifa ni dogo kwani ni **asilimia 3.95** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/2021, wakati ongezeko la Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika kipindi hicho ni **asilimia 9.45**.

Aidha, bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni sawa na **asilimia 21.19** ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeongezeka kwa asilimia 1.06 ikilinganishwa na uwiano katika mwaka wa fedha 2020/2021 ambao ulikuwa ni asilimia 20.13. Ulinganisho zaidi wa Uwiano wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bajeti ya Taifa umefafanuliwa zaidi kuitia **Jedwali Na. 06**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuongeza bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwani inaonesha kutambua na kuthamini umuhimu wa Ofisi hii ambayo ina jukumu la kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohudumia na kugusa wananchi moja kwa moja na hivyo kuunga mkono juhudii zao katika shughuli za maendeleo. Ni rai ya Kamati kwamba, fedha zitakazoidhinishwa zitolewe na kupelekwa kwa wakati ili kuwezesha kutekelezwa kwa shughuli zilizokusudiwa. Aidha, kuwe na usimamizi na udhibiti mzuri wa matumizi ya fedha hizo ili kuwezesha kupatikana kwa tija na thamani ya fedha kwa shughuli zitakazotekelzwa, sambamba na kuzuia ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa umefafanuliwa zaidi kuitia **Jedwali Na. 07**. ambalo ni Kiambatisho “A” cha Taarifa hii ya Kamati.

Jedwali Na. 06: Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2021/2022)

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya maendeleo na kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

- i. Ofisi ya Rais – TAMISEMI izisimamie kikamilifu Halmashauri nchini ili kuhakikisha zinaongeza makusanyo kwa kuweka malengo halsia. Uchambuzi umebaini kwamba, kumekuwa na ongezeko dogo la malengo ya ukusanyaji kutoka mwaka mmoja wa fedha hadi mwingine, na wakati mwingine lengo hilo limekuwa halifikiwi kikamilifu licha ya kuwa dogo;
- ii. Ofisi ya Rais – TAMISEMI isimamie na kuhakikisha Halmashauri nchini zinatenga fedha kwa ajili ya miradi ya barabara ili kuunga mkono na kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA). Kabla ya kuanzishwa TARURA, Halmashauri zilitenga bajeti ya kuhudumia barabara katika maeneo yake, hata hivyo, nyingi

zimeacha jukumu hilo kwa TARURA pekee ambayo ina bajeti finyu;

iii. Serikali iandae Kanuni za kuiwezesha TARURA kuwa na nguvu ya kisheria ya kukusanya ushuru wa maegesho katika maeneo mbalimbali nchini. Wakala hii imekuwa ikifanya vizuri katika kukusanya ushuru wa maegesho, licha ya kukumbana na changamoto za ukusanyaji kutoka kwa baadhi ya Halmashauri na Taasisi za Umma kutokana na kutokuwepo na mwongozo wa kisheria;

iv. Serikali isimamie kikamilifu halmashauri zinazokiuka kifungu cha 37 A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kuhusu utengaji na utoaji wa fedha za 10% ya mapato ya ndani ili kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Mikoa ya Lindi, Njombe na Morogoro pekee ndiyo ilizingatia utoaji wa asilimia 10 kwa ukamilifu. Aidha, Mikoa ya Lindi na Singida ilitoa Halmashauri tatu zilizoongoza katika utengaji na utoaji wa fedha za asilimia 10.

Kwa upande mwingine, mikoa ya Dodoma, Ruvuma na Manyara ilitoa Halmashauri tatu zilizofanya vibaya zaidi katika utengaji na utoaji wa asilimia 10. **Jedwali Na. 08** linafafanua zaidi.

Jedwali Na.08 Mikoa na Halmashauri zilizofanya vizuri/vibaya katika utoaji wa asilimia 10 ya Mapato ya Ndani

	Mikoa na Halmashauri zilizofanya vizuri			Mikoa na Halmashauri zilizofanya vibaya		
Mkoa	Lindi	Ruvuma	Singida	Dodoma	Pwani	Rukwa
Halmashauri	Nachingwea (DC)	Tunduru (DC)	Iramba (DC)	Mpwapwa (DC)	Kibaha (DC)	Kalambo (DC)
Asilimia (%)	180	178	175	10	14	22
Nafasi	1	2	3	1	2	3

Chanzo: Randama za Mikoa kwa Mwaka wa fedha 2021/2022

v. Serikali ihakikishe Halmashauri zinaandaa na kutekeleza mpango mahususi wa kusaidia Vikundi vya Wanawake, Vijana na Wenyewe Ulemavu kutumia fedha za asilimia 10 ya mapato ya ndani kuanzisha miradi mikubwa ya maendeleo kama vile Viwanda, Kilimo cha Kisasa, Makampuni, n.k kwa lengo la kuongeza kipato cha wanavikundi, kutoa ajira kwa wanajamii na kuchangia mapato ya Serikali;

vi. Serikali ihakikishe halmashauri nchini zinatenga na kupeleka kikamilifu asilimia 40 (Wilaya na Miji) na 60 (Majiji na Manispaa) ya mapato ya ndani kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ni mkoa wa Lindi ndiyo Halmashauri zake zilizingatia kwa ukamilifu kutenga na kupeleka fedha hizo.

Aidha, Mikoa mitatu iliyongoza katika utoaji wa fedha za maendeleo kutokana na mapato ya ndani ni Lindi (wastani wa asilimia 117); Pwani (wastani wa Asilimia 103) na Njombe (wastani wa asilimia 98). Mikoa mitatu iliyofanya vibaya ni Kagera (Wastani asilimia 26), Simiyu (Wastani wa asilimia 30) na Manyara (Wastani wa asilimia 32). **Jedwali Na. 9** linafafanua zaidi kuhusu Halmashauri zilizofanya vizuri na Halmashauri zilizofanya vibaya.

Jedwali Na.9 Halmashauri zilizofanya vizuri/vibaya katika utoaji wa fedha za maendeleo kutokana na makusanyo ya ndani.

	Halmashauri zilizofanya vizuri			Halmashauri zilizofanya vibaya		
	Halmashauri	Liwale	Kilwa	Mkuranga	Chamwino	Manyoni
Asilimia (%)	150	142	141	6.49	8.57	14
Nafasi	1	2	3	1	2	3

vii. Halmashauri ziendelee kubuni na kutekeleza vyanzo vipyta vya mapato ili kuongeza wigo wa mapato Serikalini na hivyo kuepuka kadhia ya kuongeza kodi mara kwa mara kwenye vyanzo vilevile, jambo linalokera wananchi. Aidha, kuwe na udhibiti katika matumizi ya fedha za mapato yatakayokusanywa ili kuwezesha kufikiwa kwa tija na malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa.

Miongoni mwa njia za kuongeza mapato ni kubuni miradi ya kimkakati, kuandaa maandiko na kuyawasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI ili kuyaombea fedha za utekelezaji;

viii. Serikali iboreshe usimamizi wa masuala ya kiutumishi katika Halmashauri ili kuhakikisha wanapandishwa madaraja na kubadilishiwa mishahara yao kwa wakati, na kupata stahiki nydingine kikamilifu ili kuondoa malalamiko mionganoni mwa Watumishi;

ix. Ofisi ya Rais – TAMISEMI isimamie na kuhakikisha Sekretarieti za Mikoa zinaandaa Taarifa za Bajeti za Mafungu ya Mikoa kwa kuzingatia miongozo ya uandaaji wa bajeti iliyopo ili kuondoa kasoro ambazo Kamati ilizibaini wakati wa uchambuzi wa bajeti;

x. Ofisi ya Rais – TAMISEMI isimamie kwa ukamilifu na kuhakikisha Halmashauri zote ambazo hazijakamilisha ulipaji wa madeni ya madiwani katika benki na taasisi za fedha zinafanya hivyo. Madeni hayo yalipaswa kulipwa kabla ya tarehe 30 Mei, 2020;

xi. Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihakikishe mwongozo ilioutoa mwezi Februari, 2021 kuhusiana na usimamizi na matumizi ya fedha za asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zinazorejeshwa na Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu unaeleweka na kuzingatiwa kikamilifu na Wakurugenzi wa Halmashauri;

xii. Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihamasishe na kuzisaidia kaya zinazohitimu “graduate” kutoka mpango wa ruzuku kwa Kaya masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuunda kuunda vikundi ili kutumia fedha za asilimia 10% ya mapato ya ndani kuanzisha miradi ya kiuchumi itakayowapatia ajira na uhakika wa kipato;

xiii. Ofisi ya Rais - TAMISEMI isimamie kikamilifu na ichukue hatua za kudhibiti ubadhirifu katika matumizi ya fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF) na

kuhakikisha kuna thamani ya fedha "value for money" katika miradi inayotekelizwa.

Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Halmashauri hazina matumizi sahihi ya fedha za Mfuko huu. Mfano ni katika Halmashauri ya Mlimba ambapo Kamati ilibaini ununuzi wa mfuko wa saruji kwa bei isiyo halisi ya **shilingi 20,000/=** na Wajumbe wa Kamati walipohoji kukawa na maelezo yanayokinzana baina ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo;

xiv. Ofisi ya Rais – TAMISEMI isimamie na kuhakikisha uchangiaji wa fedha za uendeshaji katika ngazi za chini (Kata na Vijiji) ambazo hutokana na asilimia 20 ya ruzuku ya utawala kwa Halmashauri kutoka Serikali Kuu, zinapelekwa kikamilifu ili kusaidia uendeshaji katika ngazi hizo;

xv. Serikali ichukue hatua ili kurekebisha hali ya kukosekana kwa ulinganifu baina ya fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za Sekondari nchini na kazi ya ukarabati iliyofanyika. Ziara ya ukaguzi wa Kamati katika baadhi ya shule zilizokarabatiwa ilibaini kwamba, kiasi cha fedha kilichotolewa ni kikubwa ikilinganishwa na kiwango na ubora wa kazi zilizofanyika.

Aidha, shule zote ambazo ukarabati wake ulianza kutekelezwa na Wakala wa Majengo (TBA), ukarabati wake haukukamilika na hakukuwa na taarifa kuhusiana na gharama za mradi (BOQ), jambo liliosababisha iwe vigumu kufanya tathmini ya gharama halisi za mradi;

xvi. Matumizi ya Force Account katika utekelezaji wa miradi ya Serikali ikiwa ni pamoja na ukarabati wa shule kongwe za Sekondari yameleta tija ikilinganishwa na matumizi ya Wakandarasi. Hata hivyo, umakini zaidi unahitajika kuhusu aina ya mafunzi na viwango vya ujuzi walivyonavyo;

xvii. Kamati inapongeza kazi kubwa iliyofanywa na Serikali katika ukarabati wa shule kongwe za Sekondari, hata hivyo yapo maeneo hayajakarabatiwa, hivyo Serikali iendelee

kutoa fedha ili kuwezesha zoezi la ukarabati kugusa maeneo yote muhimu ya shule;

xviii. Usimamizi bora wa miradi inayotekelawa na Serikali unaweza kuokoa fedha zinazoweza kutumika kutekeleza miradi mingine. Mfano ni katika ujenzi wa barabara ya Shekilango ambapo jumla ya **shilingi bilioni 5.9** zimeokolewa na kuelekezwa eneo la Mbweni ili kujenga mitaro ya maji itakayosaidia kuondoa kero ya mafuriko ya mvua; na

xix. Serikali ichukue hatua za makusudi ili kutatua tatizo la upungufu wa Watumishi wa sekta za elimu, afya, Uhandisi na TEHAMA katika Halmashauri nchini, ambao unakwamisha au kuathiri utekelezaji wa majukumu katika Halmashauri.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Kwa kuzingatia ukweli kwamba, Kamati hii ndiyo inayoshughulikia mafungu mengi ya bajeti (36) ikilinganishwa na Kamati nyingine za Bunge, na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa muda mrefu na wakati mwagine hadi usiku. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, hii ikiashiria utayari wao wa kulitumikia Bunge, Taifa na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao.

Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Humphrey Hesron Polepole, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo,Mb-Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb
5. Mhe.Mwantum Mzamili Zodo, Mb
6. Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara,Mb
7. Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe,Mb
8. Mhe.Festo Richard Sanga, Mb
9. Mhe. Rehema Juma Migila,Mb
10. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
11. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage,Mb
12. Mhe. Amandus Julius Chinguile,Mb
13. Mhe.Sebastian Simon Kapufi,Mb
14. Mhe. Michael Constatino Mwakamo, Mb
15. Mhe. Dennis Lazaro Londo, Mb
16. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb
17. Mhe. Condester Michael Sichwale, Mb
18. Mhe. Irene Alex Ndyamkama, Mb
19. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb
21. Mhe. Shanif Jamal Mansoor, Mb
22. Mhe. Zacharia Paul Issaay, Mb
23. Mhe. Seif Salum Seif, Mb
24. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
25. Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Mb
26. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mb

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Ummy Ally Mwalim (Mb) kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake. Utendaji wake na Naibu Mawaziri wake, Mhe. David Ernest Silinde (Mb) na Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb) umedhihirisha jinsi walivyo hazina kubwa kwa ustawi na maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini na maendeleo ya Taifa hili.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Prof. Riziki Silas Shemdoe, akisaidiana na Naibu Makatibu Wakuu, Ndg. Gerald Mweli na Dkt. Grace Maghembe, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Shukrani za Kamati ziwaendee pia Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa utekelezaji makini wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha, na uwasilishaji mzuri wa Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Selemani Said Jafo (Mb) kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati katika kipindi chote alichohudumu katika wadhifa huo. Alifanya kazi na Kamati kwa moyo wa kujituma na weledi wa kiwango cha juu. Ninamtakia kila lakheri na utendaji uliotukuka katika majukumu mapya ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndg. Gerlad Magili; Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima na Ndg. Rabisante Moshi, wakisaidiwa na Ndg. Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Humphrey H. Polepole (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA
NA SERIKALI ZA MITAA
19 Aprili, 2021

KIELELEZO "A"

Jedwali Na 7: Mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya OR - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Eneo la Matumizi	Makadirio 2020/2021 (Ish. 000)	Makadirio 2021/2022 (Ish. 000)	Tofauti Ongezeko/ Upunqifu (Ish. 000)	Asilimia (%)
Matumizi ya Kawaida				
Mishahara:				
OR – TAMISEMI (HQ)	11,298,245	10,278,507	-1,019,738	9.03
Ta asisi	42,148,645	47,235,991	5,087,346	12.07
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)	8,165,271	7,760,568	-404,703	4.96
Mikoa	76,896,293	71,269,064	-5,627,229	7.32
Halmashauri	3,740,229,604	3,835,605,473	95,375,869	2.55
Jumla Mishahara	3,878,738,058	3,972,149,603	93,414,545	2.41
Matumizi Mengineyo:				
OR – TAMISEMI (HQ)	70,643,361	10,054,284	-60,589,077	85.77
Ta asisi	1,318,870	1,318,870	0	0
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)	6,108,202	6,608,202	500,000	8.19
Mikoa	58,998,656	57,449,078	-1,549,578	2.63
Halmashauri	714,082,310	147,659,832	-566,422,478	79.32
Jumla Matumizi Mengineyo	849,832,529	223,090,266	-626,742,263	73.75
Jumla Matumizi ya Kawaida	4,729,880,457	4,728,008,207	-1,872,250	0.04
Fedha za Maendeleo:				
OR – TAMISEMI	578,047,184	651,343,104	114,484,061	24.7
Tume ya Utumishi wa	500,000	500,000	0	0

Chanzo: Randama ya OR - TAMISEMI (2021/2022)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mwenyekiti wa Kamati inayohusiana na masuala ya Serikali za Mitaa. (*Makof*)

Sasa tunaingia kwenye uchangiaji, tunakwenda kwa muda ule wa dakika zetu kumikumi. Atakayetufungulia sasa ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Hussein Tabasam na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka ajiandae.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa unyenyekevu mkubwa naomba kukushukuru sana kwa kunifanya kuwa mchangiaji wa kwanza wa hotuba hii ambayo ni muhimu sana. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufanya wote tuamke salama tuko hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumile dakika zangu kumi kuongea kuhusu *TARURA*. Naomba niilongelee *TARURA* katika Wilaya ya Same, *TARURA* ndani ya Same Mashariki, halafu nikipata nafasi nitakwenda mahali pengine kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba mpate picha kamili ya Wilaya ya Same. Wilaya ya Same iko ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro lakini ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Same imeketi kwenye asilimia takribani 40 ya Mkoa mzima wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, nikiwa na maana kwamba katika Mkoa mzima wa Kilimanjaro wenyewe wilaya saba, Wilaya ya Same imeketi kwenye asilimia takribani 40, mki-google mtaikuta hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wilaya ya Same ni kubwa sana ndani ya Mkoa wa Kilimanjaro. Hata hivyo, Wilaya ya Same ndiyo inayopata pesa kidogo ukilinganisha na wilaya nyingine. Hapo naona kidogo nimeeleweka.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* haikuanzishwa siku nyingi sana, imeanzishwa tarehe 2 Julai, 2017. Malengo ya *TARURA* yalikuwa ni kuimarisha uzalishaji, kwamba wananchi waweze kuzalisha lakini mazao yao yafike sokoni. Hata hivyo, nikiwa mkweli *TARURA* kwa sababu ya upungufu wa pesa

zinazotolewa haifanyi kazi ambayo ndiyo lengo la kuanzishwa kwake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye Jimbo langu la Same Mashariki, dakika siyo nyingi. Same Mashariki niseme ukweli ni jimbo korofi. Serikali fanyeni taratibu za kupitia majimbo yote myatambue majimbo ambayo ni korofi, laini na madogo ili ufile wakati mgawe sawa hizi rasilimali ndogo tulizonazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Same Mashariki lina tarafa tatu; Tarafa ya Ndungu, hii ni tambarare, tarafa zinazonisumbua sana ni tarafa mbili ambazo ni za milimani, siyo miinuko, ni milimani. Hao wanaoishi milimani wana *winter* na *summer* kama Ulaya. Wananchi wanaoishi milimani tatizo lao kubwa, nikiri na naomba Serikali muende huko ni barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, barabara zote za wananchi wangu wa Same Milimani ni za *TARURA*. Niseme ukweli, *TARURA* Wilaya ya Same hatupewi fedha, japo wananchi wa Same Mashariki nina uhakika kuwa ni wananchi tofauti na wananchi wengine, kwani wanachimba barabara zao wenyewe. Asilimia kubwa za barabara za milimani katika Tarafa ya Gonja, Tarafa ya Mambavunta kwenye milima mikubwa na wanachimba barabara zao wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki sikuwa na njia, maana wananchi wa milimani wako kipindi cha mavuno, wanavuna tangawizi; na wa maeneo ya tambarare Tarafa ya Ndungu wanalima mpunga. Barabara za *TARURA* ambazo ndiyo zingewezesha wananchi kutoa mazao yao kutoka mashambani kufikisha barabara kuu, zote zimekuwa. Sikuwa na njia nyngine, ila mimi mwenyewe kama Mbunge niliongea na Mkurugenzi, nikatumia fedha za Mfuko wa Jimbo, nikaweka Mkandarasi. Fedha zile zingenisaidia kwa vitu vidogo vidogo, lakini uone sasa fedha za Mfuko wa Jimbo nimefanya kazi ambayo ingefanya na *TARURA*, siyo hak! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimechonga barabara kilometa 93.16. Mpaka sasa hivi ninapoongea hapa, Mkandarasi yule bado yupo kwenye eneo anaendelea kuchonga barabara zile. Zile fedha ningetengeneza matundu ya vyoo, ningenunua madaftari na nini, zote nimeweka mkandarasi. Nimezungumza na Mkurugenzi, maana sikuwa na njia nyininge. Naomba nilete *documents* za huyo Mkandarasi huko kwako.

Naomba mchukue hizi *documents* mpeleke kwa Spika. *Mpe Spika. (Makof)*

(Hapa Mhe. Anne K. Malecela alimkabidhi pageboy nyaraka ziweze kumfika Mezani kwa Spika)

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, lazima Serikali ipite iangilie haya majimbo. Haya majimbo hayafanani. Zile fedha za Mfuko wa Jimbo ningependa kufanya mambo madogo madogo ya kuchocha maendeleo, lakini zote nimekwenda. Nimeweka Mkandarasi mwenyewe wakati ni kazi ya TARURA. Kwa kweli hapo sikufurahi sana. Imenibidi nifanye hivyo niokoe maisha ya wananchi wangu. Wananchi wa Same Mashariki waliniheshimu wakanichagua kwa kura nydingi sana, wakamchagua Rais wangu kwa kura nydingi, wakachagua Madiwani, tena siyo kwamba kura zimeibiwa, acheni maneno; na Madiwani wote 14. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, nilipoona wananchi hawana uwezo sasa wa kusafirisha mazao, nikachukua fedha nilizopewa na Serikali, tena Serikali angalieni vizuri, ongezeni hizi fedha kidogo. Hizi fedha mtuongezee maana mlikuwa mnaangalia na *population*, wananchi wameongezeka sana, tuongezeeni hizi fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na nilivyoongea hapa kuhusu ukubwa wa Wilaya ya Same ambayo ni takribani asilimia 40 ya Mkoa wa Kilimanjaro, tuna tatizo sana la upande wa afya. Tuna Hospitali ya Wilaya moja ambayo ipo Same Magharibi, ipo mpakani mwa Wilaya ya Same na

Wilaya ya Mwanga. Wananchi wa Same Mashariki wapo mpakani mwa Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, nawanyenyekrea Serikali, nimeshukuru juzi alikuja Naibu Waziri wa Afya, alitembelea lile Jimbo, akatembelea upande wa afya kwa siku mbili, aliona hali halisi. Niinyenyekrea Serikali, oneni umuhimu wa kuweka Hospitali ya Wilaya nyingine upande wa Mashariki kwa sababu eneo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa TARURA, nilisahau kukwambia kitu kingine, nina barabara moja ambayo ni kubwa sana, inatoka Hedaru kwenda Vunta mpaka Miamba. Hii barabara inabeba wananchi takribani asilimia 40 ndani ya Jimbo langu. Hii barabara haipitiki kabisa na ndiyo barabara inayochukua asilimia 40 ya wananchi, lakini imekufa. Barabara hii magari yanapita kwa shida na ndiyo iliyobeba tangawizi yote ya Jimbo langu. Hii barabara naomba isipewe fedha kidogo kidogo na TARURA, TARURA watafute fedha za Mradi wa Maendeleo, zipelekwe kwenye Tarafa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali...

(Hapa kengele ya kwanza illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, hiyo ni kengele ya pili?

SPIKA: Ni ya kwanza.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, tena sasa nasimama vizuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye kazi ambayo ni ya muhimu na ninaomba jibu hapa, mpite mwangalie majimbo yote ya nchi ya Tanzania. Haya majimbo hayafanani. Hayafanani! Huwezi kuzungumzia Jimbo la Same Mashariki ukaja kulinganisha na Dodoma Mjini. Hapana, hapana!

Mheshimiwa Spika, Serikali ni lazima mtuambie, mnatuangaliaje kwenye haya majimbo? Wengine tunateseka, wengine wanastarehe. Sipendi kupiga kelele hivi, isipokuwa naumia. Wananchi wangu ambao hawana hali inayoridhisha, wana hali mbaya sana. Nafikiri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amenisikia. Nitaomba nifanye naye ziara tukimaliza hii hotuba, nipite naye kwenye lile Jimbo hata siku moja tu, kama zaidi, si ataugua!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Aje Mheshimiwa Hamis Hussein Tabasam.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema, naomba kuchangia hotuba ya Bajeti ya Serikali za Mitaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Ummey Mwalimu kuwa Waziri wa Serikali za Mitaa. Ni kwamba mashine iliyotoka ilikuwa ni ya kusaga na kukoboa na mashine ilioingia sasa hii ni ya kusaga na kupepete. Kwa hiyo, shukrani sana Mheshimiwa Samia kwa jambo hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, najikita katika sehemu ya utawala bora katika Halmashauri zetu na Serikali za Mitaa katika nchi hii. Serikali imekuwa ikitafuta fedha hizi kwa shida; inakusanya kodi kwa wananchi kwa ajili ya kuhudumia miradi ya maendeleo iliyopo katika Halmashauri zetu. Hii miradi inayopewa fedha ni ya maendeleo kwa ajili ya kuwaondolea wananchi kero na adha walizonazo katika miradi ya elimu, afya, barabara, maji na kadhalika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kufanya kazi zake za miradi ya maendeleo za ujenzi kwa kutumia *force account*. Utaratibu huu umekuwa na mafanikio kwa ajili ya kupunguza gharama za uendeshaji katika miradi hii katika nchi nzima. Kuna maeneo hatua hii imekuwa ni

sehemu ya chaka la kuibia fedha za Serikali kwa kiwango cha kuchota kwa koleo; siyo kiwango cha kuchota kwa kunywa kwa mrija; zinachotwa kwa koleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Jimbo la Sengerema, namshukuru sana aliyekuwa Waziri wa Fedha na sasa hivi ni Makamu wa Rais, kwani nilikwenda kwake katika kumlilia kuhusu fedha za miradi ya maendeleo ambazo zimekwama katika Halmashauri ya Sengerema na bahati nzuri nilipewa fedha karibu shilingi 2,212,000,000/=. Fedha hizi zilikuwa katika mgawanyo ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kuna fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya shilingi milioni 749 ambazo ni za kuanzia. Wakati huo huo nikapewa fedha nyingine kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kumi shilingi milioni 125. Bado nikapewa fedha tena shillingi milioni 188 kwa ajili ya kumalizia maabara zilizojengwa na wananchi kule kwa nguvu zao wenyewe kwa ajili ya kufanya *finishing*; nikapewa fedha nyingine kwa ajili ya kumalizia zahanati shilingi milioni 150; na nimepewa fedha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kumalizia Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kipi kilichotokea katika hali hii? Kule kuna kazi. Kwa mfano, kazi moja tu ya ujenzi wa Halmashauri ya jengo la Halmashauri kwa kutumia nafasi hii ya kuwaachia wazi hawa Wakurugenzi wetu, tayari hao ma-engineer na watu wa manunuzi wanatumia nafasi hii kuchimba msingi na kujenga msingi wa jengo la Halmashauri hiyo na *structure* za nguzo fundi analipwa shilingi milioni 160. Hii ni hatari kubwa sana. Jengo ni dogo, halina upana wowote. Sasa kama kwangu Tabasam kuna hali hii, je, katika Halmashauri nyingine karibu 200 kukoje?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Ummy Mwalimu akija kumalizia hotuba yake, atoe na majibu kwa hili, kwa ajili ya ndugu yake mimi Tabasam, vinginevyo nitaing'ang'ania shilingi na kama hali hii kule Sengerema itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, katika ujenzi huu kuna hii shilingi bilioni moja inajenga majengo matano. Wodi inajengwa kwa shilingi milioni 204; kuna ujenzi wa kujenga *incinerator*, hii tu ya kuchomea takataka shilingi milioni 30. Kajengo kadogo, yaani kakizimba, sijui tunaitaje kwa Kiswahili, maana yake ni kichomea taka, kwa shilingi milioni 30. Jengo kwa ajili ya kufulia nguo shilingi milioni 115; jengo kwa ajili ya *mortuary* ambayo haina *cold room* shilingi milioni 130. Hii ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hili suala la Sengerema Mheshimiwa Ummy, unafahamu kuna Wakurugenzi wengine wanajua tayari wanatakiwa kuondoka, kwa hiyo, wanafanya haraka sasa kunyakua hizi hela. Nakuomba sana uzuie matumizi ya hizi fedha kule Sengerema haraka iwezekanavyo. Peleka timu ikaangalie ile hali iliyoko kule, kuna wizi wa kutisha! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri hizi tunashangaa zinapewa hati safi, lakini Sengerema imepewa hati yenye mashaka. Ni maajabu makubwa! Kuna fedha zinazokusanywa katika hili suala la utawala bora na makusanyo ya Halmashauri ya fedha za masoko na magilio katika *own source*. Fedha za kwenye kutumia *POShizi* mashine za kukusanya ushuru shilingi milioni 350 zimeibiwa, lakini watumishi bado wapo kazini.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo, alikuwepo pale *DT* Sengerema, ameondoka na shilingi milioni 250. Pamoja na Mheshimiwa Jafo kuja Sengerema na kuagiza kwamba wakamatwe mara moja, bado wapo kazini. Mheshimiwa Jafo aliagiza watu wa TAKUKURU Mkoa wafanye kazi hiyo, jamaa anaendelea kupeta na anaendelea kula ulanzi huko kijijini. Hii ni hatari kubwa sana katika nchi hii!

Mheshimiwa Spika, huko kwenye Wizara ya TAMISEMI ndipo ambako ni chaka la kupotezea pesa za Serikali. Ukitikia pesa za Serikali zinakusanywa; na tundu lipo wapi? Tundu lipo kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ummy Mwalimu una kazi kubwa sana dada yangu. Una kazi kubwa sana

kwenye kuzuia hilo tundu. Atakuwa anachota Mheshimiwa Mwigulu Nchemba halafu tundu kule linatoboka na wananchi wanaendelea kupata shida.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumza na wewe hapa ni kwamba majengo ambayo yanafanyiwa kazi kule hayalingani na thamani ya fedha. Wanaleta maelekezo kutoka TAMISEMI yanakwenda kule kwamba jengo moja la kumalizia kupiga ripu na kumalizia bati shilingi milioni 12, siyo kweli. Wananchi wanajenga jengo, wanamaliza boma kwa shilingi milioni sita, halafu kulimalizia jengo, kupaka rangi na kuweka madirisha na milango shilingi milioni 12; ni jambo ambalo halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, kuna haya maboma ambayo anayataja Mheshimiwa Ummy Mwalimu katika hotuba yake; maboma yaliyopo kwetu kule ni mengi. Halmashauri moja kama Sengerema tu ina maboma karibu 200 na kitu. Sasa maboma haya hatujaambiwa yatakelezwa namna gani. Haya maboma hayako kwangu tu, yapo karibu kwa Wabunge wote wanaotoka katika Halmashauri za Wilaya. Wanayo maboma ya kutosha; maboma ya zahanati hatujaelezwa kwamba kuna maboma labda 1,000 yatakelezwa hivi; ya zahanati, kuna maboma ya madarasa, kuna maboma ya nyumba za walimu, kuna maboma ya vituo vy'a afya yatamalizwa namna gani? Hili hatujaelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ummy katika hotuba yake amesema amekarabati shule, mimi nashukuru. Shule ya Sengerema Sekondari imekarabatiwa kwa shilingi bilioni 1.2 lakini shule hii...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha muda wa
Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana. Ahsante Mheshimiwa.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Namwomba tu Mheshimiwa Ummy

Mwalimu aangalie suala la Sengerema kwa upande wa watumishi wake kuanzia Mkurugenzi, *Engineer* na *DT*, ni kwamba tayari sasa hivi wanajua safari yao imeiva, wanataka wanyakue hizi fedha haraka. Nakuomba sana uzizue hizi fedha kwa haraka sana. Hizi fedha zizuiwe leo dada yangu, la sivyo nitakunyang'anya shilingi.

Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko.

MBUNGE FULANI: Jambazi!

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya TAMISEMI. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja nisije nikasahau.

Mheshimiwa Spika, kilio kikubwa kila mahali kwa kweli ni *TARURA* na waathirika nadhani ni sisi wote Wabunge ambao tupo humu. Nilikuwa na wazo moja, hivi haiwezekani kuunganisha Wakala wa barabara *TANROADS* na *TARURA*? Maana yangu ni kwamba wangeunganishwa hawa halafu labda Waziri akawa mmoja na watendaji kama Makatibu Wakuu wakawa tofauti ili *center* ya fedha iwe moja kwa ajili ya ufanisi wa hii *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, maana yake *TARURA* kwa kweli bajeti yake pamoja na kwamba imetengwa, lakini bado ni ndogo ukilinganisha na matatizo ya *TARURA* yaliyoko kila mahali. Kwa mfano, Tabora tunaitwa Toronto; ni pale mjini. Ni kweli Tabora ukitelemka usiku ni kama Toronto kweli, lakini ni mjini. Ukienda vijijini hali ni mbaya, barabara ni mbaya kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la walimu. Walimu wengi wamejaa mijini na hasa kwenye Shule za Msingi. Wengi wamejaa mijini na shule za mjini zimefurika. Vijijini kuna shida

sana ya walimu kukaa. Sasa najiuliza ni kwa nini? Moja ya sababu ni mazingira yenyewe ya maeneo ya vijijini ambayo walimu wanakimbia kukaa huko. Nilikuwa naishauri Serikali iangalie ni njia gani mbadala watafanya kuweza kuwashawishi walimu wapende kukaa vijijini kama ambavyo wanakaa mjini. Vinginevyo huu wimbo wa upungufu wa walimu vijijini utaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye vituo vya afya kuna juhudii kubwa zinafanyika, nyingine ni za wananchi wenyewe kujitolea kujenga vituo vya afya. Hali bado siyo nzuri, nadhani ni katika nchi nzima ingawa kwa mfano Tabora tunacho Kituo cha Afya cha Maili Tano; kituo kile, kile chumba chake cha upasuaaji *theater* kuna kitanda tu ambacho alitoa mdau mmoja. Hakuna vifaa vingine vyovoyote vile vya kuwezesha kile kituo kiweze kufanya kazi. Kwa hiyo, naomba Wizara iweze kutusaldia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine kwa idhini yako, nimejaribu kuangalia kwenye kanuni kama ningeweza kuomba mwongozo kwenye kanuni, nimeona siyo jambo ambalo limetokea leo, lakini kwa idhini yako hata hii Wizara naomba uniwezeshe au unipe ruhusa niweze kuchomekea jambo. Kuna vijana wale ambao wamefukuzwa, walikuwa wanajenga Ikulu, wapo kama 854. Vijana wale walikuwa mionganoni mwa wale 2,400.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkuu wa Majeshi ameshatoa *ruling* ya vijana wale kuondolewa au kufukuzwa, maana yake wamesharudishwa makwao. Nilikuwa na ombi, siyo kwamba naunga mkono vitendo ambavyo wamefanya wale vijana vya kutaka kugoma, lakini naangalia pia *impact* yake kule walikokwenda kwenye maeneo yao na sehemu mbalimbali. Hawa vijana wamefanya kazi kwa miaka karibu mitatu na kweli waliahidiwa ajira na Mheshimiwa Rais ambaye sasa ni Hayati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninahisi ni pamoja na mkanganyiko wa mawazo. Kwanza kwa kuondokewa na Mheshimiwa Rais, lazima watakuwa walichanganyikiwa.

Walisahau kwamba na Mheshimiwa Rais ambaye yupo sasa majukumu yale atayatekeleza kama kawaida. Nadhani iliwachanganya; nahisi, mimi kama Mwakasaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaombea vijana hawa kwa Amiri Jeshi Mkuu ambaye ni Mama Samia Suluhu Hassan, kama wanaweza kusamehewa, ni kweli wamefanya jambo ambalo kijeshi wanaita ni uasi, walitaka kuandamana, lakini tuangalie na *fate* zao wenye na familia zao wanakoenda. Namwomba sana Mheshimiwa Rais kama itampendeza kuwasamehe vijana hawa wamejitolea sana kujenga ikulu yetu na nina hakika waliko wanajutia kile walichotaka kukifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel A. Mwakasaka, nishamtaja Mheshimiwa Esther Matiko na atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Silanga.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami napenda kuchangia kwenye Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo ni wizara muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Nitajielekeza sana kwenye elimu na ni dhahiri kwamba kuititia elimu bila ada udahili wa wanafunzi kwa shule za msingi na sekondari umeongezeka, lakini kunakosekana mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba kunatolewa elimu bora. Nitaenda kuainisha baadhi ya maeneo. Tumeshuhudia kuwepo kwa uhaba wa Walimu ambazo ni *inputs* nzuri sana kuhakikisha kwamba tunatoa *products* au *output* ya vijana wetu wenye elimu bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uhaba wa Walimu mathalani kwa Mujibu wa *BEST* 2020, takriban walimu 50,000 kwa shule za msingi. Waliopo 191,000 na kitu na tunaambiwa hapa na waziri amesoma tuna wanafunzi milioni 11. Hasa unaweza ukaona Walimu waliopo wanaweza kukidhi kweli kufundisha kwa ikama inavyosema Mwalimu mmoja angalau kwa

wanafunzi 45, unakuta wanaenda zaidi ya hapo. Tunajua kwamba kila mwaka au kila mwezi, kuna ambao wanafariki, wengine wanaacha kazi ya ualimu wanakwenda kwenye kazi zingine na huko nyuma waliondoa wa vyeti *fake*, lakini *replacement* katika kuhakikisha kwamba Serikali inakuja na mpango mkakati kuajiri Walimu wa kutosha ili kuweza kutatua changamoto ya Walimu haipo. Unakuta shule moja huko vijiji kuna Walimu sita, wawili, watano, wanafunzi 800 *it's quite unfair*. Kwa hiyo hapa, niseme hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Walimu hao pia ni dhahiri kwamba Walimu pamoja na kwamba wanakuwa na *workload* kubwa sana, lakini wana mazingira magumu sana, sana. Hawana nyumba, haa kama wamesema wanajenga hapa, lakini Walimu wengi hawana nyumba, lakini mazingira ya kufundishia pia ni magumu, wengine wanakaa kwenye milti, hawana ofisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia hawajapandishwa madaraja na kulipwa mishahara kwa muda mrefu kwa kipindi cha miaka mitano yote, wanatoa wapi motisha. Nikawaza sana, hapo zamani Walimu walikuwa na *hardship allowance* 150,000 *I think*, kama yalivyo kwenye upande wa majeshi, tufikirie sasa Walimu ni kada moja muhimu ambayo inaelimisha wanafunzi wetu. Tufikirie kurudisha hii angalau kuweza kuwapa motisha Walimu wetu, tuwape kila mwezi, katikati ya mwezi na wenyewe waweze kupata ile 150,000 ambayo walikuwa wanapata *as a flat rate* ili kuwapa motisha zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kingine ambacho nazungumzia kama kichocheo cha kuhakikisha tunapata elimu bora; miundombinu ya kujifunzia wanafunzi wetu. Madarasa yameendelea kuwa na uhaba sana. Iazima tuje na mpango mkakati, tusikae kwa kusubiria matakamko, maana hapa juzi kati niliona Ubungo huko shule moja sijui inaitwa King'ong'o, ilitokea tafrani fulani wakaandika katika mitando na nini, hayati akatoa tamko, *within a week or two* tunaona shule imekamilika. Sasa lazima Wizara ije mpango mkakati iwekeze kuhakikisha inatatua tatizo la madarasa nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia ripoti ya *CAG*, ameainisha pale kabisa kwamba uhaba wa madarasa *out of eleven million or so* wanafunzi, zaidi ya wanafunzi milioni tano *point something* hawana madarasa, kwenye ripoti ya *CAG* imeonesha. Vile vile hata miundombinu ya vyoo, ripoti ya *CAG again nai-quote*, imeonesha kabisa kwamba takriban wanafunzi 6,150,000 hawana matundu ya vyoo. Sasa bila hivi unakuta shule zetu zingine zinapelekea kufungwa. Hatuwezi kukaa tukasema tunatoa elimu bora *while* hatuna mazingira wezeshi kuhakikisha kwamba hii elimu bora inapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, madawati, bado ni tatizo. Wanafunzi wanakaa kwenye mawe na hii ripoti ya *CAG* *quote* walivyofanya ripoti ya ufanisi katika shule hizi, 1.1 wanafunzi wanakosa madawati. Tumesema elimu bila ada lakini unakuta wazazi wanachangishwa sana, anachangishwa kupeleka madawati, anachangishwa ajenge miundombinu ya darasa, ifike kwenye *rental*, anachangishwa hela ya mlinzi, anachangishwa 1,000 au 2,000 kuweza kulipwa Walimu wa ziada kufundisha wanafunzi wetu. So, it's a burden, kama nchi lazima tujitoe. Wizara hii ikiamua kujitoa pamoja na Wizara ya Elimu tuwekeze, mbona kwenye uchukuzi tumeweza! Tunawekeza kule *trillions of money*, hebu sasa tuwekeze kwenye elimu, *once and for all* tuwe na Walimu wa kutosha, tuwe na madarasa ya kutosha, tuwe na maabara ya kutosha, tuwe na vyoo vya kutosha vyenye umeme, *we are in science and technology era*, tuwe na umeme kwenye mashule yetu, tuweze kuwa na *computer and so called*, tuweze kuwa na maji, vinginevyo hatutaweza *ku-move* popote kama Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kingine, kwenye elimu hapo hapo; ukiangalia *NECTA* kweli kupitia udahili huu, ukiangalia matokeo utasema ufaulu umeongezeka, lakini kiuhalisia ukiangalia tathmini ubora wa elimu unazidi kushuka. Ukiangalia watoto wanaofaulu kwa *rank* ya *Division IV and Division. 0* ni wengi sana. Kuna tathmini imefanyika mathalani *for last 10 years, Division 1 – 3 ni only 36%, the rest wanakuwa below that*, sasa hatuwezi kukaa hapa tukasema tumejenga

madarasa kweli, tume-enroll watu wengi shule ya msingi kuititia elimu bila ada lakini *output out of it* kama Taifa tunapata nini. Lazima tuangalie hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwenye *quality assurance*; udhibiti ubora wa elimu zetu, imekuwa ni kitendawili, bila kuwa na kitengo ambacho kinakuwa *well equipped* na *human resources* kwa maana Wadhibiti Ubora, kinakuwa *well equipped* na bajeti ya kutosha, hatuwezi kuwa na elimu bora. Nimejaribu kuangalia pale kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wadhibiti Ubora *by then* walikuwa 1,081 tu, mahitajio yalikuwa 1,541, *deficit* ya 460. Hata hivyo Bunge hili Tukufu limekuwa likipitisha hapa fedha; 2018/2019 tulipitisha 1.5 *billion*, kwa ajili ya hii Idara ya Udhibiti Ubora, lakini hakuna hata senti tano ambayo ilikwenda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020/2021 Bunge lako *liliidhinisha billion* 25 kwa ajili ya kuimarisha Idara hii ya Udhibiti Ubora, lakini mpaka Machi *by then* 2020 hakuna hata senti tano imekwenda *out of this 25 billion*. Kwa hiyo, tumeidhinisha hapa, *nothing is being done*, kama hakuna Wadhibiti Ubora wa kwenda kuhakikisha kweli elimu inayotolewa ni bora, tunafanya *mark time* tu kama Taifa. Kwa hiyo tuhakikishe tunawapeleka Wadhibiti Ubora wa kutosha, tuhakikishe tunaweka bajeti ikipitishwa hapa inaenda, kuhakikisha kwamba wanapata miundombinu imara kwa maana ya magari na kila kitu kwenda kufanya ukaguzi huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, muda unaenda, lakini kingine ambacho nilisema nitagusia, ni hili suala la elimu jumuishi kwenye shule zetu. Limekuwa likiongelewa hapa nashukuru wame-quote, kwa hiyo shule zetu hizi lazima pia tuwe na miundombinu rafiki ambayo inawezesha wenzetu mathalani wenye ulemavu kuhakikisha kwamba na wao wanapata elimu stahiki. Kama tunajua tuna shule na zingine zinachangamana kwa mfano shule ya msingi pale Buhemba Tarime, inachangama na watu wenye ulemavu. Wengine wenye uono hafifu, usikivu na watu wenye ulemavu wa akili, unakuta wapo pale, lakini Serikali haipeleki Walimu wa kutosha, haipeleki miundombinu stahiki kwa hao watu ili na

wenyewe waweze kupata elimu kama wenzao wanavyopata. Pia hata miundombinu hii tunayojenga, mathalani kwa watu wengine wenyewe ulemavu haina zile njia za kupita wao, kuhakikisha kwamba huyu mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa-*accept*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pia katika shule za msingi na sekondari, watoto wa kike wengi wanaacha kwenda shule *between four to five days*mpaka *six days*wakiwa wameingia kwenye *menstrual period*, wanashindwa kuwa na usaidizi mathalani, anashindwa kuwa usaidizi na hili tumelipigia sana kelele Mheshimiwa Ummy Mwalimu anajua tangu akiwa Waziri wa Afya unajua. Tunataka kujua katika ile ruzuku ambayo inakwenda angalau waweze kutenga *extra*, waweze kuainisha, mathalani katika shule ya msingi wanajua watoto waliofikia umri wa kwenda kwenye hii kitu wako labda 200 au sekondari wako wangapi, waweze kupeleka *extra* katika hayo. Pia na hao watu wenyewe ulemavu waweze kuwa wanaongeza *ku-catch* hiyo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Dakika mbili Mheshimiwa Spika nimalizie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, dakika mbili tu. Katika hili la ruzuku ya 10,000 tumekuwa tunashuhudia inabaki 4,000 kama *retention* ambayo inatakiwa Serikali inunue vitabu, lakini *for right four years* haijawahi kupeleka hivyo vitabu na ukifanya *calculation*, nilikuwa nafanya haraka haraka hapa, kwa mwaka wanabakisha *over 44 million*, kwa miaka mitano karibu milioni 220. Tukienda mashulenii, tunaona bado kuna uhaba wa vitabu kwa hawa wanafunzi. Kwa hiyo kama Serikali wakibakisha hizo fedha wanaona ni ngumu kupeleka, bora ziende kule, Mwalimu husika aweze kuwajibika kuweza kununua hivyo vitabu kuliko kubaki huko Serikalini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther N. Matiko, kwa mchango wako. Mheshimiwa Njalu D. Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Ezra J. Chiwelesa*. Mheshimiwa Njalu D. Silanga.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza nianze kumshukuru Waziri pamoja na Manaibu wake wawili pamoja na Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri ambayo wanayoifanya katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe ushauri katika maeneo ambayo katika hotuba yao wameelezea. Wamezungumza suala la elimu, tuko na maboma mengisana kwenye halmshauri zetu nchini, ambayo wananchi wamejenga kwenye kwa nguvu zao, lakini Serikali imeendelea ikileta fedha kidogo kidogo na kuanzisha miradi mipya. Ningetoa ushauri kwa sababu ile miradi inasimamiwa na halmashauri, fedha zinazopatikana angalau zingekuwa zinakwenda kumalizia zile nguvu za wananchi ambazo tayari majengo yalishajengwa kwa maana ya zahanati, vyumba vya madarasa, pamoja na maabara ambavyo itatusaidia. Jambo hili litawatia moyo wananchi kwenye maeneo yetu kwamba Serikali sasa inakuja kuunga nguvu ya madarasa, zahanati kwa yale ambayo yamejengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri amezungumza ataanzisha sekondari, kwenye wilaya yangu nina kata 22, lakini nina kata mbili ambazo hazina sekondari, lakini kata zile mbili, tayari wananchi wameshajenga, Kata moja ya Nkuyu imejengwa kupitia kusaidiwa na *TANAPA*, tumejenga madarasa manne na yamekamilika bado hatujapata utawala pamoja na nyumba za Walimu. Ningeomba tu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa sasa kwenye mpango huu watuletee hizo fedha kumalizia haya maeneo mawili ikiwepo Ndobola pamoja na Nkuyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *TARURA*; kwenye eneo lao la hotuba yao wameelezea vizuri sana kufungua fursa za kiuchumi. Uchumi hauwezi ukaufungua kama wananchi hawafikiwi na huduma ya barabara pamoja na zingine. Ningiomba Serikali pamoja na kile kidogo kinachopatikana, muundo huu wa *TARURA* wajaribu kuungalia vizuri. Sasa hivi mamlaka yote yapo mkoani, Afisa aliyeko kwenye halmashauri hiyo, yuko peke yake na wasaidizi wake. Kwa hiyo chochote kinachotolewa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kinafika tu taarifa, mamlaka yote yatafanyika mkoani na baadaye ndio yatashushwa huko kwenye halmashauri. Hatuwezi kwenda na *speed* tunayoitaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni muhimu sana, ukizungumza Diwani au Mbunge hawezi kuwa kila wakati anakwenda mkoani kwenda kuuliza, barabara yangu imefikia hatua gani, *tender* imetangazwa lini, yaani ni changamoto na ukiangalia kwenye hotuba yao wameelezea vizuri kwamba barabara zinazopitika ni asilimia 15. Sasa angalia nchi nzima ina halmashauri 180, ina ukubwa wa eneo gani na mahitaji ni katika maeneo yapi, lakini bado kunakuwa na changamoto hapa. Huwa najiuliza mtu wa *TARURA* yupo chini ya Ofisi ya Rais na Mkurugenzi yupo chini ya Ofisi ya Rais, kuna nini hapa katikati, haya mahusiano ya watu wawili kati ya Mkurugenzi na Msimamizi wa *TARURA* wakawa kitu kimoja na wakafanya kazi kwa pamoja. Likifanyika hili litatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninayo changamoto kubwa ya madaraja yanaunganisha kati ya wilaya nyngine na Wilaya ya kwangu Itilima. Watu wa Itilima hawawezi kutoka Itilima kwenda Bariadi mvua zikinyesha, kuna daraja linaitwa Bulolambesi. Wangetusaidia *TARURA*, watutengee bajeti kwa sababu bajeti inayokuja haitoshi kabisa kukidhi mahitaji katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo tumelizungumza sana. Mimi napakana na watu wa Kwimba na Mheshimiwa Marehemu Ndasa tulizungumza Bunge lililopita tukielezea

daraja la Sawida na hilo linaunganisha Mkoa wa Mwanza na Wilaya ya Itilima na Wilaya ya Maswa. Ningombwa watutengee kwenye bajeti hii, daraja lile lijengwe. Vile vile tunayo madaraja madogo madogo ambayo yanaunganisha kata na vijiji kwenye maeneo yetu, tunayo changamoto kubwa kwenye Daraja na Nhomango, nadhani wataalam kwenye kumbukumbu zao zipo, Walimu wanaofundisha wanatoka toka kata nydingine kwenda kijiji kile husika. Mvua ikinyesha Walimu hawawezi kwenda kutoa huduma katika Kata ya Nhomango. Nalo ningeomba Serikali iweze kututengea hicho kilichopo, ili maeneo hayo yaweze kupata huduma safi na salama, wananchi wetu waweze kupata huduma hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais, hayati Dkt. John Pombe Magufuli, lakini kuna ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye kampeni alipokuja kuzindua pale makao makuu. Tulimwomba lami, Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu, Makamu Makuu ya Lagangabuli ameshafika, tunamwomba sana angalau Wasukuma pale Lagangabuli wapate lami, wamkumbuke mtani wangu kwa kazi kubwa ambayo atakuwa anaifanya kama alivyosema mwenzangu, ameingia na yeye ni jembe kama jembe liliokuwepo kwenye eneo hilo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika vijiji vyetu, Serikali hii ya Awamu ya Sita naamini kwenye hotuba hii waliyolizungumza, watafanya mambo mengi na makubwa na matarajio ya Watanzania tunahitaji yale ambayo wameweuka kwenye hotuba yao yaweze kujibu na yaweze kuleta mabadiliko makubwa sana, hasa kwenye sekta ya afya. Wametutajia fedha nyindi ambazo wamezitenga, naamini kabisa kwa usimamizi mahiri fedha hizi zitafika na zitafanya kazi vizuri sana na sisi kule kama Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani tuko tayari kutoa msaada na ushirikiano wa hali ya juu ili kusudi azma ya Serikali ya Awamu ya Sita iweze kufikiwa kwa kutimiza malengo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunacho Kituo cha Afya Kabale, kuna daraja na bahati nzuri Naibu Waziri wa Afya ni mwenyeji

kwenye maeneo yale. Kile kituo mvua ikinyesha hakifiki, naomba kutoka Nzanzui kwenda Kabale watuwekee angalau fungu kidogo ili eneo hilo liweze kupidika; Kabale pamoja na Lalang'ombe.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, naunga mkono bajeti ya Rais kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Njalu Silanga, Mbunge wa Itilima. Nilikutaja Mheshimiwa *Engineer Ezra J. Chiwelesa* na Mheshimiwa Dennis L. Londo atafuatia.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pia nimpongeze waziri kwa hotuba nzuri ambayo ame-*present* hapa na timu yake kwa ujumla. Sitakuwa mbali na wachangiaji wenzangu walotangulia, ningependa nijikite katika suala la *TARURA* pia, ila sitajikita zaidi katika kulalamikia mazingira nataka kutoa ushauri. Nitoe ushauri hasa kwenye mgawanyo wa fedha kama Waziri ama Serikali ipo hapa itatusikia, itakuwa vizuri zaidi maana nimekuwa najaribu kupidita.

Mheshimiwa Spika, ukijaribu kuangalia *network* ya barabara ambayo ipo chini ya *TANROADS* naambiwa ipo chini ya *TARURA*, *TARURA* wanahudumia barabara nyingi zaidi. Hata hivyo, kuhudumia barabara nyingi zaidi si sababu tu, ni kwamba pesa kubwa inayoelekezwa *TANROADS* ku-*maintain* barabara ambazo zimejengwa kwa gharama kubwa zaidi ambazo tunajua ziko *durable* zaidi, naona haina uwiano halisi na fedha zinazoelekezwa *TARURA* ku-*maintain* barabara za vumbi, barabara za changarawe na barabara za udongo kwa sababu nadhani wana kilokita 78,000 za barabara za undogo. Sasa barabara ya udongo *always* mvua inaponyesha, barabara ile sio barabara tena inakuwa tope na uharibifu unaanzia hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, *TARURA* wanahudumia sehemu ambayo wengi wa wapiga kura na watu ambao

wametuchagua kutuleta hapa wanaishi huko kwenye hayo mazingira. Kwa sababu ni barabara ambazo ziko kwenye Serikali za Mitaa, ahadi tulizozunguka tukaliliwa barabara na wananchi, hawakuwa wanatulilia barabara za lami zile kubwa hapana, sehemu kubwa ya nchi imeshaunganishwa. Walikuwa wanalia na barabara za vijijini, barabara zile ambazo wakulima wapo kule wanalima lakini wanashindwa kutoa mazao na watu wanaumwa wanashindwa kufika kwenye hospitali. Hizo ndizo barabara ambazo hata sisi wakati wa kampeni walio wengi humu, tumeletwa hapa na wananchi walituuliza tukasema tutazishughulikia. Sasa niiombe Serikali, kama hawataweza kutusaidia kwenye suala hili, wakajaribu kuangalia mgawanyo mpya, aidha kama wanaona ule mgawanyo uendelee kubaki *TANROAD*, basi waje na *alternative* ya kupata fedha ili tuweze kupata fungu kubwa kwenye upande wa *TARURA* ili iweze kutusaidia sisi kama Wabunge na hasa wananchi ambaao wako kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo kwa upande wangu nilikuwa najaribu kuliangalia kwenye wilaya yangu. Nilivyozunguka kwenye kampeni na sehemu kubwa kitu ambacho nilikiona, wananchi hasa wa upande wa vijijini, naomba Serikali wajikite kwenye kujenga madaraja. Huko vijijini wananchi wanachokwama zaidi ni madaraja, maana utakuta mvua imenesha, mtu anaumwa, kuna bodaboda ndio usafiri, vijijini hawatumii magari kwa sehemu kubwa, labda nyie kwenye wilaya zenu, lakini kwangu sehemu kubwa za vijijini wanatumia bodaboda, wanatumia miguu na baiskeli. Kwa hiyo, mvua zinaponyesha kwenye msimu huu, kuna sehemu madaraja hayapitiki kabisa, unakuta daraja limefunga kata mbili, limefunga vijiji sita, limefunga vitu vingapi, kwa hiyo wajaribu kutusaidia. Fedha nyangi ya *TARURA* ieletekezwe kwenye *ku-maintain* madaraja.

Mheshimiwa Spika, kujenga madaraja sio kitu kigumu, kuna makampuni hapa yanatengeneza mabomba yale makubwa, bomba linaenda mpaka *three meters*, hata kama ni kina kikubwa sana, wapo *Pipe industries*, wapo *PLASCO* tunajua. Ukienda hata Ngorongoro *Craters* kule chini, mabomba yanayotumika sasa hivi kutengeneza madaraja

kule mbugani ni mabomba ya plastiki. Kwa hiyo wangeweza kwenda kununua, lile halihitaji mkandarasi, mtu tu wa kawaida, a *normal technician* anaweza kufanya ile kazi kule kijijini. Kwa sababu atachimba na wananchi, wataingiza lile bomba pale na watafukia, watajengea *cement* huku na huku basi kitu kinaenda. Ile *Force Account* wanayoitumia huko *TARURA* kwenye madaraja vijijini inaweza ikatusaidia zaidi tukaweza kupunguza gharama lakini tukasaidia watu wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nataka niongelee suala la shule. Niipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanazidi kuifanya. Nadhani kwa *record* kubwa tuna kikosi kukubwa sana ambacho tunategemea tunaanza kukipokea kwenye shule za sekondari, nadhani miaka miwili au mitatu, maana mazao ya elimu bure ile sasa ambayo Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli allianzisha, tunaanza kuipata nadhani miaka miwili au mitatu ijayo. Wale ambaو wallingia darasa la kwanza bure, nadhani sasa hivi wako darasa la sita, either wengine wanaeleke la tano, kwa hiyo ule wingi mkubwa tunaanza kuuona huko.

Sasa naomba Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tunaomba waje na mpango mkakati wa miaka hii miwili au mitatu inayokuja, ili waweze kutusaidia, maana Watoto kule vijijini ni wengi na wale watoto wana akili watafaulu, kwa hiyo tunachotegemea, wasifafulu wakaishia kubaki vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu sisi kama wawakilishi tutakuja na kazi nyingine ya kurudi kwa mzazi anayekwambia mimi bwana mtoto wangu amefanya vizuri lakini amekosa shule. Mimi Mbunge siwezi kujenga shule, lakini Serikali inaweza kujenga shule, kwa hiyo watusaidie. Nataka nitoe mfano hapa, kwenye jimbo langu kuna shule moja ya msingi kwenye Kata ya Nemba, shule nzima ina wanafunzi 4,819, ila ina vyumba tisa vya madarasa. Kuna maboma matatu sasa hivi wananchi wanahangaika ndio wanayanyanya matatu mengine, Wizara ingeweze kutusaidia kuyaezeka sasa angalau wawe navyo 12.

Mheshimiwa Spika, lakini nilipokuwa napitia hii shule, ni shule ya kata. Darasa la saba sasa hivi wako 276, la sita wale wako 703 kwenye shule moja tu. Hii shule inahudumiwa na shule moja ya sekondari ambapo shule moja ya sekondari ukiangalia watoto walioko darasa la sita maana yake walioko *form three* leo wanavyoondoka kumaliza *form fourwao* ndiyo watapisha *room* kwa ajili ya watoto walioko darasa la sita. Sasa *form three* wako 999 hawafiki hata 100 lakini shule hii *ita-release* watoto zaidi ya 700 wanaingia sekondari. *Of course*, hata wakifeli labda haiwezi kuwa chini ya asilimia 90 maana kwa Kagera Biharamulo sisi hatujapungua chini ya asilimia 95 kwneye ufaulu wa *primary*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina uhakika watoto si chini ya 600 kutoka kwenye shule moja tu wanatakiwa waende sekondari. Sasa wanaendaje sekondari kwenye shule ambayo leo inatoa wanafunzi 99 inapokea zaidi ya 600. Na hawa 600 ni kwenye shule moja ya msingi na hii shule ya sekondari inahudumia shule za msingi takriban nne. Kwa hiyo, ninategemea hawa watoto zaidi ya 1,000 watakuwa wanafaulu kwenda *form one*. Sasa shule hii mjaribu kutusaidia. Kwa hiyo ningeomba sasa Mheshimiwa Waziri mje na kikosi maalum cha kuzunguka kwenye kata. Shule hizi za kata tulizozianzisha za haraka haraka hizi zinaenda kuzaa matunda. Zisizae matunda watoto hawa wakabaki mtaani maana wengine ni darasa la saba akimaliza kabaki mtaani anafanya nini? Hatuna vyuo vya ufundí sehemu hizo maana ziko kwenye kata bado. Kwa hiyo, mtusaidie kwenye hilo ili watoto hawa tuwatoe hapa walipo tuweze kuwasogeza mbele zaidi na wao wayafikie malengo ya kuwa madaktari, wahandisi, walimu, maaskari, wanasheria na kada nydingine ambazo wanategemea wazifanye. (*Makofí*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili wakati wa kampeni mwaka jana kuna jambo lilitokeza. Huenda lilikuwa nchi nzima au lilikuwa kwenye wilaya yangu ya Biharamulo lakini naongelea kwa *experience* yangu. Suala la vitambulisho vya wajasiriamali. Suala la vitambulisho vya wajasiriamali mwaka jana liliteta *saga* sana Biharamulo. Watu wakawa wanaona sasa wanalazimishwa kuwa na vitambulisho vile, vurugu

zikawa kubwa sana lakini baadaye kwa busara yale mambo yakaja yakatulia. Sasa juzi wiki iliyopita wenzetu waislamu wameanza mfungo siku ya Jumatano. Biharamulo tuna gulio siku mbili, tuna gulio siku ya Alhamisi na tuna gulio siku ya Jumapili sehemu ile ambayo sasa hata wakulima na yeote yule anayejisikia kuuza anakuja sokoni kuuza.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sasa maelekezo mahsusiyatolewe. Tutofautishe wakulima wa kawaida na wafanyabiashara wadogo wadogo. Kuna mama yangu kule kijijini anabeba ndizi, shilingi 5,000 ukipeleka ndizi sokoni na *basically unachoenda kukifanya sokoni ni barter trade*. Mtu analeta mkungu wa ndizi shilingi 5,000... (*Makof*)

SPIKA: *Engineer* muda sasa.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, nimalizie dakika moja. Mtu analeta mkungu wan dizi shilingi 5,000. Anavyofikisha mkungu wa ndizi shilingi 5,000 akimaliza kuza anaondoka na chumvi, sukari, habaki hata na shilingi ya hela. Lakini mtu anataka yule mtu awe na kitambulisho cha 20,000. Ndugu zangu tuliozaliwa vijijini tunajua, kuna watu huko unamuuliza leo ni mzee, hajawahi kuwa hata na shilingi 5,000 mfukoni. Ukimuambia atafute shilingi 20,000 na kukata kitambulisho ili alete ndizi sokoni tunamuumiza. Kwa hiyo ningeomba hilo jambo tuliangalie tuweze ku-*harmonize* hao watu ili *situation* irudi kawaida na hakika Serikali hii ni Sikivu mtawenza kutusaidia ili wananchi wetu huko waweze kufanya kazi anayeuzua auze, anayelima alime lakini wafanye kazi kwenye mazingira mazuri. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Londo,

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa. Ofisi au Wizara hii ni muhimu san ana tunajadili bajeti ambayo imebeba hatma ya wengi kwenye nchi yetu. Kwa

umuhimu wake ina mafungamano ya karibu san ana Wizara nydingi na Taasisi nydingi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunapojadili Wizar aya Ofisi ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa kuna kilimo humo ndani, kuna afya humo ndani, kuna uvuvi humo ndani, kuna barabara humo ndani, kuna afya na vitu vingi humo ndani. Kimsingi kwa muundo wa Ofisi hii ya Rais Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa ndiyo ambayo inashuka mpaka chini kwa wananchi. Kwa hiyo, tunapoizungumzia Serikali kwa mwانanchi wa kawaida tunazungumzia Halmashauri za Vijiji, Mtendaji wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kijiji ambaye anaangukia katika Wizara hii. Kwa hiyo, tunazungumzia bajeti muhimu sana na utendaji kazi wa Wizara hii pamoja na majukumu yake kama yalivyoainishwa kutoka ukurasa wa tisa mpaka wa 15 inaonesha uzito na dhamana ambayo inaangukia katika Wiara hiyo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu hawakumbani na Serikali mara kwa mara. Mwananchi wa kawaida kule kijijini anakutana na Seriali pale ambapo anahitaji huduma katika kituo cha afya, katika Ofisi ya Mtendaji Kata, katika Ofisi ya Afisa Elimu Kata ama Mwalimu Mkuu na hawa wote wanaangukia katika Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kwenye majimbo yetu ambako tunatokea, wananchi wana imani kubwa sana na Serikali hii lakini hiyo haiondoi ukweli kwamba kuna nakisi ya imani kwa Serikali za vijiji ama kwa kiingereza tunaweza tukasema kwamba *public trust deficit* kwa wananchi kitu ambacho kinatuweka kwenye *dilemma* kwa kiasi kikubwa. Kuna migogoro mingi ya ardhi, viwanja, mashamba yanagawiwa bila kufuata taratibu wala sheria. Kuna changamoto kubwa ya watu kuonewa kule bila kufuata sheria lakini hayo yote ukija kufuatilia kwa makini yanatokana na uwezeshwaji wa hawa watu. Je, wana elimu ya kutosha kulingana na majukumu ambayo wameyaomba? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu wamechaguliwa katika nafasi zao kama Wenyeviti wa Serikali za Vijiji. Je, wamepata

seminary ya jinsi ya kuongoza watu, sheria ambayo inaongoza mamlaka za vijiji na vitu vingine. Kwa hiyo, vitu hivi vinatusababisha katika migogoro mingi ambayo tungeweza kuitatua kama tungeangalia jinsi gani ya kuwawezesha hawa walau kuwapa elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata uwezeshwaji wa posho. Imekuwa shida sana kwa Wenyeiti wetu wa vijiji kwa hiyo naomba wakati tunapitisha bajeti hii tuangalie ni jinsi gani tunaenda kuwaangalia hawa watu amba ni muhimu sana. Mheshimiwa Chiwelesa amezungumzia kuhusiana na jinsi gani tumejiandaa na wimbi kubwa la watoto amba ni *graduates* wa elimu bila malipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka huu watoto amba wameingi akidato cha kwanza ni 800,872 ukilinganisha na watoto amba wameingia darasa la kwanza 1,500,000. Sasa udahili wa watoto hawa amba wanaingi akidato cha kwanza 800,000 haufanani san ana hawa watoto amba wameingia darasa la kwanza 1,500,000. Kwa hiyo, ni rai yangu kwa Wizara ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kuangalia ni jinsi gani tunajiandaa na hii *influx* kubwa ya watoto amba ni zao la elimu bila malipo ambalo linatokea 2022 ambapo ni mwakani tu. Kwa hiyo, tuna bajeti moja tu ya kujadili lakini bajeti ya 2022 tutakuwa na kazi kubwa ya kuangalia watoto hawa wanaenda wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nilikuwa naomba kutoa rai Ofisi za Vijiji na Kata uendeshaji wake unategemea sana asilimia 20 ya ruzuku ambayo inatoka Serikali Kuu. Lakini wote sisi ni mashahidi vijiji vimeduwa vikihangainka jinsi ya uendeshaji wa ofisi zao lakini hata kata pia na kuna kata ambazo ziko mbali sana kimiundombinu na ofisi za Halmashauri lakini Watendaji hawa Kata, Watendaji wa Vijiji hivi wanaitwa kwenye mikutano inabidi wahangaike watoe hela zao za mifukoni lakini kuna fedha za ruzuku za Serikali Kuu ambayo asilimia 20 inapaswa kwenda *lower level*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni rai yangu kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI kuangalia namna bora ya kuhakikisha fedha

hizi asilimia 20 za ruzuku zinaenda kule katika ngazi za vijiji na kata kurahisisha uendeshaji wa ofisi hizi ili kuondoa manung' uniko kwa watendaji wetu ambaao ni muhimu sana katika utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya Serikali Kuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nilikuwa naomba niunge mkono hoja ya Wabunge wenzangu ambaao wametangulia kuhusiana na suala zima la barabara. Tunazungumzia kuhusiana na suala zima la uzalishaji wa viwandani lakini kimsingi unapozungumzia uzalishaji wa viwandani unazungumzia kilimo na katika majimbo ya pembezoni kama Mikumi, kilimo ndiyo uti wa mgongo na kuna maeneo mengi ya uzalishaji na ninaomba kupitia Bunge lako nitoe mfano wa Kata moja inaitwa Vidunda.

Mheshimiwa Spika, kata hii ni kilometra 5 tu kutoka pale Kidodi ambapo ni barabara kuu lakini ndiyo Kata ambayo inalisha bonde lote la hapa chini Ruaha, Mikumi, Kidodi mpaka Morogoro na Dar es salaam. Kilometra hizi tano huwezi kwenda kwa gari. Tangu nimezaliwa nilikuwa nashuhudia watu wakishusha mizigo na matenga toka enzi hizo mpaka sasa. Hali hii inafanana sana na kata nydingine za pembezoni kama Malolo, Ulening'ombe, lakini kuna kata za chini kama Tindiga ambaao ni wazalishaji wakubwa sana wa zao la mpunga. Jan anilirusha *clipkwa* Mkurugenzi Mkuu wa TARURA na Maafisa wengine wa Wizara ya Ujenzi waone hali ilivyo. Ni umbali wa barabara kilometra mbili haipitiki hata kwa pikipiki, hali ni mbaya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uchumi wa viwanda tunazungumzia bidhaa za kilimo, unapozungumzia bidhaa za kilimo unazungumzia suala zima la uzalishaji, usafirishaji, na ufikishaji wa mazao sokoni. Unapomnyima barabara mtu ambaye kazi yake kubwa ni kuzalisha kilimo maana yake tunahujumu uchumi wetu sisi wenyewe lakini unapandisha gharama katika uzalishaji na mwisho wa siku unampandishia gharama mlaji. Tunazungumzia hali ni ngumu, hali ni ngumu kimsingi inatokana na gharama ya bidhaa za

kilimo masokoni ambayo tungeweza kuipunguza kama tungeweza kuboresha miudombinu. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Dennis Londo.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nashukuru. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Chinguile. Mheshimiwa Mtemvu. Oh, Mheshimiwa Chinguile basi, Mbunge wa Nachingwea.

MHE. AMANDUS J. CHINGUILE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara hii Ofisi ya Rais TAMISEMI. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza pia dada yangu Waziri Mheshimiwa Ummy na Naibu Mawaziri kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hizo. Natambua kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii ya TAMISEMI kwenye sehemu ya elimu, afya mmefanya kazi kweli kweli tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, wacha nizungumzie kidogo suala la *TARURA*. Ukiona mtu mzima analia kwakweli kuna jambo. Kwenye suala la *TARURA* Waheshimiwa Wabunge wengi kila anayesimama analia kuhusu *TARURA*, *TARURA* shida, changamoto.

Katika hili niiombe sana Serikali waone namna watakavyokuja na muarobaini kuhusu *TARURA*. Lakini *TARURA* hii nitazungumzia kwenye maeneo mawili, la kwanza kwenye muundo wenyewe wa *TARURA*. Yuko mtu anaitwa mratibu anakaa pale Mkoani, yeche ndiyo anafanya kila kitu, *tender* anatoa yeche na kila kitu. Sasa tumemuacha huyu meneja ambaye Yuko Jimboni, wilayani ambaye anajua sasa barabara gani ni kipaumbele, Yuko hana shughuli yoyote na hata tukizungumzia kwamba anashauri kule mkoani bado anayeshauriwa ana mambo mawili, kukubali au kukataa huo ushauri. Siku ya siku bado mkoani ndiyo wenyе mamlaka ya kuongeza wapi kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ukosefu wa hii bajeti. Kwa kweli mimi niiombe sana Serikali, dada yangu Ummu najua ni mchapakazi sana. Mheshimiwa hebu njoo na muarobaini kuhusu *TARURA* ni namna gani tunaweza tukaongeza mapato yatakayotuwezesha kufanya kazi kwenye sehemu hii ya *TARURA*, nikuombe sana na naamini hili kwa uchapakazi wenu kwa uzuri kama mlivyofanya vizuri kwenye maeneo mengine ambayo nimewapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie pia kuhusu watumishi hasa watumishi wa afya na walimu. Huko nako ni shida, sisi tunaotoka pembezoni mwa nchi, hawa watumishi huwa wanaomba maombi ya moja kwa moja kwenda kwenye maeneo yale kwa ajili ya kupata *cheque number* tu lakini baada ya hapo wote wanaomba kuondoka kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Wizara, hebu tuwe na mpango maksudi wa kuhakikisha kwamba hao wanaoomba kwenye maeneo yale kwakweli wanakwenda wakiwa na ari ya kufanya kazi na sio tu kwenda kwenye maeneo yale kwa ajili ya kuchukua *cheque number*. Hapo hapo niendelee pia kushauri Wizara kwamba basi tuwape kipaumbele, wako vijana ambao wametoka na wana-*apply* kutoka kwenye maeneo yale wameshayazoea. Hebu tuwape kipaumbele, sizungumzii kwamba wale wengine wasipate nafasi, la hasha lakini basi tuone mpango ambao utatuwezesha na sisi tulioko pembezoni mwa nchi kuweza kupata watumishi ambao kwa kweli watakuwa na ari ya kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine nzungumzie kwenye maboma. Maboma haya yako maboma ya zahanati lakini pia maboma ya shule za msingi na sekondari. Hebu tuuone huu mpango mkakati, kabla ya kuendelea na vipaumbele vipyta tuone mpango mahsus wa kwenda kumalizia haya maboma. Lakini tukifanya hivyo twende sambamba sasa na kuhakikisha vituo vyetu, shule zetu zinakwenda sasa kupata watumishi wa hapo niende kule kwangu kwenye

jimbo langu la Nachingwea, kuna kituo chetu cha afya Kilimarondo. Mheshimiwa Waziri ikikupendeza, ukipata nafasi twende utembelee eneo lle. Daktari yupo lakini pia na watumishi wengi wapo lakini hawatoshelezi. Eneo lle ni mbali kabisa kutoka Makao Makuu ya wilaya. Tuone namna maeneo yale tunavyoweza kuyapa kipaumbele ili basi waweze kupata watumishi watakaokidhi kwenye maeneo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kuzungumzia pia suala la Posi, zile mashine za kukusanya mapato. Huko nako iko shida. Wataalam wetu walio wengi haawana ufahamu wa kutosha na hasa kwenye zile kata. Tujikite kutoa elimu namna gani ya kutumia zile mashine kwa ajili ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea, kwa sababu maeneo mengine wako walipopata shoti kwa namna hii mashine ile hawezi kuitumia vizuri. Badala yake sasa wakati wa kutoa ripoti anakuta anachotakiwa kuwasilisha ni kikubwa kuliko alichonacho. Kinachotokea sasa wanafunika zile posi, anaiweka pemberi anaendelea. Sasa tuwe na mpango huo wa kutoa elimu kwa hawa wataalam wetu kule chini, tunajua wengine hawana taaluma hiyo ya uhasibu. Basi tuwape walau zile kozi ambazo zitawawezesha kupata ujuzi huo. Lakini pia kuhakikisha tunafuatilia kadri inavyowezekana, kadri tunavyopata muda ili mapato yanakusanya kisawasawa. Kuna mapato mengi yanapotea na nina hakika tukiimarisha kwenye eneo hilo kwa kweli tutafanya vizuri kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wako vijana wengi ambao kwa kweli wanalia. Nikionesha hapa *message* za simu za kila Mbunge hakuna atakayekuwa anasema mimi sina *message* ya kijana kutoka kwenye Jimbo langu hana ajira. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, tunajua kwamba kipato chetu tunachokusanya ndicho kinachokwenda kuajiri vijana au ajira mpya. Tuone namna ya kuongeza ajira, vijana wetu wako wasomi, wako huko mashambani, vijijini wanao ujuzi wa kutosha. Tuone namna ya kuwatumia hawa kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado niendelee kuzungumzia tena wale walimu au watumishi wanaotoka kutoka maeneo mengine kuhitaji kuhamia maeneo mengine hebu tujaribu namna ya kuyaona hapa. Mheshimiwa Waziri wako watumishi ambao wanataka kutoka Tanga kwenda Nachingwea mahali ambapo tuna shida ya watumishi sasa process zile zinazotumika ili huyu mfanyakazi kurudi kule ambako moyo wake unatamani ni shida.

SPIKA: Ahsante Mheshimia Chinguile.

MHE. AMANDUS J. CHINGUILE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amandus Chinguile. Mheshimiwa Edward Olelekaita Mbunge wa Kiteto atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwanza kabisa, nimpongeze Waziri na timu yake kwa hotuba nzuri sana. Niseme tu nilifarijika sana kuwaona Machifu wale kutoka Iringa na nguo zao za asili. Tujue tu nchi yetu ina tamaduni nyngi sana na style ziko nyngi sana za namna ya kutambua tamaduni hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI ni hati ya kila kitu kinachoendelea nchi hii. Kama nilivyokwishesema siku nyngi tu Mwenyezi Mungu awabariki sana watu walioandika llani hii. Niwatambue Mheshimiwa Dkt. Bashiru na Mheshimiwa Polepole wako hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunatafuta kura safari hii hatujatoa ahadi zile nyngi za wanasiasa kwa sababu llani ya Chama cha Mapinduzi imeweka kila kitu. Kwa hiyo, kazi yetu iliyobaki sasa ni kuhakikisha llani hii inatekelezwa kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wameongea Wabunge wengi hapa kuhusu *TARURA*. Nimshukuru, nilikuwa na jirani yangu hapa ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii ameniambia imeongezwa karibu bilioni mia moja na kitu kwa *TARURA*; kama ni kweli tuwapongeze sana, lakini bado Kamati imeendelea kusitiza nia ya kuiongezea pesa *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ya Kiteto tunatengewa shilingi bilioni moja, milioni 400 na...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Tabasam.

TAARIFA

MHE. TABASAM H. MWAGAO Mheshimiwa Spika, nampa Taarifa mzungumzaji, anasema *TARURA* imeongezewa bilioni 100 ni pesa ndogo sana hizo, hazitoshii kabisa. Naomba uendelee. (*Makofi*)

SPIKA: Unapokea Taarifa hiyo Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto?

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakubali na ninapokea Taarifa hiyo, lakini lazima tuseme kwamba wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anafunga Bunge la mwezi wa pili, alisema hivi, naomba nimnukuu: "Mheshimiwa Spika kumejitokeza mjadala unaohitaji uboreshwaji wa miundombinu ya barabara za mijini na hasa vijijini. Vyombo vya *TARURA* na *TANROADS* vinafanya kazi na sasa tutakusudia kuongeza uwezo wa vyombo hivi na hivyo Waheshimiwa Wabunge tumepokea ushauri wenu." Kwa hiyo, waliyofanya tuwashukuru, lakini kama walivyosema Kamati na kama alivyosema Mbunge aliyenipa taarifa, tuendelee kuongeza pesa kwa *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natoa taarifa tu kuhusu Kiteto, mfano, tunapata karibu shilingi bilioni moja na mia

nne na hamsini na nne na chenji kidogo, lakini uhalsia ni shilingi bilioni saba. Huo ni mfano tu kwamba tunahitaji pesa nyingi sana kwa *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mbunge wa Same, Mheshimiwa Mama Kilango, ni kweli Wilaya ya Kiteto ni kubwa unachukua Mkoa wa Kilimanjaro unachukua na Jimbo la Kongwa, *combine*, ndio Wilaya ya Kiteto, kubwa sana. Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba tunapotengeneza vipaumbele hapa tuangalie jiografia ya majimbo haya, ni kubwa sana. Mheshimiwa Spika alikuja kunitafutia kura, tumetembea kata nne tu, nakushukuru sana, lakini kila mkutano tuliofanya kero namba moja ni barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna Kata yangu moja inaitwa Dongo, yaani ni kubwa saba, kwa hivyo ndugu zangu tuangalie sana suala hili. kila mkutano niliofanya na nilikuwa naangalia *notice* zangu wakati natafuta kura, kila mahali nimekwenda changamoto naandika, barabara. Tukifanya hivyo Watanzania watakuwa wamefarijika sana. Barabara za Kata za Sunya, Asamatwa, Magungu, Dongo, Makame, Katikati, Robosoid, Mserengine, Olpopori, Kiberesa, Nigish, Mbeli na Kiteto ni *bread basket*, mahindi yote yanayokuja huku yanatoka Kiteto, kwa hivyo, tuongeze juhudhi katika kutengeneza barabara hizi ili wananchi hawa waongezee bidii.

Mheshimiwa Spika, hoja nyngine ambayo hata Kamati imesema, ni hizi asilimia 10 ambazo ziko kwenye llani yetu. Kwa hiyo, sisi ni kutembea na llani tu, ukurasa wa 30, tuwe wakali kwa halmashauri zile ambazo hazitengi asilimia kumi. Sio kwamba tu wana-*violate* takwa la kisheria, lakini hawasomi llani yetu. Kati ya vitu ambavyo Wabunge tunatakiwa tuwe wakali sana hapa ni tuhakikishe llani hii inatekelezwa kwa asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vituo vya afya. Ndio maana mimi nasema llani hii naipenda sana, inasema kila mahali tutajenga vituo vya afya, Wilaya ya Kiteto kati ya kata 23

tuna vituo vya afya viwili tu. Kwa hiyo, nafikiri tukija hapa mtuulize Bwana Olelekaita una kata ngapi ambazo hazina vituo vya afya, halafu tufanye *mathematics simple*, kila mwaka mnatakiwa mnipa ngapi ili baada ya miaka mitano tutekeleze, hivyo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukisema tunapeleka *computer* kwenye sekondari kadhaa, mimi ninazo 18, kwa hiyo, ningekuja tu hapa nidai *computerzangu* 18. Labda kitu cha kufanya pia ni kujaribu ku-*cost* hii llani yetu ili tujuue tunahitaji gharama ya shilingi ngapi miaka mitano ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi sasa kwa muamko huu ambaao umeoneshwa kupitia TAMISEMI wamechanga michango kwa ajili ya vituo vya afya; Dosidosi, Matui, Ndedo, kazi zinaendelea. Kwa hivyo, inatakiwa tu mkono wa Serikali kidogo ili tushirikiane kutekeleza llani hii. Kwa hiyo, tuangalie vipaumbele hivi na tutembelee maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekwenda kwenye kata moja katika mkutano wa hadhara, kumbe nikagundua wananchi wala hawataki hata ule mkutano wananiambia tu twende tukuoneshe kituo cha afya. Nilivyofika pale ikabidi niseme na mimi kwa Mfuko wa Jimbo nitaweka mkono hapa na nimeshafanya hivyo, lakini sasa pesa ya Serikali, mtuunge mkono ili wananchi wale wajue kwamba wakihangaika Serikali na yenye inaweka mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni hati. Walimu wapo wengi sana wanajitolea, wanaomba ajira hizo tena kwa miaka mingi tu. Mimi nilikuwa naongea na Afisa wangu hapa akaniletea karibu majina 100 tu kwa Kiteto na wako walimu wazuri wenye taaluma tena za Kiswahili, mabingwa. Tumepitisha sheria hapa ya kuruhusu Kiswahili sasa kianze kutumika na tuna wataalamu wamejaa wanasubiri.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa muda wako umeisha.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mbunge wa Kiteto. Nilishamtaja Mheshimiwa Kasalali Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi na Mheshimiwa Luhaga Mpina ajiandae.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hii hotuba ya bajeti ya Wizara muhimu kabisa ya TAMISEMI, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Dada yangu Ummy, hongera kwa kupewa hili jukumu zito. Sisemi kwamba, mwanzo alikuwa una majukumu mepesi, lakini kila mara amekuwa akipewa majukumu mazito anafanya vizuri. Nategemea kwa usaidizi alionao wa Manaibu Mawaziri kazi ataifanya vizuri; ndugu yangu Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Ndugange, najua kazi yenu mlivyokuwa mnafanya na sasa mnalo jukumu la kusaidiana na Waziri Ummy kufanya vizuri zidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri katika Wizara hii. Mheshimiwa Waziri na Manaibu wako mnaweza mkawa na mipango mizuri sana ya kufanya kwenye Wizara hii, lakini sisi sote Wabunge humu ni mashahidi kwamba Wizara ya TAMISEMI imekuwa na shida kubwa sana kwenye usimamizi wa pesa zinazopelekwa kwenye halmashauri zetu. Nimeona hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna kama shilingi trilioni 2.9 karibu shilingi trilioni tatu zinaenda kwenye miradi ya maendeleo. Hizi pesa ndizo pesa watu kule kwenye halmashauri wamejipanga kuzipiga. Hizi pesa asilimia kubwa zinaenda kufanya kazi ambazo sio zenyewe. Ili tuweze kufanikiwa kwenye halmashauri zetu hizi pesa zinazotumwa kwenda kule na pesa zinazokusanywa kule ni lazima tuziimarishe halmashsuri zetu. Kwenye kuimarishe halmashauri zetu ni lazima tufahamu nani hasa ni msimamizi wa hizi

halmashauri na kama zinafeli yeye anasababisha kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunakimbilia kushughulika na watumishi wa halmashauri, simamisha Mkurugenzi na Mkuu wa Idara, kabla hatujaangalia msingi hasa wa usimamizi mbovu wa pesa za halmashauri. Kwenye halmashauri zetu na sheria zinavyoonesha wasimamizi wakuu wa halmashauri ni Baraza la Madiwani. Mimi ni *ni-declare interest* nilikuwa Diwani wa Kata ya Lyoma kabla ya kuwa Mbunge wa Sumve. Kwa hiyo, ninao uzoefu kidogo wa kukaa kwenye Baraza la Madiwani nikiwa Diwani wa Kata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Mabaraza ya Madiwani ndiko huu mwanya wa upotevu wa pesa unaanzia. Hauwezi kumwambia Diwani akasimamie Wakuu wa Idara wanaomzidi malipo mara kumi. Tumewahi kuangalia maslahi ya wasimamizi wa halmashauri zetu? Hawa Madiwani wanaosimamia halmashauri, je, wanazo nyenzo za kusimamia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kinachoangaliwa hapa ni upotevu wa mapato. Diwani anaambiwa asimamie shilingi bilioni 30, hela anazolipwa ni kidogo sana. Malipo ya Madiwani ni lazima tuyaa ngalile, hawa wasimamizi wa halmashauri; watumishi tunawalipa pesa ili wasimamie vizuri kazi zao, lakini Madiwani kwanza malipo yao yamekuwa ya hisani, wanalipwa kutokana na mapato ya ndani. Mkurugenzi akijifikiria ndio anawalipa kama hisani halafu haohao wakamsimamie. Kwa hiyo, mwisho wa siku tunatengeneza mwanya wa hawa watumishi kutumia uwezo wao wa kipesa kuwarubuni hawa Madiwani wasisimamie mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali irudi iangalie kwanza, hata kwa hii pesa ndogo ya posho ya mwezi mnayowalipa Madiwani haitakiwi kulipwa kwa hisani ya Wakurugenzi iwe inalipwa kutoka TAMISEMI ili huyu mtu awe na nguvu ya kumsimamia Mkurugenzi. Kwa sababu siwezi kuomba hisani nasimama namshukuru Mkurugenzi, mimi nimehudhuria vikao vyta Baraza la Madiwani, Diwani

akisimama kwanza anamshukuru Mkurugenzi. Unamshukuru nini wakati wanaenda kumsimamia? Wanashukuru kwa sababu ili awe kwenye mgawo vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pesa za marupurupu ya Madiwani ya ulipaji wa vikao na nini, ninyi Wabunge ni mashahidi kwa vile ni Madiwani, halmashauri nyingi wanadai. Pesa za bima za afya za madiwani hazipelekwi zinakusanywa, inaonekana ile mikopo ya benki haipelekwi kwa sababu hakuna utaratibu maalum wa usimamizi wa suala hili. Sasa kama hatuwezi kusimamia maslahi ya Madiwani nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri TAMISEMI hutaisimamia vizuri, lazima utaratibu wa wasimamizi walioko kwenye halmashauri ubadilishwe. (*Makof!*)

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mbunge wa wapi? Ndiyo nakuruhusu endelea.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, naomba tu nimpe Taarifa mzungumzaji anayeendelea kwamba, baadhi ya halmashauri, mfano Halmashauri kama kule Korogwe ambayo Madiwani waliomaliza udiwani wao mwaka 2020 mpaka leo wanaidai halmashauri. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Kasalali unapokea Taarifa hiyo?

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, naipokea hiyo Taarifa na kuongeza kwamba kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kuna Madiwani ambao wamefariki mpaka leo hata mafao yao familia hazijalipwa, akiwepo Marehemu Diwani wa Kata ya Lyoma ambayo mimi niliingia baada ya yeye kufariki na wengine. Kwa hiyo, bado tunayo kazi kubwa kwenye kusimamia maslahi ya Madiwani hawa ndiyo wanasimamia halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, niende mbele zaidi nikaangaliue jambo ambalo watu wengi wameliongelea hapa la *TARURA*.

TARURA ni tatizo kubwa sana ndiyo maana Wabunge wengi wameliongelea hapa. *TARURA* ndiyo inahudumia watu wetu kule vijjjini na mimi sielewi sababu za kutoa ujenzi Halmashauri tukapeleka *TARURA*, labda tuangalie kuna ufanisi gani upo kwa kufanya hivyo kwa sababu barabara bado hazipitiki.

Mheshimiwa Spika, nikienda Jimbo la Sumve kuna Kata kama ya Mwandum sasa hivi mvua zikinyesha huwezi kwenda, haipitiki kata nzima. Ukienda Kata ya Mwabomba haipitiki kata nzima. Nikisema nitoke Bungulwa niende Ng'undya kwenye kata hiyohiyo kuna Kijiji cha Ng'undaya huwezi kwenda kabisa, lakini tatizo kubwa *TARURA* uwezo wao wa kujenga madaraja ni mdogo sana. Barabara za vijjjini kinachokwamisha sanasana ni madaraja, kuna madaraja sugu kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kwimba hatuna Hospitali ya Wilaya, tuna Hospitali Teule ya Wilaya ambayo iko Sumve, kutokea Ngudu kwenda Sumve kuna mito mitatu ambayo mvua ikinyesha haupiti hata kama una mgonjwa na barabara ile iko *TARURA*. *TARURA* hawana hela za kujenga haya madaraja na hawana uwezo wa kujenga madaraja. Kwa hiyo, ni lazima muwaongezee uwezo na pesa ili tuweze kurahisisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini naomba Mheshimiwa Waziri apooke ushauri wangu wa kuongeza ufanisi wa Mabaraza ya Madiwani kwa kusimamia malipo ya Madiwani, lakini pia kwa kuhakikisha *TARURA* inapatiwa pesa za kutosha. Nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nami nianze kukushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwa namna ya pekee kabisa, nimshukuru Waziri na Mwenyekiti wa Kamati kwa hotuba nzuri ambayo tumeielewa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nitachangia kwenye eneo la changamoto zinazowakabili walimu wa shule za Serikali za msingi na za sekondari hapa nchini. Wote tunakubaliana kimsingi kabisa kwamba walimu kwenye jamii yetu ni watu muhimu sana, wanafanya kazi ya wito kutoka kwa Mungu kabisa. Wanatusaidia sana kufundisha watoto wetu kuanzia elimu ya awali mpaka kufika sekondari *form five* na *form six*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge tuliomo humu ndani tutakubaliana kwamba wote tumepitia kwenye mikono ya walimu kwa namna moja au nyine. Hata hivyo, nasikitika kusema pamoja na hawa watu kuwa muhimu sana, Serikali tumewasahau, kuna vitu ambavyo haviko sawasawa na kuna malalamiko makubwa sana kutoka kwa walimu wetu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu zamani walimu walikuwa wanatamba Rais wa Awamu ya Kwanza alikuwa mwalimu; Awamu ya Pili alikuwa mwalimu; Awamu ya Nne walikuwa wanamuita shemeji yetu; Awamu ya Tano alikuwa ni mwalimu na mama alikuwa mwalimu. Hata hivyo, pamoja na kuwa na bahati ya kuwa na viongozi wakuu wa Serikali waliokuwa walimu wamebaki kama yatima, stahiki zao kama Serikali hatujaziangalia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kuwasahau kwa kiasi kikubwa, nitaeleza tu machache ambayo yanatoka rohoni kwangu, kumewafanya walimu wetu wafundishe wakiwa na msongo mkubwa sana wa mawazo. Walimu wengi hawafurahii kazi kwa sababu wanaona kama vile tumewasahau. Walimu wetu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Nitatoa mfano tu; mwaka 2016 Serikali ilipunguza wafanyakazi na idadi ya walimu ilipungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hii idadi kupungua Serikali ni kweli imeshafanya jitihada za kuongeza walimu lakini haijaenda na idadi ambayo inatakiwa ambapo mwalimu anatakiwa afundishe wanafunzi 45 kwenye darasa moja ukilinganisha na walimu 33 ambao ni idadi ambayo iko

kwenye shule za *private*. Jambo hili limeshasababisha tukawa na ufaulu ambao sio mzuri sana. Wanajitahidi na tunawalaumu kwamba wakati mwingine labda hawafanyi kazi vizuri ni kwa sababu ya changamoto ambazo nitazitaja.

Mheshimiwa Spika, walimu wetu wana changamoto nydingi na niende harakaharaka, changamoto ya kwanza ni mishahara midogo. Walimu wanaingia kazini kuanzia saa moja asubuhi, wanafunzi wanashika namba wanatoka jioni, akirudi nyumbani hana hata muda wa kufanya vitu vingine, anaanza kusahihisha kazi ambazo amewapa wanafunzi na baada ya kusahihisha anaanza kuandaa somo la kesho. Kesho yake ni hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maisha yao kusema kweli ni kazini, ni wito, muda wote wanautumia kufanya hii kazi. Wao siyo kama sekta nydingine ambazo huwa wanafasifri wanapata *per diem*. Hawa watu huwa ni kwenye kituo chake cha kazi kuanzia mwaka wa kwanza mpaka wa mwisho kama hajapata fursa ya kwenda kusahihisha mitihani.

Mheshimiwa Spika, mshahara wa shilingi 420,000/= kwa mwali muhimu wa Shule ya Msingi au shilingi 560,000/= wanaopata hivyo, alipie nyumba, avae vizuri ili aonekane ni kioo kwenye jamii, ale vizuri, achangie kwenye shughuli za kijamii kama wananchi wengine, hizi fedha ni ndogo sana, hazitoshi. Kwa hiyo, nitapendekeza baadaye ni nini kifanyike.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ambayo walimu wetu wanakumbana nayo ni madaraja. Wengi wao hawapandishwi madaraja kwa muda unaostahili. Mwali muhimu akawa amekaa miaka 10 hajapanda daraja; na hii ina *effect* kubwa sana kwenye maisha yao wanapostaafu. Kwa hiyo, hili nalo ni jambo muhimu ambalo ningependa tuliangalie kwa pamoja ili tuwasaidie wapande madaraja kama sekta nydingine ambazo zinapanda madaraja.

Mheshimiwa Spika, ni takwa la kisheria kila baada ya mwaka mmoja watumishi wanaenda likizo na wanalipwa na Serikali. Walimu wengi waliopo kule vijijini hawalipwi zile fedha

za kwenda likizo. Hii ni shida! Mishahara ni midogo, mwisho wa mwaka ukifika hawezikujisafirisha kwenda nyumbani. Kwa hiyo, naomba tuwaangalie kwa mazingira ambayo tunafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni uhamisho. Kuna walimu wameshahamishwa kwenye maeneo ya kazi, lakini kwa bahati mbaya kutokana na ufinyu wa fedha, hawajalipwa fedha za uhamisho. Kuna madeni ya posho za kuhama, fedha ya kujikimu na fedha za kufunga mizigo. Kwa hiyo, naomba hii changamoto nayo tuiangalie kwa namna ya pekee ili tuweze kuwapa moyo walimu wetu kule walipo.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tano ni madeni ya kwenda kwenye masomo. Walimu wengi wanakwenda kwenye masomo na kuna wachache wanaopata fursa ya kwenda kusoma na wanapokwenda kusoma kuna sheria inaruhusu wapate fedha ya kwenda kwenye masomo. Kuna madeni makubwa sana kwenye Halmashauri zetu na hawajalipwa hizi fedha.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine kubwa ni madeni ya posho za madaraka kwa Maafisa Elimu wa Kata na pia kuna posho ya madaraka pia kwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu, hii ni changamoto. Ili kuwapa motisha walimu wetu ambapo ndugu zangu wote tumepitia kule, tuwasaidie hawa watu nao wajisikie ni sehemu ya ajira katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya saba ni nyumba za kuishi walimu wanaojiriwa kule vijijini. Wenzangu wameshalisemea hili, nami ninasisitiza kabisa kwamba ni muhimu tuwajengee walimu hasa wale wanaokwenda kwenye mazingira magumu kule vijijini wapate nyumba za kuishi, otherwise wanaishia kuwa na maisha magumu sana. Utakuta wanaishi kwa namna ambayo siyo maadili ya Kitanzania kutokana na shida ambazo zipo kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zote ambazo walimu wanapambana nazo, mimi nawashukuru

sana na ninawapongeza kwamba wameendelea kufanya hii kazi kwa upendo, hawajagoma. Wakishirikiana na vyama vyao vya taaluma, wamekuwa watifu sana na wameendelea kufundisha watoto wetu. Baada ya kusema hayo naomba niishauri Serikali mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa hii sekta na *specifically* hapa nazungumzia walimu, naishauri Serikali itafute fedha mahali popote zilipo, kama ni huku ndani ama nje ya nchi, tuhakikishe tumetatua hizi changamoto ambazo zimewakabili walimu wetu. Changamoto ambazo nashauri tuzitatue kwanza, tuwalipe mishahara mizuri ikiwezekana. Dada yangu Mheshimiwa Ummy tujipige pige tupate fedha ili hawa watu wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu sana walipwe mishahara mizuri, angalau ifanane fanane na wale wanaofundisha shule za *private*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa pili, napendekeza wapandishwe madaraja. Kwa wale waliochelewa ikiwezekana tuwapandishe. Kuna kitu wanakiita mserereko. Tuwapandishe madaraja kwa kutumia ule mtindo wa mserereko, kama mtu miaka 10 alitakiwa awe kwenye daraja fulani, sasa hivi ufanyike utaratibu kuhakikisha wamepata hayo madaraja yao kwa sababu watakapostaafu ule mshahara wa mwisho unamsaidia sana kwenye maisha yake ya izeeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine, ninapendekeza tutafute fedha kama wenzangu walivyosema, tuwajengee walimu shule kule walipo. Kama tumeweza kujenga barabara, ni nini kinatushinda kuwajengea walimu hasa wale wa vijijini wakapata nyumba za kuishi wasidhalilike kule walipo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wa nne ni madeni ambayo yapo. Napendekeza Serikali ijitahidi ilipe likizo kwa wale ambao hawajalipwa, walipwe posho za madaraka wale ambao hawajalipwa na zile za uhamisho na za kwenda masomoni. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Profesa.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Huyu ni Profesa Partick Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijiini. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Felista Deogratius Njau.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Moja kwa moja niende kwa upande wa TAMISEMI katika kipengele hiki hiki cha TARURA. TARURA imekuwa kama kibogoyo asiyekuwa na meno, lakini analazimishwa kula mifupa. Nasema maneno haya kwa sababu TARURA hawana shida. TARURA siyo tatizo, tatizo ni bajeti wanayopewa. TARURA wapo tayari kabisa kufanya kazi, lakini fikiria bajeti nzima ya barabara, TARURA wanapewa asilimia 30 badala ya kupewa asilimia 40 mpaka 50. Mimi napendekeza TARURA waongezewe fedha kwa sababu wanachezea nafasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilimsikia Mheshimiwa Waziri akisoma hapa, anasema TARURA kwenye kilometra za mraba, wako 144,000. Sijui kama ni kweli, lakini pia ina wingi sana wa barabara. Kwa hiyo, TARURA watengewe fedha za kutosha ili kilio hiki cha Watanzania basi waweze kufutwa machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda Dar es Salaam katika jiji ambalo ni kubwa, ambalo ni kitovu cha biashara na ni muunganiko wa Mikoa yote ya Tanzania. Dar es Salaam kumekuwa na msiba na kilio katika majimbo yote ya huko kuhusiana na barabara hasa zile za mitaa na barabara kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara za Dar es Salaam nyingi ambazo hazipitiki ni suluhisho la foleni za Mkoa wa Dar es

Salaam. Kwa mfano, Barabara inayotokea Kairuki kupitia Mikocheni, barabara ile inayopitia *shoppers* ilikuwa suluhisho kabisa la foleni za Dar es Salaam. Mtu anayesafiri Dar es Salaam kutoka Bunju kuelekea Posta ambapo ndipo kwenye Ofisi za Serikali, anachukua masaa matatu kama anatoka hapa kwenda Morogoro.

Mheshimiwa Spika, mtu huyu anafika ofisini anasinzia, akili imechoka, uwezo wake wa kufikiri umeshapotea. Tunaanza kusema watu wetu hawa-*perform* vizuri, hawa-*perform* kwa sababu hawapo *active*, wakifika pale kama mtu ametoka kulala kwenye msiba. Barabara nyingi ni kilio. Kuna barabara moja ipo Ununio; mwaka 2020, baada ya mvua hizi kunyesha nyumba 10, yaani familia 10 zilihama kabisa zikaondoka wakaenda *TARURA* wakaambiwa chimbени mfereji. Hakuna miundombinu pale ya mfereji kuelekeza maji baharini. Wale watu wanapeleka wapi haya maji? Familia 10 zipo juu ya nyumba. Sasa hivi wanapiga simu wanasema Mheshimiwa Njau, tunaondoka sasa, wananiaga niwapeleke wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kitu kimoja. Barabara ni kwikwi Tanzania nzima. Nikisema za vijijini, Mikoa inayohusiana na Kilimo, inayohusiana na biashara na mazao, hakika tunadumaza pato la Taifa. Kwa sababu kama vijijini barabara ni mboru, hawawezi kwenda kwenye Wilaya, hawawezi kwenda kwenye Mikoa kupeleka mazao yao, tunasema hatupati mapato. Barabara ni suluhisho la biashara na barabara ni suluhisho la kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu wengi wanaosimama hapa wanalia juu ya bajeti sehemu fulani. Twende tukatoe mzizi wa fitina kwenye miundombinu. Tukitoa hapa kwenye barabara, tunaweza kwenda vizuri. Pia niseme, hata wakijenga barabara hizi, kama Serikali hatujaweka nguvu kubwa katika kujenga mifereji, ni kazi bure. Barabara zinachongwa leo, baada ya siku tatu maji yanajaa na barabara zinakuwa vile vile. Kwa hiyo, lazima tuweke miundombinu ya mifereji. Kwa mfano, pale Mikocheni

Shoppers, kuna adha ya mafuriko; pale ni mifereji tu ndiyo mchawi.

Mheshimiwa Spika, ikipatikana mifereji thabiti, barabara zikajengwa vizuri, barabara hizi zitakuwa imara. Barabara zinaharibika kwa sababu hakuna mifereji. Tuna wataalam wetu, wakandarasi; kuna msiba na kilio cha Makandarasi. Kwenye ripoti ya CAG ameainisha zaidi ya shilingi bilioni 81.52 hazijalipwa kwa Makandarasi, tunategemea kupata matokeo chanya kwa mtu ambaye anakudai na unampa kazi mpya! Hatuwezi kupata matokeo chanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukalipe madeni haya ya Makandarasi ili tuweze kuanza nao vizuri na kumaliza vizuri. *TARURA* hawa hawa ambao wanatengewa asilimia 30, wanaidai Serikali shillingi 125,854,000/=. Hivikweli hawa ambao fedha zao hazitoshi, bado wanadai; tukawalipe *TARURA* Ninaongea haya kwa sababu tuna barabara za kimkakati; wakati tunatenga bajeti, hebu tuweke kipaumbele kwenye barabara za kimkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kawe tuna barabara inatoka Mabwepande kuelekea Kibamba - Mbezi, ile barabara ni ya kimkakati kabisa kwenda kupunguza foleni, lakini barabara ile imekaa kama haina mwenyewe. Kuna barabara zimejengwa nusu; barabara ya *Shoppers* imejengwa kwa lami nusu, mwaka wa nne leo watu wanachungulia na kurudi, iko nusu. Twendeni tukamalize miradi baada ya kuianza, ndipo tuweke miradi mipyä.

Mheshimiwa Spika, nashauri wakati tunaanza kupanga bajeti, tuangalie miaka ya nyuma: Je, tulikuwa tuna kiporo? Siyo kila siku tunaibua miradi mipyä wakati ya zamanii imesimama. Tutakuwa kila siku tunaelemewa na tunaonekana hatufanyi kazi, lakini watu wanachapa kazi.

Mheshimiwa Spika, ninakwenda kwenye ulipwaji wa motisha na madeni. Viongozi kama alivyosema msemaji aliyeppita, Madiwani hawana thamani. Kwa sababu hawa

ndio wanaosimamia mapato yetu, twendeni tukawape motisha, tusimame nao, tuwasemee. Madiwani ukikaa nao anakwambia posho yangu; ananung'unik! Tunakutana na Madiwani, anasubiri apate huruma ya Mkurugenzi wakati ye ye ndiye anatakiwa kumwajibisha Mkurugenzi. Hatuwezi kufika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, twende tukapange upya. Nina imani na Serikali hii, sasa nina imani Mheshimiwa Mama Samia amesimama na viongozi wake, siwezi kuwakosoa kwa sababu ndiyo wameanza, nawaona wanaweza kufanya mabadiliko makubwa na nchi hii ikaenda kuona maisha mengine tofauti.

Mheshimiwa Spika, nasemea Jiji la Dar es Salaam kwa sababu mwisho wa siku Jiji la Dar es Salaam ndiyo jiji ambalo limekusanya mapato ya ndani makubwa kwa asilimia 104, limevuka asilimia 100. Kama Jiji hili ndivyo liliyvo, basi turudishe mapato kule chini, kwa maana ya miundimbinu. Miundombinu ikipatikana, wafanyabiashara watafanya biashara zao na wafanyakazi watafanya kazi vizuri wala hutasi kia minong'ono.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Felista Njau.

Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizobaki hatuwezi kupata mchangiaji mwingine kwa sababu zimebaki dakika chache sana, lakini tutaendelea jioni na wachangiaji wengine. Wale wote waliojiandikisha nadhani tutapata nafasi jioni ambapo tutaanza na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Deus Sangu, Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Lucy Mayenga, nakadhalika na kadhalika.

Kwa hatua hiyo basi, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni ya leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilahirishwa hadi Saa 10.00 Jioni).

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, tuanze na Mheshimiwa Godwin Kunambi na wengine watafuata.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukushukuru, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya njema hata siku ya leo nikawa sehemu ya wachangiaji kwenye Wizara hii muhimu kwa Taifa letu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwenye eneo ambalo wananchi wa Jimbo la Mlimba wameniagiza niseme hapa halafu baadaye nitazungumza masuala ya kitaifa. Wananchi wa Jimbo la Mlimba wameniagiza nizungumze mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, hoja kuu ni mgawanyo wa miundombinu ya huduma ya afya na elimu kitaifa. Tuna changamoto kubwa sana juu ya mgawanyo wa huduma hizi za elimu na afya kitaifa. Ni kweli hakuna ubishi Wizara hii hasa Serikali ya Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa katika ujenzi wa vituo vya afya na kazi kubwa katika ujenzi wa miundombinu ya sekta ya elimu.

Hata hivyo, swali langu la msingi tufanye tathmini ya kina kitaifa tuone mgawanyo wa huduma hizi, wapo baadhi ya wananchi ukizungumzia habari ya huduma ya afya, ukiwaeleza takwimu ya ujenzi wa vituo vya afya hawaelewi lugha hii. Kwa sababu katika Jimbo zima, mfano naomba nizungumzie Jimbo la Mlimba, jimbo hili lina kata 16, vituo vya afya ni viwili tu. Uzuri wananchi wa Jimbo la Mlimba ni

wachapa kazi na kauli mbiu yetu Jimbo la Mlimba ni "tunaanza wenyewe Serikali itatukuta". Sasa tunaomba kuungwa mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tumeshakamilisha ujenzi wa kituo cha afya, jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI dada yangu Ummy, maombi ya wana Mlimba tunataka tuanze kufungua kile kituo cha afya, tafadhalii Mheshimiwa Waziri atuletee Waganga pamoja na wahudumu ili tuanze kufungua.

Mheshimiwa Spika, pia ikimpendeza Mheshimiwa Waziri anavyokuja kuhitimisha bajeti yake siyo mbaya akasema anakwenda kukamilisha kituo kile cha afya. Maadam tumeanza na siku zote unavyotaka kusafiri unaanza kukaa barabarani ndiyo unaomba *lift*. Kwa hiyo sisi tunaomba *lift* tusaidie tu tumalizie kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la hii hii sekta ya afya, kwa wahudumu, hebu tufanye tathmini Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, wapo wanaopewa nafasi hizi kwenye ngazi za Halmashauri hawana sifa, sasa tufanye tathmini ya kina halmashauri kwa halmashauri kama kuna mtu anayeshughulika na *let's say* Mkuu wa Kituo cha Afya au Mganga Mkuu wa kituo cha afya tuone elimu yake, hebu tufanye tathmini ya kina kitaifa tuone kwa sababu sekta hii ni muhimu na nyeti sana.

Mheshimiwa Spika, labda nieleze tu ikama ya sekta ya afya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, mahitaji ni watumishi takriban 432 waliopo kwa sasa ni 169 unaona *disaster* hiyo, yaani zaidi ya nusu hawapatikani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atusaidie katika eneo hilo na wananchi wa Mlimba wamenitura hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine niende kwenye suala zima la sekta ya afya kuhusu maboma. Tumeshajenga sisi Mlimba maboma 10 ya zahanati. Tunaomba tumalizie tu, kama tunaanza wenyewe siyo mbaya tukaungwa mkono na Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la elimu; kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, nitoe tu mfano mathalani elimu ya msingi, mpaka sasa tuna maboma ya madarasa 41. Ushauri wangu hapa kama wametuletea fedha kujenga madarasa, watu wa Mlimba tunaomba sana zile fedha waturuhusu hata kama kwa ajili ya kujenga shule au madarasa tuzitumie kukamilisha maboma haya kwanza, watusaidie sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine, ikama ya Walimu wa elimu ya msingi. Mahitaji ni Walimu 1,420, waliopo ni 654 maana yake tuna upungufu wa Walimu takriban 766. Sasa tungeomba maeneo haya yatiliwe mkazo kidogo kwa sababu ni maeneo nyeti sana na kwa mustakabali wa watoto wetu na wanafunzi wanaosoma ndani ya Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine niende upande wa TARURA; yapo mengi yamezungumzwa kuhusu TARURA. Mimi binafsi niseme tu, kwangu Jimbo la Mlimba mnyonge mnyongeni haki yake mpeni na nimwombe Mheshimiwa Waziri, watumishi hawa asiwahamishe ndani ya Jimbo la Mlimba. Meneja wa TARURA Wilaya ya Kilombero kwa maana ya Mlimba *super*, aniachie tufanye naye kazi. Meneja wa TARURA Mkoa wa Morogoro *super*, tauachie tufanye nao kazi. Nitasema baadaye huko kwenye maji maana yake wako wazuri zaidi kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye eneo la mgawanyo wa fedha hizi za TARURA. Nilikuwa najaribu kuangalia haraka haraka Jimbo la Mlimba lina kilometra zaidi ya 1,000, tunapata bajeti ya milioni 500 kwa mwaka. Nimeangalia na jirani zangu pale Kilosa kidogo, wao wana kilometra takriban 900 hivi wana bilioni 1.3. Sasa napata tabu kwenye mgawanyo wa hizi fedha, milioni 500 unafanya nini pale Mlimba, kilometra zaidi 1000. Yaani hata daraja moja halikamiliki. Hebu tuangalie maeneo haya, niombe tu na nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kuhitimisha bajeti yake aeleze ni vigezo gani vinatumika katika mgawanyo wa hizi fedha kwenye halmashauri, nivijue vizuri. Hii itatusaidia pia kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, sasa nijikite katika eneo la mapato na hapo kwanza natangaza maslahi na kwa kuwa nimehudumu kwenye Serikali za Mitaa kama Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma na tulifanya vizuri sana kwenye mapato, naomba nitoe elimu kidogo kwa ufupi kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hakuna muujiza kwenye kuziimarisha halmashauri kimapato, jambo la msingi niombe Wizara hebu tufanye tathmini, tuangalie fursa za kila halmashauri, nilivyokuwa Dodoma niliitazama Dodoma Jiji nikaona sina fursa nyingine mbadala zaidi ya ardhi, tukapima Dodoma zaidi ya viwanja 200,000 tukapata fedha na tulikusanya bilioni karibu 73 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Tukasema hapana hii fedha viwanja siyo *sustainable* yaani *sustainability* ya mapato ya viwanja ni ya muda mfupi tu, nikakaa na menejimenti timu yangu tukakubaliana tubuni vyanzo mbadala vya mapato ya ndani, leo tumeacha hotelli kubwa hapa inayojengwa kwa mapato ya ndani bilioni 9.9 inakamilika, ndio tunafungua mwezi ujao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Jiji la Dodoma kwa maana ya *own source* ipo. Ukienda Mji wa Serikali kuna hoteli, kuna *apartment*, kuna kumbi zinajengwa, mapato ya ndani bilioni 18. Sasa niombe na niseme tu zipo halmashauri zina fursa ya kilimo, wawekeze kwenye kilimo, zipo halmashauri zina fursa kwenye maeneo mengine wawekeze huko, hakuna eneo ambalo halmashauri tunazuiliwa kwa mujibu wa sheria kuwekeza. Tukiendelea kusubiri haya sijui kodi na nini nadhani *tuta-mark time* kidogo.

Kwa hiyo niombe na sisi pale Mlimba waturuhusu nitamwomba Waziri wa Ardhi baadaye lakini kwa sababu hapa tunazungumza na TAMISEMI, kuna shamba la Serikali la hekta 500 limetelekezwa leo hii *almost* ni miaka kama mitatu, sisi tutalichukua lile na tutalima kuanzia mwakani. Tutaanza kilimo cha mpunga, tuvune mpunga kama mapato ya ndani, tutalichukua tu sisi maana Serikali haifanyi chochote pale. Kama halmashauri tutalitumia, tutaliwekeza ili tulime kilimo cha mpunga, tuone namna gani tuweze kujikwamua

na shughuli za maendeleo Jimbo la Mlimba kuititia kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme jambo moja tutengeneze *clusters* ya hizihalmashauri. Huwezi kulinganisha Jiji la Dar es Salaam kwa maana llala na Halmashauri ya Mlimba hata kidogo. Kwa hiyo hata fedha za maendeleo tunavyopeleka tuzitengenezee madaraja. Daraja A ni halmashauri zile zote zenye uwezo kwa mapato ya ndani, tuangalie namna gani tunapeleka kwa sababu ukisema mgao wa llala uwe sawa na wa Mlimba, tunawaonea haziwezi kuwa sawasawa. Kwa hiyo tuzitengenezee madaraja, kama hawa wana uwezo wa mapato ya ndani, basi ziende fedha chache za maendeleo, wale wenye changamoto kubwa tuwapelekee za kutosha na hili ni tatizo la nchi nzima. llala ana zaidi ya bilioni 60 unampelekea fedha za nini, Dodoma Jiji sasa wanakwenda kukusanya bilioni 48, sisemi zinatosha lakini tuangalie namna ya mgawanyo kwa kuzingatia fursa au uwezo wa halmashauri kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ambalo nadhani nitoe mchango wangu ni 10%. Sheria imetungwa na nalipongeza sana Bunge liliopita na nakupongeza na wewe binafsi kwa sababu mlitunga sheria nzuri sana. Tuweke eneo kwenye kanuni au sheria, nadhani kanuni kwenye utekelezaji kwa sababu kanuni ndiyo inatekeleza sheria. Tuweke eneo ambalo halmashauri zenye uwezo mkubwa wa kuchangia 10% zisipeleke fedha kwa sababu tija zile hela tunapopeleka kwa wananchi hazifanyi chochote, tunafanya siasa tu. Dodoma sasa hivi tumepeleka bilioni sita, ziko mtaani, hebu fanya tathmini hizo bilioni sita zimefanya nini? Utaona hamna kitu kwa hiyo kama ni siasa tu. Kwa hiyo halmashauri zenye uwezo wa fedha nydingi ziruhusiwe badala ya kupeleka fedha watengenezeweh shughuli yoyote kiuchumi yaani halmashauri iamue kununua kama ni vifaa au namna gani yoyote lakini siyo kupeleka.

Mheshimiwa Spika, kingine kuwe na ukomo wa hizi fedha, leo hii Dodoma kama inatoa zaidi ya bilioni sita,

maana yake itafika mahala 10% ni zaidi ya bajeti yake tunapeleka kwa wananchi, kwa hiyo kuwe na ukomo kwa halmashauri kubwa kwamba sasa ifikie mahali kama utachangia 10% mpaka bilioni 30 i-stop, zile changa ziendelee kwa sababu wakati inatungwa sheria hii hatukutathmini kwa kina uwezo wa halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache niliyochangia, nadhani yatasaidia Wizara yetu, lakini nimwombe anapokuja kuhitimisha bajeti yake, haya niliyomwomba ayaseme na niyasikie na wananchi wa Mlimba roho zao zitapona. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Godwin Kunambi. Sasa naomba nimkaribishe Issa Jummanne Mtemvu na atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Sangu.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Awali ya yote nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili, lakini vilevile na wataalam. Pia nitumie nafasi hii kukupongeza wewe kwa kweli kwa jinsi ambavyo unatuendesha ndani ya Bunge hili ugeni wangu huu mpaka nafarijika. Kwa muda mchache umenipa nafasi mara nyingi na wananchi wangu wanayaona haya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika maeneo machache sana; eneo la kwanza ni eneo la mabonde na mafuriko katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hili ni tatizo sana, hivi pia sasa hivi tunazungumza ni nyakati za mvua kule wananchi wanalia sana. Niliwahi kusema kidogo kwenye eneo hili, lakini niseme tu kwamba mabonde sasa haya, kwanza niipongeze Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu pia, imefanya vizuri sana kwenye eneo la Mto Msimbazi, lakini pia hata kwenye Mto Jide pale ndani ya Wilaya yetu ya Ubungo ndani ya Jimbo la Rafiki yangu kaka yangu Proresa Kitila Alexander Mkumbo upande wa Ubungo, lakini bado tumebakwa na Mto Mbezi. Naiomba sana Serikali ijielekeze

vizuri ili tuone sasa mito hii inapanuka, taasisi zetu zinaondoka sasa na mafuriko. Sasa hivi tayari Shule ya Msingi Msigani pale inaondoka, Shule ya Msingi Matosa inaondoka, kwa hiyo na nyumba nyingi za wakazi wetu zinakwenda. Hivyo ni lazima, kwa sababu dhima yetu mojawapo ni kukuza uchumi pamoja na maendeleo ya watu. Kama watu hawaishi vizuri hawana maisha bora, nyumba bora maana yake tunaweza tukashindwa kwenda kwenye mpango wetu ule wa tatu ambao tumetoka kuujadili siku si nyingi.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maboresho ya miji; Waheshimiwa Wabunge wengi wa Mkoa wa Dar es Salaam wamezungumza juu ya *DMDP II*, *Dar es Salaam Metropolitan Development Programme II*. Ya kwanza ilifanya vizuri sana, tumeona Dar es Salaam inang'aa kwa mataa mengi, Dar es Salaam inang'aa kwa barabara nzuri nyingi. Niseme ukweli Hayati alivyopita tarehe 24 ndani ya Dar es Salaam katika ziara yake alipita pale Jimboni Kibamba na nilipata bahati ya kusema kidogo, katika matatu niliyosema ukweli aliyakubali yote.

Nilisema kitakwimu ndani ya mzunguko wa barabara zinazozidi zaidi ya kilomita 350 ni kilomita tano tu ndiyo zenye lami katika Jimbo la Kibamba. Hii si sawa na ukweli Waheshimiwa Wabunge wengi hasa zaidi ya 40 na Manaibu Waziri na Mawaziri zaidi ya 10 wanaishi kwenye hili Jimbo. Naomba kabisa mnisaidie ndugu zangu Jimbo limekaa kwenye hali mbaya sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niombe na Waheshimiwa Wabunge wamesema huu mradi wa *DMDP II* naomba utoke huko uliko kama umesimama ili uje utuokoe. Wakati tunaomba kura za Mheshimiwa Rais aliyepo sasa hivi akiwa anagombea kama Makamu wa Rais, lakini na Waheshimiwa Wabunge tulionyeshwa mtandao wa barabara kilomita 107 za ndani ambazo chini ya *TARURA* kupitia *DMDP II* na wananchi wakafurahi, wakaona sasa ile hali ambayo ilikuwa inawasababisha wajifungue barabarani kwa sababu ya njia nyingi kuwa za tope, sasa wanaenda kuishi katika maisha yaliyo bora.

Mheshimiwa Spika, niombe sana, huu mradi kwetu ni muhimu sana ndiyo utaenda kuwaokoa wana Dar es Salaam, lakini mpaka sasa tumeshamaliza bajeti yetu ya *TARURA* katika ngazi ya Mkoa na niliona takriban kilomita 60 zimewekwa pale, nikaanza kufurahi sana, lakini sijui kama kweli kutakuwa na sintofahamu, niombe sana kama patakuwa na nafasi ya Mheshimiwa Waziri kwenye hili, kama anaweza kuligusia kidogo ili tuweze kuona kama kweli hii *DMDP* //inakuja Dar es Salaam au hajji.

Mheshimiwa Spika, natamani pia niseme kidogo juu ya madeni ya muda mrefu na hasa kwa watumishi wa umma. Profesa wa Moshi Vijiijini, mzee wangu alisema vizuri asubuhi, nikasema ananinyang'anya ninalotaka kusema lakini akaelekea upande mwingine kidogo. Niseme kwamba, tunayo shida kwenye hili eneo, mpaka sasa kwa ripoti ya CAG anatuambia zaidi ya billioni 190 ndiyo deni ambalo lipo mpaka sasa kama madeni ya watumishi; hapo wapo Walimu pamoja na watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, bilioni 190 si nyingi sana, najua kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 tulikuwa na deni au na madeni karibu bilioni 207. Utaona zimepungua kwa bilioni 16, hii niipongeze sana sana Wizara ya Kisekta kwamba imefanya jambo jema, imepunguza bilioni 16 katika mwaka mmoja, kwa hiyo si jambo dogo, wamefanya vyema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo lakini bado kuna kazi ya kufanya. Asubuhi Profesa alishauri kidogo, anasema tunaweza tukaachaacha barabara kule na nini na ni kweli ndiyo ushauri. Sitaki kuelekea kwenye ushauri wa *CAG* amesema nini, lakini niwashauri tu, tunajielekeza sana, tunayo miradi mikubwa sana ya mabilioni ya namba na ni mizuri kweli na naipongeza ile miradi yote. Hata hivyo, hebu tutafiti jinsi ya mkakati mzuri wa kuondoa hili deni la bilioni 190, tukiamua kweli tunaenda kuzilipa zote.

Mheshimiwa Spika, hizi bilioni 190 ukiwalipa Walimu na watumishi wa umma, maana yake umepeleka hela mtaani. Ukipatikana bilioni 190, maana yake ile hali ambayo

tunaitaka sisi sasa ya kukuza uchumi na kuinua maisha ya watu, kweli yanaenda kuwagonga watu. Hii ndiyo dhamira ya Rais, mama yetu Samia Suluhu Hassan, unamwona anataka sasa kuzileta hela mifukoni kwa watu, yaani uchumi wa fedha uende kwenye mifuko ya watu na ndiyo maana ameelekeza hata madeni mengine ya wazabuni na kadhalika yalipwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe sana ukiona inafaa hili jambo liende na niseme mpaka sasa tunatenga bilioni sita za kulipa madeni, hazitoshi na bilioni nne ndiyo za ndani (*own source*), lakini bilioni nne ni za maendeleo, hazitoshi tukapunguze katika baadhi ya vifungu katika mafungu mengine huko, tutoe kwenye posho tulete hapa ili hawa watumishi wa umma waweze kulipwa hizi bilioni 190, sioni kama ni nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya Dar es Salaam kuhusu mradi huu wa *DART*, wa mabasi yaendayo kasi, yuko Mbunge mmoja siyo wa Dar es Salaam lakini nimefurahi sana, wanasimama Wabunge wengine na wenyewe wanaisemea Dar es Salaam, ndiyo maana nafurahi uwepo wa Wabunge wengi wanaoishi Dar es Salaam. Kweli ule mradi ni mzuri na najua unaendelea, lakini hata wewe umewahi kusema, miradi hii inayoendelea miundombinu ni ya kwetu Serikali, hebu tuone jinsi gani huduma hizi zitolewe kwa ushindani. Leo tunayo miundombinu mizuri, tumetoka awamu ya kwanza tunaendelea awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu, lakini ukweli mabasi hayatoshi, wananchi wa Dar es Salaam leo wanateseka kwa nini tumezua mabasi yale ya vituo vya basi kwenda Mjini Kariakoo. Tumezua tukisema tunaweza kuwamudu wote waingie kwenye mabasi ya mwendo kasi, haiwezekani! Kwa nini tuiseme ya kijani ni ya Serikali, wengine waje na mekundu, wengine waje na ya njano ili tukashindane kwenye ile barabara.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi niombe sana, leo hii barabara imekuwa ni mateso kwa hata wanaochangia kodi yenye. Leo kuna wagonjwa wanapata rufaa kutoka Mloganzila wanaenda Muhimbili, lakini unaambiwa hata yale

magari ambayo ni *ambulance* hayawezi kupita kwenye barabara ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiki ni kilio kikubwa kweli, kwa hiyo mgonjwa ambaye sehemu yake ya kodi ndiyo inajenga barabara ile, leo na yeze ili awahi maisha yake apate uhai, inawezekana asipite ile barabara na akafa kabla hajafika kwenye hospitali nytingine! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili ninasema si kwa kubahatisha, ndani ya jimbo langu Hospitali ya Mlonganzila iko hapo, na nilipata bahati kuwatemeblea Mwezi Januari, na moja ya kikao changu na menejimenti ya pale hiki kilikuwa kilio chao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe kwa jinsi ambavyo utakapoona inafaa tupate maelekezo mazuri, siyo sisi viongozi tupite mule wala siyo wengine, haya magari kwa ajili ya usalama wa maisha ya watanzania waishio Dar es Salama wapite kwenye njia ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, binafsi kwa siku ya leo niliona niyaseme hayo ya mabonde, mafuriko, *DMDP II*, eneo la madeni ya Watumishi wa Umma na hili la ushauri na maombi juu ya barabara yetu ya *DARTS*, baada ya kusema hivyo nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, nilishakutaja Mheshimiwa Deus Sangu na utafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia mawazo yangu kwenye wizara hii muhimu ya Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu na Manaibu wake pamoja na Katibu Mkuu na timu yake, niwapongeze hakika ni timu ya wachapakazi. Katika mchango wangu wa kwanza nitaongelea mfumo wa ukusanyaji mapato wa kielektroniki, kwa maana ya *Local Government Revenue Correction*

Information system kwa ku-link na pos machines, ni mfumo ambao Serikali ilianzisha kwa nia njema ili kukuza mapato kwenye halmashauri zetu mwaka 2016. Umeenda kwenye processes mbalimbali ya kuziimarisha lakini bado naona kuna changamoto kubwa na gap ninayoiona kwenye huu mfumo ni namna ya ku-entertain collection ya physical cash.

Mheshimiwa Spika, dunia ya leo imeenda mbali sana, mambo ya *physical cash* yamepitwa na wakati, lazima tutafute namna mfumo huu utakuwa *friendly* tuanze kkusanya mapato yetu kwa kutumia *soft money*, na hii ndiyo maana unaona katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, halmashauri zetu walikusanya zaidi ya bilioni 18 na hazikwenda benki. Sasa kwa sababu ya ku-entertain cash, ndiyo maana unakuta bilioni 18 haziendi benki.

Mheshimiwa Spika, sasa nikushauri Mheshimiwa Waziri, kama itawapendeza, nendeni mkaupitie huu mfumo kwa undani zaidi, kwasababu umekuwa na *loop holes* nydingi. Mfano, anayeshika hii *pos machine* ni mtaalamu wa TEHAMA na huyo anauwezo wa *ku-delete transaction*, anapigiwa simu anaambiwa bwana hiyo haikuwa laki tano ilikuwa elfu tano na hii imepelekea kwenye Hesabu za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, bilioni nne zilifutwa. Sasa hizi bilioni nne zingeweza kufanya vitu vingapi kwa kuleta maendeleo kwa Watanzania!

Mheshimiwa Spika, na nionge *with very serious note*, kwenye halmashauri yangu zaidi ya milioni 400 zilitoka huko nje mpaka leo tunavutana na tunakaa tunang'ang'ana tuwapeleke polisi, tuwafunge tutawamaliza watendaji woote, wa kata na wa vijji na wote wanaoshika *pos machine*, bila kuja na *solution* ya kuondoa *physical cash* tukawa na ile ambayo ni *soft cash*, tutawamaliza na hii *defaulters* itafutika, itakuwa historia tena mwaka huu mki-test, mtaona na kama mnataka muone *cash management solution*, nendeni kwenye benki watakupa, ni gharama ndogo tuna vijana wetu waliosomea *IT* watatupa ujuzi huu ni namna gani tunaweza kufanya *cash management solution* kwenye halmashauri zetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa spika, kwa hiyo, nikuombe *with due respect* Mheshimiwa Waziri, nendeni mkaone namna ya kufanya jambo hili ni jambo jema sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia mchango wangu wa pili, naomba kuongelea mahusiano kati Wakurugenzi wa halmashauri, Madiwani na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nitaanza msemo mmoja kwa ruhusa yako ya kilatini, unasema *Helius Beneficum cum servire regnire est* maana yake ni kwamba, ni jambo jema sana na lenye baraka kuchagua wale ambao unawatumikia ni kutawala pamoja nao. Sisi wanasiasa tulivyoenda kuomba kura kwa wananchi wakiwepo Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge, tulichagua kuwatumikia, ambao kuwatumikia ni kutawala pamoja nao, lakini kuna baadhi ya halmashauri huu msemo umekuwa ni tofauti kabisa, na nitolee mfano wa halmashauri yangu.

Mheshimiwa Spika, nimebahatika kuhudhuria vikao vya *finance* mara mbili, nimekutana na mambo ya ajabu kabisa! Inafikia Mkurugenzi anasimama na kuwatukana Waheshimiwa Madiwani, anamtukana Mbunge, anaitukana Kamati za Hesabu za Serikali *LAAC*kwamba hawezikumfanya kitu chochote, ameteuliwa na Rais, hii dharau ni ya kiwango cha juu haiwezi kuvumilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na leo hii ninavyoongea Madiwani wangu walikuwa na kikao cha baraza la Madiwani wiki hii, Mkurugenzi kwa kujisikia tu akawaita anavyotaka, wao wameenda pale wanasubiri na hivi Kamati ya Usalama na Ulinzi iko pale kesho atafanya kikao, aje asije huko ndiyo tulikoenda.

Nikuombe sana Mheshimiwa Ummy ili uweze kutusaidia sisi hasa wananchi wa Jimbo la Kwela walituchaguwa wanataka wakaone tunavyo-*deliver*, tunavyowaletea maendeleo, hatuwezi kuwa na halmashauri ambayo ina mgogoro, Mkurugenzi ana kiburi, kama anafikia

hatua ya kuweza kumtukana Mkuu wa Mkoa, anamtukana RC, anamtukana Mkuu wa Wilaya, kuna maisha hapo tena!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, halmashauri imebaki kama kijiwe tu pale, na nikuombe, fedha ambazo umepeleka juzi, nililikufua sana mkatupelekea bilioni 2.5, kazifuatilieni fedha hizi za mradi kwa sababu pale kumebaki kama kijiweni *with very serious note.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sikuongea kwa hiyo, nilimwambia, mimi ninaenda kwenye *platform* yangu Bungeni nikaeleze na Tanzania nzima isikie, kwamba sitaki mchezo, wananchi walinchaguwa na hili nimekuomba mama, tutakutana tena kwenye shilingi ya mshahara wako, ili nihakikishe limefanyiwa kazi, halmashauri yangu imerudi kati ya halmashauri ambazo zinaheshimika na Waheshimiwa Madiwani wapewe heshima yao. Hivi kweli mtu unaitukana Kamati ya Bunge, kwamba mimi niliteuliwa na Rais, mtu anayeweza kunioji ni Rais tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na ninaomba kwa kweli tuangalie hata Walaka wa Mwaka 2011, mliwapa pawa sana wakurugenzi wakabaki kwenye *loop hole* ya ku-hang, mwishowe wanaanza matusi, kunidharau Mbunge, kumdharaau Diwani, umedharau wananchi. Kwa hiyo, nikuombe sana, nimeongea kwa uchungu mkubwa, nadhani ndugu yangu Silinde wewe *classmate* wangu umenielewa, nimekueleza mara nyingi, Mkuu wa Mkoa ameleta barua nyingi RC, kumekaa kimya, nendeni mkainusuru Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu pia kuongelea jambo la TARURA, TARURA wameongea, sihami sana kwenye *concept* yao, twendeni tuka-review mgawanyo wa fedha hizi, huu mgawanyo umekuwa *unfair!* Baadhi ya halmashauri zina kilometra chache zinapewa *triple au twice* kuliko halmashauri zenye *network* kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu ni kuumiza wengine, kuna baadhi ya kata tangia watoe, halmashauri iache kuudumia

barabara, wana maisha magumu, hawajawahi kuona hata greda. Nina Kata kama Mnangalua, Kata ya Mnokola, Kata ya Nankanga, Kata ya Kalambanzite, Kata ya Kaengesa, Kata ya Kanda, ninaweza nikazitaja kata hapa, wanalia, naombeni nendeni mka-review upya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuongeza fedha *TARURA* ni jambo la kwanza, lakini jambo la pili, wajitahidi kuhakikisha mgawanyo unakuwa *fair* kwa kila halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niombe pia nichangie kuhusu huduma ya afya, na hii ndugu yangu Silinde utakuwa unamnong'oneza hapo Mheshimiwa Waziri. Wewe tunatokea jirani pale na Tarafa yangu ya Kipeta ni jirani pale na wewe, ile Tarafa tangia uhuru haina kituo cha afya na ina wakazi wanakaribia laki moja, wala haina miundombinu yoyote ya maji, wao wako kama wapo jangwani, ni kama wana ambao wametelekezwa. Nikuombe sana, wamekuwa wakija pale Kamsamba napo huduma zinaenda kwa kusua sua kwa ndugu yangu Conchesta pale.

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana, angalieni namna tutaanza kuisaidia hii Tarafa ya Kipeta, ipate kituo cha afya kwa haraka. Kwasababu maisha ya wananchi hawa ni hatari, juzi watu walikuwa wanakwenda pale kijjini kwenu Mkulwe, wameliwa wananchi 15 wamedumbukia kwenye mto, tumeishia kuzika wananchi wanafuata huduma ya afya huko ng'ambo. Nikuombe sana ndugu yangu tushirikiane kwa pamoja, tuhaakishe haya mambo yanaenda ili kuweza kuleta ufanisi ndani ya halmashauri yangu na Taifa la Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo tu, niwaombe sana mkayafanyie kazi, hakika wananchi wangu wa Jimbo la Kwela na Waheshimiwa Madiwani wangu wao tu hawaliil kilio tu cha stahiki, na kutukanwa matusi juu, na wamerudi nyuma, Mkuu wa Mkoa leo alikuwa ananipigia simu anasema, sasa tutaendaje Mheshimiwa Mbunge, nikasema hapana, wananchi walipanga mstari kutupigia kura, hili

jambo lazima Serikali itatusikia na itafanya hatua ya haraka sana.

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Deus Sangu, sasa Mheshimiwa Joseph Mkundi, na atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga. Mheshimiwa Mkundi!

MHE. JOSEPH M. MAKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa hii, kwanza kabisa nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu, lakini nitumie fursa hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na watendaji kwa uwasilishwaji wao bila kusahau Kamati ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na mchango kwenye maeneo kama mawili, kama muda utaruhusu basi nitaongeza eneo lingine moja. Eneo la kwanza ni juu ya *flow* ya pesa kwenye halmashauri zetu, dhamira ya uundwaji wa Serikali za Mitaa ni kurahisisha au kuhakikisha huduma za kijamii zinawafikia wananchi katika mazingira yaliyo mazuri na wapate huduma hizi katika mazingira yaliyo safi.

Mheshimiwa Spika, na pale ambapo halmashauri hizi zinaanzisha miradi, inatakiwa fedha ziende miradi ikamilike na iweze kuwa na tija ile thamani ya fedha iweze kuonekana. Bahati mbaya kumekuwa na shida kwa namna fulani kwenye *flow* ya pesa kwenda kwenye halmashauri zetu, matokeo yake ni kwamba miradi ama haikamili au wakati mwingine inakamilika lakini haiwezi kufikia thamani ile ambayo inakuwa imetarajiwu ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niki-*cite* kwa mfano taarifa ya CAG ya Mwaka 2019/2020 kwa mfano, utaona kwamba CAG katoa mfano kwenye mwaka huo kuna karibu bilioni 184 zilipelekwa kwa ajili ya miradi, miradi hii hajakamilika, matokeo yake nini, ni kwamba kile kilicho tarajiwu kwa ajili ya wananchi wale, ili huduma iweze kuwafikia haikuweza kuwafikia kwasababu miradi ile hajakamilika.

Mheshimiwa Spika, na hili linatokea kwasababu gani, inawezekana watumishi tulionao hawasimamii vizuri miradi ile ikaweza kukamilika, au fedha hazijaweza kwenda kama ambavyo ilitarajija ili thamani ile iweze kuonekana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe tu kama ushauri, Serikali ihakikishe kwamba miradi inapokuwa inabuniwa kwenye halmashauri zetu basi Serikali ihakikishe fedha zinakwenda kama zilivyotarajija ili yale tuliyotarajia kama manufaa kwa wananchi wetu, yaweze kupatikana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna wakati mwingine miradi inakamilika lakini haitumiki, niki-*cite* kwenye taarifa ya CAG, vile vile, utaona kwamba CAG anasema kwenye Mwaka 2019/2020, kuna biliioni 18 zimepelekwa kwenye miradi ya maendeleo, miradi imekamilika lakini haitumiki.

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni kwamba ama kuna shida kwenye ushirikishwaji wa wananchi, matokeo yake sasa miradi imebuniwa lakini siyo kwa manufaa ya wananchi na hili linatokea wakati mwingine ushirikishwaji unakuwa siyo mzuri kwasababu kuna tatizo kwenye uwakilishwi wetu.

Mheshimiwa Spika, asubuhi kuna mchangiaji mmoja ameonyesha umuhimu wa kuboreshwa kwa maslahi ya Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la msingi sana, kwasababu miradi yetu inayotekelezwa kwenye halmashauri zetu wasimamizi wakuu ni Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Waheshimiwa Madiwani, lakini maslahi yao ni duni sana! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali iliangularie jambo hili iweze kuboresha maslahi ya wawakilishi wetu hawa ili angalau waweze kusimamia shughuli hizi za maendeleo katika kiwango kilicho kizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili ambalo nilitaka nichangie ni kwenye eneo la TARURA, wengi wamesema juu

ya *TARURA* na kupitia michango mbalimbali tumesema juu ya umuhimu wa kuboresha *TARURA*. *TARURA* mpaka inaanishwa ilikuwa na umuhimu wake na ina majukumu mazito sana kwa ajili ya kuboresha miundombinu kwa ajili ya watu wetu kwasababu barabara zinazohudumiwa na *TARURA* nydingi ni zile barabara ambazo wananchi wetu kwa wingi wao wanatumia kwa ajili ya shughuli zao za maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana *TARURA* ikaangaliwa kama ambavyo tulivyokuwa tunapendekeza, na kwangu mimi ningependekeza maeneo mawili ambayo ni muhimu sana yaangaliwe kwenye eneo la *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni muundo wake, ilivyo hivi sasa *TARURA* menejiment ya *TARURA* na hasa kwenye eneo la bajeti linasimamiwa zaidi na uongozi wa mkoa, lakini huku wilayani ambako kuna watu ambaao wanajuwa kwa uhalisia matatizo na changamoto za barabara zilizoko kwenye maeneo yao, hawana nguvu yoyote ya kibajeti, kiasi kwamba wanashindwa kushughulikia matatizo madogo madogo yaliyoko kwenye maeneo yao ambayo yangewasababisha sasa waweze kuondoa hizi changamoto za barabara na hatimaye ziweze kuwasaidia watu wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe Serikali iangalie marekebisho ya muundo, ili angalau Mameneja wa *TARURA* kwenye wilaya nao wawe na nguvu ya kibajeti, jambo ambalo litawasaidia angalau kuweza kushughulikia matatizo madogo madogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, suala lingine ni ambalo tumelizingumza mara kwa mara kusaidia uvezeshaji kwa *TARURA*, fedha wanazozipata kimsingi ni ndogo sana, haziwezi kuwapa uwezo wa kushughulikia matatizo ya barabara zilizoko kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, ile fomula kama itaweza kubadilishwa, itasaidia sana barabara zetu ziweze kuwa bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la Ukerewe kuna changamoto kadhaa na niombe Mheshimiwa Waziri, tumeleta mara kadhaa karibu miaka mitatu mfululizo tunaleta ombi kwenu, mtusaidie hasa hapa pale Ukerewe, angalau mtupe kilometra moja mbili za lami ili tuweze kuchochea mzunguko wa kiuchumi kwa wananchi wa Ukerewe, jambo ambalo litatusaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kwenye eneo la Ukerewe, kuna eneo moja linaitwa Namakwekwe, kuna eneo ambalo kuna mto ambao nyakati za mvua watu hawapiti na inasimamisha hata shughuli za kiuchumi na hata watoto hawawezi kwenda shule, kwenda upande wa pili eneo la Mibungu. Mtusaidie Mheshimiwa Waziri, angalau tuweze kujengewa daraja pale kuweza kuanganisha eneo hili ili wananchi waweze kufanya shughuli zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri nikumbushe tu ahadi wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyokuja Ukerewe, aliahidi kupitia maelezo tulioota lakini na changamoto alizoziona kutujengea kituo Kituo cha Afya kwenye Kisiwa Ilungwa, lakini vile vile kutujengea zahanati kwenye Kisiwa cha Ghana, mtusaidie sana ili anghalau visiwa hivi viweze kupata huduma nzuri za kiafya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, kuna mradi wa barabara mradi wa *Tanzania Strategic Cities Projects*, ambao ulikuwa unahudumia barabara kwenye miji, mradi huu sasa umekwisha kamiliika na tumeanza mradi mwagine wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure Competitiveness* yaani TA/C ambao utasaidia miji 40 kujengewa barabara za mawe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali, kupitia mradi huu na barabara hizi za mawe zikianza kujengwa, maeneo mengi kama Ukerewe tuna fursa ya kutumia mawe kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi, lakini bahati mbaya na barabara hizi kwasababu zinafadhiliwa na Benki ya Dunia, kuna kikwazo kimoja ambacho kinafanya kama zinafanyika, basi watu wetu hawapati fursa ya kunufaika na barabara hizi. Sasa

niombe Serikali, kwasababu kuna ile Sera ya Ujenzi ya Mwaka 2003, hebu Serikali muone kama mnaweza kuifanya mabadiliko ili angalau kiwekwe kipengele kinachowenza kuruhusu matumizi ya nguvu kazi (*labour based*), hili litasaidia sana watu wetu angalau kuweza kunufaika na barabara hizi kwa kupata ajira, kwa sababu shughuli hizi za kuponda mawe kufanya nini, kupanga yale mawe barabarani itasaidia sana kuchocha uchumi wa watu wetu. Kwasababu likifanyika hili ni jambo jema sana na watu wetu ndiyo watakao nufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na hizi barabara ni nzuri ukilinganisha na lami kwa mfano kwa tathimini, ujenzi wa barabara za mawe gharama yake ni karibu robo ya barabara kilomita moja ya barabara ya mawe, ni karibu robo ya barabara ya lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, angalau ikifanyika kama nilivyopendekeza, itasaidia sana kuchocha uchumi wa watu wetu kwasababu watu wetu angalau hasa vijana wataweza kunufaifa kwa kupata ajira ndogo ndogo katika kufanya shughuli kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la mwisho ambalo nilitaka nichangie ni juu ya upungufu wa watumishi kwenye halmashauri zetu. Wamesema wachangiaji waliotangulia, kwenye maeneo tunayotoka hasa maeneo ya pembezoni kama ilivyo visiwa vya Ukerewe kwasababu ya jiografia yetu mara nyingi watumishi wanapopangwa kwenda kwenye maeneo yale, wanafika wanaripoti na kuondoka! Niombe wizara, kwa changamoto kama hizi, tuone namna ambayo tunaweza tukatoa hata posho ya mazingira magumu. Ili angalau watumishi wetu wanapopangiwa kwenye maeneo haya, waweze basi kukaa na kuwashudumia wananchi wetu, angalau wananchi waweze kufaidika na Serikali yao kupata huduma zile zinazostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye maeneo kwa mfano Ukerewe mwaka juzi tume pambana sana kuhamasisha wananchi tukajenga madarasa zaidi ya 400; tumejenga

maboma kwa ajili ya zahanati yote haya yamekamilika tunahitaji msaada angalau muweze kutushika mkono tumalizie kazi hizi. Pamoja na fedha mlizozitoa kwenye bajeti hii kwa ajili ya kusaidia ukamilishaji wa maboma Ukerewe kama *specific area* tunaomba mtusaidie angalau haya maboma tuliyoyajenga kwa kushirikikana na wananchi zaidi ya 400 tuweze kuyaezeka. Jambo hili litasaidia wananchi wetu kupata moyo na kuona Serikali inawajali na wakati mwingine hata ukiwahitaji waweze kushiriki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa fursa hii, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe. Nilishakuita Mheshimiwa Lucy Mayenga na atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia leo humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kumshukuru Mungu kwa kunijalia leo kuongea hapa ikiwa ni kipindi changu cha nne. Pia niwashukuru walionileta hapa, wapiga kura wangu wa Mkoa wa Shinyanga nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niwape pole Wabunge wote, nafahamu kwa mujibu wa Kanuni pole zilishatolewa lakini kuna kitu kinaniambia kwamba nirudie kuwapa pole Wabunge wote kwa msiba mkubwa uliotokea wa kiongozi wetu Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI. Kwanza kabisa, naomba kumpogezza Mheshimiwa Waziri, Ummy Mwalimu sina shaka naye, najua ni mfuatiliaji, ni mtu wa vitendo zaidi na nafahamu kwamba yale yote ambayo sisi kama Wabunge tuna kiu nayo ana uwezo nayo. Hongera sana Mheshimiwa Ummy. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini maendeleo yoyote yale kwenye Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaahayataweza kufikiwa ikiwa hakutakuwa na umaja na mshikamano kuanzia juu mpaka chini, kwenye ngazi za Mikoa maana Wizara hii inagusa kuanzia Mikoa, Wilaya mpaka kule chini kabisa kwenye Kijiji. Lipo jambo ambalo jana Mheshimiwa Rais amelisema, kwa nafsi yangu siwezi kuliacha likapita kimya kimya. Mheshimiwa Rais alisema kwamba humu ndani Bungeni mwenendo wetu lazima tuuangalie. Kauli ile unaweza kuiona kama ndogo fulani hivi lakini viro vitu ambavyo vinatusababishia humu ndani kukosa umaja na mshikamano.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba wapo watu tena ni wengi, ambao mtu akipinga anapinga kutoka moyoni na mtu akiunga mkono bila kungalia vyama, kuna mtu anaweza akawa yupo chama kingine wala siyo CCM, lakini akisema jambo akikosoa au akipinga anapinga kutoka moyoni. Mimi naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kuhusu uzoefu wangu wa humu ndani, kidogo tu, miaka niliyokaa wala sio mingi kiasi hicho. Mimi ambacho nakiona lipo kundi la watu ambalo wao wanataka wamchomoe Mheshimiwa Samia kutoka kwenye utawala wa Magufuli kama vile hakuwepo. Kundi hili kazi yake wanakaa, wengine wanamsifia kwa nia njema kweli kama kumsifia lakini wengine wanamsifia kwa maana ya kudhoofisha *legacyya* Magufuli. Jambo hilo hatuwezi kulikubali hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini lipo kundi lingine ambalo wao tunatofautiana yaani kila siku tangu Magufuli alivyokuwa yupo madarakani wao ni kumpinga Magufuli. Leo mtu yule yule anasimama anasema, Mheshimiwa Samia nakupongeza sana bora umekuja wewe na mtu yule hata alivyokuwa Magufuli alikuwa anapinga sana leo ukimpongeza Mheshimiwa Samia kuna ajenda za siri. Mimi naomba kusema mkakati wenu tunaujua na mfunge midomo yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu Samia na hapa naomba pia niseme inatakiwa sisi tusimame kwa nguvu moja kwa haya mambo ambayo yanayotokea na tuseme

hapana. Lazima tumuunge mkono Rais wetu kwa vitendo na siyo kumuunga mkono kwa kuzungumza humu ndani Bungeni, tumuunge mkono hata huko nje ambako tunatoka. Hiki kinachofanyika ni kumchonganisha Rais wetu Samia na umati wa watu kule nyuma. Mheshimiwa Rais Magufuli alikuwa na watu wake amba walikuwa wanampenda na kumtegemea leo unaposimama unasema kwamba wewe ulikuwa unampinga Magufuli halafu unaamua makusudi kabisa kwa mkakati amba mmekaa huko uchochoroni mmeupanga mnaanza kusema kwamba sisi tulikuwa tunampinga Magufuli tuanze kumsifia Samia sio jambo la sawasawa. Huu mkakati naomba niwaambie utafeli kwa sababu Mheshimiwa Samia hana kundi hata moja, Mheshimiwa Samia hajajiunga na mtu yeote, Mheshimiwa Samia nafasi aliyonayo ni Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani? Mambo kama haya yaliwahi kutokea mwaka 2016/2017 wapo watu amba ndiyo hawahawa yaani kila siku ni hawa hawa, kwanza najiuliza hivi ninyi ni akina nani kwa sababu kila siku huwa ni hawa hawa wenye maneno, makelele. Mimi nilikuwa natamani siku moja nimwambie Rais hata Mheshimiwa Samia kwamba hawa watu wakipewa vyeo siku wakiondolewa mtuambie sababu.

Nasema hivi kwa sababu wakati mwingine mtu anafanya mambo ya ajabu lakini mkija kuangalia mambo yake huko mengine yanatia aibu na yalikuwa ni mabaya lakini ukisamama hapa sasa hili ni Bunge jipya Wabunge wengine wapya wanatuuliza sisi ambao kidogo wa zamani jamani Mheshimiwa Mbunge ...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Lucy sasa turudi kwenye bajeti. (*Makofi/Vigelegele*)

Naomba tusiendeleze hilo Mheshimiwa Mbunge unayeomba kutoa Taarifa, tumrudishe mwenzetu kwenye bajeti halafu iwe imetosha. (*Makofi*)

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, ujumbe umefika na umekuwa *delivered*. Cha msingi ni kwamba naomba sisi tuache hayo mambo ya ajabu, tukae kwenye mstari tumuunge mkono Rais wetu kwa asilimia 100 na kwa vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu TAMISEMI, kama nilivyoeleza hapo awali najua uwezo wa Mheshimiwa Waziri wetu. Ripoti ya CAG imeeleza bayana kwamba yapo mambo ambayo yamekuwa yakifanyika huko kwa Wakurugenzi bila kusema ni wa maeneo gani lakini kwa kweli hayaridhishi. Naomba Mheshimiwa Waziri ashuke kule chini aende akafanye kazi hii kwa vitendo. Kwa kuwa najua kwa uwezo wako utafanya kazi hii kwa vitendo, ile *field* aliyokuwa anaifanya alipokuwa Wizara ya Afya naomba aende pia *field* kwenye Wizara hii kwa sababu yapo maeneo ambayo watu wanalamika sana, matatizo ni mengi, watu wanajichukulla sheria mkononi. Utawala huu kwenye Serikali za Mitaa kuna baadhi ya maeneo huko vijijini kwenye kata na kadhalika na hasa kwenye Mabaraza ya Ardhi, naomba Wizara hii ya TAMISEMI iweze kuwa na mkakati maalumu yale mambo ambayo yanazungumzwa kwenye masuala ya ardhi na kadhalika ambayo yanahusu Wizara hii yaweze kufanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kwa kuwa Waziri ametoka Wizara ya Afya najua Wizara hii ya TAMISEMI inahusika pia mambo ya afya, naomba afuatilie kuhusu matumizi ya pesa za Serikali zinazoshushwa kule chini. Pesa nyingi sana zinashushwa kule chini lakini tija inaonekana kwa kiwango fulani cha kawaida lakini kwa kiwango kikubwa upigaji unaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mimi nitoe ushauri tu kwamba Katibu wa *caucus* ya Wabunge wa CCM muitishe vikao vya mara kwa mara kama kweli mnaamini kuna makundi mionganoni mwenu basi mahali ambapo mnawenza

kudhibitiana Wabunge toka chama kimojawapo siyo kwa Spika kwa sababu hapa ni vigumu sana kufanya hivyo. Mahali ambapo mnaweza kuyazungumza wazi na mkajibiana na mtuhumiwa akapata nafasi ya kujibu kama yupo ni kwenye *caucus*. (*Makofi*)

Sasa mambo ya kwenye *caucus* mkiyaamishia hapa mnatupa ugumu tu wa namna ya kuendesha. Maana kusema ukweli mimi sijui kundi na Bunge hili ni jipya sana na kundi hilo ni la nini hata mimi nahitaji kufahamu hebu yapelekeni kwenye *caucus* na sisi tutajifunza kule kwamba kuna nini, mbona mimi naona kama kawaida tu yaani *what is the objective*, kuna mtu ana lengo gani, kuna nini, sana sana mtu akisimama anazoza kivyake tu na tunawajua. Sasa mtu akizoza haiwezi kutushughulisha kuwa ni shughuli ya Bunge. Hata hivyo, kama yapo basi hayo ni ya akina Mheshimiwa Rwekiza na Shangazi iteni hivyo vilkao, siku za Jumapili ita kikao saa tano asubuhi, ndivyo ilivyokuwa zamani, watu wanapiga mpaka saa kumi na mbili jioni, mnasemana yanaisha, kesho yake ikiwa Bunge tunafanya mambo ya Bunge, makundi tunayaacha hukohuko. (*Makofi*)

Katika siasa makundi siyo kitu cha ajabu ni kitu cha kawaida, siasa ni makundi lakini mradi hayaleti sumu ambayo inatufanya tusiweze kwenda vizuri. Katika mazingira ya sasa Bunge hili salama kabisa mimi sijaona kama tumefika mahali ambapo tunayumba sana. Hata hivyo, kama hiyo hali ipo wenzangu mnaiona basi kwenye *caucus*, mkihamishia hapa mambo ya *caucus* tunachanganya madawa. (*Makofi*)

Ahsante sana, nilishakutaja Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Marwa.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kidogo kuhusu hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Niseme tu kwamba hata jana Mheshimiwa Rais ametuambia kwamba sisi kama Wabunge tuchangie bajeti na kuishauri Serikali, mimi naomba niishauri Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na hii *issue* ya Madiwani. Mimi nimewahi kuwa Diwani kwa kiasi fulani naelewa namna vikao vinavyoendeshwa katika halmashauri. Nachopenda kuishauri TAMISEMI ni kwamba Madiwani wapewe mafunzo yaani hilo msilikwepe. Najua mnasema bajeti ni ndogo lakini mnaposhindwa kuwafundisha kama sisi tunavyofundishwa, mimi niko kwenye Kamati ya LAAC nakushukuru kunipeleka kule lakini tunapewa semina namna ya kufanya *financial tracking*, namna ya kufuatilia na hata namna ya kuhoji tupo *equipped*/kabisa tunakwenda kufanya kazi ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halmashauri inaendeshwa na vyombo viwili; *executive* na *politicians* ambao ni Madiwani. Madiwani mnawajua, sisi tunajua kusoma na kuandika unakwenda ndani ya halmashauri unakuta Mkurugenzi ana *degree* yake wengine *masters* halafu unamuweka Diwani ambaye anajua kusoma na kuandika lazima kwa vyovytote vile Wakurugenzi wata-*overpower* Madiwani na hicho chombo kinahitaji Madiwani kama wasimamizi na kile ni chombo chao.

Kwa hiyo, kuwafundisha mara kwa mara angalau mara moja kwa mwaka ni muhimu sana hata kwa bajeti ndogo kuwapelekea wataalam wawafundishe namna ya kusimamia halmashauri na fedha za umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nashauri katika hili ni kwamba...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nashauri tumsikilize Mheshimiwa Mbunge.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, Madiwani katika Kamati zote wanapaswa kusimamia miradi, ndani ya halmashauri miradi inasimamiwa na Kamati ya Fedha ambayo inaweza kuwa *corrupted* kwa urahisi sana. Kwa hiyo, mruhusu TAMISEMI iondoe hizi kanuni za kuzuia Kamati nyininge zisiende kusimamia miradi ambayo inahuusu Kamati zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kuhusu ujenzi wa vituo vya afya katika huduma ya afya, hapa nina maana ya zahanati, vituo vya afya na hospitali. Kitu ambacho nimeona ni kwamba hakuna mfumo wa kudhibiti ujenzi wa miradi hii, hakuna mfumo wa ufuutiliaji na hata TAMISEMI haitoi fedha katika Sekretarieti za Mikoa ili waweze kusimamia miradi hii. Kwa mfano, kuna hiki kitu kinaitwa *force account* inasimamiwa na Kamati ya Ujenzi katika maeneo ambayo miradi hiyo inatekelezwa hawa ujuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine hakuna ma-*engineer* hata ukisoma tu haraka haraka tu katika ukaguzi wa *CAG* japokuwa hatujafika mahali paku-*discuss* lakini tunaweza kufanya *reference* ametuambia kwamba ma-*engineer* karibu asilimia karibu 75 walihamia *TARURA*, kwa hiyo, halmashauri inafanya kazi zake kwa kutumia Kamati za Ujenzi ambazo hazina ujuzi lakini pia kwa kutumia mafundi mchundo (*technicians*). Kwa hiyo, unaweza kukuta majengo haya ambayo tunajenga ili kutoa huduma kwa wananchi yanaweza kukosa tija kwa sababu hayakusimamiwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie utaratibu wa kuajiri ma-*engineer* katika halmashauri. Mara nyingi tumependekeza kwamba kuwepo na ma-*engineer*, juzi hapa tulikuwa Singida na bahati nzuri tulikuwa na Naibu Waziri hapo, tulichokiona na yeye alikiona nisiseme mengi, hiyo inadhihirisha kwamba majengo yanayojengwa na watu hawa kupitia *force account* na usimamizi wa Kamati hizi kwa kweli mengine nina wasiwasi yakaleta *crisis* siku zijazo; yakabomoka mapema wakati yametumia fedha nyingi kwa sababu hayako vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika ufuutiliaji *CAG* ametueleza kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 mpaka 2019/2020 miaka mitano TAMISEMI haijawahi kupeleka fedha ya usimamizi katika Sekretarieti za Mikoa. Ina maana mnawanyima uwezo Sekretarieti za Mikoa kufuutilia na kusimamia miradi hii jinsi inavyojengwa katika halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niongeza machache kuhusiana na *force account*, nashauri iwe na *limitation* ya fedha, haya ni mawazo yangu, kwamba una mradi wa shilingi bilioni moja na kitu au bilioni mbili, tatu inasimamiwaje na *force account*? Kwa hiyo, Serikali mtazame kwamba *force account* kama ni mradi wa shilingi milioni 100, 200, 300 unaweza ukasimiwa na zile Kamati lakini ukishavuka pale ni lazima tufikirie namna nyingine ya usimamizi. Kwa hiyo, tuweke *limit* katika jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, niongelee uwezo wa utendaji wa halmashauri zetu. Nimefuatilia hapa wakati Waziri anasoma hotuba yake amegusia kuhusu halmashauri kupewa hati chafu. Unajua mimi huu ukaguzi umenitisha na umenishangaza sana kwa sababu katika Kamati ya LAAC tumefanya kazi kubwa na wewe umetuwezesha, tumejaribu kusimamia na mimi nashangaa hizni hati zilmetoka wapi, kwa kweli mimi sikufurahi lakini nilichoona ni kwamba kuna uwezo mdogo wa watendaji ndani ya halmashauri. Kitu kingine hata uteuzi wa Wakurugenzi hauzingatii uwezo wa kusimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu gani nasema hivyo? *Local government* ina tofauti na Serikali Kuu, kuna chuo pale Hombolo *special* kwa sababu hiyo, kwa hiyo, Wakurugenzi wanapaswa kufanyiwa *vetting* japokuwa Katiba inasema tuwatue. Mimi kwa mawazo yangu nafikiri watu wangeomba, wakafanyiwa *vetting* ndiyo waajiriwe au mtazame wale ambao wameshafanya kazi kwenye *local government*; amekuwa Mweka Hazina au Afisa Mipango ana uzoefu wa aina fulani wa kuendesha *local government*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo kiutendaji ndani ya halmashauri kwa kweli hata kwenye idara huku mnapatupa lakini mkumbuke bajeti mliyoomba leo shilingi trilioni saba na kitu *is a lot of money*. Kwa hiyo, mnakwenda ku-deal/na pesa nyingi sana na halmashauri ndiyo zinasimamia maendeleo ya watu, zinatekeleza sera ya Serikali Kuu, ndiyo zinazelekezwa kama ni kuandikisha watoto kwenda shule kila kitu ninyi kama

Serikali Kuu mnaelekeza halmashauri inafanya kazi. Kwa hiyo, tunapaswa kuwa na watendaji wazuri lakini pia tunapaswa kuziwezesha kwa sababu sasa hivi mnajua kwa muda wote tulikuwa tunalia halmashauri zimenzang'anywa mapato yote.

Mheshimiwa Spika, nimalizie haraka haraka nasikia kengele ya kwanza imeshagonga, hata hii *ten percent* ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni kitu kizuri kabisa lakini ukitazama ametueleza ni zaidi ya shilingi bilioni 29 ambazo zimeshatolewa kwa makundi. Naomba niulize hiso pesa huwa zinarejeshwa na zinawekwa wapi?

Mheshimiwa Spika, kama hamjawahi kuona kama kuna pesa inapigwa, ni pesa hii. Nenda kwenye Halmashauri, ikirejeshwa inawekwa kwenye akaunti ipi? Hakuna *rotation* hapo. Maana yake, nafikiria kwamba tungeweza kuwa na *barkwamba* sasa Halmashauri ina mfuko wenye shilingi bilioni tano, hiyo pesa nyiningine itajenga kitu kingine na hii itakuwa ina-*rotate*. Fedha hizi hazirudishwi, yaani inakuwa kama zaka; kama sadaka vile. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi fedha zinapelekwa kisiasa, watu hawazirudishi. Zikirudishwa, uliza Halmashauri, zinawekwa akaunti ipi? Tulipewa taarifa kwamba kuna akaunti zimeelekezwa kufunguliwa, hatujafuatilia sana labda tutafuatilia wakati huu tukienda kugakua baada ya *CAG* kutoa ripoti yake, lakini hakuna akaunti yoyote ambayo inahifadhi hizi fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zinarudishwa, zinawekwa kwenye akaunti ya amana; mara zisemwe ni za maendeleo na kadhalika. Huwezi kumwuliza Mkurugenzi ziko wapi? Ina maana anapashwa kukata kila mwaka. Anapaswa kukata kwenye kila mapato, anakata wee, mpaka lini? Kwa hiyo, anapaswa kukata, lakini kuwepo na *bar ili* huu mfuko ufanye *rotation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza. Nilishakutaja Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa na baada yako atakuwa Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii. Kwanza nampongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Ummy kwa kuteuliwa. Naamini kabisa wewe ni jembe, unaweza na yale mazuri yote yaliyoanzishwa naamini kabisa utayaboresha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa hapo ulipo presha inakupanda, unasema, huyu ndio Agnes wangu za zamani! Hivi kweli nini kinaendelea? Ila mimi ni Agnes mpya, nimefundwa na wewe, sasa hivi niko vizuri, usiwe na wasiwasi. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, dada yangu Mheshimiwa Waziri Ummy, , kama vile ulivyokuwa unafanya ziara kipindi kilichopita, nakuomba sana, ukipata nafasi dada yangu njoo Mkoa wa Mara, ikiwezekana niite nami nikuoneshe baadhi ya vichochoro kule kwetu vijijini; Wilaya za Serengeti, Rorya, Tarime, Bunda, Musoma Vijijini, Mwibara na kwingine uone jinsi barabara zetu zilivyokuwa mbovu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi ili unielewe kwamba *TARURA* wana mzigo mbito sana. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, bajeti ya *TARURA* ikiletwa ndogo kwa kweli inabidi tumrudishe kidogo Mheshimiwa Waziri aende akachakate ili airekebishe iongezwe. Kwa sababu *TARURA* wamepata mzigo mkubwa sana, lakini kutokana na kazi zao wanazozifanya, kwa kweli huwezi ukawalaumu kwa bajeti wanayopewa. Bajeti yao ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kubeba jukumu la kujenga kwenye mitaa na bajeti waliyopewa iwe ndiyo hii ambayo tumeiona, halafu tuseme kwamba *TARURA* watafanya vizuri, siyo kweli. Tutabaki kuwalaumu kila siku *TARURA* bila kujua tatizo liko wapi? Tunapaswa kwanza

kutatua tatizo halafu baadaye tuone utendaji kazi wao ukoje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba sana dada yangu, Mheshimiwa Ummy, jipinde sana uangalie kuhusiana na hili suala la *TARURA*. Siku ukirudi hapo mezani, basi utuelezee vizuri hili suala limekaaje na bajeti yao umeirekebisha vipi?

Mheshimiwa Spika, pia namshukuru mama yetu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu. Kwa kweli hotuba yake ya jana ilikuwa nzuri sana. Binafsi nilifurahi kusikia akisema kwamba ataboresha mishahara ya wafanyakazi. Kwa kweli wafanyakazi hawa mama yetu wana imani sana na wewe. Siyo tu kwamba wana imani sana na wewe kwa sababu eti utawaongezea mishahara au kuboresha mishahara yao. Wana imani kubwa kwa sababu utendaji kazi wa mama wanaujua toka kipindi kilichopita akiwa na baba yetu Hayati JPM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kabisa wafanyakazi wana imani na wewe mama, kaa vizuri mama, angalia vizuri, chakata chakata na Wizara yako, hawa wafanyakazi kama ulivyo sema nao wafurahi, kwa sababu kila kukicha bajeti zinazidi kubadilika na hasa bajeti za kifamilia zinakuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande huo wa wafanyakazi, nakwenda kwa Madiwani. Ndugu zangu, Wabunge wezangu, Madiwani wetu ndio wanaotulindia magoli. Wana kazi kubwa sana. Bila Diwani wewe ukitoka hapa Bungeni ukienda, unamwuliza Diwani, sehemu fulani kuna nini?

Mheshimiwa Spika, sehemu fulani kuna tatizo gani? Huyo ni Diwani, naye ndio yuko kule muda wote. Mtu akiugua anaenda kumdai yeye Diwani; akitokea Mjumbe amekuja; wale ambao si mnajua tena, Wajumbe noma, lakini Diwani anamtuliza yule Mjumbe wako. Pia hawa Madiwani ndio wametuweka sisi madarakani na ndio wameiweka Serikali hii madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa maana ya kwamba wao ndio wanaishi moja kwa moja kwa siku zote kule Majimboni kwetu au kwenye Kata zao na wananchi wetu. Kwa hiyo, ukweli ni kwamba Madiwani wanapaswa kuongezewa posho zao, kwani hazitoshi, hazikidhi mahitaji yao, kwa kweli wanapata kiasi kidogo sana ukilinganisha na majukumu walijonayo.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana dada yangu, Mheshimiwa Waziri Ummy, hili suala sasa aliangalie zaidi. Ikiwezakana jamani, kwenye Wizara basi mwangalieangalie, kwa sababu mmeshaona kule kwa Wakurugenzi kuna shida, basi mlipe moja kwa moja kutoka Wizarani wale Madiwani angalau wajue kwamba tuna mshahara wetu unatokea huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hata kwangu, Mkoa wa Mara ni kati ya mikoa ambayo ni wahanga wa Madiwani kukopwa. Jamani, kweli tunawakopa Madiwani ambao ndio wanaofanya kazi kubwa sana. Hata huyo Mheshimiwa Mkurugenzi mwenyewe anamtegemea Diwani kule chini na Mheshimiwa *DC* anamtegemea Diwani kule chini, lakini bado. Siyo tu kwamba wanawakopa, hawajatuambia hizo fedha wanazowakopa ziko wapi? Wamepeleka wapi?

Mheshimiwa Spika, nakuomba dada yangu, Mheshimiwa Ummy, ukienda kawaangalie hawa Wakurugenzi, ukawafanyie ukaguzi. Utakuta uharibifu mwangi sana na upotevu mwangi sana wa fedha ambao wanaufanya na hasa pale wanapowafanya uonevu Madiwani. Kwa kweli haikubaliki, Wabunge wenzangu, haikubaliki, tukatae kabisa wasiwaonee hawa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, kipekee niende moja kwa moja kwenye suala la shule. Shule zetu na hasa za vijana wetu wa kike zimekuwa ni nzuri sana ambapo kwa sasa vijana wa kike wamejitalidi, kiasi fulani kwa kweli wamepanda katika ufaulu, wameanza kuwa na ufaulu mzuri, lakini changamoto inayokuja ni pale ambapo vijana wetu wa kike wengine

ambao hawawezi ku-afford kupata taulo za kike, inawapa shida, wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu sikivu, moja kwa moja kama vile tunavyoweka bajeti nyingine za shule kwa watoto wa shule kama watoto wa kiume wanavyowekewa zile *packages* zao, basi tuangalie na kwa watoto wa kike wawekewe moja kwa moja. Kama vile ambavyo Serikali inakuwa imewalipia ada, basi waangalie pia na kwa hawa watoto wa kike wawekewe ili wale watoto ambao hawajiwezi, umri ambao wanakuwa wameanza kupata hedhi, basi waweze na wao kujiangalia kwamba wanaweza kusoma na hawawezi kupata matatizo madogo madogo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Agnes. Nilishakutaja Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Awali ya yote, nami namshukuru Mwenyezi Mungu kuwepo mahali hapa wakati huu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Serikali za Mitaa, kwa misingi hiyo, mambo mengi tunayoongea haya tulipata nafasi ya kuyajadili katika ngazi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, niendelee kushukuru katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa maana ya fedha iliyotoa...

SPIKA: Nawaomba Wabunge ambao mmesimama upande huu, mnaopiga soga, kwanza mkae kwenye viti vyenu ili uchangaji uweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Kapufi, endelea.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa maana ya lile zoezi la ukarabati wa shule kongwe. Zoezi hili limekwenda vizuri. Kote tulikopita; Jangwani, Azania, Kilakala, tumeona kazi nzuri iliyofanyika. Pamoja na kazi nzuri hiyo, changamoto hazikosekani, ni pamoja na eneo hilo la *force account* kama walivoyzungumza Wajumbe wengine.

Mheshimiwa Spika, rai na ushauri wangu kwa Serikali, *force account* linaweza likawa ni jambo jema, lakini tusipojikita kwenye thamani ya fedha, suala la *force account* nalionna lina matatizo pia. Tuliweza kupita kwenye shule moja, kama sikosei kama siyo Kilakala itakuwa ni Mzumbe; jengo la nyuma wataalam walishindwa kutindua *cement*. Walishindwa kutindua sakafu kwa sababu ya uimara wake, kiasi kwamba wakaamua kuiacha ilivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna baadhi ya majengo yanajengwa leo, kesho sakafu ni mbovu. Narudia kushauri suala la thamani. Tusipojikita hapo, tutajikuta tuna idadi kubwa ya viti vilivyotengenezwa vyenye ubora hafifu. Naomba sana hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Kibunge cha Idadi ya Watu na Maendeleo. Kwa nyakati tofauti tumekuwa tukikuita kushiriki katika semina zetu. Kama Mwenyekiti wa Chama hicho, nataka kusema nini kwenye Bunge hili? Idadi ya watu siyo tatizo, lakini ukiwa na idadi kubwa ya watu ambao ni tegemezi, tatizo linaanzia hapo. Tafsiri yangu ni nini? Leo tutaishia kutamani kujenga madarasa mengi, kuongeza madawati, lakini bila kwenda kuzingatia suala la idadi ya watu, kwa sababu kwa kupitia

idadi ya watu ndiko huko ambako tunaweza tukapanga mambo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikilisema hilo namaanisha nini? Unapokuwa na kundi kubwa la watu ambaao ni tegemezi na wachache ambaao ni wazalishaji, hapo lipo tatizo; lakini kwa maana ya idadi ya watu na maendeleo, bado inaweza ikatumika vizuri ikawa ni chanzo cha maendeleo pia. Ikitumika vizuri! (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikilisema hilo naendelea kumaanisha nini? Tukijikita kwenye kujuja idadi ya watu, leo hatuna sababu ya kukimbizana na kufanya mambo kwa *design* ya zimamoto. Unajua kabisa tuna idadi hii ya watoto ndani ya muda huu watatakiwa kufika shuleni, ndani ya muda huu watahamia hapa, na hapa na watakwenda pale. Kwa hiyo, mipango yetu yote italiangalia hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaendelea kushauri, katika hilo, tukiwa na idadi ya watu, bado mimi naweza nikasaidia kuishauri Serikali, tunafanya nini katika hili? Ni pamoja na kutoa elimu. Tusiache elimu kwa watoto wa kike. Mtoto wa kike tunapompa elimu maana yake ni nini? Kwanza ule muda atakaokaa shuleni na akapewa elimu nyingine ya kumsaidia kuepuka mimba za utotoni na ndoa za utotoni inatusaidia kuepuka kuwa na idadi ya watu wengi ambaao baadaye wanakuja kuwa tegemezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke hapo. Wengi wameongelea habari ya *TARURA*. Namkumbuka Marehemu Baba wa Taifa, alisema hivi, "ukiwa kiongozi, ukapita mtaani, ukamwona mtu mmoja labda hana chakula, yule hana nguo, mwингine hajapata dawa hospitali, kiongozi unatakiwa kusema, huu ni mzigo au msalaba wangu."

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni nini? Leo ukienda kwa mfano Manispaa ya Mpanda, ule mji siyo tu kwamba barabara hazipo, lakini kwa mvua zinazoendelea kunyesha tumetengeneza mitaro. Kwa hiyo, *TARURA* wasipoongezewa fedha ile shida iliyokuwa inajitokeza ya mitaa ambayo

barabara zake hazieleweki, tunakuja kwenye tatizo lingine, nyumba za wananchi wetu zimekuwa zikining'inia.

Mheshimiwa Spika, leo ukipita Mbunge, kama nilivyosema, Baba wa Taifa alikuwa anasema huu ni mzigo wangu, nami kama Mbunge, japo ule ni mzigo wangu, lakini nimetimiza haki yangu ya Kikatiba ya kulisemea suala hilo hapa Bungeni. Kwa hiyo, nisaidieni kunitua mzigo wataalam ninyi kwa sura ile iliyopo ya barabara pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili Mtendaji Mkuu wa *TARURA* ni mtu rahimu, lakini peke yake bila kumpa fedha atafanya nini? Kwa hiyo, naomba sana. Wakati wote tukipiga kelele *TARURA* iongezwe fedha, tunaishauri nini Serikali katika suala la kuongeza fedha eneo la *TARURA*? Wapo wanaozungumzia labda kwenye miamala ya simu tukiongeza kidogo hapo, sasa wataalam nendeni huko mkatusaidie kwamba chanzo gani kingine tunaweza tukakibuni kikatusaidia watu hao wakapata fedha ili wakati tunatafuta haki na wajibu uwepo pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa eneo la elimu; mimi kwangu Katavi ni bahati mbaya yale maeneo yanatosomeka kama maeneo ya pembezoni. Kipindi cha nyuma wakati wa Awamu ya Nne ilikuwepo mikakati ya makusudi ili kuikomboa mikoa ya pembezoni. Leo maeneo yetu yale, kwa mfano, ukiacha tatizo la barabara, leo unaweza ukakuta hata kama mmeipatia fedha Halmashauri jirani ya Nsimbo kwa barabara moja, mfano barabara ya kutoka Mpanda kwenda Mtapenda, barabara ile ukiwa umeipa Halmashauri ya Nsimbo fedha, wakati yule mtu lengo lake aje mkoani nami wa Manispaa hujanipa fedha na daraja halipitiki, bado ile thamani ya fedha hutaiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hayo mambo yanafanyika maeneo mengi. Tanganyika *likewise*; unakuta mwenzangu amepewa fedha lakini hawesi kuunganika kuja mjini. Barabara za kuja mjini hazipitiki. Kwa hiyo, naomba sana hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la elimu kama nilivyosema, kuna mazingira ambapo baadhi ya watendaji; walimu, mimi mwaka 2014 ndiyo mara ya mwisho kupata walimu wa Shule ya Msingi. Mpaka leo sijawahi kupata walimu wa Shule ya Msingi. Walimu wa Shule ya Sekondari unaweza ukaletewa wanne. Kwa sababu sisi ni mikoa ya pembezoni, inafika mahali wengine wanahama, kwa hiyo, kuna shida kubwa katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo la afya, wengi wameongelea. Nami pale Manispaa ya Mpanda nina kituo kimoja tu cha afya. Sasa unapokuwa na kituo kimoja, hospitali ya mkoa haijaisha, mnafanya tunakuwa pembezoni zaidi. Tungeweza kupunguziwa upembezoni huo kwa kusogezewa huduma hizi karibu na maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu eneo la miradi mingineyo, sisi leo tunakwenda karibia awamu ya pili upande wa barabara za lami. Sisi ni Manispaa. Manispaa nyingine wanabahatika kupewa kilometra chache za lami, lakini Mpanda sijui tumesahaulika katika nini? Naomba nalo hilo lijaribu kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho tulipiga kelele, hata fedha tu za maendeleo kwa maana ya Mpanda Manispaa hatukuletewa. Ni baada ya kupiga kelele ndiyo tukaletewa fedha hiyo. Ni bahati mbaya, kuna kipindi fedha ikiipelekwa ambayo leo ni Tanganyika, kipindi hicho ikiitwa Mpanda kama sisi; au ikiipelekwa maeneo mengine, watu wa Manispaa tunaonekana tumeletewa fedha. Hilo tatizo limetuathiri sana. Mgao kwa maana ya Manispaa, tumeathirika sana katika eneo hilo. Kwa hiyo, naomba, kama nilivyosema upande wa walimu na mambo mengine ya namna hiyo, naomba sana tujaribu kuzingatiwa hapo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie, kipindi cha nyuma walikuwa wanasema usiniletee biashara ya nyanya. Tafsiri yake ilikuwa nini? Maana yake katika ubovu wa barabara, unaweza usiifikishe nyanya sokoni. Leo hii katika mazingira ya barabara nzuri, hata nyanya bado ni biashara. Kuna

maeneo mbalimbali, llula huko na kwingineko, miji imekua, biashara ya nyanya imesababisha maendeleo ya watu. Kwa hiyo, hata ile kauli iliyokuwa ya kubeza biashara ya nyanya imetoweka baada ya uwepo wa barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sebastian Kapufi. Mheshimiwa Bonnah Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Kyombo.

Mheshimiwa Bonnah.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Ummy kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa TAMISEMI na wasaidizi wake wote. Nimekuwa hapa katika miaka yangu mitano, namjua uwezo wake na ninajua yupo sehemu sahihi. Kwa hiyo, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie katika suala la *TARURA*. Katika llani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 – 2025, ukurasa wa 71 - 82, Serikali imesema itajikita kuongeza fedha *TARURA* ili iweze kupambana na matatizo yake au kutatua matatizo yake kuhusiana na barabara.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema Wabunge wenzangu *TARURA* ni taasisi ambayo kwanza inafanya Wabunge wengi tuweze kuonekana kwamba hatufanyi kazi *especially* sisi Wabunge wa Mjini ambao tunatakiwa kuonekana kwamba barabara za mitaa zinatengenezwa, lakini pia barabara zingine. Kutokana na huu ufinyu wa bajeti wa *TARURA* na kwa sababu tumekuwa tukienda nao kila mahali, tunaahidi haya mambo na hayatokei.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii imetufanya sisi Wabunge hasa wa mjini kuonekana kwamba hatufanyi kazi kabisa na tunakuja tu huku Bungeni kwa ajili ya kuuza sura. Sasa naomba Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mama Samia wakati anawaapisha Makatibu, alitoa kauli alisema kwamba, Manispaa ambazo zinakusanya pesa nyingi ziweze kutenga asilimia fulani kwa ajili ya kutengeneza barabara zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Dar es Salaam, Manispaa zote zinakusanya pesa nyingi. Ukianzia na Manispaa ya llala, lakini cha kushangaza pamoja na kwamba Manispaa ya llala ndiyo tunaongoza kwa mapato, lakini bado wananchi wetu wanaotuchangia wanatembea kwenye barabara mbovu sana. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri Ummy, kwa sababu Mheshimiwa Rais wakati anatoa hii kauli nafikiri Wakurugenzi na Wataalam wetu wallkuwa wameshakaa vikao vyao na wameshapanga bajeti. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Ummy aweze kulitolea kauli hili jambo la Mheshimiwa Rais kwamba Wakurugenzi watatenga vipi fedha kuhusiana na barabara zetu za mitaa.

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa bajeti umefanya Mkoa wa Dar es Salaam kuonekana barabara zake ni mbovu sana. Mfano Jimbo langu la Segerea, katika miaka mitano *TARURA* wameshindwa kujenga barabara ya *Airport* – Karakata ambayo ina urefu wa kilometra moja na nusu. Tumekuwa tunaahidi kila mwaka lakini barabara haijengwi na lile eneo la *Airport* ni eneo ambalo wageni wote wanaokuja, yaani ni kama mlango wa Tanzania. Wageni wanapofika tu pale ina maana wanakutana na barabara mbovu. Kwa hiyo kama Mheshimiwa Ummy atatoa kauli hii kwa Wakurugenzi wetu ili waweze kuangalia ni sehemu gani ambayo ni vipaumbele ambavyo sisi tumeviweka kwa ajili ya kuboresha mazingira basi itakuwa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *TARURA* hao hao kuna barabara sasa hivi inajengwa; Barabara ya Vingunguti – Barakuda wameijenga kuanzia mwanzo mpaka katikati, wameishiwa na pesa, kwa hiyo barabara hii imefungwa. Hii

inawasababishia wananchi matatizo makubwa, ina maana daladala haziwezi kupita pale, hakuna usafiri wowote ambao unaweza kupita pale na imekuwa pia ni changamoto kwetu sisi Wabunge, ina maana ukiamka tu asubuhi unakutana na hayo matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia *TARURA* hii hii pamoja na ukusanyaji mkubwa wa mapato wa Wilaya ya Ilala, kuna barabara ambazo za Kimanga, barabara ambayo ni kilometa mbili imejengwa kwa miaka mitano. Vile vile *TARURA* wameshindwa kumalizia Barabara ya Liwiti - Chang'ombe, mpaka sasa hivi haijawahi kumaliziwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Ummy na najua kabisa ana uwezo huo, aweze kuitolea kauli hasa Mkurugenzi wetu wa Manispaa ya Ilala. Kwanza napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwa kweli Mkurugenzi wetu ni mchapakazi, lakini pia anafanya kazi nyingi kwa ajili ya kutusaidia na tunaelewana vizuri. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Ummy atoe kauli ili sisi sasa tuweze kutengenezewa hizo barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni jambo la kuhusiana na *DMDP*. Najua pia hii *DMDP*ipo TAMISEMI. Mheshimiwa Mama yetu Mama Samia alikuja katika Wilaya ya Ilala, ndiye aliyezindua kampeni na matatizo aliyoyakuta pale yalikuwa ni matatizo ya barabara. Pia kuna ahadi ambazo tumezitoa pale kuhusiana na Mradi wa *DMDP* naongea hivyo kwa sababu huu mradi wa *DMDP* kuna hati hati kwamba umefutwa. Kwa hiyo tuna ahadi pale ambayo tuliahidi na Mheshimiwa Mama Samia. Jimbo la Segerea kuna matatizo makubwa, kwanza tuna bonde la Mto Msimbazi ambalo tuliahidi kwamba ikifika mwezi Januari tutaanza kuweka kingo.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ni mwezi Aprili kingo hazijaanzwa kuwekwa na wananchi wanaendelea kupata mafuriko na wananchi wanaendelea kuhama. Kila mwaka wanahama zaidi ya wananchi elfu arobaini katika

Jimbo la Segerea, kwa sababu ya hilo bonde la Mto Msimbazi. Kwa hiyo tunaomba Serikali iweze kuamua hili jambo na kuweka hizo kingo ili wananchi waweweza kama tulivyoahidi kwamba totalitengeneza hili Bonde la Msimbazi ili wananchi waendelee kukaa lakini pia na maji yaendelee kupita. Kwa hiyo tunaomba hicho kitu kisitolewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni barabara zetu za *DMDP* ambazo tumeziahidi tukiwa na Mheshimiwa Mama Samia kwamba barabara hizi kuna wananchi kule wanasubiri na wanajua kwamba tumeahidi kuna barabara ambazo zitajengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika Wilaya ya Ilala hasa huku kwetu Mheshimiwa Zungu anapenda kusema maji matitu Segerea, *water table* yetu ipo juu sana, kwa hiyo mvua ikinyesha kidogo hata hizi barabara ambazo tunaziwekea changarawe zinakuwa haziwezi kufanya kazi. Kwa hiyo nilikuwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Bonnah, tayari muda wako.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Kyombo nilishakutaja, utafuatiliwa na Dkt. Christina Mnzava.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi. Niungane na wasemaji waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu, lakini pia Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Dkt. Dugange kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na niwapongeze pia kwa kumpata Katibu Mkuu mzuri Profesa Shemdoe.

Mheshimiwa Spika, nataka nijielekeze katika maeneo machache ya kushauri ndani ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na

hasa yenyewe ikiwa ni kiungo kikubwa katika kuwafikia wananchi maana yake kutekeleza sera na miradi mbalimbali kwa wananchi wetu. Nianze na utayari wa kazi na ari ya kazi ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama Taifa. Mojawapo ya sifa ya kiongozi mwema ni kuweza kutambua upungufu au mahitaji halisi ya watendaji kazi wake ambao wanategemea waweze kutekeleza sera na miradi mahsusimbalimbali ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sifa nyingine ya pili ni kuweza kuwapa *motivation*, maana yake kuwaamini na kuwatambua. Nimekuwa nikiongelea hili suala mara kwa mara na leo limepata wizara yenyewe inayohusika. Eneo la halmashauri nikimaanisha Wakurugenzi wa Serikali za Mitaa na Wakuu wa Idara, nisikitike kusema kwamba imekuwa ni kama *punching boxya* viongozi wa aina mbalimbali, viongozi wa ngazi mbalimbali kuwa kundi hilli la watendaji ambao tunawategemea kufanya kazi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mazingira wanayofanyia kazi hawastahili kuhukumiwa kama wanavyohukumiwa. Mheshimiwa Ummy Mwalimu amefanya kazi ya Uwaziri katika Wizara mbalimbali kwote alikotoka ameacha alama na watu wanamkumbuka, nimwombe sana katika michango tunayoitoa hapa aipokee, aitafakari na akaifanyile kazi kule. Wale watu wanafanya kazi usiku na mchana, watu hawalali wanatekeleza miradi. Haya anayoyasikia tunayasema humu mengine ni kweli yana ukweli wake, lakini wachache hawawezi kufanya wote waonekane kwamba hawafai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana baada ya kipindi chake cha bajeti atenye muda wake, bahati nzuri amepata viongozi wazuri Profesa Shemdoe ni tunda la *U-DED*, Dugange huyu amekuwa *DMO* na amekuwa *RMO*, anajua mazingira mazima kwenye halmashauri. Mheshimiwa Silinde anajua, akaa nao aangalie mapungufu waliyonayo, akiwa-*console* matokeo makubwa ndani ya TAMISEMI atayaona, lakini tukikaa kuwanyooshea kidole, kila anayesimama Mkurugenzi,

Mkurugenzi wengine hatujajifunza taratibu za uendeshaji wa halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naongea haya nilikuwa Mkurugenzi na nimetoka hapa naingia hapa Bungeni, lakini mazingira yaliyopo kule kama tungekuwa tunapima *job weight* inawezekana Wakurugenzi wangkuwa katika ya watu wanaofanya kazi nyingi ndani ya Taifa hili, kuliko watu wengine, lakini ni kwa sababu ni kundi ambalo halisemewi, kila mtu anawageuza wale ni *punching box*, hivyo niombe auchukue ushauri wangu aufanyie kazi. Wale wachache ambao ni kweli wameshindikana, tutawachukulia wameshindikana, lakini wale *learned brothers and sisters* wanafanya kazi kwa weledi, naomba wawatumie wafanye kazi tutekeleze miradi kule chini.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa pili, ni upande wa afya. Naomba niipongeze TAMISEMI kwa kazi nzuri ambayo wamefanya hasa katika eneo la afya. Tunaona tumejenga hospitali nyingi katika kipindi hiki, tumejenga vituo vya afya, tumejenga zahanati. Haya mambo yamewezezana kwa sababu ya usimamizi mzuri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwa hiyo niombe tu tuendelee na *speed* kubwa ya kuweza kuboresha. Katika eneo hili naomba nishauri, nimesoma randama ya Fungu 56, kuna fedha ambazo Serikali wanazipata kutoka kwa wafadhili za Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Health Sector Basket Fund*).

Mheshimiwa Spika, mwaka jana fedha hizi kutoka kwa wafadhili zilichelewa *fourteen point something billion*, tukafunga mwaka tunazo, lakini mpaka leo hizo hela bado hazijaingia kwenye mfumo kwenda kufanya kazi kule. Fedha hizi ni za muhimu sana kuweza kuongeza nguvu kwa fedha zinazotokana na Serikali kwa ajili ya kununua dawa, kununua vifaa tiba, chanjo lakini na *supervision* kule chini, lakini mpaka mwezi Februari kwa ripoti ya TAMISEMI hizi fedha *fourteen point one billion* bado hazijaenda.

Mheshimiwa Spika, suala hili sio la TAMISEMI kwa sababu sisi tunashauri Serikali na Serikali ni moja tuiombe

Wizara ya Fedha masuala haya ya kutopata vibali vyatia matumizi ya fedha yamekuwa ni mengi. Serikali yetu yenye we inaweza ikawekea *checks and balance* yenye kwamba fedha zikija nje ya muda kuna jinsi ambavyo wanaweza wakaingia kwenye bajeti wakazipa vibali. Haya tumeyaona sio kwa TAMISEMI peke yake hata kwenye fedha za barabara tumeona hapa zilikuwa zimechelewa sana, wakandarasi, Wizara ya Ujenzi wakawa wamesimama kazi. Kwa hiyo naomba kushauri kwamba hizi fedha ni za msingi najua TAMISEMI inawezekana wanakimbizana kuomba vibali ili waweze kuhakikisha kwamba zinaingia katika mfumo na zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa tatu ni kwenye *force account*. Nchi hii imepiga hatua ndani ya miaka mitano kwa utaratibu mzuri wa *force account* ambao tumeutumia katika miradi mbalimbali, lakini tumpata michango mingi kutoka kwa Waheshimiwa wengine. Eneo hili lina mapungufu kidogo na hasa upungufu kidogo na hasa kama walivyosema ni kwa upande wa wataalam.

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha TARURA *ma-engineer* wote tumewachukua tumewapeleka TARURA, kwa kweli mimi niombe hatuhitaji kuwa na majengo ambayo *life span* yake itakuwa ni chini ya miaka mitano baada ya miaka mitano unakuta jengo linapasuka, lote linaharibika. Niwaombe sana TAMISEMI Waheshimiwa Wabunge wengine wametangulia kulisema, tujitahidi tupate Wahandisi wawe *stationed* moja kwa moja kwa Wakurugenzi, wale wanaoazimwa TARURA ikitokea kazi ya TARURA wanaacha ile kazi ambayo ni ya msingi ipo pale. Najua eneo hili kwa *force account* tutaendelea kusonga mbele, tuombe basi tuongezewe watalaam.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nishauri kwenye suala la TARURA. Najua kuna *formula* ambayo wanaitumia TARURA kuweza kupata fedha ndani ya wilaya fulani, lakini kuna vigezo vingine nahisi hatuvipi kipaumbele. Ukiangalia Mkoa wa Kagera ni Mkoa ambao kwanza una mvua nyingi katika kipindi kizima cha mwaka, karibu asilimia 75, lakini sehemu

hiyo imejaa mito, imejaa maziwa kila sehemu kuna maji na *water table* ipo juu sana. Sasa tukipewa bajeti sawa na eneo lingine ambalo kimsingi lina hali *conducive* kwa barabara hatuwezi kulingana, hizo barabara ndani ya muda mfupi zinaharibika.

Kwa hiyo niombe sana kupitia Ofisi yetu ya Rais, TAMISEMI wauangalie kwa jicho la pekee Mkao wa Kagera na *specifically* Wilaya ya Misenyi. Tunao mtandao wa barabara kilometra 921, tunapopata milioni 700, hata ile *formula* ambayo wanapiga kilometra moja kwa milioni mbili haitoshi. Kwa hiyo niombe sana...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, nakushukuru kwa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo. Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava na atafuatiwa na Mheshimiwa Luka Kitandula.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Kwanza napenda nimpongeze sana dada yangu Ummy Mwalimu kwa kupata nafasi ya kutumikia katika Wizara hii ya TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine nimpe pole kwa sababu wizara hii ni wizara ambayo imebeba wizara nydingine nyingi. Elimu ipo kule, afya ipo kule, kilimo kipo kule, kila kitu kipo kule, lakini naamini kwa jinsi ambavyo anafanya kazi, anachapa kazi pamoja na timu yote ya TAMISEMI naamini Insha' Allah Mwenyezi Mungu atamsaidia kama alivyofanya vizuri kwenye Wizara ya Afya, basi na TAMISEMI atafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyopita nimeona kwamba Wizara ya TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya trillion 5.26, lakini fedha ambayo ilitolewa mpaka inafika Februari, 2021 ilikuwa ni trillion 2.92. Ukiangalia ukubwa na majukumu makubwa ya Wizara ya TAMISEMI kwa fedha hii ambayo ni sawa na asilimia 39.8 haitoshi kukidhi yale yote tumeyazungumza mahali hapa. Waheshimiwa wengi wanalamika kuhusu maboma wanasema kuhusu miundombinu ya vituo vya afya, miundombinu ya *TARURA* kwa kweli kwa kiasi hiki cha fedha hakitoshi kukidhi yale ambayo tunyatamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ndijo maana kuna Mbunge mmoja alichangia akasema ikiwezekana iletwe kanuni humu Bungeni au sheria ya kuishinikiza mamlaka inayohusika kutoa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, itoe kadri ambavyo tumepanga.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya afya tumeona Wizara imejitahidi sana hospitali nyingi zimejengwa takribani 99 katika halmashauri lakini vituo vya afya 487, Hospitali za Kikanda tatu lakini haitoshi zahanati takribani 1,198. Pamoja na kujenga vituo hivyo lakini mahitaji bado ni makubwa sana ukilinganisha na jiografia ya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika hospitali ambazo zimejengwa au zimekwishajengwa bado kuna changamoto ambazo zinajitokeza, miundombinu bado haijakamilika. Hiyo haitoshi, bado wafanyakazi, kwa sababu huwezi kujenga Hospitali ukaacha kupeleka watenda kazi. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tuna hospitali ambayo kimsingi haijakamilika bado inafanya huduma za *OPD*, lakini bado tuna maboma ya vituo vya afya na zahanati 42 ambayo mpaka leo hii hayajakamilika, mengine yameanza kujengwa toka mwaka 2012, 2013 na 2014, mpaka sasa hivi hayajakamilika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani katika bajeti hii na natamani sana nisitoe shilingi ya Waziri kuhusu haya masuala ya kumalizia majengo ya maboma. Yale maboma

yana muda mrefu kama Butini kule, Kuni na sehemu zingine nyingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Sinyanga, hayajakamilika kwa muda mrefu. Tuliwahamasisha wananchi wetu, wakajitolea nguvu zao wakajenga yale maboma, lakini yamefika kwenye lenta mpaka sasa hivi bado hayajakamilika. Basi naomba katika bajeti hii inayokuja Serikali ione umuhimu wa kuweza kumalizia maboma haya na kuweza kuwatia nguvu wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujenga vituo vya afya, hospitali, zahanati na kuweka miundombinu tuna wafanyakazi ambao tunawahitaji katika maeneo yale. Hata hao wachache waliopo kwa kweli tunahitaji tuwakumbuke kama Serikali. Wafanyakazi wengi madaraja hayapandishwi, wafanyakazi wengi haki zao za kimsingi kama fedha ya likizo, matibabu wengi wao wengine hawapati. Tufike mahali tuangalle tuwape motisha hata ng'ombe unapomkamua maziwa ni lazima umpe mashudu. Wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hasa sekta ya afya pamoja na Walimu wote ambao wanafanya chini ya TAMISEMI.

Tunajua mazingira ambayo ni magumu, sehemu zingine hata usafiri haufiki. Sehemu nyingine kutoka Makao Makuu ya Wilaya kwenda kwenye kituo anachofanya kazi ni karibia km100, 110. Kwa kweli inasikitisha sana unakuta mfanyakazi anafanya kazi peke yake katika zahanati lakini stahili zake anazostahili kuzipata hazipati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwasababu inahusika na wafanyakazi wa Idara ya Afya wengine, inahusika na walimu, inahusika na Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji ione utaratibu wa kuwapa maslahi yanayostahili watumishi wetu. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana. Ahsante Dkt. Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika ni dakika tano tu?

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Dunstan L Kitandula

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu, kama mchangiaji wa mwisho.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya Wizara ya TAMISEMI iliyopo mbele yetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni kwa upendeleo wake tu kwamba tunaendelea kuwa salama, akizidi kutupa baraka zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pili, niipongeze Serikali, kwa hotuba iliyopo mbele yetu, ni hotuba ambayo inatutia matumaini, inatutia matumaini kwenye maeneo mengi. Kwenye eneo la elimu sisi wengine tukisia kwamba zinakwenda kujengwa sekondari za kata, kwenye kata ambazo zilikuwa hazina sekondari kwetu wengine ni faraja kubwa. Hongereni sana Serikali kwenye sekta ya afya mmesema mengi, hongereni. (*Makofi*)

Mhesimiwa Spika, lakini niseme machache, nianzie TARURA ambayo wenzangu wengi wamesema, wote tunakubaliana kwamba kiasi cha fedha kinachopelekwa TARURA ni kidogo na kwamba lazima tutumie maarifa mapya ili kupata vyanzo vya kuongeza mapato ya kupeleka fedha kwenye eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yametoka mawazo mengi, naomba Serikali iwe sikivu, tuongeze fedha hizi twende tukazijenge barabara za vijijini. Maana barabara hizi, zinahusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa uchumi lakini vilevile kuondoa umaskini kwa watu wetu. Lakini wakati tukizungumzia eneo la kuongeza fedha, kuna eneo lingine

lazima tuliangalie, udhibiti na ufuutiliaji. Ni eneo ambalo nalionia kama hatujalizungumzia sana na hapa nitatoa mifano, mifano ambayo inagusa Mkinga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019, Mkoa wa Tanga ulipata majanga ya mafuriko, miundombinu mingi ikaharika, Wilaya ya Mkinga tulipata bahati mbaya madaraja ya barabara za *TARURA* lakini hata zile za *TANROADS*. Barabara za *TANROADS* zilifanyiwa kazi lakini *TARURA* kipindi kile ilishindikana, tukaambiwa jambo lile linachukuliwa liingizwe kwenye bajeti ya mwaka 2020 ikaingizwa, Mwezi wa Julai, 27 ikifunguliwa zabuni kwa ajili ya kutengeneza barabara zile na madaraja yaliyokuwa yameharibika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Agosti, 2020, Zabuni ile ikafunguliwa lakini Wakandarasi hawakupatikana. Ikatangazwa tena mwezi Novemba, 2020 akapatikana Mkandarasi, tarehe 03 Machi, 2021 wakaingia Mkataba, Mkandarasi akakabidhiwa eneo la kazi, alitakiwa tarehe 15 Aprili, 2021 awe ameanza kazi, mpaka leo hajaanza kazi. Hii ni dalili mbaya, kwamba Mkandarasi huyu anakwenda kushindwa, akishindwa maana yake tutangaze tena apatikane Mkandarasi, hapa imebakie miezi miwili mwaka wa fedha huu uishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tangu 2019, watu hawa wa Kuze, watu wa Mhiduro, watu wa Bosha, hawawezi kuitisha mazao yao kwenye barabara kwasababu daraja limevunjika, fedha zipo lakini tunashindwa kuhudumia barabara hizi kwasababu ya taratibu za kirasimu za ununuzi niwaombe sana, tufuutilie eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, zinaweza kuwa nitaratibu za kimanunuzi lakini vileyile inaweza kuwa ni uchochoro wa fedha zisitumike eneo hili ziende zikatumike eneo lingine, tusaidieni daraja lile la Kauzeni liweze kushughulikiwa. Lakini hata kwenye *allocation* ya fedha, *TARURA* wana mpango wa kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa nje ya zile za kibajeti kwenye wilaya hizi ili iweze kusaidia miradi ile ambayo inahitaji fedha nyngi iweze kushughulikiwa. Sisi wa Mkinga

tangu mwaka 2013 hatujawahi kupata fedha hizi, wilaya hii ina maeneo ya milima, barabara za kwenye milima ni changamoto kwa hiyo, tunashindwa kutengeneza barabara hizi kwasababu kabajeti ketu ni kadogo. Mtendaji Mkuu wa TARURA alikuja kule, akaiona hali akasema watu wa Mkinga mnastahili kupata fedha hizi mpaka leo, tangu mwaka 2013 mpaka leo, hakuna senti tano iliyokwenda. Hii haiwezi kuwa sawa, tunaomba mtusaidie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Afya, nakwenda kulekule kwenye ufuatiliaji, tunaishukuru Serikali imetupatia fedha kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya. Tulipata milioni 500 mwaka wa fedha uliokwisha lakini kwasababu zilichelewa kuletwa mwezi wa Juni fedha zile zikarudishwa. Mwaka huu wa fedha Januari tumepata bilioni 1, tunaishukuru Serikali lakini naomba Serikali mfuatilie, ninashida na utekelezaji wa mradi huu, kwa sababu tumepata fedha Januari... (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, mpaka leo.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, mpaka leo, katika bilioni 1 ni milioni 200 tu zimetumika. Kuna Kamati ya Manunuzi kule ya hovyo nendeni mkafumue kamati ile, haiwezekani miaka miwili mfululizo Serikali inatoa fedha halafu ifike mwezi Juni hapa hakutuveza kutumia fedha zile zirudi serikalini, haiwezekani! Sasa Serikali mtusaidie, msingoje ufike mwezi Juni mtuambie Mkinga hamkuweza kutumia fedha. Nendeni sasa mkasimamie jambo lile. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Sekondari ya Maramba. Tumekamilisha madarasa pale, ya kuipandisha hadhi sekondari ile iwe na kidato cha tano na cha sita. Tunaishukuru Serikali ililetu milioni 300 pale, wananchi wamechangia, Mbunge wao kuitia Mfuko wa Jimbo nimechangia, tumakamilisha mabweni, tumeweka samani, ilikuwa ianze mwaka jana kukawa na tatizo la kuweka bajeti ya chakula kwa sekondari ile ikashindwa kuanza. Naomba kipindi hiki sekondari ile ianze. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Lazima ianze.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kutoa kibali cha zahanati zetu karibu tano hivi tulikuwa tumeziombea zipate kibali zianze. Kibali kimetoka tumeziweka zahanati hizi kwenye mpango wa bajeti vifaa tiba viende. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho na hili Mheshimiwa Waziri wewe unalijua, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara, akaja Maramba, tukampeleka kwenye Kituo cha Afya cha Maramba. Maramba kuna zaidi ya watu 12,000 tumeomba hospitali ile kwasababu ina hudumia kata saba ipewe hadhi ya kufanya kama hospitali ya wilaya ili mzigo ule wa kuhudumia zile kata sana uishe. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula naikumbuka Maramba nilikuwa pale JKT enzi hizo. Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu. (*Makof*)

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na naomba nimpongeza waziri kwa hotuba yake nzuri na kimsingi ni kwamba ni mpongeze pia mtangulizi wake kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano iliyokwisha, Jimbo langu la Geita Mjini, llijenga shule mpya za sekondari 13. Na likajenga shule mpya za msingi 13, maana yake tulipata shule mpya 26. Lakini katika kipindi chote hicho, mgao wa walimu ajira mpya umekuwa mdogo sana. naipongeza Serikali kwa kuziba mapengo ya walimu waliostaafu hizi ajira 6,000 ambazo imesema itatangaza hivi karibuni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kama Jimbo langu peke yangu lina shule 26 na sasa hivi najenga shule zingine nane maana yake ni kwamba walimu wanaokuja hawawezi kwenda kumaliza tatizo la walimu katika hal mashauri zetu. Niiombe Serikali kwa sababu tulikuwa na hizi ajira 6,000 lakini

tuna ajira zingine ambazo zilikuwa zimetangazwa na zikaacha kuajiriwa ni vizuri Serikali ikaajiri walimu wa kutosha katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kutokuwa na walimu kwenye shule ni makubwa sana. Huku juu ambako tunakwena watoto wanakwenda Chuo Kikuu, wanashindanishwa kwa ufaulu na ufaulu wao hauangalii historia kwamba huyu mtoto kwa bahati mbaya hakupata elimu ya kutosha kutokana na uhaba wa walimu alipokuwa sekondari. Na hata wakati mwингine, mikopo inaangalia aliyefaulu vizuri sana, sasa utaangalia shule ambayo ina walimu wanne na ina Watoto 600 ametoa mfano hapa Mheshimiwa Mbunge asubuhi, ipo kata yangu mimi *form one* walioanza mwaka huu wapo 850, lakini shule nzima ina walimu 32, na wanafunzi wengine wapo zaidi ya 2,000 utaona shule hii kama wanafunzi hawa wataendelea kufika *form 4* na baadaye waende Chuo Kikuu hata kama watafaulu, hawataweza kushindana na wale ambaa walikuwa kwenye shule yenye walimu wa kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna Watoto wana adhibiwa huko Chuo Kikuu kwa kuoneokana hawakufaulu vizuri lakini kwasababu ya mapungufu waliyoyapata walipokuwa sekondari. Niombe sana, wizara ituletee walimu wa kutosha. Kinachofanyika sasa tunaongeza idadi ya shule, tunaongeza idadi ya wanafunzi, tuna-deal/na *quantity* na hakuna *quality* ya Watoto wanaomaliza shule. Tunaweza kufikiri tunafanikiwa lakini kimsingi tunapeleka kundi kubwa la watu ambaa hawakupata elimu ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa spika, tatizo hili lipo pia kwenye afya, tumejenga zahanati mpya 24. Zahanati 24, zahanati unakwenda unakuta *nurse* peke yake. Mwaka juzi na mwaka jana tulajiri madaktari, nikaamini sasa Serikali inakuja kuajiri hizi kada za kati ma-*clinical officerna* ma-*nurse* hawa katikati, lakini hizi kada zimekuwa zinaajiriwa taratibu sana matokeo yake sasa tuna zahanati nyingi tunajenga kila Kijiji, lakini zahanati ina mhudumu mmoja na huyo mhudumu akiugua zahanati inafungwa. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa

Waziri, najua hizi zinasimamiwa na TAMISEMI lakini inawezekana wanaoratibu ajira hizi wakawa ni wengine lakini uwepo tunahamasisha wananchi kujenga ni vizuri wakapata huduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kwenye mradi ambao ulikuwa unaitwa *LGSP*mradi huu ulikwisha na tukapata mradi mwingine unaitwa *TACTICS* wamesema wenzangu hapa. Taarifa tulizonazo ni kwamba fedha hizi tayari zipo, kinachotakiwa ni Serikali kutoa *commitment* ili pesa ziweze kutoka. Mazungumzo ya fedha hizi yalianza tangu mwaka jana tumeshirikishwa na wale wataalam waliokuwa wanakuja, ikaaminika zingesainiwa kabla ya bajeti hii haijapita, sasa tunaona mwaka wa fedha unaisha, hii miji 45 anbayo inahitaji pesa hizi ni muhimu sana Serikali ikatoa *commitment* ili tukaweza kupata fedha hizi zikaenda kusaidia watu wa *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, pale kwangu pale Geita Mjini barabara zote ni mbovu lakini mradi huu ukianza utachukua sehemu kubwa ya barabara za pale mjini na *TARURA* wata-deal/na barabara zingine sehemu za vijijini. Hatujui ni kwa nini mradi huu unachelewa kuanza kwasababu wanaotoa fedha hizi walishatoa, fedha ziko Serikalini, Serikali inatakiwa kufanya *commitment* tu fedha ziweze kutumika. Miji 45 Tanzania itapata fedha.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ambalo tunalo hapa ni kuchelewa sana kufanya maamuzi. Kwa sababu tungechelewa kutafuta fedha, tumeshatafuta fedha tumepata, kufanya maamuzi ya kuzitumia fedha tunachelewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *TARURA* ilichukua ma-*engineer* wote kwenye halmashauri, Tanzania nzima ma-*engineer* waliopo kwenye halmashauri ni 84. Halmashauri tulizonazo ni 180 na kitu, kwa hiyo utagundua kuna upungufu wa ma-*engineer*100. Lakini niombe, kwenye majeshi yetu huko hasa Jeshi la Ulinzi la Wananchi kuna ma-*engineer* kuna ma-*engineer* wamejaa. Badala ya kutuletea washauri wa

Mgambo ambao hawana taaluma wachukue washauri wa mgambo ma-*engineer* wawapeleke kwenye halmashauri huko, kwenye wilaya tunaweza tukawaazima kwenye miradi.

Mheshimiwa Spika, amesema Mheshimiwa mmoja hapa, tunatumia *force account*, ubaya wa *force account* hakuna retention kwa hiyo inapotokea mradi ule umekosewa usitegemee kuna mtu atakuja kurekebisha, kwa hiyo lazima ufanyike kwa usahihi tangu mwanzo. Tunajenga majengo makubwa milioni 500, milioni 400 hakuna *engineer* waliopo ni ma-*technician*. Niiombe sana wizara, kama kuajiri itashindikana vipo vyombo vina ma-*engineer* waazime walete hao watu wafanye kazi kule hii ndo maana ya Serikali moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitoa ushauri kwenye *TARURA*. *TARURA* walipoundwa ilionekana kama chombo fulani hili kinajitegemea, na matokeo yake kikajikuta huku halmashauri ni kama halmashauri hawatusiki. Kabla ya *TARURA*, Mkurugenzi alikuwa na uwezo wa barabara ikiharibika anatumia fedha zake kwenda kurekebisha barabara kwasababu kuna *emergence*. Leo mkurugenzi hawezи kwanini! kwasababu *TARURA* ni ka chombo fulani kanachojitegemea. Mimi nikuombe Mheshimiwa waziri, pitia upya muundo wa jambo hili, kama ni lazima hawa watu wapo halmashauri pale warudishwe halmashauri waendelee kuwa na pesa zao lakini warudishwe halmashauri wawzeze kushiriki, kusimamia na Madiwani na Kukaguliwa.

Mheshimiwa Naibu spika, Hii itawawezesha halmashauri wanapotoa fedha wawzeze kuamini kwamba tunawapa wenzenetu. Leo mkurugenzi akitaka ripoti lazima aombe, Madiwani wakitaka taarifa lazima waombe, na huyu meneja wa *TARURA* wa wilaya ni kama karani kazi zote zinafanya mkoani. Aliyeko pale hawezи kufanya chochote. Mheshimiwa hii imekata mawasiliano kabisa ya wawakilishi wa wananchi na matatizo ya barabara na unajua sehemu kubwa ya kura za Madiwani na Wabunge ziko kwenye barabara. Kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa utazame upya huu muundo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilipitia bajeti za mikoa, tumegundua kwenye asilimia 10 tumetunga sheria nzuri sana ya asilimia 10. Halmashauri nyingi zimetimiza agizo hilo, shida iliyopo hakuna ufuutiliaji wa kutosha wa fedha zilizokopeshwa, lakini hakuna utaalama wa kutosha kwenye halmashauri wa *ku-manage fund* kubwa.

Nataka kutoa tu mfano, Halmashauri ya Mji wa Geita inakusanya takriban shilingi bilioni mpaka bilioni 8, shilingi bilioni nane kwa mwaka. Fedha hizi ni nyingi sana, matokeo yake unatenga milioni 8 kwa miaka mitano unazungumzia takriban shilining bilioni 4, shilingi bilioni 4 tuligiza kwenye Kamati zifunguliwe akaunti maalum zisiende kwenye *general account* maana yake kwa miaka mitano tuna 20 billion. Lakini halmashauri zote, mikoa yote iliyokuja kuhojiwa hakuna *continuation* ya akaunti ya mwaka uliyopita na mwaka mwingine. Maana yake fedha hizi hazijulijani zikowapi? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu muda huu, malizia sentensi mbili, tatu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa kuwa tulisema halmashauri zifungue akaunti inayojitegemea, tunachotarajia sasa akaunti hii itakuwa inakuwa *at time five years* tutakuta kuna 20 *billion*, kuna 10 *billion* na halmashauri zitaacha kusubiri makusanyo ya mwezi kukopesha wananchi. Lakini kwa sasa fedha hizi zinapotea, hazijulikani ziko wapi, wanaokuja wanakuja na hesabu za mwaka jana hawaji na *collection* ya mwaka wala haijulikani wana shilingi ngapi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mhesimiwa Constantine J. Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, tutaendelea bado na uchangiaji kwa TAMISEMI kesho, mtu ye yeye ambaye hakupata nafasi leo asiwe na wasiwasi. Kesho tunaendelea na kesho kutwa siku ya Jumatano tutakuwa *windup*, lakini kwa kweli kama unapenda kuchangia basi jitahidi kesho upate nafasi. Kwa

sababu Jumatano inategemeana na hali halisi na mafungu ya TAMISEMI ni mengi kwa hiyo tunaweza kuanza mapema kuanza kuyapitia mafungu yale.

Baada ya hilo, kuna tangazo la ofisi yetu, linawakumbusheni kwamba niliwatangazia asubuhi ya leo kwamba siku ya Alhamisi tarehe 22 Aprili, 2021 tutakuwa na ugeni wa Mheshimiwa Rais, ambaye baada ya hotuba yake jioni atafuturu nasi hapa hapa katika viwanja vya Bunge.

Kwa jinsi hiyo kuanzia kesho, tarehe 20 Aprili, 2021 tunawaomba Waheshimiwa Wabunge msiegeshe magari yetu katika eneo la maegesho ya Wabunge, kwa kuwa maeneo hayo yatakuwa na kazi maalum. Kwahiyo, tuegeshe magari yetu nje ya uzio wetu wa Bunge na kandokando ya barabara hasa kule na niwahakikishie kabisa Ofisi ya Bunge itatoa ullnzi wa uhakika katika maeneo hayo muda wote. Iakini pia kutakuwa na mabadiliko ya hapa na pale mtuvumilie Waheshimiwa Wabunge na katika mageti yetu yote hali ya ulinzi itaongezeka kidogo. Kwa hiyo, tukichekiwa chekiwa kidogo tusishangae shangae.

Basi baada ya matangazo hayo kama unavyojuua Mwezi huu Mtukutu, saa kama hizi wenzetu Waislam waliofunga wanahitaji waanze kusogea sogea kwenye maeneo husika wawewe kupata futari na kwa kuwa kazi zillizopangwa zote zimekamilika tena kwa wakati, basi naomba nahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu Asubuhi

*(Saa 12.04 Jioni Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumanne,
Tarehe 20 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*